# Kiswahili

# Mchepuo: LFK

# Kidato cha 4

## Mwongozo wa Mwalimu

*©2024 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi*
*Haki zote zimehifadhiwa.*
*Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.*
*Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.*

# DIBAJI

Mwalimu Mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa kitabu hiki cha mwalimu wa somo la Kiswahili, mchepuo wa Lugha kidato cha nne. Kitabu hiki ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo katika kila ngazi ya elimu ili aweze kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira. Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa wa ujifunzaji. Mambo mengi yanaathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahsusi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo. Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unakuwezesha kuendeleza mawazo yako na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi, kwa msaada wa walimu ambao majukumu yao ni kufanikisha ufundishaji. Wanafunzi, kwa msaada wa mwalimu, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa.

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mwalimu litakuwa:

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;
- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;

- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti nay ale wanayojifunza;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Mwongozo huu umeganyika katika sehemu tatu (3) zifuatazo:

**Sehemu ya 1**: Huelezea muundo wa kitabu hiki na kukupa mbinu na maelekezo ya ufundishaji.

**Sehemu ya 2**: Hukupa sampuli ya andalio la somo kama marejeleo ya mchakato wa kuandaa somo.

**Sehemu ya 3**: Hutoa mwongozo au maelekezo ya ufundishaji kwa kila dhana iliyotolewa ndani ya kitabu.

Napenda kutoa shukrani kwa wale wote walioshiriki kutoa mchango wa kuboresha kitabu hiki, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (REB-CTLR ) walioandaa mchakato wa kazi hii tangu ilipoanza.

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mawazo yoyote yanakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo yatakayofuata.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

# SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mwalimu. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana (CTLR)**

## YALIYOMO


DIBAJI ........................................................... iii

SHUKRANI ........................................................... v

SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA. ........................................ 15

1.1.Muundo wa Mwongozo wa mwalimu .................................... 15

1.2 Mwelekeo wa ufundishaji .......................................... 15

1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo .................................. 15

1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala mtambuka.. ................................ 16

1.2.3. Uangalizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ................... 16

1.2.4. Mwongozo wa Tathmini ........................................... 17

1.2.5 Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji. ....... 17

1.2.6. Mbinu za Ufundishaji Zinazokuza Shughuli ya Ujifunzaji Shirikishi. ....... 18

SEHEMU II: SAMPULI YA ANDALIO LA MASOMO .............................. 19

SEHEMU III: UUNDAJI WA MADA .......................................... 37

MADA KUU YA 1: LUGHA NA JAMII. ........................................ 37

*MADA NDOGO YA 1: LUGHA YA KISWAHILI* ................................. 37

1.1 Uwezo Upatikanao katika Mada: .................................... 37

1.2 Ujuzi wa Awali .................................................... 37

1.3 Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada.. ...................... 37

1.4 Mwongozo kuhusu Kidokezo cha Mada ................................. 39

1.5 Orodha ya Masomo. ................................................. 39

**SOMO LA 1: MAANA YA LUGHA** ......................................... 41

1.1 Ujuzi wa Awali/ Utangulizi ........................................ 41

1.2 Zana na Vifaa vya Ufundishaji ..................................... 41

1.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji ............................... 41

1.4 Majibu ............................................................ 42

1.4.1 Zoezi la Ufahamu .................................................. 42

1.4.2. Matumizi ya Msamiati ............................................. 42

1.4.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti –nge- ...... 43

1.4.4. Matumizi ya Lugha: Mazoezi ya Makundi. ........................... 44

1.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........................................... 45

**SOMO LA 2: UMUHIMU WA LUGHA** ....................................... 45

2.1 Ujuzi wa awali. . . . . . . . 45
2.2 Zana au vifaa vya kujifunzia . . . . . . . . 46
2.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . 46
2.4 Majibu . . . . . . . . 46
2.4.1. Maswali ya Ufahamu . . . . . . . . 46
2.4.2. Msamiati kuhusu Umuhimu wa Lugha . . . . . . . . 47
2.4.3. Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -nge- . . . . . . . . 48
2.4.4. Matumizi ya Lugha . . . . . . . . 50
2.4.5. Kusikiliza na kuzungumza . . . . . . . . 51
2.4.6. Kuandika . . . . . . . . 51
**SOMO LA 3: LUGHA KATIKA JAMII . . . . . . . . 52**
3.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi. . . . . . . . 52
3.2 Zana za kujifunzia . . . . . . . . 52
3.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . 52
3.4 Majibu . . . . . . . . 53
3.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . . . . . . 53
3.4.2 Msamiati kuhusu lugha katika jamii . . . . . . . . 54
3.4.3 Matumizi ya Lugha . . . . . . . . 54
3.4.4 Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . 55
3.4.5 Kuandika . . . . . . . . 55
**SOMO LA 4: FAIDA NA HASARA ZA KUTUMIA LUGHA MOJA. . . . . . . . 56**
4.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi. . . . . . . . 56
4.2 Zana za kujifunzia . . . . . . . . 56
4.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . 57
4.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . . . . . . 57
4.4.2 Msamiati kuhusu Faida na Hasara za Kutumia Lugha Moja . . . . . . . . 58
4.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -ngeli . . . . . . . . 59
4.4.4 Matumizi ya Lugha . . . . . . . . 60
4.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . 60
4.4.6 Kuandika . . . . . . . . 61
**SOMO LA 5: ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI . . . . . . . . 61**
5.1 Utangulizi/ Marudio . . . . . . . . 61
5.2 Vifaa vya kujifunzia . . . . . . . . 61

5.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . 62
5.4 Majibu . . . 62
5.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 62
5.4.2 Msamiati kuhusu Asili ya Lugha ya Kiswahili . . . 63
5.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -ngali- . . . 64
5.4.4. Matumizi ya Lugha: Mazoezi ya Makundi . . . 65
5.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . 66
5.4.6 Kuandika: Utungaji . . . 66
**SOMO LA 6: Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili . . . 66**
6.1 Utangulizi/Marudio . . . 67
6.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia . . . 67
6.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji . . . 67
6.4 Majibu . . . 67
6.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 67
6.4.2 Msamiati kuhusu Ueneaji wa Kiswahili . . . 68
6.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti . . . 69
6.4.4 Matumizi ya lugha: Mazoezi ya Makundi . . . 68
6.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 70
6.4.6 Kuandika . . . 70
**SOMO LA 7 : HISTORIA YA KISWAHILI NCHINI RWANDA . . . 70**
7.1 Utangulizi . . . 70
7.2 Vifaa . . . 70
7.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . 70
7.4 Majibu . . . 72
7.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 72
7.4.2 Msamiati kuhusu Historia ya Kiswahili Nchini Rwanda . . . 73
7.4.3 Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti "-ngeli-" . . . 74
7.4.4 Matumizi ya lugha . . . 75
7.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 76
7.4.6 Kuandika: Utungaji . . . 76
7.5 Muhtasari wa Mada . . . 76
7.6 Maelezo ya Ziada . . . 77
1.8 Tathmini ya Mada ya Kwanza . . . 77

1.9.1 Mazoezi ya urekebishaji . . . 77
1.9.2Mazoezi jumuishi. . . . 78
**MADA KUU YA 2: LUGHA KATIKA SANAA . . . 81**
***MADA NDOGO YA 2: FASIHI KATIKA KISWAHILI. . . . 81***
Uwezo Upatikanao katika Mada . . . 81
Ujuzi wa Awali . . . 81
Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada . . . 81
Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada . . . 83
Orodha ya Masomo na Tathmini . . . 83
**SOMO LA 8: DHANA YA SANAA . . . 85**
8.1. Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi . . . 85
8.2 Zana za Kujifunzia . . . 85
8.3. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . 85
8.4 Majibu. . . . 86
8.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 86
8.4.2 Msamiati kuhusu Sanaa na Manufaa yake . . . 87
8.4.3 Sarufi : Nomino za Ngeli ya LI-YA . . . 89
8.4.4 Matumzi ya Lugha : Dhana ya Sanaa . . . 90
8.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 91
8.4.6 Kuandika. . . . 91
**SOMO LA 9: DHANA YA FASIHI . . . 91**
9.1 Utangulizi/Marudio . . . 91
9.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia . . . 92
9.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji . . . 92
9.4 Majibu. . . . 93
9.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . 93
9.4.2 Msamiati kuhusu Dhana ya Fasihi. . . . 94
9.4.3 Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Idadi katika Ngeli ya LI-YA . . . 95
9.4.4 Matumizi ya Lugha: Dhana ya fasihi. . . . 96
9.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza . . . 97
9.4.6 Kuandika. . . . 97
**SOMO LA 10: Dhima ya Sanaa katika Jamii . . . 97**
10.1 Ujuzi wa Awali . . . 97

10.2 Zana na vifaa vya Ufundishaji . . . . . . . . . . 97
10.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . . . 98
10.4. Majibu . . . . . . . . . . 98
10.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . . . . . . . . 99
10.4.2 Msamiati kuhusu Sanaa katika Jamii . . . . . . . . . . 99
10.4.3 Sarufi: Nomino za ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki. . . . . . . . . . . 100
10.4.4 Matumizi ya lugha: Dhima ya Fasihi . . . . . . . . . . 102
10.4.5 Kuzungumza na Kusikiliza . . . . . . . . . . 102
10.4.6 Kuandika: Utungaji . . . . . . . . . . 102
**SOMO LA 11: Hadithi . . . . . . . . . . 102**
11.1 Ujuzi wa awali . . . . . . . . . . 102
11.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia . . . . . . . . . . 103
11.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . . . 103
11.4.Majibu . . . . . . . . . . 104
11.4.1 Maswali ya ufahamu . . . . . . . . . . 104
11.4.2 Msamiati kuhusu Hadithi . . . . . . . . . . 104
11.4.3 Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Kuuliza katika Ngeli ya LI-YA . . . . . . . . . . 105
11.4.4 Matumzi ya Lugha : Aina za Hadithi . . . . . . . . . . 106
11.4.5 Kusikiliza na kuzungumza : . . . . . . . . . . 107
11.4.6 Kuandika: . . . . . . . . . . 107
**SOMO LA12: METHALI. . . . . . . . . . . 108**
12.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi . . . . . . . . . . 108
12.2 Zana za kujifunzia . . . . . . . . . . 108
12.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji . . . . . . . . . . 108
12.4 Majibu . . . . . . . . . . 109
12.4.1 Maswali ya Ufahamu . . . . . . . . . . 109
12.4.2 Msamiati kuhusu Methali . . . . . . . . . . 110
12.4.3 Sarufi: Vivumishi vya Kuonyesha katika Ngeli ya LI-YA . . . . . . . . . . 111
12.4.4 Matumizi ya lugha: Maana ya Methali na uUhambuzi Wake . . . . . . . . . . 112
12.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza . . . . . . . . . . 113
12.4.6 Kuandika . . . . . . . . . . 113
**SOMO LA 13: NAHAU . . . . . . . . . . 114**
13.1 Uwezo wa Awali / Marudio / Utangulizi. . . . . . . . . . . 114

13.2 Vifaa . . . . . . . . . . 114
13.3 Mbinu za ufundishaji . . . . . . . . . . 114
13.4. Majibu . . . . . . . . . . 115
13.4.1 Majibu ya Ufahamu . . . . . . . . . . 115
13.4.2 Msamiati . . . . . . . . . . 116
13.4.3 Sarufi: Nomino za Ngeli ya LI-YA na Vivumishi vya Pekee . . . . . . . . . . 117
13.4.4 Matumizi ya Lugha: Nahau . . . . . . . . . . 118
13.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano . . . . . . . . . . 119
13.4.6 Kuandika: Utungaji . . . . . . . . . . 119
13.5 Muhtasari wa Mada . . . . . . . . . . 119
13.6. Maelezo ya Ziada . . . . . . . . . . 120
13.7. Tathmini ya Mada . . . . . . . . . . 120
13.8. Mazoezi ya Ziada . . . . . . . . . . 120
13.8.1. Mazoezi ya urekebishaji . . . . . . . . . . 120
13.8.2. Mazoezi ya Nyongeza: . . . . . . . . . . 121
**MADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI . . . . . . 123**
***MADA NDOGO YA 3: MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI . . . . . . . . . . 123***
Uwezo upatikanao katika mada . . . . . . . . . . 123
Ujuzi wa Awali kwa Mwanafunzi . . . . . . . . . . 123
Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada . . . . . . . . . . 123
Orodha ya Masomo ya Mada hii Pamoja na Tathmini . . . . . . . . . . 124
**SOMO LA 14: MAANA YA MUHTASARI NA SIFA ZAKE . . . . . . . . . . 125**
**SOMO LA 15.: TARATIBU ZA KUTOA MUHTASARI MZURI . . . . . . . . . . 129**
**SOMO LA 16: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI . . . . . . . . . . 133**
**SOMO LA 17: MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI . . . . . . . . . . 139**
**SOMO LA 18: UHAKIKI WA HADITHI SIMULIZI . . . . . . . . . . 145**
**MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO . . . . . . . . . . 157**
***MADA NDOGO YA 4: MIDAHALO NA MIJADALA . . . . . . . . . . 157***
**SOMO LA 19: MAANA YA MDAHALO NA MJADA. . . . . . . . . . 161**
**SOMO LA 20: MDAHALO NA MJADALA . . . . . . . . . . 167**
**SOMO LA 21: UTEKELEZAJI WA MDAHALO . . . . . . . . . . 175**
**SOMO LA 22: UTEKELEZAJI WA MJADALA . . . . . . . . . . 185**
22.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi . . . . . . . . . . 185

22.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia .......................................185
22.3 Mbinu za kufundishia na Kujifunza ................................ 186
22.4 Majibu.............................................................. 186
22.4.1 Majibu ya Ufahamu ............................................... 186
22.4.2 Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo na Mjadala ....................187
22.4.3 Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha katika Vitenzi vyenye Silabi Moja Hali Yakinishi na Kanushi ...................................... 188
22.4.4 Matumizi ya Lugha: Utekelezaji wa Mjadala......................... 190
22.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........................................ 190
22.4.6 Utungaji..............................................................191
22.5.. Muhtasari wa Mada .....................................................192
22.6. Maelezo ya Ziada........................................................192
22.7. Tathmini ya Mada........................................................193
22.8. Mazoezi ya Ziada .......................................................195
22.8.1. Mazoezi ya urekebishaji..............................................195
**MADA KUU YA 5: UTUNGAJI** ...............................................**199**
***MADA NDOGO YA 5: INSHA ZA MASIMULIZI AU KUBUNI NA UANDISHI WA RIPOTI*** .... ***199***
**SOMO LA 23: MAANA YA INSHA**........................................... **204**
23.1: Ujuzi wa Awali / Utangulizi ......................................... 204
23.2: Zana au Vifaa vya Kujifunzia......................................... 204
23.3: Mbinu za Kufundishia na Kujifunza.................................... 204
23.4 Majibu.............................................................. 205
23.4. 1Maswali ya Ufahamu ................................................. 205
23.4.2 Msamiati kuhusu Maana ya Insha...................................... 205
23.4.3: Sarufi: Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa ( katika wakati uliopo).... 207
23.4.4 Matumizi ya Lugha .................................................. 208
23.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........................................... 208
23.4.6 Utungaji............................................................. 208
**SOMO LA 24: AINA ZA INSHA**........................................... **209**
24.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi ................................... 209
24.2 Zana za Kujifunzia.................................................. 209
24.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza ....................................210
24.4 Majibu...............................................................210

24.4.1 Majibu ya Ufahamu .......................................210
24.4.2. Msamiati ....................................... 211
24.4.3. Sarufi .......................................212
24.4.4. Matumizi ya Lugha: .......................................214
24.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza. .......................................214
24.4.6. Kuandika .......................................215
**SOMO LA 25: Insha ya Masimulizi .......................................216**
25.1 Ujuzi wa Awali .......................................216
25.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia .......................................216
25.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza .......................................216
25.4Majibu .......................................217
25.4.1 Maswali ya Ufahamu .......................................217
25.2 Msamiati .......................................219
25.4.3: Sarufi : Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa. .......................................221
25.4.4 : Matumizi ya Lugha .......................................222
25.4.5: Kusikiliza na Kuzungumza. .......................................222
25.4.6: Utungaji .......................................222
**SOMO LA 26: INSHA YA KUBUNI. ....................................... 223**
26.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi. ....................................... 223
26.2. Zana za Kujifunzia ....................................... 223
26.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza ....................................... 224
26.4 Majibu. ....................................... 224
26.4.1. Maswali ya Ufahamu ....................................... 224
26.4.2. Msamiati ....................................... 225
26.4.3. Sarufi .......................................227
26.4.4. Matumizi ya Lugha. ....................................... 228
26.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza ....................................... 229
26.4.6 Kuandika. ....................................... 230
**SOMO LA 27: RIPOTI .......................................231**
27.1. Ujuzi wa Awali /Utangulizi. .......................................231
27.2. Zana au Vifaa vya Kujifunzia .......................................231
27.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza. .......................................231

27.4 Majibu ........ 232
27.4.1Maswali ya Ufahamu ........ 232
27.4.2 Msamiati ........ 233
27.4.3 Sarufi ........ 234
27.4.4. Matumizi ya Lugha ........ 235
27.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza. ........ 236
27.4.6 Kuandika ........ 236

**SOMO LA 28: UTUNZI WA RIPOTI ........ 237**
28.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi ........ 237
28.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia ........ 238
28.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza ........ 238
28.4. Majibu ........ 239
28.4.1 Maswali ya Ufahamu ........ 239
28.4.2 Msamiati ........ 239
28.3 SARUFI : Usemi Halisi/Usemi wa Asili ........ 241
28.4.4 Matumizi la Lugha ........ 244
28.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza ........ 245
28.4.6 Kuandika ........ 245
28.5. Muhtasari wa Mada ........ 246
28.6. Maelezo ya ziada ........ 246
28.7 Tathmini ya Mada ya Tano (majibu) ........ 249
28.8. Mazoezi ya Ziada ........ 250
28.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji ........ 250
28.8.2. Mazoezi Jumuishi ........ 251
28.8.3. Mazoezi ya Nyongeza ........ 252

**MAREJEO ........ 254**

# SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1. Muundo wa Mwongozo wa mwalimu

Kitabu hiki ni mwongozo wa mwalimu katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili, kidato cha nne, mchepuo wa lugha katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kimetayarishwa kwa mwelekeo wa mtaala uegemeao kwenye uwezo. Mwongozo huu wa mwalimu umezingatia mada kuu tano kama ifuatavyo:

1. Lugha na jamii
2. Lugha katika Sanaa
3. Uhakiki wa hadithi za masimulizi katika Kiswahili
4. Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo
5. Utungaji.

Kila mada hujigawa katika mada ndogo na kila mada ndogo katika masomo mbalimbali. Kila somo hufuata muundo ufuatao:

1.1.Kusoma na kufahamu
1.2.Maswali ya ufahamu
1.3.Matumizi ya msamiati wa msingi
1.4.Sarufi
1.5.Matumizi ya lugha
1.6.Kusikiliza na kuzungumza
1.7.Kuandika.

Mwongozo wa mwalimu hutia mkazo kwenye majibu ya mazoezi yaliyotolewa pamoja na mbinu za kufundishia kwa kila zoezi.

## 1.2 Mwelekeo wa ufundishaji

Kinyume na mtaala uegemeao kwenye ujuzi, mtaala uegameao kwenye uwezo huwa na lengo kuu la kumfanya mwanafunzi mlengwa wa somo na kumshirikisha kimatendo katika mchakato wa ujifunzaji wake. Hapa mwalimu hatawali somo bali wajibu wake ni kumuelekeza au kumwongoza mwanafunzi katika somo lote. Kwa ufupi, mwanafunzi hachukuliwi kama mgeni katika somo lake bali huchukuliwa kama mshiriki – mlengwa.

### 1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo

Katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili, uendelezaji wa uwezo wa jumla kwa mwanafunzi unapewa kipaumbele sana. Uwezo huo wa jumla wa kuendelezwa ni kama vile tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti, utatuzi wa matatizo na ushirikiano. Haya yote yanafanikishwa katika ufundishaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahitaji ya mwanafunzi yametoshelezwa. Hivyo basi, wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji ushirikiano kati yao ili kukamilisha kufanya tafiti zao au kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika maisha.

Kila ujifunzaji na ufundishaji wa kila somo lililoandaliwa unazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya kimaisha kama mtu aliye na uwezo wa kushilikiana na watu mbalimbali katika miradi tofauti ya kijamii na kimaendelezo. Uwezo unaotakiwa katika kumjenga mwanfunzi utajikita katika mazeozi ya kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika kama njia muhimu za kudumisha mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

Ili kumwezesha kuwasiliana kwa usahihi na katika hali inayoweza kuyatatua matatizo yanayowakabili wanafunzi, mwalimu akumbuke kumwezesha katika kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA). Pia ufundishaji unaotarajiwa katika masomo husika ni kumwezesha mwanafunzi kupata menejimenti yake kama mtu binafsi aliye na malengo mahususi na pia katika mahusiano yake na watu wengine. Haya ni kusema kwamba mada mbalimbali zilizojadiliwa zinajenga muktadha wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kukuza na kuendeleza uwezo wa kila mwanafunzi.

Katika uendelezaji wa uwezo huu, mwanafunzi hushirikishwa katika kuyaelewa vyema maisha ya nchi na matatizo yake ya kila siku. Ndiyo sababu jambo la masuala mtambuka hutiliwa mkazo ndani ya kila somo. Ukweli ni kwamba uwezo peke yake wa mwanafunzi hauwezi kuendelezwa wakati ambapo masuala mtambuka yamewekwa pembeni. Masuala mtambuka yote manane yanayojitokeza katika mtaala wa taifa kama vile: Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari, mazingira na maendeleo ya kudumu, usawa wa kijinsia, mafunzo kuhusu ujinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili mema, mafunzo kuhusu uzalishaji mali, desturi ya usawa, mafunzo kuhusu elimu isiyo na ubaguzi. Uingizaji wa masuala mtambuka katika somo hufaulu zaidi kutokana na jinsi mazoezi ya kimajadiliano yalivyotayarishwa na mwalimu.

### 1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala mtambuka.

Katika kitabu hiki mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia maswala mtambuka yafuatayo:

- Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari/kuangamiza.
- Mazingira na maendeleo endelevu
- Usawa wa jinsia
- Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia
- Mafunzo kuhusu Amani na maadili.
- Elimu kwa wote/Elimu isiyo na ubaguzi
- Mafunzo kuhusu uzalishajimali
- Mila na desturi ya uchunguzi wa viwango

Mwalimu awasaidie wanafunzi kuingiza masuala mtambukahaya kwa kila somo wanalojifunza na kutafuta suluhisho kuhusu masuala hayo.

### 1.2.3. Uangalizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

Malengo ya ujifunzaji na ufundishaji humhusu kila mwanafunzi darasani bila ubaguzi au utengano wowote. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kuyakumbuka na kuyahudumia makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu au ya kipekee katika ujifunzaji wao.

Hao ni kama vile wanafunzi wenye tatizo la kutoona, kutosikia, kutoandika, kutosoma, kutozungumza na matatizo mengine ya kiakili. Kwa kuwashirikisha wote, mwalimu hulazimishwa kutayarisha mazoezi ya aina aina kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa zinaandaliwa na mwalimu kutokana na jinsi mahitaji maalumu ya wanafunzi darasani yalivyo.

### 1.2.4. Mwongozo wa Tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika njia hii ya ufundishaji na ujifunzaji. Lengo kuu la tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mwalimu huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake.

- **Tathmini Endelezi**

Tathmini hii hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au kama makusudi au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yamefikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu uboreshaji wa baadaye. Tathmni hii inafanywa wakati masomo yangali yanaendelea na hulenga kuangalia uhusiano uliopo kati ya ufundishaji na ujifunzaji yaani uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Hujumuisha upimaji wa mwenendo wa somo kabla somo lifikie kikomo. Tathmini endelezi inapaswa kuwa na dhima mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji. Inambidi mwalimu kuwahamasisha wanafunzi kufanya mazoezi na majaribio binafsi, mazoezi ya makundi, kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo husika.

- **Tathmini ya jumla**

Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, tathmini ya mwishoni mwa mada itafikiriwa na itafanyika mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka zitakuwa mojawapo ya tathmini za jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba walimu, viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa. Tathmni zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi zitamwelekeza mwalimu kubashiri matatizo yaliyopo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha kuwaelekeza wanafunzi kupata uwezo walio nao katika somo hili. Hivyo basi, tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni msingi wa mambo mengine ambayo mwanafunzi atayakuta katika miaka mingine ya masomo yake ya Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 1.2.5 Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu achunguze mambo yafuatayo:

- Upekee wa somo,
- Kielelezo cha somo,
- Malengo maalum ya kutimiza,
- Kuchunguza idadi ya vipindi mahususi kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya somo,

- Maelekezo muhimu kuhusu vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika mazingira halisi,
- Jinsi wanafunzi watakavyokaa darasani,
- Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu,
- Uwezo na mtindo wa ujifunzaji.

### 1.2.6. Mbinu za Ufundishaji Zinazokuza Shughuli ya Ujifunzaji Shirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mwalimu azingatie njia zifuatazo:

- **Njia Shirikishi:** Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi ambapo mwalimu huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa ya kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hali hii hutokana namazingira yanayojengwa na mwalimu ambapo kila mwanafunzi ndiye ambaye huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mwalimu kama vile majadiliano, midahalo na mazungumzo ya aina tofauti kama yalivyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Njia ya kibinafsi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi ama mazoezi yake binafsi iliaweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa. Baada ya kufanya kazi na mazoezi hayo, ni vyema mwalimu akumbuke kuambatanisha njia aliyoitumia na njia shirikishi kwa kumwomba mwanafunzi achunguze maoni na hoja za wanafunzi wenzake katika makundi yao. Katika njia ya kibinafsi, mwalimu anaweza kuomba mwanafunzi kwa mfano kujisomea kifungu cha habari, kutambua maana za maneno mapya na kuyatumia katika sentensi zake, n.k.

- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kumwuliza mwalimu wao naye akawajibu. Vilevile, maswali na majibu haya yanaweza kujitokeza kati ya wanafunzi wenyewe. Katika hali hii, mwalimu atawaelekeza wanafunzi wake kujitafutia majibu kwa maswali wanayouliza huku akiwapa maelekezo muhimu au mwongozo unaofaa kwa kusahihisha makosa wanayoyafanya.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mwalimu atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu itaegemea kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

# SEHEMU II: SAMPULI YA ANDALIO LA MASOMO

## MADA KUU YA 1 : LUGHA NA JAMII

## MADA NDOGO YA 1: LUGHA YA KISWAHILI

## ANDALIO LA SOMO

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule:…………………….** **Jina la mwalimu:……………………..**

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/3/2018 | Kiswahili | 4 | 1 | 1 kwa 7 | Dakika 80 | 45 |

**Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu pamoja na idadi yao:**

Mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika: 1

| | | |
|---|---|---|
| **Mada kuu** | LUGHA NA JAMII | |
| **Mada ndogo** | LUGHA YA KISWAHILI | |
| **Uwezo upatikanao katika mada** | Kusikiliza , kusoma, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano | |
| **Kichwa cha somo** | Sarufi : **Matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti " -nge- "** | |
| **Malengo ya kujifunza** | Kupitia mifano katika kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kutumia kiambishi chenye dhana ya masharti -nge- bila tatizo | |
| **Mahali ambapo somo litatolewa** | Darasani | |
| **Zana au vifaa** | Kitabu cha Kiswahili (Kidato cha nne, kitabu cha mwanafunzi na mwongozo wa mwalimu ), Kamusi ya Kiswahili Sanifu , ubao, chaki, n.k | |
| **Marejeo** | - Kiswahili sanifu, darasa la saba<br>- Masomo ya Kiswahili sanifu,Kitabu cha mwanafunzi, kidato cha pili. | |
| **Muda na hatua** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji** | **Uwezo wa jumla na** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Kwa kupitia kazi za kusoma kifungu, kutazama mifano, kufanya mazoezi katika makundi, wanafunzi wataelewa matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti -nge- | | **Maswala mtambuka na maelezo mafupi** |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **1. Utangulizi**<br>Dakika 7 | - Mwalimu awaamkie wanafunzi.<br>- Mwalimu awaulize maswali kuhusu somo lililopita.<br>- Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu.<br>- Mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika mwalimu amuweke katika kundi pamoja na wanafunzi wengine. | - Wanafunzi wajibu salamu za mwalimu.<br>- Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuhusu somo lililotangulia.<br>- Wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu | **Uwezo wa jumla**<br><br>**Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br>Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi, wanafunzi watumie lugha rasmi ya Kiswahili.<br>**Tafakuri tunduizi:** wanafunzi kwa kutafuta maana ya matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti -nge- watafakari kwa kuchunguza maana. |
| **2. Somo lenyewe**<br>Dakika 60 | | | |
| **2.1. Zoezi la ugunduzi** | - Mwalimu aandike sentensi zenye kiambishi chenye dhana ya masharti -nge-<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari na kuandika sentensi ambazo | - Wanafunzi wasome sentensi ubaoni.<br>- Wanafunzi katika makundi yao, waandike sentensi zote ambazo zinafanana na sentensi | **Ujifunzaji wa muda mrefu:** kwa kuelewa matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti -nge-, walitumia ujuzi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | zinafanana na sentensi ya ubaoni.<br>- Mwalimu amsogelee mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandikana kumsaidia kisha amuombe kuwakilisha kundi lake. | yaubaoni. | waliokuwa nao kuhusu nyakati.<br>. |
| **2.2.Uwasilishaji wa wanafunzi** | Mwalimu aombe wanafunzi kuwasilisha matokeo ya zoezi kwa kila kundi. | Kwa kuwasilisha, wanafunzi kutoka makundi waandike ubaoni sentensi zote walizosoma kutoka kifungu cha habari | **Masuala mtambuka**<br>❖ **Elimu isiyo na ubaguzi:** katika makundi ya wanafunzi, mwanafunzi mwenye matatizo ya kuandika asaidiwe na mfano wa sentensi unaonyesha kuwa elimu isiyo na ubaguzi inashughulikiwa |
| **2.3.Uchambuzi** | Mwalimu awaombe kuchunguza maana ya sentensi hizo.<br><br>Mwalimu atoe mfano mwingine:<br><br>-Ni**nge**kuwa na pesa ni**nge**nunua gari. | Katika makundi, wanafunzi wajaribu kueleza maana ya sentensi hizo. Kila kundi litatoa maelezo yake.<br><br>Wanafunzi katika makundi wasaidiane kutoa maana | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | -Ningekaa na mwenzangu mwenye matatizo ya kuandika, ningemsaidia ipasavyo.<br><br>Nini maana ya sentensi hii?<br><br>Nini maana ya matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti -nge-?<br><br>Mwalimu awape wanafunzi mazoezi tofauti kuhusu matumizi ya kiambishi chenye dhana ya masharti-nge-:<br>- Kutumia kiambishi chenye dhana ya masharti -nge- na kueleza maana zake<br>- Kukamilisha sentensi ili zilete maana kamili. | ✓ Mimi sina pesa wala sikununua gari. Lakini nikipata pesa sasa hivi ninaweza kuinunuwa.<br><br>✓ Mimi sikai na mwenzangu mwenye matatizo ya kuandika. Lakini tukikaa pamoja ninaweza kumsaidia<br><br>Katika makundi watatoa maelezo<br><br>Wanafunzi katika makundi yao wafanye mazoezi waliyopewa. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mwalimu awaombe wanafunzi kuwasilisha kazi zao. Na kuwasaidia kutoa majibu sahihi. | Wanafunzi katika makundi yao, wawasilishe matokeo yao. | |
| **2.4. itimisho** | - Mwalimu awaombe wanafunzi kutoa muhtasari wa somo .<br><br>Mwalimu naye atoe muhtasari. | - Wanafunzi watoe muhtasari wa somo kulingana na maelezo waliopewa. | |
| **3. Tathmini** Dakika 13 | - Mwalimu atoe jaribio dogo.<br><br>- Mwalimu awaongoze wanafunzi kusahihisha jaribio.<br><br>- Mwalimu atoe kazi ya nyumbani. | - Wanafunzi binafsi wafanye jaribio katika madaftari yao.<br><br>- Wanafunzi wajaribu kusahihisha jaribio<br><br>- Wanafunzi waandike kazi ya nyumbani. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Baada ya somo mwalimu ahakikishe kwamba lengo la ufundishaji na ujifunzaji limefikiwa au la. | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule: ....................................Jina la Mwalimu: ....................................**

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 28/2/2018 | Kiswahili | 4 | 2 | Masomo 6 | Dakika 80 | 42 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao** | Hakuna |
| **Mada** | Lugha katika sanaa. |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kuelewa fasihi katika Kiswahili kwa ujumla kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano ndani yake; kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia majina ya ngeli ya LI-YA kwa ufasaha |
| **Somo lenyewe** | Kusoma na kufahamu kifungu cha habari "Asili ya Kiswahili." |
| **Malengo ya kujifunza** | Baada ya kusoma na kufahamu kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kusema, kueleza na kujivunia kwa makini asili ya Kiswahili. |
| **Mahali somo litakapofundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, kitabu cha mwalimu, ubao, chaki, madaftari, kalamu, redio. |
| **Vitabu vya rejea** | Kitabu cha mwanafunzi kidato cha nne, Mwongozo wa mwalimu |

| **Muda na hatua** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | | **Uwezo wa jumla na masuala mtambuka vielezewe+maelezo mafupi** |
|---|---|---|---|
| | **Kazi katika makundi:** Mara nyingi wanafunzi watafanyia kazi yao katika makundi kwa kushirikiana ili wafanikiwe na mambo kadhaa.<br>**Kazi ya kibinafsi:** Wanafunzi watapata muda mfupi wa kufanya kazi ya kipekee. | | |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Utangulizi** Dakika 5 | Mwalimu achangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali mawili kuhusu somo lililopita, na maswali mengine kuhusu mchoro unaotangulia kifungu cha habari. Mwalimu akiuliza, achague wanafunzi wa kujibu kwa kuchanganya wavulana na wasichana. | Wanafunzi watajibu maswali yote yaliyoulizwa na mwalimu | **Uwezo wa jumla:** Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na mawasiliano katika lugha rasmi.<br><br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia. |
| **Somo lenyewe** Dakika 62 | - Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne ya wavulana kwa wasichana. Baadaye, awape vitabu vya wanafunzi na awaombe kusoma kimya kifungu cha habari cha "Asili ya Kiswahili." Awaombe kutumia dakika kumi.<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma tena kifungu cha habari na kujibu maswali ya ufahamu katika dakika kumi.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kutafuta maneno magumu katika kifungu cha habari katika dakika zingine kumi na kutumia kamusi kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kumwambia maneno ambayo wameshindwa kuyafafanua.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi mwongozo wa kusoma kifungu cha habari katika dakika kumi. | - Wanafunzi wakae katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kusoma kifungu walichopewa kwa kutumia muda maalum.<br><br>- Wanafunzi wasome tena kifungu cha habari na wajibu maswali ya ufahamu.<br><br>- Wanafunzi watafute maneno magumu na kuyaandika mahali fulani, kisha wayafafanue kwa kutumia kamusi.<br><br>- Wanafunzi wamwambie mwalimu maneno yanayowashinda na kujaribu kuyafafanua pamoja na mwalimu.<br>-Wanafunzi wasikilize kwa makini namna mwalimu anavyosoma na waige mwenendo na | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi. Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha. Mawasiliano katika lugha rasmi. Utafiti: Kwa kujibu maswali ndani ya makundi, wanafunzi watafanya utafiti, watashirikiana kupata majibu, na kuchagua viongozi wa makundi hivi wakiwasiliana katika lugha rasmi.<br><br>**Masuala mtambuka:** Usawa wa kijinsia: Wanafunzi wafanye kazi pamoja; wasichana na wavulana na wapewe fursa sawa.<br><br>Mafunzo kuhusu amani na maadili: Kwa kufanyia kazi katika makundi, |

-

| | | | |
|---|---|---|---|
| | - Mwalimu awape wanafunzi muda wa kusoma kwa sauti kubwa hivi akiwasahihisha katika dakika kumi na mbili.<br><br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kujichagulia wasimamizi wa kuandika majibu ya maswali ya ufahamu kwenye ubao kundi kwa kundi. Mwalimu awaongoze wanafunzi ili majibu yanayofanana yasiandikwe mara mbili kwa kutumia muda vizuri. Dakika kumi na tano zitumiwe hapa. Mwalimu asahihishe majibu ya wanafunzi itakiwavyo. | lafudhi nzuri.<br>- Wanafunzi wasome mmoja baada ya mwingine kwa kubadilisha makundi.<br><br>- Wanafunzi waandike matokeo ya makundi yao yenye kujibu maswali ya ufahamu wa kifungu cha habari kundi baada ya kundi jingine, mvulana na msichana kimpango. Wamfuate mwalimu iwapo kuna majibu ambayo yanahitaji masahihisho yake. | wanafunzi wajadiliane hivi wakitoa na kupokea fikra tofauti kwa amani. |
| **Hitimisho**<br>Dakika 13 | - Mwalimu awape wanafunzi maelezo muhimu kimuhtasari katika dakika tatu.<br><br>- Mwalimu awape wanafunzi maswali matano ya tathmini la somo. Awape dakika kumi za kuyafanya. | - Wanafunzi wamfuate mwalimu vizuri mwalimu katika kutoa maelezo.<br><br>- Wanafunzi wajibu maswali hayo kwenye karatasi na kumpa mwalimu karatasi hizo ili azisahihishe. | **Uwezo wa jumla:** Tafakuri tunduizi na stadi ya utatuzi wa matatizo: wanafunzi wafikirie kwa upana na kujibu maswali wenyewe. |
| **Tathmini ya mwalimu** | | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule:………………….** **Jina la mwalimu:…………………..**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/3/2018 | Kiswahili | 4 | 2 | 5 kwa 6 | Dakika 80 | 45 |

| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na idadi yao:** Mwanafunzi mwenye matatito ya kutoona vizuri: 1 | | |
|---|---|---|
| **Mada kuu** | LUGHA KATIKA SANAA | |
| **Mada ndogo** | FASIHI KATIKA KISWAHILI | |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | - Kuelewa fasihi katika Kiswahili kwa ujumla kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano ndani yake.<br>- Kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya LI-YA. | |
| **Kichwa cha somo** | Methali | |
| **Malengo ya kujifunza** | Kulingana na kifungu cha habari kilichochambuliwa hapo kabla, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kueleza na kuzitumia methali kwa ufasaha katika mazungumzo yao. | |
| **Mahali ambapo somo litatolewa** | Darasani | |
| **Zana au vifaa** | Kitabu cha Kiswahili (Kidato cha nne, kitabu cha mwanafunzi na mwongozo wa mwalimu ), Kamusi ya Kiswahili Sanifu , ubao, chaki, michoro. | |
| **Marejeo** | - Kitabu cha Kiswahili, MINEDUC, Kigali (2018)<br>- Kunga za Kiswahili, Paul Masau, Nairobi (1999)<br>- Kamusi ya Kiswahili Sanifu, TUKI, Dar-es-Salaam (2013) | |
| **Muda na hatua** | **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji** | **Uwezo wa jumla** |
| | Kazi katika makundi: wanafunzi watajadiliana | **Maswala mtambuka** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kuhusu msamiati, maana za methali na utumiaji wa methali. | | **Vielezewe+maelezo mafupi** |
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **4. Utangulizi**<br>Dakika 10 | - Mwalimu awaamkie wanafuzi.<br>- Mwalimu awaulize maswali kuhusu somo lililopita.<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kuunda makundi ya watu watano watano.<br>- Kwa kumhusisha katika somo mwanafunzi yule aliye na matatizo ya kutoona vizuri, mwalimu ampe nafasi karibu na ubao. | - Wanafunzi wajibu salamu za mwalimu.<br>- Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuhusu somo lililotangulia. | **Uwezo wa jumla**<br><br>**Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br>Kupitianjia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi.<br><br>**Mawasiliano katika lugha.**<br>Katika makundi, wanafunzi watumie lughakwa njia ya kujibu maswali ya mwalimu na kuwasiliana kati yao.<br><br>**Maswala mtambuka**<br>❖ **Elimu isiyo na ubaguzi:** katika makundi wanafunzi washirikiane na mwenzao ambaye ni mwenye ulemavu wa kutoona vizuri. Wat |
| **5. Somo lenyewe**<br>Dakika 60 | | | |
| **5.1. Zoezi la ugunduzi**<br><br>**5.2. Uwasilishaji wa** | - Mwalimu atoe sentensi moja kutoka kifungu cha habari na aombe mwanafunzi mmoja kuandika sentensi hiyo ubaoni.<br>- Mwalimu awaombe wanafunzi kueleza maana ya sentensi hiyo. | - Mwanafunzi aandike sentensi ubaoni.<br>- Wanafunzi katika makundi yao wajaribu kueleza maana ya sentensi iliyoko ubaoni. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **wanafunzi** | Mwalimu aombe wanafunzi kuwasilisha matokeo ya zoezi kundi kwa kundi. | Wanafunzi wawasilishe maana ya sentensi kundi kwa kundi. | mifano ya methali isiyo na ubaguzi wowote.<br>❖ **Usawa wa jinsia**: kwa kuunda makundi yao wanafunzi wafuate utaratibu unaozingatia usawa wa jinsia na methali watakazotoa haziwe zikiegemea jinsia fulani.<br>❖ **Amani na maadili:** katika makundi yao wanafunzi wafafanue na kutoa mifano ya methali zinazozingatia amani na maadili. |
| **5.3.Uchambuzi** | Mwalimu awaelezee wanafunzi maana za sentensi hizo.<br>Mwalimu awaombe kufungua vitabu vyao kwenye ukurasa husika na kusoma kwa kimya kifungu cha habari huku wakitafuta sentensi zenye mafumbo zilizotumiwa katika kifungu cha habari.<br>Mwalimu aombe wanafunzi kujadiliana kuhusu methali hizo.<br>Mwalimu awombe wanafunzi kuwasilisha maana za methali walizopata kutoka kifungu cha habari.<br>Mwalimu aongoze | Katika makundi, wanafunzi wasome kifungu cha habari na kutafuta methali zilizotumiwa katika kifungu hicho.<br>Wanafunzi wajadiliane kuhusu methali hizo.<br>Wanafunzi katika makundi yao, wawasilishe matokeo ya majadiliano kwa sauti ili kumshirikisha mwenzao asiyeona vizuri.<br>Wanafunzi katika makundi | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wanafunzi kuonyesha muundo wa methali huku akiwapa maelezo yanayohitajika.<br><br>Mwalimu aongoze wanafunzi kuhusisha methali na maelezo anayowapatia. | yao wajaribu kuonyesha miundo ya methali.<br><br>Wanafunzi, katika makundi yao wajaribu kuhusisha methali na maelezo waliyopewa. | |
| **5.4. itimisho** | - Mwalimu awaombe wanafunzi kutoa muhtasari wa somo . | - Wanafunzi watoe muhtasari wa somo kulingana na maelezo waliyopewa. | |
| **6. Tathmini** Dakika 10 | - Mwalimu atoe jaribio dogo.<br><br>- Mwalimu awongoze wanafunzi kusahihisha jaribio.<br><br>- Mwalimu atoe kazi ya nyumbani. | - Wanafunzi binafsi wafanye jaribio katika madaftari yao.<br><br>- Wanafunzi wajaribu kusahihisha jaribio.<br><br>- Wanafunzi waandike kazi ya nyumbani. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Baada ya somo mwalimu atahakikisha kwamba lengo la ufundishaji na ujifunzaji limefikiwa au la. | | |

**ANDALIO LA SOMO**

**Jina la shule: ………………………  Jina la Mwalimu: ………………………………**

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Wa kwanza | | Kiswahili | Cha nne | Ya pili | 3/7 | Dakika 40 | 45 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao** | Matatizo ya kutosikia vizuri: 1 |
| **Mada** | Lugha na jamii |
| **Uwezo unaopatikana katika mada** | Kusikiliza, kusoma, kuzungumza na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha na umuhimu wake kama chombo cha mawasiliano katika jamii. |
| **Kichwa cha somo** | Msamiati kuhusu "Lugha katika jamii." |
| **Malengo ya kujifunza** | Kulingana na msamiati uliopendekezwa kutokana na kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kutumia kwa usahihi msamiati huo kakika mawasiliano yanayohusu shughuli mbalimbali zinazotendeka katika jamii. |
| **Mahali ambapo somo litafundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu, daftari, chaki, kalamu. |
| **Vitabu vya rejea** | Kamusi ya Kiswahili sanifu,Toleo la pili, Oxford University press, Dar-es-Salaam (2004), Mpangilio wa masomo, Muhtasari wa somo. |

| **Muda na hatua za somo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia** | **Uwezo wa jumla na**<br>**Maswala mtambuka**<br>**Vielezwe+maelezo** |
|---|---|---|
| | Katika makundi, wanafunzi wajadiliane kuhusu msamiati husika kabla ya kuchunguza maana yake kutoka kamusi ya Kiswahili sanifu. | |

| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | **mafupi** |
|---|---|---|---|
| **1. Utangulizi**<br>Dakika 5 | Mwalimu aanze kwa kuamkia wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki katikasomo.<br><br>Mwalimu aulize wananafunzi mmoja kwa mmmoja maswali kuhusu ufahamu wa kifungu cha habari walichosoma katika somo lililotangulia na kuhakikisha kwamba wanakumbuka maelezo yaliyotolewa.<br><br>Mwalimu aulize wanafunzi ikiwa wameelewa msamiati wote uliotumiwa katika kifungu cha habari.<br><br>Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne. Kwa kumhusisha yule mwanafunzi aliye na matatizo ya kutosikia vizuri, mwalimu analazimika kusema kwa sauti na kuomba wanafunzi wafanye vivyo hivyo. | Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuhusu kifungu cha habari walichosoma katika somo lililotangulia. | **Uwezo wa jumla**<br><br>**Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br><br>Kupitia njia ya kujadiliana na kujibu maswali ya mwalimu katika makundi.<br><br>**Mawasiliano katika lugha.**<br><br>Katika makundi, wanafunzi watumie lughakwa njia ya kujibu maswali ya mwalimu na kuwasiliana kati yao. |
| **2. SOMO LENYEWE**<br>Dakika 30 | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| **2.1. Zoezi la ugunduzi** | Mwalimu awaombe wanafunzi wafungue vitabu vya Kiswahili kwenye ukurasa husika na kusoma kwa kimya aya moja moja za kifungu cha habari huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. | Wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa kimya na kisha waandike msamiati mpya katika madaftari yao. | **Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha.**<br>Wanafunzi washirikiane katika makundi yao na ku<br>waheshimu haki na maoni ya wenzao.<br>**Maswala mtambuka**<br>**Usawa wa jinsia**<br>Wavulana na wasichana wafanye kazi pamoja katika makundi yao bila ubaguzi wowote.<br>**Malezi yasiyokuwa na ubaguziwowote.**<br>Wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama kutosikia vizuri wasaidiwe kushiriki katika somo. |
| **2.2. Uwasilishaji wa wanafunzi** | Mwalimu awaombe wanafunzi kuandika maneno mapya waliyokutana nayo kwenye ubao huku akiwaongoza kusoma maneno hayo kwa usahihi. | Wanafunzi kutoka makundi yao waandike msamiati mpya kwenye ubao na wausome kwa usahihi. | |
| **2.3. Uchambuzi** | Mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu maneno hayo na wajaribu kuyafafanua katika makundi yao.<br>Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao wafanye zoezi la kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi kwa kutumia msamiati waliouandika kwenye ubao kuhusu kifungu | Wanafunzi wajaribu kutoa maana za msamiati mpya kulingana na matumizi yake katika kifungu cha habari.<br>Katika makundi yao, wanafunzi wafanye zoezi la kujaza mapego wakitumia msamiati waliopewa. | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | cha habari.<br><br>Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze wasahihishekwenye ubao. | Wanafunzi washiriki katika usahihishaji wa zoezi kwenye ubao. | |
| **2.4. Hitimi sho/ Ufupisho** | Mwalimu aandike ufupisho wa somo ubaoni na aombe wanafunzi kuandika ufupisho huo katika madaftari yao. | Wanafunzi waandike ufupisho wa somo katika madaftari yao. | |
| **3. Tathmini** Dakika 5 | Mwalimu aandike misamiati mitano miongoni mwa misamiati iliyoelezewa, kisha aombe wanafunzi kila mmoja kwabinafsi kutunga sentensi tano wakitumia msamiati waliopewa. | Wanafunzi watunge sentensi haraka haraka na kutoa majibu yao kwa njia ya matamshi. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Baada ya somo, mwalimu ahakikishe ikiwa lengo la ufundishaji limefikiwa au la. | | |

# SEHEMU III: UUNDAJI WA MADA

# MADA KUU YA 1: LUGHA NA JAMII

1

## MADA NDOGO YA 1: LUGHA YA KISWAHILI

### 1.1 Uwezo Upatikanao katika Mada:

Kusikiliza, kusoma, kuzungumza, na kuandika kwa minajili ya kuelewa lugha kama-chombo cha mawasiliano katika jamii.

### 1.2 Ujuzi wa Awali

Katika shule za awamu ya kwanza (kidato cha 1, 2, na 3), wanafunzi walisoma masomo ambayo yanahusu kidogo madahii na yanaweza kumsaidia kuelewa "lugha ya Kiswahili": Masomo hayo ni:

- Uimarishaji wa stadi ya uandishi na masimulizi kupitia lugha ya Kiswahili: Utungaji wa insha. ( mada ya nne, kidato cha tatu)
- Lugha na teknolojia : Kiswahili katika teknolojia ya habari na mawasiliano. (mada ya tano, kidato cha tatu)
- Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimzungumzo. ( mada ya tatu, kidato cha tatu.)
- Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (kidato cha pili)

### 1.3 Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada.

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha na katika mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu atawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

**Mafunzo kuhusu uzalishajimali**

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, utumiaji wa msamiati, katika sentensi; mwalimu atawaongoza wanafunzi

a. Kwa kutumia lugha ya Kiswahili, Mnyarwanda anaweza kusafiri katikanchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kufanya biashara na raia tofauti kwa kuwasiliana katika lugha ya Kiswahili bila tatizo.

b. Kama unafanya biashara, ukipata mteja mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili ambayo unaifahamu vizuri. Mtajadiliana bei bila tatizo na utafaidika.

c. Mnyarwanda mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili, anaweza kutumia lugha ya Kiswahili kama njia moja ya kujitajirisha. Kama vile kuwa mkalimani, mfasiri, n.k

**Mafunzo kuhusu amani na maendeleo.**

Lugha ni chombo cha mawasiliano. Watu wakitumia lugha moja wanaweza kuelewana katika maisha yao ya kila siku na kutumia lugha hiyo kwa kutatua baadhi ya matatizo ya kutoelewana ili waishi kwa amani.

**Mila na desturi ya uchunguzi wa viwango**

Kwa kununua bidhaa tofauti katika maisha ya binadamu ya kila siku, ni lazima kuwa na tabia ya kuchunguza kwenye bidhaa husika tarehe ya mwisho kutumika. Mtu hawezi kusoma maelekezo katika lugha bila kuelewa lugha hiyo. Kwa mfano kwenye bidhaa kunaandikwa maelekezo katika lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo ni lazima kuelewa lugha hiyo.

Kwa kufanya kazi yoyote, kuwa na tabia ya kuheshimu na kutimiza majukumu ya kazi yote uliyopewa.

**Elimu Jumuishi**

Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile: Wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu /ulemavu wa mwili, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza, n.k.

Mwalimu anapaswa kukumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima mwalimu awasaidie ipasavyo. Kama vile:

- Kuwaambia wale wenye tatizo la kutoona au kutosikia vizuri wakae kwenye madawati yaliyoko sehemu za mbele karibu na mwalimu.

- Kuzingatia matatizo ya kila mwanafunzi, kumtega sikio na kuelewa mahitaji yake

- Kupanga kazi maalum zilizoandikwa kwenye karatasi kwa wanafunzi wenye matatizo ya kusikia.

- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kuongea na kuwasiliana na wengine, kupewa muda wa kuongea.

- Kuunda makundi ya wanafunzi kutokana na ujuzi na uwezo wao katika kujifunza;

- Kupanga kazi au mazoezi kutokana na makundi ya wanafunzi wenye matatizo maalum ya kielimu.

- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kimwenendo na kuwachunga ipasavyo;

- Kuwasiliana na wazazi wa wanafunzi wenye matatizo maalumu ili kusaidiana katika kupata suluhisho kwa matatizo yao.

- Kushirikiana na viongozi wa shule na wazazi katika kuweka mikakati thabiti ili lugha ya kufundishia isije ikawa kizuizi kwa masomo yao;

- Kutowasimanga na kutowakashifu wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama vile wale wanaotoka katika familia fukara, wale wenye matatizo ya kielimu, wale wasiosema vizuri na kadhalika.

- Kuwa mwenye wingi wa huruma na kujua kwamba ulemavu wao au matatizo yao yanajitokeza kwa ghafla na hayatokani na utashi wao au matendo yao.n.k.

**Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia**

Katika vifungu au katika mifano ya sentensi, mwalimu kwa kutumia lugha atawasaidia wanafunzi kuelewa matumizi ya kondomu na sababu za kuitumia kama kujikinga ukimwi na kuzaa watoto ambao utakidhi mahitaji yao.

**Mazingira na maendeleo endelevu**

Mwalimu kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

**Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari/kuangamiza.**

## 1.4 Mwongozo kuhusu Kidokezo cha Mada

- Mwalimu atoe mwongozo wa kutoa jibu kwa kazi.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia kazi zingine zilizotayarishwa au masomo ya mada yote.

## 1.5 Orodha ya Masomo

| | **Kichwa cha somo** | **Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema)** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|
| 1 | Maana ya lugha | **Maarifa na ufahamu:** kufafanua maana ya lugha kama chombo cha mawasilino.<br><br>**Stadi :** Kuonesha kimazungumzo na kimaandishi maana ya lugha.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujivunia lugha | 7 |
| 2 | Umuhimu wa lugha | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza umuhimu wa lugha katika jamii<br><br>**Stadi** : Kuonesha matumizi ya lugha<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kutumia vizuri lugha | 7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Lugha katika jamii | **Maarifa na ufahamu:** kueleza umuhimu wa lugha katika jamii<br><br>**Stadi**: Kutumia lugha katika jamii<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: | 6 |
| 4 | Faida na hasara ya kutumia lugha moja | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza faida na hasara ya kutumia lugha moja<br><br>**Stadi :** Kutumia lugha katika jamii<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kutumia lugha kama njia moja ya kuboresha mawasiliano kati ya watu. | 6 |
| 5 | Asili ya lugha ya Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza chimbuko la lugha ya Kiswahili.<br><br>**Stadi**: Kuonesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili toka pwani<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kujivunia Kiswaili kama lugha yenye asili ya kiafrika**.** | 8 |
| 6 | Kuenea kwa Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:**Kueleza jinsi lugha ya Kiswahili ilivyoenea<br><br>**Stadi :** Kuonesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili toka pwani<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:**Kujivunia Kiswahili kama lugha yenye asili y kiafrika | 8 |
| 7 | Kiswahili nchini Rwanda. | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza historia ya Kiswahili nchini Rwanda.<br><br>**Stadi:** Kuonesha njia ya ueneaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda | 7 |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | **51** |

## SOMO LA 1: MAANA YA LUGHA

### 1.1 Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu dhana ya lugha. Mwalimu aanze somo na maamkizi kwani mamkizi ndiyo ufunguo wa mawasiliano katika jamii yoyote. Wanafunzi wajibu maamkizi husika kisha mwalimu awaulize wanafunzi wanachojua kuhusu mawasiliano kati ya watu wanaokutana njiani. Anaweza kuwauliza maswali yafuatayo:

- Katika familia zenu mnapotaka kuomba vifaa mnavyotumia darasani mnatumia nini?
- Mnapotaka kusema kitu kuhusu hisia zenu mnatumia nini?
- Lugha ni nini?
- Tajeni lugha mnazojua zinazotumiwa na binadamu kueleza hisia zao.

### 1.2 Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Ubao, chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana, n.k.

Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwa wale wanafunzi ambao wana ulemavu Fulani. Hapa Mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji.

### 1.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili, watatu, wanne. Ni vyema mwalimu asizidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana.

  **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi vya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

## 1.4 Majibu

***Zoezi la kwanza: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame michoro kwenye ukurasa husika kisha watoe maoni yao kuhusu nafasi ya lugha katika jamii.*

### 1.4.1 Zoezi la Ufahamu

1. Wanaozungumziwa katika kifungu cha habari ni Mzee Gakuba, mke wake na watoto Kagabo na Mutesi.
2. Mzee Gakuba alizitembelea nchi kama Kenya, Tanzania na hata Uganda
3. Aliweza kubahatika sana na kufanikisha shughuli zake nyingi katika mataifa yote aliyotembelea kama vile kufanya biashara mbalimbali na kujenga urafiki na wafanyabiashara wengine wengi kutoka mataifa hayo.
4. Alikuwa katika kidato cha nne katika shule ya Sekondari ya Mugari.
5. Mzee Gakuba alikuwa anatumia lugha ya Kiswahili.
6. Mzee Gakuba alimpongeza Simoni mtoto wake kutokana na swali alilouliza kuhusu kutoelewana kwa watu wasemao lugha fulani kufika kwake kwenye kiwango hiki cha kutaka kujua mengi zaidi ya yaliyosemwa na watu.
7. Watu wanaweza kutoelewana, wakati watu hao wanaowasiliana hawaelewani juu ya lugha wanayoitumia, wanatumia lugha mbili tofauti.
8. Mama alisema kwamba maana ya lugha ni pana sana na hugusia kila sehemu ya maisha ya binadamu."
9. Lugha ni chombo muhimu sana kinachotumiwa na binadamu wakati wanapotaka kuwasiliana kati yao na kuelewana. Lugha kama chombo cha mawasiliano humsaidia binadamu kueleza hisia zake, mawazo, na jinzi anavyoiona dunia na mazingira yake.
10. Ufupisho: Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufupisha kifungu cha habari.

***Zoezi la 2: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika utungaji wa sentensi wanazounda kwa kutumia msamiati waliopewa. Mwalimu achunguze kwamba wanafunzi wanatumia msamiati huo kwa njia mwafaka.

### 1.4.2. Matumizi ya Msamiati

***Zoezi la tatu: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kutumia mshale na kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.

**Majibu:**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Utamaduni | Jumla yote ya namna watu wanavyoishi |
| 2. Kusimulia | Kutoa maelezo |
| 3. Shughuli | Kazi |
| 4. Kitindamimba | Mtoto wa mwisho kuzaliwa |
| 5. Bara | Pande kubwa la nchi kavu la dunia lenye jumla ya nchi kadhaa na kuzungukwa na maji |
| 6. Mwananchi | Mwenyeji wa nchi |
| 7. Kuunganisha | Kushikanisha pamoja |
| 8. Busara | Kufanya uamuzi wa mambo yanayofaa |
| 9. Maoni | Mtazamo wa mtu juu ya jambo fulani |
| 10. Kuridhika | Kutosheka na hali ilivyo au kukubaliana na jambo |
| 11. Lengo | Shabaha |
| 12. Kujivuna | Kuringa |
| 13. Kushukuru | Kupongeza |

### 1.4.3. Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti –nge-

***Zoezi la 4: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili,wanafunzi wajadili kuhusu maana ya sentensi yenye kiambishi -**nge-***

*Mwalimu awaombe wanafunzi kuunda sentensi zenye dhana ya masharti kwa kutumia kiambishi -**nge**-, halafu watunge sentensi tano zenye kiambishi hicho.*

***Hii ni mifano ya sentensi hizo:***

1. Tu**nge**kuwa na muda wa kutosha, tungezungumzia mengine mengi kuhusu lugha.”
1. Watoto wale wa**nge**jifunza, vizuri wangepewa zawadi nyingi”
2. Angejua Kiswahili, angeajiriwa.
3. Tungeamka mapema, tungemuona kiongozi.
4. Wangezingatia mawaidha ya mwalimu, wangeepuka adhabu waliyopewa.

***Zoezi la tano: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu**

1. Wa**nge**jua nia yangu katika kutetea haki za wanawake,wasingepuuzia maoni niliyotoa.
2. U**nge**onana na daktari, ungeshauriwa kutotumia madawa ya kulevya.
3. Vijana wa**nge**upiga marufuku uasherati, bila shaka wangeepukana na maradhi ya ukimwi.
4. Barabara zote zi**nge**kuwa za lami, kila eneo nchini Rwanda lingekuwa na wasafiri wengi.
5. Wanafunzi wa**nge**elewa somo vizuri, wangefaulu mitihani yao.
6. Wazazi wa**nge**zingatia ushauri kutoka kwa walimu wa watoto wao, wangewasaidia watoto wao katika masomo yao.
7. Wa**nge**jua kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano, wangetafuta mbinu za kujifunza lugha nyingi.
8. Wangejua kwamba Kiswahili ni lugha iliyovuka mipaka, wa**ngeki**teua Kiswahili kuwa lugha rasmi nchini mwao.
9. Wa**nge**chezea kiwanjani kwao, wangefunga magoli mengi.
10. Wa**nge**jua kuwa Kamali amekwishatoka hospitalini, wa**nge**mjulisha habari za harusi za dada Rehema.

**Zoezi la sita**

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, watunge sentensi tano kwa kutumia kiambishi-nge- cha masharti; kisha waeleze maana za sentensi hizo.*

### 1.4.4. Matumizi ya Lugha: Mazoezi ya Makundi

***Zoezila saba: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, wapange maneno kwa utaratibu unaofaa ili yaweze kuleta maana katika sentensi kamili. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.*

1. Kitabu cha lugha ambacho baba yetu alitununulia kimefurahisha watoto wote.
2. Baba yangu alipokea ujumbe kutoka kwa shangazi ambaye anaishi Kenya lakini hakuweza kumjibu.

**Zoezi la nane:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu;**

*Kamilisha sentensi hizi kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo: alipuliza, rais, anafinyanga, rubani, ukaanza, nahodha, anacheza, anazungumza, anabweka, ananguruma, alitaga.*

1. Refarii**alipuliza** filimbi, mchezo **ukaanza**

2. Mwanamziki huyu **anapiga** ngoma vizuri sana.
3. Mtoto wangu **anazungumza** vizuri lugha ya Kiswahili.
4. Mbwa **anabweka** nje ya nyumba yangu.
5. Kuku wetu **alitaga** mayai mengi sana.
6. Simba **ananguruma** huku msituni.
7. Baba yake **anafinyanga** vyungu vizuri sana
8. **Nahodha** huyu ni bingwa wa kuendesha meli.
9. **Rais** wetu anaongoza nchi vizuri sana.
10. **Rubani** yule anaendesha ndege za Rwandair.

### 1.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

***Zoezi la tisa: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu aombe wanafunzi kufanya makundi ya wanafunzi wawili wawili, wajadili kuhusu **"Nafasi ya lugha katika mawasiliano"** akitilia mkazo kwenye jinsi lugha inavyowaelimisha watu. Kisha wanafunzi wawasilishe mbele ya wenzao. Mwalimu ahakikishe kila mwanafunzi anaweza kuziandika hoja zilizowasilishwa na wenzake. Zaidi ya hayo aoneshe hoja anazokubaliana nazo na zile asizokubaliana nazo.

### 1.4.6 Kuandika:

***Zoezi la kumi: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge kifungu cha habari kuhusu mada: "***Lugha ni chombo cha mawasiliano"*** wakizingatia matumizi ya kiambishi **"-nge-"**. Hapa, mwalimu awaombe wanafunzi kuelekeza fikra zao kwenye matumizi ya lugha katika shughuli za kibiashara.

## SOMO LA 2: UMUHIMU WA LUGHA

### 2.1 Ujuzi wa awali

Mwalimu aulize wanafunzi mmoja kwa mmoja maswali tofauti kuhusu somo lililotangulia kwa kuchunguza ikiwa wanakumbuka maana ya lugha. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu awaambie wanafunzi kuchukua vitabu vya Kiswahili na kutazama mchoro kwenye ukurasa……. Kisha awaulize wanafunzi maswali kuhusu mchoro walioutazama. Mwalimu anaweza kuwauliza maswali yafuatayo:

- Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.
- Tukio hili linatukia wapi?
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye mchoro?
- Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?

- Kuna uhusiano wowote kati ya kichwa cha habari na mchoro?

Kutokana na maswali yaliyoulizwa na majibu yaliyotolewa, mwalimu aombe wanafunzi wajaribu kufumbua somo linahusu nini.

## 2.2 Zana au vifaa vya kujifunzia

- Mchoro wa watu wanaozungumza
- Kitabu cha mwanafunzi, kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Magazeti, ubao, chaki, kalamu na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu wanafunzi wanaohitaji msaada maalum.

## 2.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Mwalimu aandike kichwa cha somo ubaoni, pamoja na malengo mahususi ya somo husika. Baada ya kuunda makundi ya wanafunzi kulingana na idadi ya vitabu vilivyoko, mwalimu awaombe wanafunzi wafungue kwenye ukurasa husika na kusoma kimya kifungu cha habari kuhusu umuhimu wa kujua lugha huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao.

Hatimaye mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kimya na kuelewa, mwalimu awaombe wanafunzi mmoja baada ya mwingine kusoma kwa sauti inayosikika kifungu kilichopo. Mwalimu aongoze wanafunzi kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo. Halafu mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao wafanye mazoezi yapatikanayo katika kitabu cha mwanafunzi ukurasa husika na mwalimu atoe msaada kunapohitajika. Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha kwenye ubao.

## 2.4 Majibu

***Zoezi la kwanza: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi watatu, watazame michoro kwenye ukurasa husika. Watoe maoni yao kuhusu wanachokiona kwenye picha pamoja na kueleza picha hizo zinazungumzia nini. Wanafunzi wajadili kuhusu majibu ya kila mwanafunzi. Mwalimu awaelekeze kuhusu umuhimu wa lugha kutokana na majibu wanayoyatoa.

### 2.4.1. Maswali ya Ufahamu

Majibu kuhusu ufahamu

1. Watu wanaozungumziwa katika kifungu hiki ni mzee Yakobo, Petero, Maria, Bi Hassani na Musoni
2. Mzee Yakobo alikuwa anawahimiza watoto wake kujifunza lugha mbalimbali

kwa madhumuni ya maisha yao ya usoni.

3. Maria amepewa kazi katika kitengo cha utalii katika Taasisi inayoshughulikia maswala ya utalii na mazingira.
4. Yakobo aliamua kwenda kumtembelea dada yake aliyeishi katika nchi jirani.
5. Petero alilipa shilingi zaidi kwa mkate mmoja na hata hivyo akapewa mkate uliopitisha tareha ya kuula.
6. Hassani ameonyesha tabia mbaya dhidi ya mteja wake kwa kumtoza shilingi nyingi kwenye mkate mmoja na kuuza kimakusudi chakula kibovu.
7. Petero angekula chakula hicho kingeweza kuharibu afya yake.
8. Petero alijuta akisema "Nisingepuuza mawaidha ya baba yangu, nisingekutana na matatizo haya". Alijuta kwa sababu hakueza kuwasiliana na mfanyabiashara kwa hiyo akapoteza shilingi zake bure.
9. Aliporudi nchini Rwanda alianza kujifunza Kiswahili kwa bidii.
10. Kutokana na kifungu cha habari nimejifunza kuwa ujuzi wa lugha zaidi ya moja ni muhimu sana kwa kila mtu hivyo ni lazima tujifunze lugha mbalimbali.

### 2.4.2. Msamiati kuhusu Umuhimu wa Lugha

***Zoezi la pili: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanaandika sentensi sahihi wakitumia maneno waliyopewa na awaelekeze panapohitajikwa. Hii ni mifano ya sententensi ya maneno husika:

1. Mwalimu **huwahimiza** wanafunzi kujifunza kwa bidii masomo yote.
2. Alianzisha shule kwa **madhumuni** ya kusaidia watoto wenye ulemavu.
3. Ni vizuri kusikiliza **mawaidha** tunayopewa na viongozi wetu.
4. **Mtazamo** wangu kuhusu jambo hilo ni tofauti na mitazamo yenu.
5. Mtoto huyu ni **mtukutu**, hasikii mawaidha ya babaye.
6. **Utalii** unaleta wageni wengi nchini Rwanda
7. Mwanafunzi ameomba mwalimu ruhusa ya **kwenda haja.**
8. Amepokea habari hiyo **kwa shingo upande**
9. Alishinda mtihani wa Taifa baada ya kusoma masomo yote kwa **bidii.**
10. Alishikwa na **bumbuazi** aliposikia habari hiyo na akakosa la kufanya

***Zoezi la tatu: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Inayoshughulikia | Iliyo na harakati za kutekeleza jambo fulani |
| 2. | Mtazamo | Namna ya kuangalia au kutazama kitu au mtu |
| 3. | Madhumuni | Sababu ya kufanya jambo; kusudi; nia; lengo |
| 4. | Alijitihadi | Alifanya jambo kwa bidii |
| 5. | Aliyazingatia | Aliyatia moyoni na kuyafikiria |
| 6. | Wasafiri | Watu wanaokwenda au walio katika safari |
| 7. | Bumbuazi | Hali ya kuwa kimya na kutojua la kufanya au kutosikia lisemwalo |
| 8. | Bidii | hamu ya kufanya jambo, juhudi |
| 9. | Mazingira | Hali au mambo yanayomzunguka kiumbe katika sehemu anapoishi au maisha yake |
| 10. | Mawaidha | Maneno ya maonyo au ya mafunzo yenye mwongozo na mashauri |
| 11. | Kupuuza | Kuacha kutia maanani, kudharau |
| 12. | Shingo upande | Hali ya kutoridhika, kutopenda, kuchukizwa |
| 13. | Kwenda haja | Kwenda chooni wa ajili ya kujisaidia haja ndogo au kubwa |
| 14. | Maarufu | Enye kujulikana kila mahali, mashuhuri |

**Zoezi la nne:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu**

1. Madhumuni
2. Ratiba
3. Bidii
4. Bumbuazi
5. Mawaidha
6. Kwenda haja
7. Mtazamo
8. Kwa shingo upande
9. Maarufu
10. Kupuuza

### 2.4.3. Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -nge-

*1.Sentensi zenye dhana ya masharti -nge-kutoka kwenye kifungu cha habari*

1. Kingeweza kuharibu afya yake.
2. Nisingepuuza mawaidha ya baba yangu, nisingekutana na matatizo haya.
3. Kama angekwenda shuleni asingefanyiwa hayo.

   Wanafunzi watunge sentensi tano kwa kutumia kiambishi cha mashariti "**nge**" katika hali kanushi. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanatunga sentensi sahihi.

**2. Majibu:** Mwali achunguze usanifu wa sentensi zilizotungwana na wanafunzi ikiwa zinakanusha kwa kutumia kiambishi cha masharti "nge"

**Mfano:**

- Asingejua kusoma, asingeweza kufanya biashara yake mjini Kigali.
- Wasingepika chakula kizuri, sisi sote tusingekifurahia.

***Zoezi la sita: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

| **Hali yakinishi** | **Hali kanushi** |
|---|---|
| 1. Ningekuja nyumbani kwako, ningemuona mgeni wako. | Nisingekuja nyumbani kwako, nisingemuona mgeni wako. |
| 2. Ungejifunza kwa bidii, ungeweza kumaliza masomo yako mapema. | Usingejifunza kwa bidii, usingeweza kumaliza masomo yako mapema. |
| 3. Angejua kusoma, angeweza kufanya biashara yake mjini Kigali. | Asingejua kusoma, asingeweza kufanya biashara yake mjini Kigali. |
| 4. Mngeomba msamaha, mngehurumiwa | Msingeomba msamaha, msingehurumiwa |
| 5. Wangepika chakula kizuri, sisi sote tungekifurahia. | Wasingepika chakula kizuri, sisi sote tusingekifurahia. |

***Zoezi la saba:***

*Wanafunzi wakamilishe sentensi kwa namna yao.*

*Huu ni mfano wa jinsi wanavyoweza kukamilisha sentensi hizi.*

1. Wanafunzi wasingemuuliza mwalimu wao, wasingeelewa somo hilo.
2. Nisingepuuza mawaidha ya baba yangu, nisingejuta namna hii.
3. Tusingechelewa shuleni, tusingeadhibiwa
4. Mutoni asingetumia pesa zake vibaya, asingekuwa maskini
5. Sisi tusingetoroka shuleni,wasingetutuma wazazi wetu
6. Binti yule asingeomba msaada, asingeweza mzigo wake.
7. Asingenunua gari hilo, asingeishiwa na pesa zake.

8. Nyinyi msingedharau ushauri wake, msingekuwa katika hali mbovu ya maisha.
9. Mfanyabiashara huyu asingenijulisha shida zake, nisingeelewa shida za kazi hii.
10. Tusingekuja, tusingeonana.

***Zoezi la nane: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Wasingekuja, wasingetukuta hapa.
2. Msingekuwa hodari, pesa zenu zisingemalizika
3. Mahali hapa pasingeoshwa, pasingependeza.
4. Msingetusalimia, tusingewajibu.
5. Wasingesoma, wasingejua
6. Tusingepata tatizo, tusingerudi kwetu kijijini.
7. Msingeomba, msingepewa.
8. Wasafiri wasingekuja mapema, wasingewahi basi kabla ya kuondoka.
9. Wazee wasingekuweko, mambo yasingesawazishwa.
10. Wasingekuwa na ukakamavu, wasingemshika mwizi.

***Zoezi la tisa: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Gari hili lingeoshwa, lingependeza.
2. Mtoto angeanguka, angevunjika.
3. Mngepumzika, mngeshinda.
4. Mngekuwa wajumbe, mngesaidia shule yetu.
5. Mngekuwa na pesa, mngefanya kitendo hicho.
6. Mngekuja, mngetuona.
7. Mngekuwa hodari, pesa zenu zisingemalizika.
8. Wazee wangekuwepo, mambo yangenyooshwa.
9. Wasafiri wangekuja mapema, wangewahi kuondoka kwa muda uliopangwa.
10. Wangekuwa makini siku ile, wangemshika mwizi.
11. Matumizi ya lugha

### 2.4.4. Matumizi ya Lugha

***Zoezi la kumi : (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaambie wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kujadili kuhusu "Umuhimu wa lugha katika jamii", kisha wawaelezee wenzao.*

Mambo ya kuzingatiwa:

- kuwasiliana

- kushirikiana
- kudumisha utamaduni
- kudumisha amani

### 2.4.5. Kusikiliza na kuzungumza

***Zoezi la kumi na moja: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaambie wajadiliane katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu na majadiliano yao yajikite kwenye hoja zinazotokana na:*

1. Matatizo yawezayo kujitokeza baina ya watu wawili wanaposhindwa kusikilizana kimawasiliano.
2. Umuhimu wa lugha katika jamii
3. Mambo mbalimbali yanayoweza kukwamisha mawasiliano yenye kutumia lugha

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao kujadili maafa yawezayo kujitokeza baina ya watu wawili wanaposhindwa kusikilizana kimawasiliano. Mwalimu anaweza kuwapa mifano ifuatayo:

- *Mimi ninaona kwamba....................................................................*
- *Kwa upande wangu, .......................................................................*
- *Maafa yanayoweza jitokeza ni pamoja na.......................................*

### 2.4.6. Kuandika

***Zoezi la kumi na mbili: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu amwoongoze mwanafunzi kutunga kifungu cha habari kwa kutoa hoja na maelezo kamili.

# SOMO LA 3: LUGHA KATIKA JAMII

## 3.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu utumiaji wa lugha katika jamii. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu utumiaji wa lugha kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi wafanye makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha Mwanafunzi (Ukurasa 18). Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- *Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.*
- *Matukio haya yanafanyikia wapi?*
- *Ni shughuli zipi unazoziona kwenye michoro?*
- *Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?*
- *Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?*

## 3.2 Zana za kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro ya watu wanaozungumza.
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu kwa hiyo yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 3.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).

- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao wajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 3.4 Majibu

***Zoezi la kwanza: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchorowakiongozwa na maswali waliyoulizwa kuhusu mchoro.

### 3.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Wao huiona lugha kama kitu cha kawaida.
2. Shughuli za usafirishaji wa watu na vitu, ununuzi na uuzaji, ujenzi wa taifa, uongozi na utawala, huduma mbalimbali na shughuli nyingine nyingi.
3. Jamii huweka mikakati ya kulinda na kufihadhi lugha zao ili zisitoweke au zisichafuliwe na lugha nyingine.
4. Mtu huyo ndiye hupewa heshima na majukumu mengi katika jamii yake.
5. Lugha hizo ni pamoja na Kiswahili, Kirundi, Luganda, na kadhalika.
6. Tabia mbaya hizo ni pamoja na matumizi ya madawa ya kulevya, ubakaji, ubaguzi, ulevi, uvivu, uzembe, uzururaji, umalaya, na kadhalika.
7. Tabia mbaya hizo zitakomeshwa kwa njia ya mazungumzo pamoja na wahusika, yaani lugha itatumiwa kama chombo cha mawasiliano.
8. Wanajamii wasingeelewana kimawasiliano, shughuli zote za jamii zingekwama.

9. Lugha ni sehemu ya utamaduni wa jamii ambapo kaida na maadili ya wanajamii yote hupatikana katika lugha ya jamii hiyo.
10. Umuhimu wa lugha katika jamii, thamani ya lugha katika jamii, lugha na jamii, lugha na utamaduni n.k.

### 3.4.2 Msamiati kuhusu lugha katika jamii

**Zoezi la pili:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**1. Wajibu:** Mnyarwanda kindakindaki ana wajibu wa kulinda nchi yake.

**2. Huduma:** Kila mfanyabiashara anahimizwa kuwapa wateja wake huduma nzuri.

**3. Pana:** Darasa hili ni pana.

**4. Uti wa mgongo:** Maria hawezi kutembea kwa sababu anaumwa kwenye uti wa mgongo.

**5. Kukadiriwa:** Gharama ya mradi wa kujenga soko kubwa ilikadiriwa.

**6. Mila:** Kila jamii ina mila zake.

**7. Imani:** Kamali ana imani ya dini yake.

**8. Mathalani:** Wanyarwanda hupanda mbegu nyingi mathalani maharagwe, mahindi, mpunga, mtama na kadhalika.

**9. Kuposa :** Wiki ijayo wazazi wangu wataenda kumposa binti atakayekuwa mke wangu.

**10. Mahari:** Katika jamii ya Kinyarwanda mahari hutolewa na baba ya bwana arusi.

***Zoezi la tatu:***

1m, 2h, 3g, 4k, 5a, 6l, 7c, 8d, 9f, 10j, 11b, 12i, 13e

***Zoezi la nne: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Usafirishaji
2. Maadili
3. Umalaya
4. Usawa wa jinsia
5. Mikakati
6. Mvuvi
7. Uzalendo
8. Uvivu
9. Unadhihirisha
10. Kuhifadhi

### 3.4.3 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la tano:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1.

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | S | A | F | I | R | I | S | H | A | J | I |

2.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | T | A | W | A | L | A |

3.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| T | A | M | A | T | I |

4.

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| D | E | S | T | U | R | I |

5.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| H | A | R | U | S | I |

**Zoezi la sita:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

- Lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano kati ya wanadamu.
- Lugha ni ufunguo wa mawasiliano kati ya wanajamii.
- Lugha hutumiwa na binadamu kuwasilisha maoni yake, fikra zake, hisia zake, matata na nia zake kwa binadamu wengine.
- Lugha hutambulisha jamii.

### 3.4.4 Kusikiliza na Kuzungumza

***Zoezi la saba: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaambie wanafunzi wajadiliane, katika makundi ya watu wawili wawili, kuhusu mada isemayo: ***"Hakuna jamii isiyo na lugha na hakuna lugha isiyo na jamii"***, kisha wawasilishe maoni yao mbele ya wenzao.

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Maana ya ya fasihi
- Maana ya lugha
- Umuhimu wa lugha katika jamii
- Uhusiano wa jamii na lugha

### 3.4.5 Kuandika

***Zoezi la nane: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaambie wanafunzi kutunga kifungu cha habari kwa kutumia viambishi vya masharti kuhusu mada isemayo "Shughuli zote anazofanya binadamu huhitaji lugha".*

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Maana ya lugha
- Matumizi ya lugha kama chombo cha mawasiliano
- Utumiaji wa sentensi mbalimbali zenye viambishi vya masharti yasiyowezekana.

# SOMO LA 4: FAIDA NA HASARA ZA KUTUMIA LUGHA MOJA

## 4.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu faida na hasara za utumiaji wa lugha katika jamii. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni awashirikishe wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu faida na hasara za utumiaji wa lugha moja, kisha afanye chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Mwalimu anaweza kuuliza wanafunzi maswali yanayohusiana na

- Utumiaji wa lugha katika jamii.
- Kutaja lugha zinazotumiwa nchini Rwanda.
- Kutaja faida za kutumia Kinyarwanda tu nchini Rwanda.
- Kutaja hasara za kutumia Kinyarwanda tu nchini Rwanda.
- Kutaja faida za kutumia lugha nyingi nchini Rwanda.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awambie wanafunzi waunde makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha Mwanafunzi (Ukurasa wa 20) Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: **« Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo » :**

- *Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.*
- *Matukio haya yanafanyikia wapi?*
- *Ni shughuli zipi unazoziona kwenye michoro?*
- *Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?*
- *Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?*

## 4.2 Zana za kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro ya watu wanaozungumza.
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu aandae vifaa kadhaa vitakavyomsaidia kufanikisha somo lake. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu yeye mwenyewe,kwa hiyo ajibunie vifaa mbalimbali vitakavyomsaidia.

## 4.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atilie mkazo kwenye:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mbinu zote za ujifunzaji zinapaswa kumuweka mwanafunzi juu ya mambo yote darasani, wanafunzi watumie makundi yao kwa kufanya matendo yote watakayoombwa na mwalimu, kwa kufanya kazi na mazoezi yaliyo ndani ya kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakapokuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/ zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari au kwa kufanya tathmini).
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi wamuulize mwalimu naye awajibu. Tena maswali na majibu haya yaweze kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi amepewa kipaumbele katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu angali msuruhifu katika somo. Kwa hiyo, mwalimu atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

**Majibu**

***Zoezi la kwanza:*** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchoro.

### 4.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Jamii ni kundi la watu wanaoishi katika eneo moja.
2. Jamii ikitumia lugha moja, uchumi wake utaimarika kwa sababu mfanyabiashara atakuwa na uwezo wa kuwasiliana na kila mteja anayekuja kununua kwake. Pia mteja huyu huweza kutafuta kile anachohitaji katika maeneo tofauti katika jamii yake bila kukutana na kikwazo cha mawasiliano.
3. Ndiyo! Kuna faida za kisiasa zinazotokana na kutumia lugha moja katika jamii. Kwa mfano viongozi wanawasiliana na kuelewana na raia kiurahisi. Serikali itasambaza siasa na matangazo kwa raia kiurahisi.
4. Jamii hii haitatajirika sana kwa sababu raia wake hawataingia kwenye soko la watumiaji wa lugha tofauti na lugha yao. Jamii hii itakuwa imejifungia mahali pamoja.

5. Lugha huchukuliwa kama chombo cha mawasiliano katika jamii kwa sababu lugha hutumiwa na mwajamii kwa kupashana habari.

6. • Mtu anayejua lugha nyingi anaweza kujiongezea ujuzi kwa kusoma magazeti, majarida, kwa kufuata vipindi mbalimbali kwenye redio, runinga na tovuti.

   - Mtu anayejua lugha nyingi anajipatia marafiki kutoka sehemu tofauti.
   - Mtu anayejua lugha nyingi anaweza kwenda kusomea sehemu tofauti ulimwenguni.
   - Mtu anayejua lugha nyingi anaweza kutembelea sehemu tofauti ulimwenguni.
   - Mtu anayejua lugha nyingi anaweza kufanyia biashara katika sehemu tofauti ulimwenguni.
   - Mtu anayejua lugha nyingi anaweza kutumia vifaa (simu, mashine, mitambo, tarakilishi,...) mbalimbali vyenye taratibu mbalimbali zilizochapishwa kwa lugha mbalimbali.

7. Jamii hii haitasonga mbele kwa sababu itakuwa imejiwekea mipaka na ulimwengu mzima.

8. Serikali ya Rwanda ilihalalisha utumiaji wa lugha nyingi hapa nchini. Lugha hizo ni Kinyarwanda, Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

9. Ndiyo! Utumiaji wa lugha nyingi unaweza kuathiri utamaduni wa jamii kwa njia mbili. Kwanza utumiaji huu unaweza kufanya utamaduni upotee au ufifie. Pili utumiaji huu wa lugha nyingi unaweza kutajirisha utamaduni kwa kuleta mambo mapya kutoka tamaduni nyingine.

### 4.4.2 Msamiati kuhusu Faida na Hasara za Kutumia Lugha Moja

***Zoezi la pili:* (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)**

**Eneo:** mahali, sehemu ya ardhi.

1. **Manufaa:** faida
2. **Kufahamika:** kujulikana
3. **Mteja:** mnunuzi
4. **Kikwazo:** kizuizi
5. **Madhara:** uharibifu, athari mbaya
6. **Kusambaza:** kueneza
7. **Mtazamo:** fikra, wazo, maoni.
8. **Ulimwengu:** dunia
9. **Maarifa:** hekima, elimu, ujuzi

***Zoezi la tatu:* (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)**

1. Manufaa
2. Lugha ya Kiswahili
3. Hushirikiana
4. Chombo
5. Pato
6. Watawala
7. Madhara
8. Utamaduni
9. Kiungo
10. Imeteuliwa

### 4.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -ngeli

***Zoezi la nne: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aongoze majadiliano ya wanafunzi kuhusu maana ya sentensi za zoezi la nne katika kitabu cha mwanafunzi. Baadaye awaelekeze kutunga sentensi.*

**Sentensi za Mfano:**

1. Ningelikuwa na pesa, ningelinunua nyumba nzuri.
2. Tungelionana siku ile, tungelijadiliana.
3. Wangeliamka mapema, wangelienda na basi.
4. Angelitumia pesa zake vizuri, angelikuwa tajiri.
5. Angelijua lugha nyingi, angeliwasiliana na watalii

***Zoezi la tano:* (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)**

a. Kingelitumiwa.
b. Kisingelitumiwa
c. Usingeliliwa
d. Ingeliwafaidi
e. Isingeliwafaidi
f. Angelishinda
g. Ningeliwahudumia wagonjwa
h. Tungelinunua magari
i. Ungelitusaidia
j. Wangelipika pilau

### 4.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la sita:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Kujua lugha moja kunasababisha maelewano mazuri kati ya raia. Kujua lugha nyingi kunasaidia kujiapatia marafiki wengi, kujiongezea ujuzi, kusafiri nje ya nchi yako, na kadhalika.
2. Amekubali kuwa yaliyosemwa na mwenye kujua lugha nyingi yalikuwa kweli.

***Zoezi la saba: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**a. Ulumbi:** umilisi wa lugha nyingi, uhodari wa kuzungumza.

**b. Fazaa:** wasiwasi, hangaiko la moyo

**c. Hadhaa:** hila, udanganyifu

**d. Nimeduwaa:** nimepumbaa, nimestaajabu

**e. Mtaji :** mali inayotumiwa kwa kuanzisha biashara.

**f. Kujifariji :** kujiliwaza, kujiburudisha

**g. Fununu :** tetesi, habari za mnong'ono, habari zisizo na hakika.

**h. Sisimizi :** nyenyere, mdudu mdogo wa kahawia au mweusi mwenye umbo na sura kama siafu.

**i. Manani:** Mungu

**j. Kutakadamu :** kuanza kufanya jambo kabla ya wengine.

***Zoezi la nane: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | F | F | V | K | I | M | K |
| L | A | A | A | N | M | T | U |
| U | D | J | D | D | A | A | T |
| M | H | I | J | J | H | A | A |
| B | A | F | A | M | H | A | K |
| I | A | A | G | D | F | A | A |
| H | Z | R | O | B | O | I | D |
| E | U | I | T | I | M | I | A |
| W | A | J | I | B | U | K | M |
| A | P | I | U | S | U | M | U |

Majibu : Mlumbi, kutakadamu, wajibu, fomu, fadhaa, jifariji, sumu, mtaa, fadhaa, mtu

### 4.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

***Zoezi la tisa : (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaagize wanafunzi, katika makundi ya watu wawili wawili, kuigiza mazunguzo kati ya anayezungumza lugha moja tu na yule anayezungumza lugha nyingi.

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Matamshi bora ya maneno ya Kiswahili
- Utumiaji wa vitabia

### 4.4.6 Kuandika

***Zoezi la kumi: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaambie wanafunzi (kila mmoja) kutunga kifungu cha habari chenye anwani ifuatayo :*

« Lugha ni Ufunguo wa Maisha Mazuri kwa Binadamu »

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Uzalishajimali

## SOMO LA 5: ASILI YA LUGHA YA KISWAHILI

### 5.1 Utangulizi/ Marudio

Mwalimu aanze somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi wake. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu ajue hali za wanafunzi na baadaye awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kujibu maswali hayo na awachangamshe kidogo hivi akielekeza maswali yake kwenye somo jipya. Baadaye, mwalimu awaweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awape kazi hii:

- T*azameni michoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoonekana kwenye michoro hiyo.*

### 5.2 Vifaa vya kujifunzia

Kwa minajili ya somo kuweza kufika kwenye malengo yake, mwalimu atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ramani ya Afrika au Afrika ya Mashariki inayoonyesha chimbuko la Kiswahili
- Michoro au picha za maeneo mbalimbali
- Kompyuta
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa ipo
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo juu ya hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na upatikanaji wavyo. Mwalimu kwa ubunifu wake aandae vifaa mbalimbali vya kumsaidia kufanikisha somo lake.

## 5.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake hivi akitilia mkazo mbinu zifuatazo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wane. Ni vizuri kutozidi idadi ya watu watano katika kundi moja kwa kujilinda uzembe ndani ya kundi. Mwalimu aendelee kuchunguza kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yachanganye wasichana na wavulana. Baada ya kazi, mwalimu aombe makundi kuwasilisha matokeo kwa darasa. Kazi katika makundi itiliwe mkazo kwa kusaidia wanafunzi kushirikiana na kujifunza kutoka kwa wenzao.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya kibinafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. (Asome kifungu cha habari mwenyewe au afanye zoezi mwenyewe).
- **Maswali na majibu:** Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu aweke maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi na wanafunzi. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali na wao wamjibu, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu naye atoe majibu yake.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu katika kazi yake na ubunifu wake ajue vizuri uelewaji wa wanafunzi wake, kisha atambue ujuzi unaohitaji maelezo yake binafsi. Ikiwa anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee vya kutosha wanafunzi wake somo kwa kusisitizia kasoro aliyoitambua. Ni vizuri kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya majadiliano kuhusu maelezo yake.

## 5.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoonekana kwenye michoro hiyo. (Wanafunzi wataangalia mchoro na kuzungumzia vile wanavyoona).*

### 5.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Neno Kiswahili lilianza kutumika karne ya kumi na nne (Baada ya Kristo Kuzaliwa).

2. Neno hili lilitoka kwa wageni wa Kiarabu waliokuja barani Afrika kwa shughuli zao za kibiashara na kufika pwani ya Afrika Mashariki. Eneo hili lilipewa jina la "sawahil" (au sahel) kwa maana ya eneo la watu wa pwani, na "sawahiliya"(Sawahel) kumaanisha wenyeji wa sehemu hiyo. Neno "Sahel" baadaye lilileta jina jingine "Kiswahili" kwa maana ya lugha ya watu wa sehemu hiyo ya pwani, ambapo watu wenyewe waliitwa Waswahili.

3. Kuna mitazamo minne muhimu kuhusu asili ya Kiswahili: Mtazamo wa kwanza unatetea kuwa asili ya Kiswahili ni Kiarabu. Mtazamo wa pili hutetea Kiswahili kama lugha chotara, yaani mchanganyiko wa lugha za pwani na Kiarabu. Mtazamo wa tatu hutetea Kiswahili kuwa lugha ya kibantu, lakini mtazamo huu una mitazamo miwili ndani yake. Kwanza, lugha ya Kiswahili ilikuwepo toka zamani, kabla ya majilio ya wageni kwa baadhi ya watetezi. Kwa watetezi wengine, lugha ya Kiswahili ni mchanganyiko wa lugha tofauti za Kibantu zilizotumiwa sehemu ya pwani.

4. Baadhi ya watu walifikiria kuwa Kiswahili kilitokana na Kiarabu kwani katika lugha ya Kiswahili kuna maneno mengi ya Kiarabu, tena Kiswahili kilitumiwa na wenyeji wa sehemu pwani ambao walikuwa Waislamu. Kwa kuwa uislamu ulietwa na Waarabu, basi wao husisitiza kuwa lugha ya Kiswahili imeletwa na Waarabu hao.Maneno matatu ya Kiarabu yanayopatikana katika Kiswahili ni kama laki, elimu, fahamu.

5. Kusema kwamba lugha ni "chotara" ni kumaanisha kuwa lugha hiyo inatokana na mchanganyiko wa lugha mbili au zaidi.

6. Asili ya Kiswahili ni sehemu ya pwani ya Afrika Mashariki.

7. Lahaja za Kiswahili ambazo zinapatikana katika kifungu ni Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbatu, Kibajuni, Kisiu na Kiamu.

8. Waarabu walifika kwenye sehemu za pwani Afrika Mashariki kwa lengo la kufanya biashara.

9. Ni lazima kuchunguza kwa makini maoni ya watu mbalimbali kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kutopotosha watu wenye hamu ya kujua mengi kuhusu asili ya lugha ya Kiswahili ambayo ni ya thamani kubwa katika Afrika nzima na hata nje yake.

10. Taja lugha za kibantu zilizozungumziwa katika kifungu ulichosoma.

    Lugha nyingine za kibantu zilizozungumziwa kifunguni ni Kinyarwanda, Kirundi na Kiswahili.

### 5.4.2 Msamiati kuhusu Asili ya Lugha ya Kiswahili

***Zoezi la 2: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu ya zoezi la 2 A**

1. **Kibantu:**Kundi la lugha zenye mfumo wa ngeli za majina na viambishi ambazo zinazungumzwa kusini mwa jangwa la Sahara kama vile Kiswahili, Kinyarwanda, Kilingala, Kizulu kwa uchache.
2. **Chotara:** Mtu aliyezaliwa na wazazi wa rangi mbalimbali ama mbegu zinazotokana na mchanganyiko wa aina mbili za mbegu. Lugha chotara ni ile inayotokana na mchanganyiko wa lugha mbili.
3. **Chimbuko:** mahali kitu kilipoanzia
4. **Pwani:** Sehemu iliyo kandokando ya bahari yaani mwambao.
5. **Mawasiliano:** Upashanaji wa habari kwa njia mbalimbali kama simu, barua, mdomo, n.k.
6. **Maarufu:** Mtu au kitu ambacho kinajulikana kila mahali.
7. **Utu:** Hali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya mtu/ ubinadamu.
8. **Utamaduni :** Mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani.
9. **Lahaja:** Tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja.
10. **Watetezi:** Watu ambao wanapigania haki au jambo la mtu mwingine ili asionewe/ wagombozi.

### 5.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti -ngali-

***Zoezi la 3: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kama kiambishi chenye dhana ya masharti -nge- ambacho tulikiona awali, kiambishi cha masharti -ngali-huweza kutumika kwa hali moja na -nge- bila tofauti. Ni kusema kwamba kiambishi kimoja kinaweza kutumika badala ya kingine. Katika kukanusha kiambishi -si- huongezwa na kuwa -singali-.*

***Zoezi la 4:***(Ukurasa wa 31)

1. Tungalikuja, **tungalionana.**
2. Tungalionana, **tungalimaliza.**
3. Tungalikuwa na pesa, **tungalisafiri.**
4. Wapishi wangalikuwa na viungo, **wangalipika.**
5. Wafanyabiashara wale wangalilipa ushuru **wasingaliadhibiwa.**

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. **Msingalipendana, msingalijenga** umoja.
2. **Msingalifanya** kazi vizuri, **msingalifaulu** mtihani.
3. **Wasingaliomba, wasingalipewa.**
4. Wazee **wasingalikuwepo**, mambo **yasingalisawazishwa.**
5. Kioo **kingalianguka, kingalivunjika.**

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Yeye **angalizungumza** vizuri, **tungalielewana.**
2. **Ungalijua** hatari ya ukimwi, **usingaliyafanya** hayo.
3. Chumba **kingalisafishwa, kingalipendeza.**
4. Mwashi **angalikuwa** makini, nyumba i**ngalikuwa** imara.
5. Gari **lingalikuwa** zuri, **tungalifika** mapema.

### 5.4.4. Matumizi ya Lugha: Mazoezi ya Makundi

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Maneno yafuatayo ndiyo yaliyopendekezwa:**

Mzee Ngirimana na mkewe huwasiliana katika lugha ya Kinyarwanda. Lugha hiyo ni lugha ya **Kibantu** kama vile Kiswahili na Lingala. Mzee Hassan ambaye ni rafiki yake Mzee Ngirimana ni Muislamu. Kila Ijumaa huenda **msikitini** na kusali katika lugha ya **Kiarabu.** Zabibu Binti yake Hassan aliolewa na mwanaume Mwarabu. Hivi sasa **amejifungua** watoto wawili. Watoto hao **huwasiliana** katika mchanganyiko wa Kinyarwanda na Kiarabu. Lugha wanayoitumia huitwa lugha **chotara**. Asili ya Kiswahili ni **pwani** ya Afrika Mashariki, ilhali ya Kinyarwanda ni nchini Rwanda. Sasa **asili** ya lugha ya watoto hao ni ipi?

Kasimu na Tumusifu, wajukuu zake Mzee Hassan wanasoma katika kidato cha nne mchepuo wa lugha. Jana mwalimu wa Kiswahili aliwapa kazi ya nyumbani. Kazi hiyo ni ya kutaja lahaja kumi za Kiswahili.

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha awaombe kusoma maelezo muhimu waliyopewa kuhusu asili ya Kiswahili. Wanafunzi nao wasome maelezo katika kitabu cha mwanafunzi huku wakibainisha hoja muhimu zinazoambatana na asili ya lugha ya Kiswahili. Mwalimu kwa upande wake ahakikishe kwamba hoja zifuatazo zimebainishwa:*

- **Kuna mitazamo tofauti kuhusu asili ya Kiswahili:**
    - Kiswahili ni Kiarabu.
    - Kiswahili ni lugha Chotara yaani mchanganyiko wa lugha za pwani na Kiarabu.

- Kiswahili ni lugha ya Kibantu.
- Kiswahili ni pijini ambayo baadaye ilikomaa na kuwa krioli.

- Waarabu walikuja sehemu za pwani ya Afrika ya mashariki ambapo lahaja za Kiswahili zilikuwa zikitumika.
- Lugha ya Kiswahili  ilikuwa ikitumiwa na Waswahili waliokuwa na utamaduni wao.
- Lugha ya Kiswahili ilikuwepo toka zamani kabla ya maajilio y awageni.
- Kiswahili ni luha yenye thamani kubwa barani Afrika na hata nje yake.
- Kiswahili ni lugha ya Kibantu yenye uhusiano na lugha nyingine za Kibantu.
- Chimbuko la Kiswahili ni sehemu ya pwani ya Afrika Mashariki.
- Kiswahili kina lahaja mbalimbali:

Lahaja walizopata ni hizi zinazofuata: **Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbatu, Kibajuni, Kisiu, Kiamu, Kingozi, Kingwana, Kimvita, Kimashomvi, Kivumba, kimwami, Kipate, Kimtang'ata, ...**

**Zoezi la 9*: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kwanza. Kisha, ahakikishe kwamba wanafunzi wanajadiliana kuhusu mitazamo minne ya asili ya lugha ya Kiswahili. Vilevile mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kwa kuchunguza ikiwa makundi yote yameweza kupata hoja za kutosha kwa kutetea kila mtazamo na kuutathminini kulingana na ukweli uliopo kuhusu asili ya Kiswahili.*

### 5.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**Zoezi la kumi: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

- Wanafunzi wajadiliane katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kuhusu mitazamo mbalimbali ya asili ya lugha ya Kiswahili
- Wanafunzi watoe mtazamo wao

### 5.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la kumi na moja:**

Wanafunzi watunge kifungu chenye mada ifuatayo:

"*Manufaa ya Kiswahili kwa wananchi wa Afrika Mashariki*"

## SOMO LA 6: Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili

### 6.1 Utangulizi/Marudio

Mwalimu aulize wanafunzi mmoja kwa mwingine maswali tofauti kuhusu somo lililotangulia kwa ajili ya kuchunguza ikiwa wanakumbuka maana ya lugha. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu awaombe wanafunzi kuchukua vitabu vya Kiswahili na kutazama michoro ambayo inatangulia kifungu cha habari. Baada ya wanafunzi kutazama michoro, mwalimu awaulize maswali yanayofuata:

- Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye mchoro?
- Unafikiria nini kuhusu namna unayowatazama wahusika?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?

Baada ya maswali aliyouliza na majibu yaliyotolewa, mwalimu aendelee na somo mara kwa mara.

### 6.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

- Ramani ya bara la Afrika ioneshayo eneo la nchi zinazotumia Kiswahili.
- Kitabu cha mwanafunzi, kalamu, ubao, n.k.
- Mwongozo wa mwalimu, Kamusi ya Kiswahili sanifu.

### 6.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kimya kifungu cha habari kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Hatimaye mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma kuhakikisha kuwa wamekielewa. Baada ya hayo, mwalimu awaombe wanafunzi mmoja bada ya mwingine kusoma kwa sauti kifungu hivi akiwasahihisha itakiwavyo. Halafu mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi kujibu maswali ya ufahamu. Wanafunzi wamulike majibu ya makundi yao kisha mwalimu awasahihishe kunapohitajika na kuwapa tathmini.

### 6.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watazame michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza*

#### 6.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Mbali na nchi za Bara la Afrika, Kiswahili kinafundishwa huko Ujerumani, Uingereza, Ufaransa na Marekani.
2. Tunaposema kwamba lugha imeenea ni kumaanisha kuwa lugha hiyo imeongeza idadi ya watumiaji wake katika nchi inamotumika, hata nje ya nchi hiyo.

3. Kiswahili hutumika sana katika shughuli za kibiashara, elimu, siasa, dini pamoja na vyombo vya habari.
4. Watumwa ni raia weusi wa Afrika waliouzwa toka bara la Afrika kuelekea Marekani na kufanyishwa kazi bila ujira.
5. Wakifikiri kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa rahisi kujifunza kuliko lugha za kiasili, hivyo ilirahisisha mawasiliano baina yao na Waafrika.
6. Wamishenari waliamua kutumia lugha ya Kiswahili kuwahubiria waumini wao kwa madhumuni ya kuweza kueneza Injili.
7. Wakoloni walikuja barani Afrika kwa malengo mbalimbali k.v ukoloni, kueneza Injili, kutafuta mali, n.k.
8. Lugha zingine ni pamoja na Kifaransa, Kingereza, Kireno, n.k.
9. Kiswahili kimezitajirisha lugha nyingi na msamiati wake. Mfano wa Kinyarwanda: maneno k.v sahani, meza, nyundo, mpanga, kijiko, n.k. Maneno haya yalitoka katika Kiswahili.
10. Ujuzi wa Kiswahili una umuhimu mkubwa kama vile; kufanya shughuli mbalimbali katika nchi zinazotumia lugha ya Kiswahili, kuwa na marafiki wengi, n.k.

### 6.4.2 Msamiati kuhusu Ueneaji wa Kiswahili

***Zoezi la 2:** (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*

**Maana za msamiati**

**1. Sambaa:** enea kila mahali, zagaa.

**2. Wenyeji:** watu ambao wamezaliwa mahali fulani na wakaendelea kukaa hapo.

**3. Watumwa:** watu wanaomilikiwa na wengine na kufanyishwa kazi bila ya ujira.

**4. Rasilimali:** jumla ya mali alizo nazo mtu, shirika au nchi.

**5. Warishurutisha:** walilazimishwa

**6. Kamati :** kikundi cha watu waliochaguliwa ili kushughulika na kazi fulani.

**7. Mathalani:** kwa mfano

**8. Ubakaji:** hali ya kumkamata mtu na kuzini naye bila ridhaa yake.

**9. Imani :** mambo anayokubali mtu kuwa ni ya kweli na anayopaswa kuyaheshimu, hasa katika dini.

**10. Kuimarisha:** kufanya kuwa imara, madhubuti.

**Zoezi la 3:** *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*

**Majibu.**

1. walishurutishwa
2. Watumwa
3. kimesambaa
4. wenyeji

5. vituo
6. idhaa
7. kamati
8. mamlaka
9. imani
10. kuimarisha

### 6.4.3 Sarufi: Matumizi ya Viambishi vyenye Dhana ya Masharti

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu**

1. Mngalipendana, mngaliunda umoja.
2. Mngalijifunza kwa bidii, mngalishinda mtihani.
3. Wangaliomba, wangalipewa
4. Wazazi wangalikuwepo, mambo yangalisawazishwa.
5. Mtoto angalianguka, angalivunjika mguu.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Majibu**

1. Msingalionana, msingalisalimiana.
2. Msingaliamka mapema, msingalifika shuleni kwa wakati ufaao.
3. Wasingaliomba msaada, wasingaliupewa.
4. Wazee wasingalikuepo, mambo yasingalisawazishwa.
5. Asingalishiriki mashindano hayo, asingalichaguliwa.

### 6.4.4 Matumizi ya lugha: Mazoezi ya Makundi

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaongoze wanafunzi kutambua kwenye jedwali msamiati uliofundishwa katika kifungu cha habari.*

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | O | P | **K** | **I** | **S** | **W** | **A** | **H** | **I** | **L** | **I** | **T** |
| G | **A** | C | I | D | H | **A** | A | N | O | **E** | **M** | **E** |
| A | **F** | G | **W** | **W** | D | **L** | R | T | L | **N** | **A** | **L** |
| J | **R** | A | **A** | **A** | V | **I** | H | K | U | **G** | **N** | **E** |
| K | **I** | U | **T** | **A** | **A** | **S** | **I** | **S** | **I** | **O** | **I** | **V** |
| L | **K** | Y | **U** | **R** | J | **H** | O | **P** | **W** | **A** | **N** | **I** |
| O | **A** | R | **M** | **A** | **B** | **U** | **R** | **U** | **N** | **D** | **I** | **S** |
| D | A | F | **W** | **B** | A | **R** | **W** | C | D | S | O | **H** |
| E | R | D | **A** | **U** | D | **U** | **A** | S | I | A | M | **E** |
| **K** | **E** | **N** | **Y** | **A** | H | **T** | **N** | F | O | A | A | **N** |
| **A** | B | C | V | T | I | **I** | **D** | **A** | **D** | **I** | L | **I** |
| **M** | N | H | E | **K** | **U** | **S** | **A** | **M** | **B** | **A** | **A** | L |
| **A** | L | I | L | I | S | **H** | W | A | L | E | W | E |
| **T** | S | O | P | R | S | **W** | U | V | W | Y | I | Z |
| **I** | **N** | **J** | **E** | Z | **B** | **A** | **R** | **A** | C | D | H | A |

**Zoezi la 7 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanasoma maelezo muhimu kisha mwalimu awaongoze katika majadiliano kuhusu ueneaji wa lugha ya Kiswahili. Maswali ya kuongoza mjadala ni pamoja na Nini maana ya kuenea? Kiswahili kilienea kuanzia wapi? Zipi ni njia zilizotumika kueneza Kiswahili? Njia zipi zilitumika kueneza Kiswahili nchini Rwanda?*

### 6.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awambie wajadili kuhusu nafasi ya Kiswahali barani Afrika. Badaye wawasilishe maoni yao mbele ya wenzao.*

### 6.4.6 Kuandika

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao, kutunga kifungu cha habari kuhusu "Kiswahili ni lugha muhimu" Wakitumia kivumishi cha masharti "-ngali". Mwalimu awaongoze kunapohitajika.*

# SOMO LA 7 : HISTORIA YA KISWAHILI NCHINI RWANDA

## 7.1 Utangulizi

Mwalimu aanze somo kwa kuuliza wanafunzi maswali yafuatayo :

1. Katika somo letu tunatumia lugha gani?
2. Kwa sababu gani tunahitaji lugha ya Kiswahili nchini Rwanda ?
3. Lugha ya Kiswahili ililetwa na nani nchini Rwanda ?
4. Wanyarwanda tangu zamani mpaka leo wanafurahia kutumia lugha hiyo?
5. Je, kuna umuhimu wowote wa kusoma lugha ya Kiswahili nchini Rwanda?

## 7.2 Vifaa

Kitabu cha mwanafunzi na kitabu cha mwalimu kidato cha nne, muhtasari wa somo la Kiswahili, kamusi ya Kiswahili sanifu, ramani ya Rwanda, ……….

## 7.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Somo hii linahusu historia ya Kiswahili nchini Rwanda. Mwalimu arahisishe ufunzaji wake kwa kuleta vifaa vyote vitakavyosaidia wanafunzi kuelewa somo. Mwalimu awachangamshe kwa kuwauliza maswali kuhusu mchoro uliomo katika kitabu cha mwanafunzi (ukurasa 50) kwa mfano: "mnaona nini kwenye mchoro huu?" wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza kile kinachoendelea katika mchoro huo. Katika sehemu hii mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata uwezo kuhusu tafakuri tunduizi , ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha mchoro husika.

- **Kusoma na kufahamu kifungu kuhusu historia ya Kiswahili nchini Rwanda.**

  Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kimya kifungu cha habari kilichopo huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kimya kifungu, awaombe kusoma kwa sauti. Mwalimu akumbuke umuhimu wa kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

  Hatimaye, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa.

- **Ujifunzaji wa msamiati kuhusu kifungu**

  Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali ya ufahamu, wanafunzi katika makundi mwalimu awasaidie kuelewa kila swali na baadaye kutoa majibu kwa wanafunzi.

  Mwalimu baada ya kusahihisha maswali ya ufahamu, anaongoza kazi ya kutafuta maana ya msamiati . Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wanatumia kamusi ya Kiswahili sanifu kutafuta maana ya msamiati . Swali jingine ni kuchagua kwenye msamiati neno sahihi na kukamilisha sentensi. Kwa hivyo,mwalimu azunguke katika makundi yote.

- **Sarufi**

  Kwa kufundisha somo la sarufi, Mwalimu awaombe wanafunzi kuandika sentensi kutoka kifungu cha habari zenye kiambishi chenye dhana ya masharti na kujadiliana maana zake. Kwa kuendelea kutoa maelezo, mwalimu awaombe kutunga sentensi tano na kukamilisha sentensi.

- **Matumizi ya lugha**

  Mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza herufi kwenye jedwali na kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili.

- **Kusikiliza na kuzungumza**

  Hapa mwalimu awaombe kutunga mazungumzo kuhusu Historia ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda na kuwasilisha kazi hii na kuigiza mazungumzo haya. Hapa mwalimu achunguze mambo muhimu yafuatayo:

  Matumizi ya lugha kwa ufasaha; matumizi ya msamiati; sentensi zenye maana

- **Kuandika**

  Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga kifungu cha habari "Umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa Wanyarwanda" hapa mwalimu achunguze kama mwanafunzi anatunga sentensi sahihi na matumizi yake kwa ufasaha wa kisarufi; n.k

## 7.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watazame michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza.*

### 7.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Kabano na Muhire wanazungumzia kuhusu historia ya Kiswahili nchini Rwanda.
2. Historia ya Kiswahili nchini Rwanda hueweza kugawika katika vipindi vitatu: Kipindi cha kwanza kinahusu "Kiswahili wakati wa ukoloni", cha pili "Kiswahili baada ya ukoloni" na cha tatu "Kiswahili baada ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mwaka 1994."
3. wageni waliosaidia kuenea kwa Kiswahili nchini Rwanda ni Daktari Oscar Bauman na Von Gotzën alipopitia.
4. Wakalimani walifanya kazi ngumu ya kuwaelezea Wanyarwanda wengine yaliyokuwa yakizungumzwa katika lugha ya Kiswahili.
5. Kwenye utawala wa ukoloni wa Ubelgiji, matumizi ya lugha ya Kiswahili yalipunguka kwa sababu Wabelgiji walikuwa wanapenda Kifaransa kitumike zaidi katika shughuli nyingi na jambo hili lilitokea baada ya Wajerumani kushindwa Vita vya Kwanza ya Dunia. Tangu wakati huo, Kiswahili kilifumbiwa macho na utawala wa Wabelgiji, kikaanza kupoteza hadhi na nafasi yake katika jamii ya Wanyarwanda. Wengi wa waliokionea walikuwa wakiita lugha hii lugha ya watu wenye vitendo vibovu , majambazi na watu wengine wenye kukosa nidhamu na mienendo mizuri inayomtambulisha kila Mnyarwanda.
6. Mambo yaliyofanywa na Serikali kati ya miaka ya 1962 na 1994 na ambayo yalichangia kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Rwanda ni:
   a. Kukifundisha katika baadhi ya shule
   b. Kukitumia katika matangazo mbalimbali kwenye redio.
   c. 1970 Rwanda na Tanzania ziliamua kushirikiana katika masuala kadhaa ambapo ufundishaji wa Kiswahili sanifu ulipewa kipaumbele.
   d. Serikali na Wizara ya Elimu walijaribu kukuza na kuendeleza ufundishaji wa lugha hiyo, wakaajiriwa walimu, vitabu na vifaa vingine vya ujifunzaji vikanunuliwa.
7. Katika utawala wa Ubelgiji, Kiswahili kilihusishwa na watu wenye vitendo vibovu , majambazi na watu wengine wenye kukosa nidhamu na mienendo mizuri inayomtambulisha kila Mnyarwanda.
8. Wanyarwanda walianza kubadili mtazamo wao kuhusu Kiswahili na kutambua umuhimu wake kuanzia baada ya kupata uhuru.

- Hali hii ilitokana na Rwanda kupata uhuru na Wabelgiji kupoteza madaraka. Na kwenye utawala wa ubelgiji Kiswahili kilifumbiwa macho, na kikaanza kupoteza hadhi na nafasi yake katika jamii ya Wanyarwanda

9. Tangu 1994 serikali ya Rwanda kwa kuimarisha lugha ya Kiswahili ilifanya vitu muhimu vitatu:
   - Somo la Kiswahili hufundishwa katika shule za sekondali zote nchini Rwanda.
   - Nchi yetu ilijiunga na Jumuia ya Afrika ya Mashariki ambapo ndipo kitovu cha matumizi ya Kiswahili.
   - Rwanda imeshaidhinisha kuwa Kiswahili kiwe lugha rasmi kando ya lugha nyingine rasmi zinazotumiwa nchini Rwanda.
5. Funzo ninalopata kutokana na kifungu cha mazungumzo ni kuwa Kiswahili kilipigwa marufuku na Ubelgiji kama njia moja ya kupindua ukoloni wa Ujerumani ambao kwenye utawala wao walikuwa wanatumia lugha hiyo.

### 7.4.2 Msamiati kuhusu Historia ya Kiswahili Nchini Rwanda

**Zoezi la 2:**

*Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia neno sahihi kati ya haya kutoka kifungu chetu cha mazungumzo: wanajivunia, lugha rasmi, kushirikiana, Jumuiya Afrika Mashariki, taarifa ya habari, utawala, walipongeza, matokeo, waliajiriwa, huvuka, kipaumbele.*

1. Serikali ya Rwanda inapendekeza usawa wa jinsia kwa kila ngazi ya utawala.
2. Bwana karekezi **huvuka** mpaka wa Gatuna mara moja kwa wiki kwa ajili ya biashara zake nchini Uganda
3. Wanyarwanda wengi **walipongeza** Serikali ya Rwanda baada ya kuidhinisha kuwa Kiswahili ni lugha rasmi.
4. Wananchi wa Jamhuri ya Tanzania wanapenda **kushirikiana** na Wanyarwanda katika shughuli nyingi za kibiashara.
5. **Jumuia yaAfrika Mashariki** inaundwa na nchi sita: Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya, Tanzania na Sudani ya Kusini
6. **Matokeo** ya mitihani yameshatoka, wanafunzi wote wameyafurahia.
7. **Taarifa ya habari** kutoka redio ya taifa inasema kwamba kila mwananchi ana haki ya kusoma bila ubaguzi.
8. Wazazi wetu walifurahia kuwa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili umepewa **kipaumbele** katika shule zote za Sekondari nchini Rwanda.
9. Wafanyakazi hawa **waliajiriwamwa**ka jana ili wafanye kazi iliyowashinda wengi. Wao **wanajivunia** matunda ya kazi yao na pato lao limeongezeka sana.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, eleleza maneno yafuatayo kulingana na matumizi yake katika kifungu cha mazungumzo mlichosoma:*

1. **Wenyeji:** Watu waliozaliwa na kukulia kwenye mahali fulani; watu wanaoishi mahali fulani hata hawakuzaliwa hapo.
2. **Kupenyeza** : kupitisha kitu mahali pembamba kwa taabu.
3. **Nidhamu**:tabia nzuri inayolingana na maadili.; adabu; staha ; heshima.
4. **Kushirikiana** : kujumuika kufanya jambo na mtu au watu wengine
5. **Uungwana**: hali ya kustaarabika au kuwa muungwana
6. **Kitovu** :chanzo; asili; chimbuko la jambo au kitu.
7 **Kujivunia**: kuonea fahari; kufurahia.
8. **Lugha rasmi**: lugha ambayo inaruhusiwa kutumiwa na raia wa nchi fulani katika shughuli zote za utawala
9. **Kutia bidii:** kutumia nguvu na maarifa ili kazi fulani imalizike vizuri

### 7.4.3 Sarufi: Matumizi ya Kiambishi chenye Dhana ya Masharti "-ngeli-"

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

- Mwalimu awaambie wanafunzi wasome kifungu cha mazungumzo kuhusu historia ya Kiswahili nchini Rwanda kwa kuandika sentensi zenye kutumia kiambishi -ngeli-,
- Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za sentensi zenye kiambishi -ngeli-

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Tunga sentensi tano kwa kutumia kiambishi "ngeli" chenye masharti

- Mwalimu awaambie wanafunzi watunge sentensi zao kwa kutumia kiambishi cha masharti "-ngeli-"

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kamilisheni tungo zifuatazo

1. **Mtoto yule angelizingatia mawaidha ya wazazi wake**, angeliishi bila ukimwi.
2. Watoto wetu wangelifuata mashauri yetu kuhusu usawa **wa jinsia, wangeliishi bila matatizo ya kijamii**
3. Watu wale wangelijua njia za kuifadhi mazingira**, mvua ingelinyesha muda mrefu**
4. Ningelisomea Kiswahili nchini Tanzania**, ningelijua mengi katika sarufi**
5. **Wangelijua sheria vizuri,** wangeliwashtaki watu wale wote kwa makosa yao.
6. Angelitumia muda wake wa kusoma ipasavyo, **angelifaulu mitihani yote.**
7. **Angelijua anwani yake**, angeliandikia mwalimu wake wiki iliyopita.
8. Familia yake ingelikuwa na fedha za kutosha**, ingelinunua gari zuri.**
9. Mariya angelinipatia shauri lake kuhusu uzalishajimali, **ningelitajirika haraka.**
10. **Angelikuwa na mwenendo mwema,** angelipata kura zote za uchaguzi.

### 7.4.4 Matumizi ya lugha

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | A | S | K | A | Z | I | N | I |
| U | I | F | G | D | H | O | | S |
| C | B | S | M | P | E | J | P | E |
| H | A | R | W | M | T | K | Z | R |
| A | L | A | A | A | R | A | Y | I |
| N | U | S | K | O | H | Z | L | K |
| G | G | M | A | N | K | I | Q | A |
| I | H | I | U | I | M | W | L | L |
| A | A | Y | X | J | A | M | I | I |

**Majibu:**

Serikali
Lugha
Mwaka
Maoni
Kiswahili
Jamii
Kazi
Kuchangia
Kaskazini

**Matumizi ya maneno katika sentensi**

1. Nchi ya Uganda inapatikana **kaskazini** mwa nchi yetu
2. Wanyarwanda **anachangia** maoni yao kama njia moja ya kujenga nchi.
3. **Serikali** ya Rwanda inawasidia wananchi wake kwa kuendelea kiuchumi.
4. **Lugha** yetu Wanyarwanda hutuuanganisha na hutumiwa kwa kila sehemu nchini.
5. **Mwaka** uliopita Wanyarwanda walifanya uchaguzi wa rais wa nchi kwa usalama.
6. Katika mkutano wa wabunge, **maoni** ya kila mbunge yanatakiwa.
7. Lugha ya **Kiswahili** ni lugha inayotumiwa na watu wengi katika Afrika ya Mashariki.
8. **Jamii** ya Wanyarwanda huwa na tabia ya kuwapokea vizuri wageni kutoka nje.
9. Wanyarwanda wanahimizwa kufanya **kazi** kama njia moja ya kujenga nchi.

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Maigizo**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wasome kifungu cha mazungumzo kuhusu "Historia ya Lugha ya Kiswahili Nchini Rwanda" kisha wayaigize mbele ya darasa.*

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mambo muhimu yaliyozungumziwa

- Lugha ya Kiswahili ililetwa na Wajerumani nchini Rwanda
- Kiswahili hakikupewa thamani na wanyarwanda wengi
- Baada ya uhuru Kiswahili kilipiga hatua kikafundishwa katika shule za upili na hata katika vyuo vikuu.
- Baada ya mauaji ya kimbari dhindi ya watutsi kilipiga hatua zaidi na kikaingizwa katika lugha rasmi zinazotumiwa nchini Rwanda.

### 7.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:*(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi yao wazungumze kuhusu lugha Kiswahili nchini Rwanda kwa kutoa hoja muhimu zinazobainisha mambo yafuatayo:*

1. Wageni walioleta Kiswahili nchini Rwanda
2. Watu mbalimbali waliojihusisha na maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda
3. Matatizo yaliyojitokeza kukwamisha maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda
4. Hali ya kisasa ya lugha ya Kiswahili nchini Rwanda

### 7.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge kifungu cha habari chenye mada ifuatayo:

"Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili kwa Wanyarwanda."

## 7.5 Muhtasari wa Mada

Mada hii ya kwanza "**Lugha ya Kiswahili**" ina vipengele saba yaani masomo sita yanayohusiana na mada husika. **Somo la kwanza** linaeleza maana ya lugha kama chombo cha mawasiliano. **Somo la pil**i linashughulikia umuhimu wa lugha na kusema kwamba lugha ni mojawapo ya vipengele vya utamaduni wa jamii na tena ni chombo cha utamaduni. **Somo la tatu na la nne** yanatoa maelezo kuhusu matumizi ya lugha katika jamii na kuonyesha faida na hasara ya kutumia lugha moja kwa kusema kuwa lugha kama chombo muhimu katika jamii hufanikisha na kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji wake na umuhimu wa kutumia lugha moja ni kukuza umoja, ushikamano, ushirikiano, na amani miongoni mwa wanajamii wanaotumia lugha hiyo.

Hasara ni kuwa wanajamii hawawezi kuwasiliana na ulimwengu mzima. **Somo la tano na la sita** yanaeleza chimbuko la Kiswahili ni pwani ya Afrika Mashariki na lugha hiyo ilienea kwa kupitia shughuli mbalimbali kama vile safari za kibiashara baina ya watu kutoka pwani hadi bara,uandishi wa vitabu vya Kiswahili, n.k. **Somo la saba** linaonyesha kwamba lugha ya Kiswahili nchini Rwanda ilifanya njia ndefu kutoka mwaka 1890 mpaka leo. Sasa hivi ni lugha rasmi ya kuheshimiwa nchini Rwanda.

Kila kipengele kinaundwa na vipengele vidogo vidogo kama vile maswali ya ufahamu, msamiati, matumizi ya lugha na sarufi.

## 7.6 Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.Mwalimu awasaidie wanafunzi kuwasiliana kwa mazungumzo na maandishi na watu au jamii katika miktadha mbalimbali. Katika mada hii mwanafunzi anapaswa kuelewa na kueleza dhima ya lugha katika jamii, kueleza asili, kukua, na kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

## 1.8 Tathmini ya Mada ya Kwanza

**MaJibu**

1. Mwalimu awawongoze wanafunzi kufanya mazungumzo kuhusu ueneaji wa lugha yaKiswahili katika sehemu mbalimbali.

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Asili ya Kiswahili na chimbuko lake
- Shughuli zilizochangia kukieneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali
- Nchi za Afrika zinazotumia Lugha ya Kiswahili leo hii
- Jinsi Kiswahili kilivyoenea nchini Rwanda

2. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga kifungu cha habari kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili wakitumia hali ya masharti.

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Elimu kuhusu ulimwengu
- Shughuli za biashara
- Mawasiliano
- Ushirikiano

**Mazoezi ya ziada**

### 1.9.1 Mazoezi ya urekebishaji

Majibu ya maswali ya kuwasaidia wanafunzi wenye kiwango cha chini.

Mwalimu awaombe wanafunzi kukamilisha sentensi

- Ningekuwa daktari, ningesaidia mgonjwa.

- Angalizungumza vizuri, angalielewana naye.
- Wanafunzi wasingalijifunza kwa bidii wasingalifaulu mtihani.
- Nisingekuwa na ujuzi kamili, nisingejibu swali hilo.
- Gari lingalikuwa zuri, lingalifika mapema.

### 1.9.2Mazoezi jumuishi

**Swali**

1. 1. Tunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo

**Majibu :**

- Kuenea
- Jumuiya
- Wenyeji
- Lugha rasmi
- Jamii

Mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi sahihi

**Sentensi pendekezi:**

- Baada ya uhuru lugha ya Kiswahili ilienea sana nchini Rwanda.
- Jumuiya ya Afrika Mashariki inaundwa na nchi sita.
- Wenyeji wa pwani walizungumza Kiswahili kwa mara ya kwanza
- Nchini Rwanda kuna lugha rasmi nne ambazo ni pamoja na Kinyarwanda, Kiingereza, Kifaransa na Kiswahili.
- Jamii ya Watanzania inatumia lugha ya Kiswahili.

2. Tumia -**ngeli- katika njia mwafaka.**

   **Kwa mfano** : Hakumuona daktari na hakupona.

   **Jibu** : Angelimuona daktari angelipona

- Hakupewa kitabu ndipo hakufaulu
- Alikataa kunisalimia na sikumjibu.
- Hakufika mapema ndipo hakuniona
- Ulisahau kufunga mlango na tukaibiwa
- Kalamu haikuwepo ndipo hakuandika

**Majibu :**

- Angelipewa kitabu angelifaulu.
- Asingelikataa kunisalimia ningelimjibu.
- Angelifika mapema angeliniona.
- Usingelisahau kufunga mlango tusingeliibiwa.
- Kalamu ingelikuwepo, angeliandika.

**Mazoezi ya nyongeza:**

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi werevu wenye kipaji cha hali ya juu.

**Jibu maswali yafuatayo**:

- Ni nini maana ya lugha?
- Taja nchi za Afrika zinazotumia Kiswahili.
- Asili ya Kiswahili ni ipi ?
- Ni shughuli gani zilizochangia kueneza Kiswahili kwenye sehemu mbalimbali ulimwenguni?
- Kiswahili kina umuhimu gani kwa Wanyarwanda?
- Serikali ya Rwanda ilifanya nini kwa kuimarisha matumizi ya Kiswahili nchini Rwanda?

**Majibu**

- Lugha ni chombo cha mawasiliano kati ya watu.
- Nchi za Afrika zinazotumia Kiswahili ni Tanzania, Kenya, Rwanda, Burundi, Uganda, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Msumbiji, n.k
- Asili ya Kiswahili ni pwani ya Afrika Mashariki.
- Shughuli zilizochangia kueneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali ulimwengunini shughuli ya kibiashara, ukoloni, dini na kuingiliana kwa wageni na Waswahili.
- Umuhimu wa kiswahili kwa Wanyarwanda ni kuwawezesha kuwasiliana na raia wa Afrika ya Mashariki, kufanya biashara nao na kupanga miradi ya kujiendeleza.
- Serikali ya Rwanda iliingiza lugha ya Kiswahili katika shule za Rwanda na kuiidhinisha kuwa mojawapo ya lugha rasmi zinazotumiwa nchini Rwanda.

# MADA KUU YA 2: LUGHA KATIKA SANAA

2

## MADA NDOGO: FASIHI KATIKA KISWAHILI

### Uwezo Upatikanao katika Mada

Kuelewa fasihi katika Kiswahili kwa ujumla kama sanaa inayoshughulikia jamii kwa kurahisisha mawasiliano ndani yake, kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya" LI-YA"

### Ujuzi wa Awali

Kwenye mada ya kwanza kidato cha nne, mwanafunzi alisoma masomo yenye uhusiano na mada hii. Masomo hayo ni: Maana ya lugha, umuhimu wa lugha na lugha katika jamii, historia ya Kiswahili. Masomo haya yatasaidia kuelewa mada kuu hii **"Lugha katika Sanaa"** na mada ndogo " **Fasihi katika Kiswahili**" Mwalimu hatapata muda wake kwa kueleza maana ya lugha na kueleza historia ya Kiswahili.

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro au picha, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza, na katika mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu anawaongoza wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

**Mafunzo kuhusu amani na maadili.**

- Lugha katika sanaa. Watu wakitunga hadithi ambazo zinafundisha watu kuishi kwa amani.
- Kwa kutunga sentensi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye mafunzo yanayohusu amani na maendeleo.

**Mila na desturi na kuzalisha kwa viwango**

Kwa kufanya kazi yoyote, kama kuandika inafaa kuchunguza kama unafuata taratibu za kuandika.

**Elimu isiyo na ubaguzi**

**Makundi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu kama vile:** wanafunzi wenye matatizo ya ulemavu / ulemavu wa mwili, wanafunzi wenye kipaji maalumu katika uwezo wa kujifunza n.k.

Kumbuka kuwa wanafunzi wenye matatizo kama haya ni kama wengine; walikuja shuleni ili wapate maarifa na maadili yanayotakiwa. Kwa hiyo, ni lazima wewe mwalimu uwasaidie ipasavyo. Kama vile:

- Kuwaambia wale wenye tatizo la kutoona au kutosikia vizuri wakae kwenye madawati yaliyoko sehemu za mbele karibu na mwalimu;
- Kuzingatia matatizo ya kila mwanafunzi, kumtega sikio na kuelewa mahitaji yake
- Kupanga kazi maalum zilizoandikwa kwenye karatasi kwa wanafunzi wenye matatizo ya kusikia;
- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kuongea na kuwasiliana na wengine, kupewa muda wa kuongea,...;
- Kuunda makundi ya wanafunzi kutokana na ujuzi na uwezo wao katika kujifunza;
- Kupanga kazi au mazoezi kutokana na makundi ya wanafunzi wenye matatizo maalum ya kielimu;
- Kuwachanganya na wengine katika makundi mbalimbali wanafunzi wenye matatizo ya kimwenendo na kuwachunga ipasavyo;
- Kuwasiliana na wazazi wa wanafunzi wenye matatizo maalumu ili kusaidiana katika kupata suluhisho kwa matatizo yao;
- Kushirikiana na viongozi wa shule na wazazi katika kuweka mikakati thabiti ili lugha ya kufundishia isije ikawa kizuizi kwa masomo yao;
- Kutowasimanga na kutowakashifu wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama vile wale wanaotoka katika familia fukara, wale wenye matatizo ya kielimu, wale wasiosema vizuri na kadhalika;
- Kuwa mwenye wingi wa huruma na kujua kwamba ulemavu wao au matatizo yao yanajitokeza kwa ghafla na hayatokani na utashi wao au matendo yao;
- N.k.

**Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia**

Katika vifungu au katika mifano ya sentensi, mwalimu kwa kutumia lugha anawasaidia wanafunzi kuelewa matumizi ya kondomu na sababu za kuitumia kama kujikinga ukimwi na kuzaa watoto ambao una uwezo wa kutimiza huduma zote kwao.

**Mazingira na maendeleo endelevu**

Mwalimu kupitia mazoezi ya msamiati na sarufi, anaweza kueleza umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa maisha ya watu.

**Usawa wa jinsia**

- Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonesha usawa wa jinsia.
- Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia.

- Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili darasani msiwe na kundi la jinsia moja.

**Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari/kuangamiza.**

Mwalimu kupitia mazoezi ya ufahamu, msamiati na sarufi, anaweza kutoa mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi mnamo mwaka 1994.

### Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada

- Kwa kutangulia mada, mwalimu aulize maswali ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii.
- Wanafunzi wanaweza kushindwa kutoa majibu sahihi mwanzoni, lakini wanaweza kufanikiwa kwa kupitia masomo tofauti, mazoezi, vifungu, na kazi zingine zilizotayarishwa kwenye mada hii.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (kutoka muhtasari: Maarifa na ufahamu,stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | **Dhana ya sanaa** | **Maarifa na ufahamu**: Kufafanua dhana ya sanaa.<br><br>**Stadi**: Kujadili kimazungumzo na umuhimu wa fasihi katika jamii<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: kuipenda na kuikuza sanaa | 8 |
| 2 | **Dhana ya fasihi** | **Maarifa na ufahamu** :Kueleza dhana ya fasihi<br><br>**Stadi:** Kutofautisha tanzu za fasifi simulizi na fasihi andishi<br><br>Maadili na mwenendo:Kutoa mchango katika maendeleo ya utamaduni na uchumi wa raia kwa kutumia tanzu tofauti za fasihi | 13 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | **Sanaa katika jamii** | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza maana ya sanaa katika jamii.<br><br>**Stadi:** Kuhusianisha sanaa na fasihi<br><br>Maadili n mwenendo mwema: Kutumia sanaa kwa maendeleo ya utamaduni. | 8 |
| 4 | **Hadithi** | **Maarifa na ufahamu:**Kueleza maana ya hadithi<br><br>**Stadi:** Kutunga hadithi<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuitumia hadithi kwa malengo chanya na kuepuka matumizi mabaya ya hadithi | 8 |
| 5 | **Methali** | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza maana ya methali<br><br>**Stadi:** Kutunga kifungu kuhusu methali<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Kuzitumia methali ambazo zitasaidia jamii | 6 |
| 6 | Nahau | Maarifa na ufahamu :Kueleza maana ya nahau<br><br>Stadi: Kutunga kifungu kwa kueleza mtumizi ya nahau<br><br>Maadili na mwenendo mwema: Kutumia nahau kwa kujenga jamii ya Wanyarwanda. | 6 |

## SOMO LA 8: DHANA YA SANAA

### 8.1. Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu dhana ya sanaa katika jamii. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yawe na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yawe na uhusiano wa karibu na dhana ya sanaa katika jamii.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu utumiaji wa lugha kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kuunda makundi na kutazama michoro iliyoko katika Kitabu cha Mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.
- Matukio haya yanafanyikia wapi?
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye michoro?
- Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?

### 8.2 Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu atafute zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu andae vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu kwa hiyo yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

### 8.3. Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi

katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watumie makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Itakuwa lazima kila mwanafunzi apewe kazi/mazoezi yake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao wajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wanaweza kumwuliza mwalimu maswali kadhaa naye awajibu. Tena maswali na majibu haya yawe kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- **Majadiliano:** Mbinu hii iwape wanafunzi uwezo wa kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti:** Mbinu hii iwaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Watafute habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Waweze tena kujadiliana na watu wengine wa nje ya darasa lao.

## 8.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watatazama michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza.*

### 8.4.1 Maswali ya Ufahamu

***Majibu ya maswali ya ufahamu***

1. Sanaa ni kazi ya ustadi na ufundi wowote wa kuibusha mawazo yaliyomo katika akili ya binadamu na kuyaonyesha kwa njia mbalimbali
2. Kazi yoyote ya sanaa inapaswa kuwa na uzuri, upya na ujumbe.

| **Msanii** | **Kazi ya sanaa** |
|---|---|
| Mutesi | Mfinyanzi |
| Muteteri | Seremala |
| Majyambere | Msusi |
| Mutesi na Kiza | Wapishi |
| Agasaro na Mugemana | Wahunzi |
| Kabeja | Mwanamuziki |

3. «Ulemavu si ugonjwa». Jadili msemo huu kwa kuhusisha na yale uliyoyasoma katika kifungu cha habari hapo juu. Ulemavu si ugonjwa kwa sababu kuna kazi ambazo zinaweza kufanywa na wenye ulemavu. Kwa mfano katika kifungu cha habari Agasaro na Mugemana ni walemavu wa miguu lakini wanaongoza Chama cha Ushirika cha wahunzi kinachopatikana mjini Rubavu.

4. Methali hii inamaanisha kuwa katika maisha watu lazima wasaidiane kwa kufanya kazi mbalimbali ili waweze kusonga mbele kimaendeleo.

5. Hawatumii udongo wowote kwa sababu udongo wanaotumia ni udongo maluum ambao ni bora kwa shughuli zao kwani unanata na kushikana kwa urahisi. Ni udongo wenye umbile laini.

6. Serikali ya Rwanda inawahimiza mafundi kujiunganisha katika vyama vya Ushirika vya kuzalisha mali ili waweke nguvu pamoja kwa kufanya kazi zao pamoja na kuwezesha serikali kufuatilia karibu kazi zao ili iweze kuwasaidia panapohitajika msaada wake.

7. Vijana wanaokaa bila kufanya kazi ninaweza kuwapa ushauri wa kutafuta kazi ya sanaa wanayoiweza bila kusema kuwa kazi hii au ile si ya heshima, kisha wakajiunga pamoja katika vyama vya ushirika vya kuzalisha mali..

8. Sanaa ni muhimu katika jamii kwa sababu

- Inaboresha na kurahisisha maisha ya jamii kwa kuipa zana mbalimbali za kutumia.
- Inainua kiwango cha uchumi wa jamii kwa sababu sanaa huletea kipato wasanii na jamii kwa ujumla.

9. Kwa kuimarisha vipaji vya wasanii na kulinda kazi zao serikali ya Rwanda ilifanya mambo yafuatayo:

- Kuwahimiza wasanii kujiunga pamoja katika vyama vya ushirika vya kuzalisha mali.
- Kujenga nyumba za maonyesho ya kisanaa (Mfano: Jumba la makumbusho la Rwesero/Nyanza).
- Kuandaa maonyesho na matamasha ya kumulikia na kuuzia kazi za sanaa.
- Kuweka taratibu zinazolinda haki za wasanii na kazi zao.

### 8.4.2 Msamiati kuhusu Sanaa na Manufaa yake

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**1. Ustadi :** hali ya kuwa na ujuzi na maarifa katika kufanya kitu au kazi, ubingwa.

**2. Umbo :** mkao wa kitu kilivyoumbwa au kilivyoundwa ; sura.

**3. Karakana :** mahali palipo na mitambo ya kutengenezea vitu.

**4. Kuburudisha :** kufanya mtu astarehe.

**5. Chama :** kikundi cha watu waliojiunga pamoja kwa lengo la kutekeleza matakwa yao ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, n.k.

**6. Shabiki :** mtu mwenye kupenda sana jambo au kitu fulani ; mpenzi.

**7. Madini:** kitu kinachochimbwa ardhini kama vile chuma, shaba, bati, dhahabu, almasi, chumvi, n.k.

**8. Kutumbuiza :** kuburudisha au kustarehesha kwa muziki au nyimbo.

**9. Fuawe :** chuma anachotumia mhunzi kwa kuwekea chuma anachofua.

**10. Jifya :** jiwe moja kati ya mawe matatu au zaidi yatumiwayo kutelekea chungu au sufuria jikoni ; figa.

**Mifano ya sentensi**

**1. Ustadi :** kazi ya msanii huyu ilionyesha ustadi wa hali ya juu.

**2. Umbo :** mfinyanzi alichukua udongo na kuupa umbo la kondoo.

**3. Karakana :** Kijijini kwetu kuna karakana kubwa ya maseremala.

**4. Kuburudisha :** Bendi ya muziki ya Impala ilijitayarisha kwa kuburudisha wakazi wa jiji la Kigali.

**5. Chama :** Chama kile cha kisiasa kinahimiza utunzaji bora wa mazingira.

**6. Shabiki :** Kalisa ni shabiki wa timu ya « Amavubi ».

**7. Madini :** Uchimbaji wa madini huharibu mazingira yetu.

**8. Kutumbuiza :** Jana mwanamuziki analitumbuiza wafuasi wake na kuwahimiza kuishi kwa amani.

**9. Fuawe :** Niazime fuawe ili nitengeneze majembe nipeleke sokoni.

**10. Jifya :** Katika mila za kinyarwanda, kupasua jifya ni mwiko.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Nzuri na ya gharama kubwa
2. Wanajisifu
3. Msusi
4. Atafunga pingu za maisha
5. Aliajiriwa
6. Makamu
7. Bendi
8. Jifya
9. Wahenga
10. Kitita cha fedha

***Zoezi la 4: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1i, 2h, 3a, 4g, 5d, 6c, 7j, 8e, 9b, 10f.

### 8.4.3 Sarufi : Nomino za Ngeli ya LI-YA

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Kundi la wanamuziki liliwatumbuiza watu jana. (li-)
2. Mashirika haya yaliundwa na vijana mbalimbali. (ya-)
3. Koti hilo limeshonwa na mshonaji hodari. (li-)
4. Makabati yalitengenezwa na maseremala. (ya-)
5. Gari zuri lile lilitengenezewa nchini Rwanda. (li-)
6. Mifano ya sentensi
7. Kabati kubwa lilitenegenezwa.
8. Magunia hayo yalitoboka.
9. Darasa hilo litajengwa na waashi hodari.
10. Dede limejazwa mafuta.
11. Makanisa haya yanahimiza wafuasi wao umoja na maridhiano.

***Zoezi la 6: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| Kabati | makabati |
| Koti | makoti |
| Bega | mabega |
| goti | magoti |
| Panga | mapanga |
| Janga | majanga |
| Jangwa | majangwa |
| Jina | majina |
| Jibu | majibu |
| Jembe | majembe |

- Majina haya huchukua **ma-** yanapowekwa katika wingi.

***Zoezi la 7: (Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Kabati lilitengenezwa na seremala yule.
   - **Makabati yalitengenezwa na maseremala wale.**
2. Koti hili litafuliwa.
   - **Makoti haya yatafuliwa.**
3. Bega linamuuma.
   - **Mabega yanawauma.**
4. Goti lilipata jeraha.

- **Magoti yalipata majeraha.**

5. Panga hili litatumiwa kufyekea kichaka kile.
   - **Mapanga haya yatatumiwa kufyekea vichaka vile.**
6. Janga la ukimwi linasumbua sana ulimwengu.
   - **Majanga ya ukimwi yanasumbua sana ulimwengu.**
7. Jangwa linasababishwa na ukataji wa miti.
   - **Majangwa yanasababishwa na ukataji wa miti.**
8. Jina hili linanitambulisha.
   - **Majina haya yanatutambulisha.**
9. Jibu sahihi lilitolewa kwa swali hili.
   - **Majibu sahihi yalitolewa kwa maswali haya.**
10. Jembe hili lilinolewa jana.
    - **Majembe haya yalinolewa jana.**

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Mifano:**

1. Maji safi yanahitajika maishani.
2. Mazingira haya yanapaswa kuhifadhiwa vema.
3. Mawaidha hayo yalitolewa na mwalimu mkuu.
4. Mafuta mengi ndani ya vyakula yanasababisha ugonjwa wa saratani.

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Sisi tuna malengo ya kupambana na majangwa.
2. Wewe utaondoa jani hilo kavu.
3. Jani lilikauka.
4. Mashavu yananiuma.
5. Vijana warefu walibeba makasha kwenye mabega.
6. Madebe hayo yanavuja kwa sababu yametoboka.
7. Mtoto mmoja alilazwa hospitalini kwa sababu ya tatizo la pafu.
8. Daftari linapaswa kuhifadhiwa vizuri.
9. Matarumbeta yalitumiwa wakati wa burudani.
10. Mashirika ya reli yaliagiza magarimoshi makubwa.

### 8.4.4 Matumzi ya Lugha : Dhana ya Sanaa

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaagize wanafunzi, katika makundi yao, kutaja aina moja ya sanaa na kujadili kuhusu namna ambavyo wasanii huweza kutimiza masharti yanayopatikana katika kazi yoyote ya kisanaa: uzuri, ujumbe na upya.*

**Jambo la kuzingatiwa:**

- Kueleza uzuri wa kazi ya sanaa.
- Kueleza upya wa sanaa.
- Kueleza ujumbe wa sanaa.
- Kueleza uwiano wa uzuri, upya na ujumbe katika kazi ya sanaa.

### 8.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaagize wanafunzi, katika makundi yao ya watatu watatu, kujadiliana kuhusu u*muhimu wa vyama vya ushirika vyenye kuzalisha mali kama mojawapo ya njia za kuondoa tatizo la ukosefu wa kazi pamoja na uzururaji miongoni mwa viajana.*

**Mambo ya kuzingatiwa:**

1. Kueleza maana ya vyama vya ushirika vyenye kuzakisha mali.
2. Kueleza umuhimu wa vyama vya ushirika vyenye kuzalisha mali.
3. Kuonyesha mchango wa vyama hivi kwa kupambana na ukozefu wa kazi kwa vijana.

### 8.4.6 Kuandika

**Zoezi la 12: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu amwambie kila mwanafunzi kutunga kifungu kuhusu mada ifuatayo:

"Uwasilishaji wa Mawazo ya Binadamu ni wa Njia Nyingi Mno."

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Kueleza maana ya uwasilishaji wa mawazo.
- Kutaja mifano ya njia za uwasilishaji wa mawazo ya binadamu.

## SOMO LA 9: DHANA YA FASIHI

### 9.1 Utangulizi/Marudio

Baada ya mwalimu kuamkiana na wanafunzi, mwalimu awaulize maswali machache kuhusu somo lililopita. Mwalimu awaulize kwanza mambo muhimu wanayoyakumbuka kwa ujumla, kisha ajichagulie maswali maalum ya kujibiwa na wanafunzi. Ajaribu kuwashirikisha wanafunzi wote iwezekanavyo na kuwachangamsha kwa wimbo au shairi dogo au atafute namna nyingine ya kuwaingiza katika somo jipya hivi wakifurahi. Baadaye, mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwapa kazi hii:

- *Eleza wahusika unaowaona kwenye picha hii.*
- *Wahusika hao wapo wapi?*

- *Eleza shughuli zinazoendelea kwenye mchoro huo.*

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na msimamizi wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine. Mwisho wake mwalimu asahihishe wanafunzi ikiwa inatakiwa kufanya hivyo

## 9.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufika kwenye malengo ya somo lake. Mwalimu atumie jumla au mojawapo ya vifaa hivi:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Vitabu vya hadithi fupi, riwaya, shairi na tamthilia,
- Michoro ya kisanii,
- Kompyuta,
- Projekta ya kuonyesha picha kutoka mtandao ikiwa ipo
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Mwalimu anaweza kutafuta zana nyingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake kuwa na vifaa mbalimbali. Mwalimu kwa ubunifu wake anaweza kuandaa vifaa vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo.

## 9.3 Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mbinu za kumfikisha mwalimu kwenye malengo ya somo lazima zitafutwe na mwalimu. Hapa chini kuna mbinu tofauti za kurahisisha maendeleo ya somo darasani. Ni vizuri kwa mwalimu kutafuta mbinu zingine za kuwasaidia wanafunzi kusoma vilivyo lakini atilie mkazo mbinu hizi:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Mwalimu awape wanafunzi kazi ya kufanyiwa katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne. Ni vizuri kutozidi idadi ya wanafunzi watano katika kundi moja ili uzembe ukose nafasi kabisa. Mwalimu achunguze mara kwa mara kazi inafavyonyika. Wakati wowote, mwalimu atumie muda vizuri na atoe msaada ambao unatakiwa. Makundi yaundwe na mchanganyiko wa wasichana na wavulana, na wanafunzi wenye shida za kibinafsi kama walemavu na wengineo. Ni vizuri kwa kazi ya makundi kumulikwa kwa darasa ili wanafunzi wote wajue mafanikio ya wanafunzi wenzao.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Katika somo hili, kuna mazoezi ya kutosha ambayo ni ya kufanywa kibinafsi kwa ajili ya kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. Hata hivyo, mwalimu awape wanafunzi mazoezi hayo wakiwa katika makundi.

- **Maswali na majibu:** Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na kuyajibu wenyewe, wanafunzi kwa wanafunzi. Hivi ni kusema kwamba maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kupitisha maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi peke yao. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa na wanafunzi, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu ajibu ikiwa inatakiwa.
- **Maelezo ya mwalimu:** Katika kazi yake ya ubunifu, mwalimu atambue ujuzi unaohitaji mwelekeo na maelezo yake binafsi. Mwalimu atahakikisha kwamba kasoro zote zinatoweka iwezekanavyo. Ni muhimu sana kufanya hivi kwa kuwapa pia wanafunzi fursa ya kutoa maoni yao kuhusu maelezo yake.

## 9.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Angalia kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo***

- Eleza wahusika unaowaona kwenye picha.
- Wahusika hao wapo wapi? Wanafanya nini?
- Unaona shughuli zipi kwenye picha?

### 9.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Kifungu cha habari kinazungumzia somo la fasihi.
2. Mwalimu anayezungumziwa katika kifungu cha habari ni mwerevu, mzuri na mpole. Yeye anaheshimu watu wote na tabasamu yake wakati wake kuwasiliana na watu hao.
3. Mambo matano yanayoweza kugusiwa katika kazi ya fasihi ni matatizo, mitazamo, migogoro, imani, na shughuli mbalimbali zilizopo katika jamii.
4. Wanafunzi waliamua kujifunza vizuri lugha ya Kiswahili kwa kuwa somo la dhana ya fasihi liliwapendeza wote, na vilevile walihitaji kutumia lugha hii kisanaa?
5. Fasihi hutumia lugha kisanaa. Kila mtu anayejishughulisha na utunzi wa kazi ya fasihi huitazama kwanza jamii yake na kueleza mambo yote ambayo yanatendeka katika jamii hiyo kwa njia ya lugha. Anatumia lugha namna isiyo ya kawaida, yenye kuvutia wengi katika kuwasilisha ujumbe wake.
6. Fasihi ni kioo na mwavuli kwani fasihi hupata mambo yatendekayo katika jamii ; maovu na mema, na kuyawasilisha kwenye jamii hiyo kwa njia ya lugha ya kisanaa ambayo huelemisha wanajamii hivi wakiburudika na kustarehe. Papo hapo huwaonya watenda maovu kuacha maovu yao, na kuwahimiza watenda mema kuendeleza matendo yao mazuri.

7. Fasihi inahusiana na utamaduni : Fasihi huilinda jamii kwa kuhifadhi na kueleza vitendo vyake, vitendo vizuri vikihimizwa na kuchochewa, vitendo vibaya vikikatazwa. Mwanafasihi hutumia lugha kwa kujulisha jamii mengi yaliyopo katika utamaduni wake.
8. Kwa sasa msimulizi anafanya kazi ya kuandika vitabu.
9. Fasihi inahusiana na utamaduni kwa kuwa fasihi husawiri na kuakisi jumla yote ya namna ya maisha ya watu. Kwa namna hii, fasihi huakisi utamaduni wa jamii.
10. Fasihi ni sanaa ambayo hutumia lughya kushughulikia masuala yanayomhusu binadamu. Inazungumzia na kuonyesha maisha ya jamii, kwa kuelezea mambo yote yaliyomo katika jamii hiyo yaani matatizo, mitazamo, migogoro, imani, na shughuli mbalimbali za kijamii.

### 9.4.2 Msamiati kuhusu Dhana ya Fasihi

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu, tungeni sentensi zenu kwa kutumia maneno haya:*

1. Hisia: Msanii anaweza kuwasilisha hisia zake kwa kuwastarehesha watu.
2. Kuvutia: Mwalimu yule hutumia lugha ya kuvutia ili atuelimishe au atusahihishe.
3. Mtenda maovu: Tenda wema wewe! Usiwafuate watendamaovu kwani wanaharibu.
4. Kuburudisha: Kama mziki, hadithi nayo inaweza kuburudisha jamii.
5. Kudhihirisha: Kazi za wanafunzi hawa zinadhihirisha kwamba ni werevu.
6. Kuhimiza: Jumamosi mkurugenzi alituhimiza kufanya usafi ili tuangalie michezo.
7. Kioo: Eti mfanyabiashara! Kioo mita moja ni faranga ngapi?
8. Mwavuli: Mwavuli unasaidia sana wakati ambapo mvua inanyesha.
9. Mwanafasihi: Nitakapomaliza masomo yangu, nitakuwa mwanafasihi mkongwe.
10. Kuchochea: Katika shirika letu tunachochea tabia nzuri na kukataza tabia mbaya ili tuweze kufanikiwa katika mipango yetu yote.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia maneno yanayofuata: sanaa, mwanafasihi, jamii, utamaduni, imani, mtazamo, wanajishughulisha, fasihi, maovu, waliamua.*

1. **Mwanafasih**i anatarajiwa kutumia vizuri vipaji vyake vya kisanaa.
2. Sote tunalazimika kukuza **utamaduni** wa usafi katika kazi.
3. Mimi nitaendelea na masomo ya **fasihi** chuoni.
4. **Mtazamo** wake kuhusu michezo shuleni ni tofauti na ule wa mkurugenzi.
5. Fasihi kama **sanaa** inaweza kumpa mtu faida na kumtunza.
6. Baada ya majadiliano makali waliamua kusikilizana kabisa kwa ajili ya kuishi kwa amani kati yao.

7. Kila mwanadamu anatarajiwa kuepuka mambo **maovu.**
8. Watu wengi ambao tuliosoma pamoja **wanajishughulisha** na kazi mbalimbali za kisanaa wakitumia lugha ya Kiswahili.
9. Ninapenda **jamii** yetu ya Rwanda kwani inapiga marufuku ubaguzi wowote.
10. Ndugu zangu wana **imani** kwamba watamaliza masomo yao na kuwa wasanii maarufu.

### 9.4.3 Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Idadi katika Ngeli ya LI-YA

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Someni kifungu cha habari hapo juu kuhusu "Dhana ya fasihi" huku mkiandika vivumishi vya idadi vilivyotumiwa.*

Vivumishi vya idadi vilivyotumiwa katika kifungu cha habari ni hivi vifuatavyo: (madarasa) matano na (madaftari) matatu.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Andika sentensi zifuatazo kwa kutumia vuvumishi vilivyomo ndani ya mabano***

1. Mawe **matatu** yamewekwa kando ya barabara.
2. Madirisha **matano** yamefunguliwa. Meno **mawili** yameng'oka.
3. Matunda **manane** yameimeiva.
4. Mabega **manne.**
5. Madarasa **matatu.**
6. Taja mambo **matatu** yanayozingatiwa katika kazi ya fasihi. (tatu)
7. Makoti **matano** yameuzwa na mfanyabiashara huyu. (tano)

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, chunguzeni sentensi zifuatazo, kisha mueleze muundo wa vivumishi vilivyotumiwa.*

1. Jibu moja limepatikana.
2. Mawe sita yameanguka chini.
3. Matunda saba yameiva.
4. Madarasa tisa yanasafishwa.
5. Makoti kumi yatashonwa.

Muundo wa vivumishi vilivyotumiwa ni huu: Vivumishi vya idadi tulivyoona hapo juu, tarakimu **moja, sita, saba, tisa** na **kumi** havichukui kiambishi ma- katika wingi. Vivumishi hivi hubaki vile vilivyo yaani **moja, sita, saba, tisa**, na **kumi.**

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Tungo anazoweza kutunga mwanafunzi ni hizi zifuatazo zenye vivumishi vya idadi isiyo dhahiri***

1. Kasri la mfalme lina mapambo **lukuki** ya kuvutia.
2. Magonjwa **kadhaa** yamebainishwa kuwa hatari zaidi.
3. Matunda **machache** yameoza.
4. Maembe **mengi** yamenunuliwa

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kanuni za Mungu ni **kumi.**

Mwaka una miezi kumi na **miwili.**

Ni rahisi kujua kwamba wiki moja ina siku **saba.**

Watu wa zamani walipika kwa kuweka chungu juu ya mafiga **matatu.**

Wanyarwanda huwapa majina watoto wao katika siku ya **nane.**

Nchi ya Rwanda ina majimbo/mikoa **minne na mji wa Kigali.**

Nchi yetu inapakana na nchi **nne.**

Dunia ina mabara **matano.**

Rwanda ina milima ya volkeno **mitano.**

Katika mchezo wa soka, timu moja inakuwa na wachezaji **kumi na mmoja** uwanjani.

Siku moja ina saa **ishirini na nne.**

### 9.4.4 Matumizi ya Lugha: Dhana ya fasihi

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu amwelekeze mwanafunzi kutafuta majibu kwenye maelezo muhimu kuhusu fasihi.

**Majibu**

1. Fasihi ni sanaa ya lugha, inayoshughulikia masuala yanayomhusu binadamu, matatizo yake, ndoto zake, matumaini yake, migogoro yake na mazingira yake.
2. Mifano ya kazi za fasihi ni kama vile: hadithi, methali, vitendawili, riwaya , tamthilia, mashairi , nyimbo.
3. Chombo anachotumia ni lugha.
4. Maudhui ya fasihi huhusu masuala mbalimbali yaliyomsukuma msanii kisana kazi yake ya fasihi. Hujumuisha mawazo aliyonayo, mafundisho, migogoro, na hata falsafa.
5. Kuna fasihi simulizi na fasihi andishi.
   - Fasihi simulizi huhusika na hadithi, nyimbo, vitendawili, methali, nahau, mashairi.
   - Fasihi andishi huhusika na riwaya, tamthilia, ushairi, n.k.

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutafuta majibu ya maswali waliyopewa katika kitabu cha mwanafunzi.*

### 9.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wanne, wanafunzi wajadiliane kuhusu "Uhusiano kati ya Fasihi na Kazi Zingine za Kisanaa."*

Majadiliano yao yajikite kwenye masharti ya sanaa:

1. Uzuri
2. Upya
3. Umuhimu

### 9.4.6 Kuandika

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge kifungu cha habari chenye kichwa kifuatacho:

**"Fasihi ni kioo cha jamii"**

## SOMO LA 10: Dhima ya Sanaa katika Jamii

### 10.1 Ujuzi wa Awali

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu sanaa katika jamii. Mwalimu awaulize wanafunzi somo walilojifunza wakati uliopita. Wanafunzi wajibu maswali husika kisha mwalimu awaulize wanafunzi wanachojua kuhusu fasihi katika jamii. Awaulize maswali yafuatayo:

- Mnadhani fasihi ina umuhimu gani katika jamiii?
- Mnaposimulia hadithi nyumbani kwenu mnadhamiria nini?
- Nyimbo ni mojawapo ya utanzu wa fasihi unaoweza kuonya na kukosoa jamii husika. Jadili.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake kwa kutumia njia shirikishi ili awawezeshe wanafunzi, katika makundi, kujadiliana kuhusu umuhimu wa fasihi katika jamii kisha afanye chochote ili wanafunzi wafikie kile kiwango cha kujieleza wakizingatia fasihi na umuhimu wake. Kiwango kinachohitajika ni kile kinacholengwa na muhtasari wa somo la Kiswahili, kidato cha nne.

### 10.2 Zana na vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Picha ,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,

- Magazeti mbalimbali,
- Ubao, chaki,
- Michoro ya watu wanaowasiliana kuhusu umuhimu wa fasihi, n.k.

Mwalimu atafute zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Kwa wale wanafunzi walio na ulemavu fulani watahitaji vifaa maalum vitakavyowasaidia kukidhi mahitaji yao. Mwalimu kama mbunifu aweze kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake. Hapa Mwalimu ajibunie vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyokosekana kutoka uongozi wa shule.

## 10.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika kipindi hiki, mwalimu atafute mbinu mwafaka zinazomwezesha kufanikisha malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atayazingatia yafuatayo:

- **Njia shirikishi:** Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi na humwezesha mwanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa hapa ni kumfanya mwanafunzi ashiriki katika shughuli zote darasani. Hivi hutokana na kwamba mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mwalimu, kwa kufanya kazi na mazoezi yaliyomo ndani ya kitabu cha mwanafunzi.
- **Njia isiyoshirikishi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za mwanafunzi.Ni lazima kila mwanafunzi apewe kazi/zoezi lake binafsi ili naye afikie kile kiwango chake cha umilisi wa lugha baada ya kufanya zile kazi katika makundi. Hapa mwanafunzi ajisomee kifungu cha habari, atunge sentensi zake binafsi kwa kutumia msamiati mpya.
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao wajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi waweze kumwuliza mwalimu naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe. Mwalimu awaelekeze pale ambapo wanahitaji maelezo yake au mwongozo. Mwalimu akosoe makosa yanayofanywa na wanafunzi.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo, mwalimu yeye awe mwelekezi na msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 10.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watatazama michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza*

### 10.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Kutathmini na kutoa maelezo ya mashindano. Jopo lenyewe lilikuwa limeundwa na watu watatu : wanaume wawili na mwanamke mmoja
2. Walipongezwa kwa kuwa walicheza ngoma kwa ustadi mkubwa.
3. Waliambiwa kufanya mchoro wa ng'ombe watatu pamoja na mchungaji wao. Aliyeshinda ni msichana
4. Ulitokana na ajali ya gari.
5. Maudhui ya wimbo wake yalielekea kuwasifu wazazi.
6. Maudhui yalikuwa yanalenga umuhimu wa fasihi katika jamii
7. Watunzi wa mashairi, watambaji hadithi, waigizaji wa michezo mbalimbali kama vile wacheshi.
8. Umma uliweza kuelimika na kufungua macho na kutambua udhaifu uliojitokeza katika jamii na mambo mbalimbali yaliyotakiwa kurekebishwa na kunyooshwa katika jamii yao.
9. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha ili kufikisha ujumbe wake kwa jamii inayokusudiwa.
10. Ni kutokana na umuhimu wake katika jamii: Fasihi huendeleza, huhifadhi na kurithisha utamaduni, mila na desturi za jamii na pia kwamba fasihi huwaelimisha wanajamii kwa njia moja au nyingine.
11. Ni kusema kwamba michezo si uadui bali nguzo ya kuburudisha na kukuza ujamaa, kwa hivyo unaposhindwa usigombane na mshindi.

### 10.4.2 Msamiati kuhusu Sanaa katika Jamii

**Zoezi la 2 :** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi, elezeni maana ya maneno yafuatayo kulingana na muktadha wa matumizi yake katika kifungu cha habari mlichosoma, kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno hayo.*

1. Umahiri: uhodari
2. Umati : watu wengi sana
3. Jopo : paneli
4. Mashindano : mapambano baina ya pande mbili au zaidi
5. Kuthamini : kutia kitu gharama
6. Kuahidi : kutoa ahadi
7. Kuburudisha : kufanya mtu astarehe kwa muziki, michezo n.k.
8. Kuelimisha : kumpatia mtu elimu
9. Kuhifadhi : kuweka mahali pa salama
10. Desturi : jambo la kawaida linalotendwa kila siku

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watumie mishale kwa kuoanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B. Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kwamba wanafunzi wake wanafanya kazi katika makundi.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. shairi | Mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalumu wa lugha ya mkato katika usemi |
| 2. vipawa | Uwezo mtu aliozaliwa nao ambao humwezesha kufanya jambo fulani vizuri. |
| 3. tamasha | Furaha kubwa inayohusisha michezo na burudani inayofanywa kusherehekea jambo fulani |
| 4. jukwaa | Sehemu iliyoinuliwa ndani ya jengo kubwa au katika uwanja ambayo hutumika kuonyesha michezo au kutolea hotuba |
| 5. umahiri | Uhodari wa kufanya jambo fulani. |
| 6. fasihi | Somo linalohusiana na tungo za sanaa kama vile mashairi, riwaya, tamthiliya, tenzi, semi, vitendawali, hadithi na ngano. |
| 7. mashabiki | Watu wenye kupenda sana jambo au kitu fulani. |
| 8. kuhudhuria | Kuwako mahali penye shughuli fulani k.v. mkutanoni au kwenye sherehe. |
| 9. mawaidha | Maneno ya maonyo au mafunzo, mashauri. |
| 10. tumbo joto | Hali ya kuwa na woga |
| 11. umati | Watu wengi sana |
| 12. uwanja umefurika | Uwanja umejaa watu wengi kupita kiasi. |

### 10.4.3 Sarufi: Nomino za ngeli ya LI-YA na vivumishi vya kumiliki.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wawili, wasome kifungu cha habari hapo juu kuhusu "Sanaa katika Kamii", kisha waandike sentensi zenye nomino za ngeli ya LI-YA

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge sentensi tano zenye nomino za ngeli ya LI-YA.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi waandike wingi wa sentensi hapa chini, kisha watoe maelezo yao kuhusu muundo wa umoja na wingi wa nomino zilizotumiwa.*

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Jembe langu limepotea. | Majembe yangu/yetu yamepotea |
| 2. Janga kubwa limesababisha maafa. | Majangamakubwa yamesababisha maafa |
| 3. Jaribio la leo limesahihishwa. | Majaribio ya leo yamesahihishwa |
| 4. Jeshi lao lina askari wengi. | Majeshi yao yana askari wengi |
| 5. Jeraha lake lina uchafu sana. | Majeraha yake/yao yana uchafu sana |
| 6. Jambo hili liliwafurahisha wengi. | Mambo haya yaliwafurahisha wengi |
| 7. Jicho lake linaoona mbali sana. | Macho yake/yao yanaoona mbali sana |
| 8. Jiwe langu lina thamani kubwa. | Mawe yangu/yetu yana thamani kubwa |
| 9. Jino lako limeng'oka? | Meno yako/yenu yameng'oka |
| 10. Jiko langu limeharibika. | Meko yangu/yetu yameharibika |

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu, wachunguze mifano ya sentensi hapa chini, kisha waeleze aina za maneno yaliyopigiwa mstari.*

1. Nilikosa koti **langu**. (Kivumishi cha kumiliki)
2. Magari **yao** yameibwa. (Kivumishi cha kumiliki)
3. Nitakununulia koti **jingine**(kivumishi cha pekee)
4. Majengo **yote** yalijengwa karibu na ziwa. (Kivumishi cha pekee)
5. Nipe embe **lolote** la kula. (Kivumishi cha pekee)

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, watunge sentensi zao tano kwa kutumia nomino za ngeli ya LI-YA pamoja na vivumishi vya kumiliki*

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Wanafunzi waandike sentensi zifuatazo kati wingi***

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Koti langu limechafuka. | Makoti yangu yamechafuka |
| 2. Shirika lako linajulikana sana. | Mashirika yako yanajulikana sana |
| 3. Gari lake ni la kifahari. | Magari yake ni ya kifahari |
| 4. Jumba letu linapendeza | Majumba yetu yanapendeza |

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Wanafunzi waandike sentensi zifuatazo katika hali kanushi***

1. Koti langu halinipendezi
2. Gari lake halijapata ajali.

3. Mashirika yenu hayataimarishwa.
4. Mavuno yetu hayajakuwa mazuri mwaka huu.
5. Jumba lake halijakarabatiwa.

### 10.4.4 Matumizi ya lugha: Dhima ya Fasihi

**Zoezi la 11: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu "Madhara yanayoweza kujitokeza katika jamii, fasihi inapotumiwa vibaya".Mwalimu awaongoze wanafunzi katika mjadaa husika. Taratibu zote za mjadala zizingatiwe.*

### 10.4.5 Kuzungumza na Kusikiliza

**Zoezi la 12: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi wabainishe dhima ya lugha kama ilivyodhihirishwa katika sehemu ya maelezo yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi:

1. Kuelimisha jamii
2. Kuburudisha jamii,
3. Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii,
4. Kudumisha na kuendeleza lugha
5. Kuunganisha jamii,
6. Kukuza uwezo wa kufikiri,
7. Kumtajirisha msanii,

### 10.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 13: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge kifungu cha habari chenye mada hii:

*"Umuhimu wa fasihi katika jamii".*

## SOMO LA 11: Hadithi

### 11.1 Ujuzi wa awali

Mwalimu aulize wanafunzi maswali kuhusu somo lililotangulia na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameshirikishwa kuyajibu maswali haya. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu awaambie wanafunzi wachukue vitabu vya Kiswahili na kutazama mchoro kwenye ukurasa husika, kisha awaulize wanafunzi maswali kuhusu mchoro walioutazama. Mwalimu awaulize maswali yafuatayo:

- *Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.*
- *Unadhani watu hawa wanafanya nini?*
- *Tukio hili linatukia wapi?*
- *Unafikiri tukio hili linatukia majira ya saa ngapi?*
- *Kuna uhusiano wowote kati ya kichwa cha habari na mchoro?*

Kutokana na maswali yaliyoulizwa na majibu yaliyotolewa, mwalimu aombe wanafunzi kufumbua somo linahusu nini.

### 11.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

- Mchoro wa wazazi wanaosimulia hadithi kwa watoto wao.
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu, kalamu, chaki na ubao.

### 11.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne kulingana na jumla ya idadi ya wanafunzi darasani. Wanafunzi wafanye kazi wanayopewa na mwalimu kila mwanafunzi ashiriki kwa kutoa mchango wake katika kujibu maswali waliyopewa. Mwalimu achunguze kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yahusishe wasichana na wavulana.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:**

Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya kinafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake bila msaada wa mwalimu au mwanafunzi mwenzake.

- **Mihadhara:** Mwalimu atumie njia hii kwa kuwapa wanafunzi fursa ya kutumia lugha. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao ili watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao iwezekanavyo. Mwalimu aongoze mihadhara hii na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wameshirikishwa kwa kutega sikio na kuuliza maswali. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wameshindwa kuyajibu vilivyo.

- **Maelezo ya mwalimu:** Mwalimu kwa ujuzi wake ahakikishe kwamba maelezo anayotoa yanawawezesha wanafunzi kuelewa somo wanalojifunza. Ikiwa mwalimu anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi vya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

## 11.4.Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watatazama michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza*

### 11.4.1 Maswali ya ufahamu

1. Wahusika katika hadithi hii ni Sungura na Kobe
2. Tukio hili lilitukia msituni.
3. Kobe alitambua kwamba Sungura alimuamkia kwa kutaka kumchokoza na kumdharau.
4. Mashabiki hao ni kina fisi, tembo, twiga, nyati, nyani, ngorombwe, pundamilia na chui.
5. Waamuzi wa shindano hili walikuwa kina Sokwe na Farasi.
6. Sungura alikuwa na uhakika kwamba Kobe hawezi kumshinda pamoja na mwendo wake wa polepole.
7. Sungura alishindwa na majivuno yake.
8. Baada ya kushindwa, Sungura alimuomba Kobe msamaha
9. Sungura ana tabia mbaya zenye majivuno, kudharau wengine na kujisifu wakati Kobe yeye yu mpole, mtulivu na mkakamavu.
10. Nimejifunza kwamba si vizuri kumdharau mtu yeyote. Ni lazima watu wote waheshimiane bila ubaguzi wowote.

### 11.4.2 Msamiati kuhusu Hadithi

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika zoezi hili wachunguze maana za maneno waliyopewa kulingana na jinsi yalivyotumiwa katika kifungu cha habari. Wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili panapohitajika.

***Maana ya maneno***

1. **Kiburi:** hisia za mtu kujiona yeye ni bora na kutosikiliza anachoambiwa na wengine.
2. **Hamu:** hali ya kutaka kitu fulani, kutaka sana
3. **Wajibu:** jambo linalomlazimu mtu kulitimiza
4. **Kukata tamaa:** kupoteza tumaini.
5. **Haikufua dafu:** haikufaulu, haikufanikiwa
6. **Kikomo:** mahali pa kumalizia mwisho
7. **Kupongeza:** kumuambia mtu maneno ya kufurahikia mafanikio aliyoyapata.
8. **Kuunga mkono**: kujiunga na mtu katika kazi yake au mradi wake

9. **Ilipowadia:** ilipofika, wakati ulipotimia
10. **Dhahiri:** waziwazi, bayana.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi wawili wawili wafanye zoezi hili na mwalimu achunguze kwamba wanatumia maneno ipasavyo.

**Majibu**

1. *Wajibu*
2. *ilipowadia*
3. *haikufua dafu*
4. *dhahiri*
5. *hamu*
6. *kiburi*
7. *kikomo*
8. *kata tamaa*

### 11.4.3 Sarufi: Matumizi ya Vivumishi vya Kuuliza katika Ngeli ya LI-YA

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watafute vivumishi viulizi ambavyo vinaambatana na majina ya ngeli ya LI-YA katika kifungu cha habari walichopewa.*

*Vivumishi hivyo ni:* ***lipi?,***

***mangapi?,***

***wapi?***

**Zoezi 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, watunge sentensi zenye nomino za ngeli ya LI-YA. Mwalimu afuatilie kwa karibu jinsi wanafunzi wanavyotunga sentensi hizo na kuwaongoza panapohitajika.*

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi wafanye zoezi hili binafsi wakitumia vivumishi viulizi ambavyo walipewa ndani ya mabano kwa kujaza sentensi.*

**Majibu**

1. Jibu **lipi** limeishapatikana?
2. Mawe **mangapi** yamewekwa kando ya barabara?
3. Madirisha **gani** yamefunguliwa?
4. Meno **yapi** yameng'oka?
5. Tunda **gani** limeiva?

**Zoezi la 7 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi, mmoja mmoja aandike sentensi hizi katika umoja au wingi, mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi anafanya zoezi hili.*

**Majibu:**

1. Majengo yapi makubwa?
2. Papai lipi limeiva?
3. Nikupe magunia mangapi?
4. Shirika gani linasaidia wakulima?
5. Sasa ninyi mnataka niwape majembe yapi?

### 11.4.4 Matumzi ya Lugha : Aina za Hadithi

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu maelezo yanayofuata ili waweze kubainisha aina za hadithi kama zilivyoelezwa katika kitabu cha mwanafunzi*

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi waoanishe aina ya hadithi katika kundi A na maelezo yake katika kundi B, kisha watoe mifano miwili kwa kila aina ya hadithi na mifano hiyo itolewe kutoka jamii ya Kinyarwanda. Wanafunzi wapewe fursa ya kutoa mifano mbalimbali.*

| **Aina za hadithi** | **Maelezo** |
|---|---|
| Ngano | Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni mchanganyiko wa watu, wanyama, miungu, mazimwi, na vitu vingine ambavyo hupewa uhai na kutenda kama watu<br><br>***Mfano:*** *Nyasha na Baba,……….* |
| Hurafa | Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni wanyama na vitu vingine ambavyo hupewa uhai na kutenda kama watu.<br><br>***Mfano:*** *impyisi na Bakame, Hadithi ya Sungura na Fisi, Hadithi ya Kobe,……….* |
| Hekaya | Aina ya hadithi ambayo wahusika wake ni watu tu.<br><br>***Mfano:****Wanafunzi wafikirie mifano ya hadithi kama Hekaya za Abunuwasi kutoka Kiswahili ambazo zipo katika Kinyarwanda ……….* |
| Visakale/ Migani | Aina za hadithi ambayo wahusika wake ni mashujaa wa kitaifa.<br><br>***Mfano:*** *Hadithi ya Ruganzu, Hadithi ya Fumo Liyongo kutoka Kiswahili………* |

### 11.4.5 Kusikiliza na kuzungumza :

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Baada ya kusoma maelezo muhimu kuhusu hadithi, wanafunzi wajibu maswali yaliyopendekezwa kwenye kitabu cha mwanafunzi.*

1. Kwa ufupi maelezo yaliyotolewa yanahusu umuhimu wa hadithi na aina za hadithi
2. Aina za hadithi ni: ngano, tarihi, visasili, vigano, soga, migani.
3. Hadithi ni tungo za fasihi za masimulizi ambazo zinatumia lugha ya nathari (lugha ya mjazo, ya maongezi ya kila siku). Masimulizi hayo hupangwa katika mtiririko wa visa na matukio.
4. Hadithi hutoa sababu za hali mbalimbali katika dunia kama jamii inavyoiona. Husifu mema na kukashifu maovu. Hadithi hutoa maonyo, huadhibu, huelimisha na kushauri. Hutoa mafunzo na maadili ya kufuatwa na jamii na kuiwezesha kubadili tabia. Hadithi huzingatia historia na utamaduni wa jamii. Huendesha uhusiano wa jamii kwa kuiburudisha na kuboresha uwezo wa kukumbuka.
5. Mwalimu amuombe mwanafunzi mmoja kusimulia wenzake hadithi yoyote ile kutoka kwa jamii ya Kinyarwanda. Hadithi hiyo isimuliwe katika lugha ya Kinyarwanda.

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu aombe mwanafunzi mmoja kuja mbele ya wenzake na kusimulia hadithi moja kwa kuzingatia mianzo na miisho ya hadithi katika lugha ya Kiswahili.

### 11.4.6 Kuandika:

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aombe wanafunzi kuandika hadithi moja wanayoifahamu kutoka katika jamii ya Wanyarwanda wakitumia Kiswahili fasaha. Hadithi ihusuyo ushujaa.*

# SOMO LA12: METHALI

## 12.1 Ujuzi wa awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu utumiaji wa methali katika jamii kama utanzu wa fasihi simulizi. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya. Maswali haya yatakuwa na uhusiano wa karibu na fasihi, fasihi simulizi pamoja na tanzu zake zikiwemo methali.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu utumiaji wa methali kisha afanye chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile ambachoanadhamiria kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha Mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro.

Awaambie: Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- *Elezea wahusika unaowaona kwenye mchoro.*
- *Matukio haya yanafanyikia wapi?*
- *Ni shughuli zipi zinafanyika kwenye mchoro?*
- *Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?*
- *Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na michoro?*

## 12.2 Zana za kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika somo hili zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo juu ya hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum kama wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali.

Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu aandae vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu mwenyewe ajibunie vifaa mbalimbali vya kumsaidia.

## 12.3 Maelekezo kuhusu kazi za ujifunzaji

Katika hatua hii, mwalimu atafute mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atilie mkazo mambo yafuatayo:

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu itumiwe ili kumshirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watumie makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** Ni lazima kila mwanafunzi apewa kazi/ mazoezi yake binafsi (kwa mfano: Kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani).
- **Maswali na majibu:** Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao wajibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi kwa upande wao wamuulize mwalimu maswali kadhaa naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yawe kati ya wanafunzi wenyewe.
- **Maelezo ya mwalimu:** Mbali na kuwa mwanafunzi hupewa kipaumbele katika somo, mwalimu angali msuluhifu katika somo lake. Kwa hiyo, mwalimu atumie mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.
- Majadiliano: Mbinu hii iwawezeshe wanafunzi kujadiliana kuhusu kazi watakayopangiwa na mwalimu.
- **Utafiti:** Mbinu hii iwaruhusu wanafunzi kutafuta maelezo zaidi kuhusu kazi watakazopangiwa na mwalimu. Watafute habari mbalimbali katika vitabu vya maktabani au kwa kutumia tovuti. Tena wajadiliane na watu wengine wa nje ya darasa lao.

## 12.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watatazama michoro na kutoa majibu mwalimu akiwaongoza.*

### 12.4.1 Maswali ya Ufahamu

1. Mzee Gahigi na mtoto wake Kagabo.
2. Maneno yake yalikuwa yamejaa hekima.
3. Alikuwa mpatanishi.
4. Kagabo alianza kuwa na tabia ya uzembe. Lakini kutokana na mawaidha ya baba yake alibadilika akawa mtendakazi.
5. Kagabo alitumia ngunvu zote alizokuwa nazo alipokuwa akisoma kwa kutayarisha maisha yake yajayo na mwishowe akafanikiwa.
6. Kagabo alisoma lugha katika kitivo cha Lugha na Sanaa.
7. Alipata kazi ya kuwa mhariri mkuu wa Televisheni ya Taifa.
8. Alikuwa akijitolea kwa kazi yake na kuwapa maonyo wenzake.
9. Alipewa zawadi kama malipo ya malezi mema aliyompa mtoto wake.

10. Ni vizuri kufanya kazi tukiwa bado na uwezo bila kungoja kesho. Hivi ni kwa sababu na Kagabo anayesimuliwa katika kifungu alitenda haya na kufanikiwa baadaye.

### 12.4.2 Msamiati kuhusu Methali

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Mafumbo: maneno yasiyojulisha maana waziwazi
2. Mawaidha: maneno yenye maonyo au mafunzo, mashauri.
3. Maktaba: nyumba au chumba mnamohifadhiwa vitabu ambamo watu huruhusiwa kuvisoma au kuviazima kwa muda.
4. Hekima: busara, akili
5. Mpatanishi: msuluhishi, mtu anayesuluhisha watu au pande mbili zinazogombana.
6. Shaka: hali ya kutokuwa na hakika ya jambo; wasiwasi, tuhuma, hatihati, wahaka.
7. Baraka: mambo mema kwa jumla; mafanikio, fanaka, neema, heri.
8. Bidii: juhudi, jitihada, hima, ari ya kufanya jambo.
9. Nyati: mnyama wa porini mithili ya ng'ombe mkubwa mwenye pembe zilizopinda kwa mbele; mbogo.
10. Runinga: chombo kinachopaza picha, sauti na maandishi kutoka kituo cha kurushia matangazo na kuzionyesha pamoja na kutoa sauti iliyonaswa; televisheni

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Mifano ya sentensi**

1. Mafumbo: Aliniambia mafumbo yaliyonilazimu kuyafumbua.
2. Mawaidha: Ingekuwa vizuri kama tungefuata mawaidha ya walimu wetu.
3. Maktaba: Shule yetu ina mpango wa kujenga maktaba ili kusaidia wanafunzi kwa kusoma.
4. Hekima: Igeni matendo ya mzee yule kwa sababu ni ya hekima.
5. Mpatanishi: Pande mbili zikizozana, lazima mpatanishi aingilie kati kwa kuziunganisha.
6. Shaka: Kwa sababu ya kujitayarisha vilivyo, Mutesi alifanya mtihani bila shaka lolote.
7. Baraka: Ninawaombea baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
8. Bidii: Kalisa alitia bidii katika masomo.
9. Nyati: Nyati ni myama asiyependa kuchokozwa sana.
10. Runinga: Wakati wa likizo si vizuri kwa wanafunzi kukaa mbele ya runinga tu na kusahau kuwasaidia wazazi.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Nyati
2. Ya mafumbo
3. Ndege
4. Muongo
5. Maktaba
6. Mpatanishi
7. Elewa
8. Kunyanyuka
9. Runinga
10. Bidii

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Jambo lilalowezekana kutendwa sasa hivi, lazima litendwe bila kuahirishwa.
2. Ukisubiri kutenda jambo kama likiwa likiwezekana hutapata manufaa yake.
3. Mtu anayeamka mapema na kutenda kazi ndiye anayefanikiwa.
4. Usipochunga wakati unaokuwa nao na kuutumia vilivyo, unaweza kukuacha bila kufanya ulichotarajia kufanya.
5. Usifanye mambo kwa pupa.
6. Kusubiri jambo fulani kwa muda mrefu kunasumbua.
7. Wakati unakimbia sana.
8. Mtu anayefanya kazi ngumu ikiwepo hata katika mazingira ya jua huja kufaidi matunda ya kazi ngumu akiwa amestarehe.

### 12.4.3 Sarufi: Vivumishi vya Kuonyesha katika Ngeli ya LI-YA

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaagize wanafunzi katika makundi yao ya wawili wawili, kuchunguza katika kifungu cha habari walichosoma na kuonyesha vivumishi vya kuonyesha katika ngeli ya Li-Ya.*

**Zoezi la 7:*(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. hili
2. lile
3. hayo
4. hayo
5. lile

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Kabati **lileli**livunjwa na wezi.
2. Maji haya **ya**limwagwa ovyo sakafuni.
3. Alipotaka kujenga nyumba alitafuta **mawe** makubwa.

4. Mafuta haya ha**ya**mwagwi ziwani kwa sababu yanaweza kuua samaki.
5. Maboga haya **tikitiki** yana manufaa **mengi** kwa mwili wako.

### 12.4.4 Matumizi ya lugha: Maana ya Methali na uUhambuzi Wake

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaagizie wanafunzi, katika makundi yao ya watatu watatu, kusoma maelezo muhimu, kisha wajibu maswali yanayohusika.*

Methali ni tungo fupi za sentensi moja ambazo hutoa funzo fulani kwa njia ya mafumbo.

**Mifano ya methali**

<u>Chelewa chelewa</u>, <u>utamkuta mtoto si wako.</u>

(Hoja) (Matokeo)

<u>Wakati titi la nyati</u>, <u>hukamuliwa kwa shaka.</u>

(Hoja) (Suluhisho)

**Mifano: 1. Mpanda Ngazi hushuka**

- Maana ya nje: *Mtu yeyote anayepanda juu ya ngazi ni lazima itafika muda way eye kushuka kutoka juu ya ngazi hiyo*
- Maana ya ndani: *Katika maisha mtu anayepata cheo au madaraka kuna siku anaweza kuyapoteza madaraka au cheo hicho*
- Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo

- Maana ya nje: *Siku hii ni siku hii, anayenena siku ifuatayo ni mdanganyifu.*
- Maana ya ndani: *Tendo linalowezekana kufanyika sasa lazima lifanyike, lisiahirishwe.*

1. <u>Bandu banduhumaliza gogo.</u>
2. <u>Chovya chovyahumaliza buyu la asali.</u>
3. <u>Asiye funza na mamayehufunzwa na ulimwengu.</u>
4. <u>Mtoto akililia wembempe.</u>
5. <u>Mtoto umlevyo ndivyo akuavyo.</u>
6. <u>Mchelea mwana kuliahulia yeye.</u>
7. <u>Heri kufa macho kuliko kufa moyo.</u>
8. <u>Atangaye sana na juahujua.</u>
9. <u>Kuishi kwingi kuona mengi.</u>
10. <u>Tamaa mbele mauti nyuma.</u>

**Mifano:**

| **Kinyarwanda** | **Kiswahili** |
|---|---|
| Igiti kigororwa kikiri gito. | Ngozi ivute ingali mbichi/maji. |
| Inyana ni iya mweru. | Mtoto huangalia kisogo cha mama yake. |

| | |
|---|---|
| Uko umureze ni ko akunyarira. | Umleavyo ndivyo akuavyo. |
| Utumviye se na nyina yumvira ijeri. | Asiyesikia la mkuu huvunjia guu. |
| Uburere buruta ubuvuke. | Kulea mimba si kazi kazi ni kulea mwana. |

***iv. Oanisha methali katika sehemu A namethali zinazokaribiana kimaana katika sehemu B***

1g, 2i, 3a, 4b, 5h, 6c, 7f, 8j, 9d, 10e

**v. Oanisha Methali zilizopo katika sehemu A na maana zake zilizopo katika sehemu B**

1e, 2d, 3b, 4a, 5c

### 12.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaagize wanafunzi, katika makundi yao ya wawili wawili, kujadiliana juu ya mada zifuatazo:*

1. Umuhimu wa methali katika jamii.
2. Akili ni mali.

**Mambo ya kuzingatia :**

- Kueleza methali kifani na kimaudhui.
- Kutoa mifano ya hali halisi kulingana na methali.

### 12.4.6 Kuandika

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Mwalimu aombe kila mwanafunzi kutunga kifungu cha habari chenye mada moja kati ya hizi zifuatazo:**

1. Mchumia juani hulia kivulini.
2. Chovya chovya humaliza buyu la asali.
3. Asiyekubali kushindwa si mshindani.

**Jambo la kuzingatia :**

- Kutunga kifungu cha habari chenye maoni yanayohusiana na mada moja miongoni mwa zilizotajwa hapo juu.

# SOMO LA 13: NAHAU

## 13.1 Uwezo wa Awali / Marudio / Utangulizi.

Somo hili linalohusu **“nahau”**.Si mara ya kwanza kusikia neno nahau kwa sababu katika somo la tatu “**Dhana ya Fasihi”** kunasemwa aina ya fasihi na tanzu zake. Nahau inapatikana kwenye fasihi simulizi kama vitendawili... kwa hiyo mwalimu aanze somo lake kwa kuwauliza maswali mengi kuhusu tanzu za fasihi simulizi. Kama vile:

- Mnakumbuka nini kuhusu somo lililopita “Dhana ya Fasihi” ?
- Kuna aina gani ya fasihi?
- Toa mifano ya tanzu za fasihi andishi unazozikumbuka.
- Kwa sababu gani tunasema kwamba nahau ni utanzu ya fasihi simulizi?

- **Utangulizi:**

Hapa mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali ya utangulizi wa somo kwa kumkumbusha somo lililopita “ methali” na kutambulisha somo la nahau. Mwalimu anaweza kuanza kwa kuuliza Methali ni nini? Methali zina umuhimu gani katika matumizi ya lugha? Kutaja mifano miwili ya methali anazozikumbuka na kusema uhusiano kati ya methali na kichwa cha habari. Baada ya hapo atambulishe somo jipya kwa kuwauliza,Umewahi kusikia kuhusu nahau? Toa mifano ya nahau

**Nahau zinatofautiana vipi na methali?**

**Kwa maneno yako, eleza maana ya nahau**

## 13.2 Vifaa

- Kitabu cha mwanfunzi kidato cha nne.
- Kitabu cha mwalimu kidato cha nne.
- Kamusi ya Kiswahili sanifu.
- Silabasi ya Kiswahili kidato cha 4-6.

## 13.3 Mbinu za ufundishaji

Somo hili linahusu nahau. Mwalimu arahisishe ufunzaji wake kwa kuleta vifaa vyote vitakavyosaidia wanafunzi kuelewa somo. Mwalimu awachangamshe kwa kuwauliza maswali katika kitabu cha mwanafunzi (ukurasa 110) wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Katika sehemu hii mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata uwezo kuhusu tafakuri tunduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha kujibu maswali husika.

- **Kusoma na kufahamu kifungu “Fitina ni mzigo”**

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kimya kifungu cha habari kilichopo huku wakiandika msamiati mpya wanaokutana nao. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kimya kifungu, awaombe kusoma kwa sauti. Mwalimu akumbuke umuhimu wa kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Hatimaye, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu kifungu cha habari walichokisoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa.

- **Ujifunzaji wa msamiati kuhusu kifungu**

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujibu maswali ya ufahamu, wanafunzi katika makundi mwalimu awasaidie kuelewa kila swali na baadaye watoe majibu kwa wanafunzi.

Mwalimu baada ya kusahihisha maswali ya ufahamu, aongoze kazi ya kutafuta maana ya msamiati na kuutumia. Wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili watumie kamusi ya Kiswahili Sanifu kutafuta maana ya msamiati . Hapa kazi ya mwalimu ni kuzunguka na kutoa maelekezo kwa kila kundi pale yanapohitajika.

- **Matumizi ya lugha**

Katika sehemu hii,mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wajadiliane juu ya nahau na maana zake ili watunge sentensi kwa kutumia nahau. Mwalimu awasaidie katika kazi hiyo kwa kuiwasilisha.

- **Kusikiliza na kuzungumza**

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajadiliane juu ya maana na matumizi ya nahau. Mwalimu atoe maelezo kwa kila kundi.

- **Kuandika**

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe kutunga kifungu cha habari ambacho kinadhihirisha matumizi ya nahau zisizopungua tano. Mwalimu awasaidie kutumia nahau zinazofaa.

- **Sarufi**

Katika hatua hii, mwalimu awape mifano ya sentensi zenye kutumia ngeli ya "LI-YA" na vivumishi vya pekee: -enye, -enyewe, -ote, -o-ote, -ingine. Mwalimu aeleze matumizi hayo. Baadaye mwalimu awaombe wanafunzi kutunga sentensi tano na kueleza matumizi hayo. Mwalimu aendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ambayo yatawasaidia kuelewa vizuri matumizi ya ngeli hiyo na vivumishi vya pekee katika umoja na wingi.

## 13.4. Majibu

### 13.4.1 Majibu ya Ufahamu

**Zoezi la 1** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1. Wahusika wanaozungumziwa katika kifungu hiki ni Sungura, Simba, Binti mchumba wake Simba, polisi,vijana, na Kiongozi wa Simba.
2. Sungura alikuwa na tabia ya fitina.
3. Kwa sababu alikuwa na mipango mingine mibaya dhidi ya rafikiye Simba.
4. Vijana wengine wanampenda binti aliyekuwa mchumba wa Simba kwa sababu alikuwa mrembo.

5. Kuna uhusiano kati ya kichwa cha habari na kifungu cha habari kwa kuwa tangu mwanzoni fitina ya Sungura inaonekana katika mfuatano wa matukio.
6. Simba hakufukuzwa kazini. Kwanza, Sungura alikuwa anapanga kisirisiri ili kijana Simba apigwe kalamu mahali alipokuwa akifanyia kazi. Alitumia hila zote ili kumchonganisha na mkuu wa kazi. Simba hakufukuzwa kazini kwa kuwa alikuwa akifanya kazi yake vizuri na kupendwa na mkuu wake wa kazi. Pili, baada ya gazeti moja kutangaza habari kuhusu ulevi wa Simba. Kiongozi wake aliona kwamba ilikuwa njama iliyopangwa na adui.
7. Sungura alipanga kisirisiri ili kijana Simba apigwe kalamu mahali alipokuwa akifanyia kazi. Alitumia hila zote ili kumchonganisha na mkuu wa kazi.
    - Sungura alisambaza katika gazeti picha za Simba ambazo yanamuonesha akizungukwa na pombe za aina nyingi.
8. Kwa sababu alikuwa anamuamini Sungura kama rafiki yake wa kufa na kupona.
9. Mapenzi kati ya binti yule na Sungura hayakudumu muda mrefu kwa kuwa polisi walikuwa wameshatambua aliyekuwa na hatia. Sungura alipelekwa gerezani akaadhibiwa kifungo cha mwaka mzima kwa vitendo vyake vibaya na alilazimishwa pia kulipa faranga elfu hamsini za Rwanda kwa kosa la wizi.
10. Sungura aliadhibiwa kwa vitendo vyake vibaya na kuiba suti ya Simba. Alipewa adhabu ya kifungo cha mwaka na kulipa elfu hamsini faranga za Rwanda.
11. Mafunzo ninayoyapata kutokana na kifungu hiki cha habari ni haya yafuatayo:
    - Kabla ya kuchagua mpenzi inafaa kuchunguza tabia za mpenzi wako
    - Kutokuwa na tabia ya fitina.
    - Kabla ya kuamua ni lazima kufanya uchunguzi
    - Kutotendea mabaya rafiki yako
    - Kuwa na tabia ya kuomba radhi
    - Kuwa na tabia ya kusamehe
    - Kuwa na tabia ya kushukuru
    - N.k

### 13.4.2 Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, toeni maelezo ya msamiati ufuatayo kutoka kifungu cha habari hapo juu, kisha mtunge sentensi zenu kwa kutumia maneno hayo.*

1. **Kushuhudia :** Kuona na kusikia tukio fulani wewe mwenyewe.

**Mfano :** Mwaka uliopita nilishuhudia pambano la Rayon Sport na Kiyovu Fc.

2. **Fitina :** Maneno ya kuchonganisha watu.

**Mfano:** Bada ya kuondoa tabia ya fitina katika familia yetu, sasa hivi tunaishi kwa amani ya kutosha

3. **Mchumba:** Mwanamume aliyeposa mwanamke au mwanamke aliyeposwa.

**Mfano:** Kaka yangu kesho atafanya harusi na yule mchumba ambaye anatumia kiti cha magurudumu kutembea.

4. **Mrembo:** Msichana au mwanamke mwenye sura nzuri.

   **Mfano:** Yule mwanamke mrembo anapenda kusaidia watoto wenye matatizo ya kutoona

5. **Kulewa:** Kuwa katika athari ya pombe,dawa kali au kitu kingine kinachobadilisha akili.

   **Mfano:** Ni tabia mbaya kwa watu wote kuwa na tabia ya kulewa.

6. **Kukata tamaa :** Kupoteza matumaini.

   **Mfano:** Majambazi walikata tamaa ya kunyanganya wananchi kutokana na usalama wa nchi

7. **Njama :** Mpango wa siri wenye lengo la kufanya jambo baya dhidi ya mtu mwingine.

   **Mfano :** Kijana Sambakare alikuwa na njama ya kuiba pesa za yule bibi lakini alishikwa na polisi kabla ya kufanya chochote.

8. **Bumbuazi:** Mshangao mkubwa unaofanya mtu awe kimya na asijue la kufanya.

   **Mfano :** Mama yake alishikwa na bumbuazi kuona mtoto wake mwenye matatizo ya kuona anapata alama za kwanza kushinda wanafunzi wengine.

9. **Kuomba radhi:** Kuomba msamaha.

   **Mfano**: Kiongozi wa kanisa letu anasema kwamba tukiomba radhi kwa Mungu husamehewa dhambi zetu.

10. **Kung'aa :** Kupendeza au kuvutia kwa usafi, kutoa mwangaza.

    **Mfano:** Dhahabu kutoka ardhini mwetu inang'aa

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tumieni mshale kwa kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B*

**1e; 2d; 3f; 4g; 5b; 6j; 7c; 8h; 9i; 10a.**

### 13.4.3 Sarufi: Nomino za Ngeli ya LI-YA na Vivumishi vya Pekee

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wachunguze sentensi zilizotolewana waonyeshe kuwa maneno yaliyopigiwa mstari ni vivumishi vya pekee pamoja na nomino za ngeli ya LI-YA*

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Tungeni sentensi zenu tano kwa kutumia nomino za ngeli ya LI-YA pamoja na vivumishi vya pekee: -enye, -enyewe, -ote, o-ote, -ingine**

1. ***Funzo lenye*** *malengo ya kuigiza linapendeza wanafunzi.*
2. ***Mapengo yenyewe*** *yamejazwa.*
3. ***Masomo yote*** *yalifundishwa.*
4. ***Jibu lolote*** *linaandikwa.*
5. ***Kundi jingine*** *linasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.*

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Andika sentensi zifuatazo kati wingi

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| 1. Gari lenye magurudumu makubwa. | 1. Magari yenye mgurudumu makubwa |
| 2. Jiwe lenyewe ni hili. | 2. Mawe yenyewe ni haya . |
| 3. Tamasha lote lilikuwa zuri. | 3. Matamasha yote yalikuwa mazuri. |
| 4. Kundi lolote linapaswa kujitayarisha. | 4. Makundi yoyote yanapaswa kujitayarisha |
| 5. Alifua koti jingine. | 5. Walifua makoti mengine |
| 6. Kamati yote imefika | 6. Kamati zote zimefika |

### 13.4.4 Matumizi ya Lugha: Nahau

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadiliane kuhusu semi (nahau) zilizopendekezwa katika sehemu A na maana zake katika sehemu B, kisha watunge sentensi kwa kutumia nahau hizo. Mifano mingine anayoweza kuitumia mwalimu ni hii ifuatayo:*

| **Nahau** | **Maana ya nahau** |
|---|---|
| **Kupekua** | Kutembea kwa miguu bila viatu |
| **Kuponda raha** | Kufurahi sana |
| **Kuvaa miwani** | Kulewa pombe |
| **Mbavu za mbwa** | Nyumba iliyojengwa kwa miti bila kukandikwa sawa sawa. |
| **Kwenda kujisaidia** | Kwenda choo |
| **Kujipatia jiko** | Kuoa |
| **Pete na kidole** | Kuwa marafiki |

### 13.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili, wajadiliane kuhusu maana na matumzi ya nahau zifautazo:*

1. Kuchemsha bongo
2. Kuchongea mtu
3. Kubeza mtu
4. Kuchungulia kaburi
5. Kufafanua kinagaubaga

### 13.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, watunge kifungu cha habari ambacho kinadhihirisha matumizi ya nahau zisizopungua tano.*

**Mfano wa kifungu chenye kutumia nahau zisizopungua tano**

Kulikuwa familia moja ya Baba , bibi na watoto. Wanaishi kijiji cha Maendeleo. Familia hii ina matatizo ya malazi. Zaidi ya hivyo, kupata chakula si kitu rahisi kwao, watoto hupekua pia. Kila wakati baba akipata pesa, kazi yake ni kuponda raha na kuvaa miwani. Haleti chochote nyumbani.

Kwa ushirikiano wa watoto na mama yao walijijengea nyumba ya mbavu za mbwa na mahali pa kwenda kujisaidia. Badaye, baba naye alitoa mchango wake na kuepukana na tabia zote mbaya alizokuwa nazo. Walianza kuwa na maendeleo na kuishi kwa amani.

Watoto wao walikua na kufikia umri wa kujipatia jiko. Binti yao alipata kijana ambaye alikuwa na nia ya kumuoa. Walikuwa pete na kidole.

Watoto wote walibahatika kawa na familia zao. Baba na mama walishukuru Mungu kwa kuwasaidia watoto wao.

## 13.5 Muhtasari wa Mada

Mada hii ya pili**" Lugha katika Sanaa"** ina vipengele sita yaani masomo makuu sita yanayohusiana na mada husika. Kila **somo lina** vipengele vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika, sarufi, na maelezo muhimu. **Somo la kwanza** linaeleza maana ya sanaa, aina ya sanaa na zana za sanaa. **Somo la pili** linaeleza maana ya fasihi.**Somo la tatu** linaeleza kuwa vipawa vinasaidia jamii kwa kukuza utamaduni na kujipatia pesa. **Somo la nne** linaeza maana ya fasihi katika fasihi simulizi, aina ya fasihi, na umuhimu wake katika jamii. **Somo la tano** linaeleza maana ya methali, matumizi ya methali, muundo, na umuhimu. Somo la mwisho linaeleza maana ya nahau, umuhimu wa nahau katika jamii, na badhi ya nahau na maana yake.

## 13.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 13.7. Tathmini ya Mada

Mwalimu awaongoze wanafunzi kujibu maswali ya tathmini na kuchunguza kuwa mambo muhimu yanayozingatiwa na maswali yanapatikana katika majibu ya wanafunzi

## 13.8. Mazoezi ya Ziada

### 13.8.1. Mazoezi ya urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye kipaji cha hali ya chini.

1. **Andika sentensi zifuatazo katika wingi**

a. Mimi nina lengo la kupambana na jangwa.
b. Kijana mrefu alibeba kasha kwenye bega.
c. Shirika la reli liliagiza garimoshi kubwa.
d. Daftari linapaswa kuhifadhiwa vizuri.
e. Jambo hili liliwafurahisha wengi.
f. Jiwe langu lina thamani kubwa.
g. Papai lipi limeiva?
h. Jino lako limeng'oka?
i. Jaribio la leo lemesahihishwa.
j. Janga kubwa limesababisha maafa.

**Majibu:**

a. Sisi tuna malengo ya kupambana na majangwa.
b. Vijana warefu walibeba makasha makubwa.
c. Mashirika ya reli yaliagiza magarimoshi makubwa.
d. Madaftari yanapaswa kuhifadhiwa vizuri.
e. Mambo haya yanawafurahisha wengi.
f. Mawe yangu yana thamani kubwa.
g. Mapapai yapi yameiva ?
h. Meno yako yameng'oka?
i. Majaribio ya leo yamesahihishwa.
j. Majanga makubwa yamesababisha maafa.

**Mazoezi jumuishi**

1. **Eleza nahau zifuatazo:**

a. Kupigwa kalamu

b. Kumpa nyama ya ulimi

2. **. Chagua neno sahihi katika mabano kwa kujaza pengo.**

a. Debe ………….. lilitoboka (hii, haya, hili, hiyi).

b. Jambazi ……….aliadhibiwa (yule, hii, hiyo).

c. Anakuomba umnunulie machungwa ………….(hizo, hayo, yayo).

d. Meno ...................... yameng'oka. (mbili, wawili, mawili)

e. Matunda ....................... yameiva. (nane, manane)

f. Madarasa .............................. (tatu, matatu) yamekarabatiwa.

g. Shavu.............................. linaniuma (yangu, langu).

h. Ondoa majani...........................hapa (hizo, hayo).

i. Nimepoteza jembe..........................(yangu, langu).

j. Jengo ............................unasimulia (lipi, ipi) ?

**Majibu:**

1. a. Kufukuzwa kazini

   b. Kudanganya mtu kwa maneno matamu

a. Debe hili lilitoboka.

b. Jambazi yule aliadhibiwa.

c. Anakuomba umnunulie machungwa hayo

d. Meno mawili yameng'oka.

e. Matunda manane yameiva.

f. Madarasa matatu yamekarabatiwa.

g. Shavu langu linaniuma.

h. Ondoa majani hayo hapa.

i. Nimepoteza jembe langu.

j. Jengo lipi unasimulia?

### 13.8.2. Mazoezi ya Nyongeza:

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi werevu wenye kipaji cha hali ya juu.

**Maswali**

1. Ni nini maana ya sanaa?
2. Toa aina kumi za sanaa.
3. Sanaa ina umuhimu gani kwa binadamu?
4. Taja tanzu za fasihi simulizi.

5. Fasihi ina umuhimu gani katika jamii?
6. Namna gani fasihi inavyoweza kuhatarisha utengamano wa jamii?
7. Ni aina gani ya hadithi inayosimulia kuhusu watu waliotenda matendo ya kishujaa katika jamii?
8. Hadithi huishia kwa fomula gani?
9. "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo." Methali hii inamaanisha nini?
10. Ni methali ipi inayoweza kutumiwa wakati mtu fulani ameshindwa kutimiza aliyoyasema?

**MAJIBU**

1. Sanaa ni ufundi unaowakilisha mawazo na hisia alizo nazo binadamu kwa njia ya ubunifu.
2. Kuna aina mbalimbali za sanaa kama vile uchoraji, uchongaji, ususi, uhunzi, usonara, fasihi, uashi, sinema, uimbaji, ufinyanzi, ufumaji, upishi, ushonaji, udarizi. n.k.
3. Sanaa ina nafasi kubwa kwa ujenzi wa taifa, kwani hupunguza ukosefu wa ajira na huwezesha jamii kutosheleza baadhi ya mahitaji yao ya kila siku kupita kazi mbalimbali zinazofanywa na wasanii. Wasanii nao hujiendeleza kiuchumi kutokana na pato linalotoka kwenye kazi zao .
4. Tanzu za fasihi simulizi ni hadithi, methali, nahau, vitendawili, nyimbo na mashairi
5. Fasihi ina umuhimu mkubwa katika jamii. Katika jamii fasihi inaweza:

   *Kuelimisha jamii*

   *Kuburudisha jamii,*

   *Kuhifadhi na kurithisha amali za jamii,*

   *Kudumisha na kuendeleza lugha*

   *Kuunganisha jamii,*

   *Kukuza uwezo wa kufikiri,*

   *Kumtajirisha msanii*
6. Fasihi inaweza kuwa chanzo cha madhara katika jamii inapotumiwa vibaya kupitia nyimbo na methali zinazochochea ubaguzi na uadui baina ya wanajamii. Mfano ni jinsi nyimbo zilivyochochea uhasama baina ya wananchi na kuishia kwenye mauaji ya kimbari dhidi ya watutsi yaliyotokea Rwanda mwaka wa 1994.
7. Visakale
8. Huu ndio mwisho wa hadithi au Hadithi inakomea hapa.
9. "Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo" Methali hii inamaanisha kwamba jinsi unavyomlea mtoto wako ndivyo atakavyokua. Yaani ukimpa malezi mazuri naye atakuwa mzuri, yakiwa mabaya naye atakuwa mbaya vile vile.
10. Mithali hiyo ni "*Ahadi ni deni*"

# MADA KUU YA 3: UHAKIKI WA HADITHI ZA MASIMULIZI KATIKA KISWAHILI

3

## MADA NDOGO : MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI

### Uwezo upatikanao katika mada

Kuelewa na kufuata mtindo wa kuandika muhtasari wa hadithi aliyoisikiliza au kuisoma; kuchambua hadithi za Kiswahili kwa kuzingatia fani na maudhui yanayojitokeza katika hadithi; kusimulia hadithi rahisi za masimulizi; kujuamabadiliko ya kisarufi katika matumizi ya majina ya ngeli ya PA-M-KU-

### Ujuzi wa Awali kwa Mwanafunzi

Mwanafunzi aliyagusia mambo mengi katika mada ya pili 'Lugha katika sanaa'pamoja na mada ndogo yake Kiswahili katika sanaa. Katika mada hii, mwanafunzi alieleza fasihi simulizi ni nini na tanzu zake hususan hadithi simulizi. Alisoma na kufahamu vifungu vya habari na kuvitolea muhtasari wake kimasimulizi.

#### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Kutokana na dhana yake, mada hii inazungukazunguka masuala mtambuka mbalimbali, na hayo hujitokeza katika kitabu cha mwanafunzi kwa kupitia mazoezi kadhaa yaliyojitokeza kutekelezwa na mwanafunzi chini ya mwelekeo wa mwalimu.Baadhi ya masuala mtambuka yaliyosisitiziwa katika mada hii ni yafuatayo:

**a. Elimu kuhusu Amani na Maadili**

Kwa kupitia kifungu cha habari "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu" pamoja na mazoezi tofauti, falsafa kuhusu umoja na maadili iligusiwa sana na kuendelezwa katika mantiki ya kila mwanafunzi shuleni, nyumbani hata mahali popote atakapokuwa.

**b. Elimu kuhusu mauaji ya kimbari**

Mauaji ya kimbari dhidi ya Watutsi ni jambo baya lililoiathiri historia ya Wanyarwanda. Kwa hiyo, ni wajibu wa mwalimu pamoja na wanafunzi kuipitia historia hii kwa kuchukua mbinu za kuzuia itikadi ya mauaji ya kimbari mahali popote ingeweza kutokea. Kifungu cha habari "Mchango wangu" humwalika mwanafunzi kutoa mchango wake katika mchakato wa uzuiaji wa udhalimu, mizozo ya kifamilia pamoja na itikadi ya mauaji ya kimbari.

c. **Elimu kuhusu uzalishajimali**

**"Urithi wa wazazi"** ni kifungu cha habari ambacho kimeendeleza ndani yake dhana ya uzalishajimali. Kutobagua kazi, kuipenda na kuiheshimu kazi na kuendeleza akili kwa ajili ya mavuno mazuri kutoka kazi iliyofanywa ndiyo mawaidha ambayo yamezingatiwa katika kifungu cha habari.

d. **Usawa wa jinsia**

"Sikio la kufa halina dawa" ni kifungu cha habari ambacho kinatoa ushahidi kuwa mchango wa mume na mke huisaidia familia kuendelea kiuchumi. Wanafunzi watahusisha msimamo huu na ukweli uliopo katika jamii ya Wanyarwanda leo.

e. **Uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu**

Pia kifungu hiki hapa juu huligusia lajambo la uhifadhi wa mazingira. Wanafunzi watapewa fursa ya kujadili suala la uindaji wa kiholelaholela kama matokeo mabaya au hasara kubwa kwa uchumi wa nchi yetu.

## Orodha ya Masomo ya Mada hii Pamoja na Tathmini

| **Kichwa cha somo** | **Malengo ya kujifunza** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|
| 1. Maana ya muhtasari na sifa zake | Tazama Mtaala wa Kiswahili (maarifa na ufahamu, stadi pamoja na maadili na mwenendo mwema) | 6 |
| 2. Taratibu za kutoa muhtasari mzuri | | 7 |
| 3. Fani katika hadithi simulizi | | 11 |
| 4. Maudhui katika hadithi simulizi | | 11 |
| 5. Uhakiki wa hadithi simulizi | | 13 |
| Tathmini | | 2 |
| **Jumla ya vipindi** | | **50** |

**Zoezi la 1 : Utangulizi wa Mada/ Kidokezo**

*Mwalimu atumie mbinu tatu tofauti:*

1. *Amchague au amvutie mwanafunzi mmoja aliye tayari kusimulia mbele ya darasa hadithi yake na kuwaomba wengine tumtega sikio kwa ajili ya ufahamu.*
2. *Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi kulingana na maswali yaliyotolewa kujadiliwa*

3. Baada ya ushirikiano wa wanafunzi katika makundi, kazi waliyoshughulikia iwasilishwe mbele ya darasa.

# SOMO LA 14: MAANA YA MUHTASARI NA SIFA ZAKE

## 14.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Ujuzi wa awali kwa wanafunzi katika somo hili unashahidiwa na mambo yafuatayo :

- Walijifunza somo la ufupisho katika kidato cha tatu.
- Mitihani yote ya lugha ilikuwa inaligusia jambo hili.
- Mada ya pili ya kidato hiki ilitoa mwangaza juu ya utangulizi kwa muhtasari wa habari.

## 14.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Mwalimu anaweza kutumia vifaa vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Michoro ya mzazi na watoto wake, n.k.
- Flipchati
- Karatasi manila

Mwalimu achague vifaa vingine husika kulingana na muktadha. Ajaribu kuwa mbunifu katika ufundishaji wake.

## 14.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atumie mbinu zifuatazo:

- **Kazi za kimakundi:** Wanafunzi washirikishwe katika mazoezi yanayofanyiwa katika makundi. Mwalimu aunde makundi kulingana na mpango wa zoezi.
- **Mjadala:** Wanafunzi wafanye mjadala kulingana na mada zilizopendekezwa katika zoezi.
- **Fikiri – jozi – shiriki:**Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu anapata habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hii.
- **Kazi ya kibinafsi:** Mwanafunzi afanye kazi ya kibinafsi wakati wa kufanya zoezi lililopendekezwa kufanywa kibinafsi. Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kumwonyesha makosa ya kurekebishwa.

## 14.4.Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, watazame michoro kwenye ukurasa husika. Watoe maoni yao kuhusu wanachokiona kwenye picha pamoja na kueleza picha hizo zinazungumzia nini. Wanafunzi wajadili kuhusu majibu ya kila mwanafunzi. Mwalimu awaelekeze kuhusu hadithi simulizi kutokana na majibu wanayoyatoa.

### 14.4.1 Maswali ya Ufahamu

Katika makundi ya watatu watatu, wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa ufasaha na kujibu maswali ya ufahamu. Mwalimu arekebishe makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.

**Majibu pendekezo**

1. Katika kijiji cha Chapakazi.
2. Sebahire, Nyirabagenzi, Jitegemee, Mugeni, Rulinda na watoto wengine wawili.
3. Ndiyo. Jitegemee na Mugeni walikuwa wafanyakazi kwa bidii wengine watatu walikuwa wazembe.
4. Mzee Sebahire alitumia picha ya fimbo tatu zilizokuwa zimebanishwa na kamba. Aliwaomba watoto wake kuzivunja na wakashindwa.
5. Vijana waliamua kuwa wanaacha utengano kati yao na kufanya kazi pamoja. Waliikumbuka methali isemayo kuwa "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu"
6. Umoja unahitajika katika kazi za kila siku. Kusaidiana na wengine katika kazi za kila siku ni jambo muhimu sana. Siyo vizuri kutengana na wanafunzi wengine katika kazi ya kila siku.
7. Kichwa cha hadithi kinahusiana na yaliyomo kwa sababu yaliyofanywa na watoto wake sebahire na Nyirabagenzi yanalinganishwa na kichwa cha hadithi

### 14.4.2 Matumizi ya Msamiati wa Msingi

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amwombe mwanafunzi kufanya zoezi hili kibinafsi. Mwanafunzi atumie kamusi kwa kueleza maana ya msamiati mpya, na kuutumia katika sentensi. Mwalimu achunguze kazi zinazofanywa na wanafunzi. Achague sampuli ya wanafunzi watatu wawasilishe kazi yao mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza.*

***Maana ya pendekezo la msamiati***

a. **Kifunguamimba:** mtoto wa kwanza kuzaliwa na mama
b. **Juhudi:** namna ya kutumia uwezo na nguvu za mtu katika kufanya jambo.
c. **Mawaidha**: maneno ya mafunzo ama maonyo hususan yenye mwongozo fulani.
d. **Kutingisha:** kusukuma kitu nyuma na mbele
e. **Maskini:** mtu ambaye ni dhaifu kiuchumi au kimwili katika maisha yake.
f. **Kutenganisha:** kufanya kuwa kando ama kuweka kandokando; kuachanisha.
g. **Kuchonganisha:** kuchochea watu ili wagombane.
h. **Timamu:** - enye kukamilika; - enye kutimia
i. **Uamuzi:** makubaliano au mapatano yaliyopitishwa kama vile katika mkutano ili kutekeleza jambo fulani.
j. **Maendeleo:** hali ya kufanikiwa kama vile kijamii, kiuchumi au kisiasa.

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa kushirikiana na mwenzake, mwanafunzi aelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kutumia mshale na kuoanisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B. Mwalimu asahihishe zoezi na kuwarekebisha wanafunzi.*

**Majibu:**

c

e

a

b

d

### 14.4.3 Sarufi: Usanifishaji wa Majina ya Ngeli ya PA- M- KU

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi kutazama sentensi katika vitabu vyao, wajibu maswali mmoja baada ya mwingine. Zoezi hili lifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili. Wanafunzi wawasilishe kazi. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.*

Zoezi la 5:

*Zoezi hili lifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Mwalimu asahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.*

***Masahihisho:***

1. Sipendi kutembea mahali **pabapasipo** na mazingira bora.
2. Nchini Rwanda kuna pahali **pa**zuri pa kutembelea .
3. Nilimkuta katika baa, mahali **pa**baya sana.
4. Mukamana hapendi kukaa mahali **pa**chafu.
5. Wakiristo wa makanisa tofauti huomba Mungu mahali **pa**takatifu.

**Zoezi la 6:**

*Mwalimu awalekeze wanafunzi kufanya zoezi kibinafsi. Asahihishe zoezi kwa kila mwanafunzi na kusahihisha makosa yatakayojitokeza.*

***Masahihisho***:

1. Rukundo atatembelea mbuga za wanyama. Ni mahali **pazuri.**
2. Tunapaswa kuishi mahali **safi.**
3. Si vizuri kulala mahali **pabaya** kwa sababu panaweza kuharibu maisha yako.
4. Mahali **pachafu** huweza kuambukiza maradhi.
5. Mahali **patakatifu** hupatikana katika nchi chache duniani.

### 14.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezila 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu. Wanafunzi wasome kifungu cha habari katika vitabu vyao, wajibu maswali katika makundi. Wanafunzi wawasilishe kazi kundi moja baada ya jingine. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.*

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu amuombe mwanafunzi asome kifungu cha habari. Mwanafunzi afanye muhtasari wa kifungu cha habari kimaandishi na baadaye asimulie hadithi mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa ya kimaandishi na kimasimulizi yaliyojitokeza.*

### 14.4. 5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi wasome vifungu vya habari . Wanafunzi wafanye muhtasari wake kimaandishi. Mwalimu atumie flipchati na kuwapa karatasi manila waandike muhtasari. wanafunzi wawasilishe kimazungumzo vifungu vya habari. Mwalimu arekebishe makosa ya kimaandishi na kimazungumzo.*

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi watano watano. Wajadili masuala waliyoyapewa na kila kundi liwasilishe kazi. Mwalimu arekebishe makosa ya kimazungumzo yatakayojitokeza.*

### 14.4.6Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 11: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi lifanywe kibinafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi watunge vifungu vya habari kwa kutumia ngeli ya PA- M- KU-. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi.*

## SOMO LA 15.: TARATIBU ZA KUTOA MUHTASARI MZURI

### 15.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Kusoma somo hili si mara ya kwanza kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Waligusia somo hili katika kidato cha pili, na kidato cha tatu. Somo lililotangulia lilitilia mwangaza zaidi kuhusu sifa za muhtasari mzuri.

### 15.2. Zana na vifaa vya ufundishaji

Vifaa vifuatavyo huweza kutumiwa na mwalimu wakati wa kufundisha somo hili:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Magazeti mbalimbali,
- Michoro ya watoto wanaokwenda shuleni, n.k.
- Flipchati
- Karatasi manila

Mwalimu achague vifaa vingine husika kulingana na muktadha. Ajaribu kuwa mbunifu katika ufundishaji wake.

### 15.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu atumie mbinu zifuatazo:

- **Kazi ya kibinafsi:**Nilazima kila mwanafunzi apewe kazi/zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari au kwa kufanya tathmini).
- **Kazi za kimakundi:** Wanafunzi washirikishwe katika kazi za kimakundi na kuwasilisha kazi yao. Mwalimu afanye masahahisho
- **Mjadala:** Katika somo hili wanafunzi wafanye mijadala ili kukuza stadi ya kusikiliza na kuzungumza.
- **Fikiri – jozi – shiriki:**Baada ya maoni tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu apate habari juu ya ujuzi wa awali wanafunzi wake walio nao kuhusu somo hii.Mwalimu asahihishe zoezi hili pamoja na kusahihisha makosa.

### 15.4.Majibu

**Zoezi la 1: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa sauti. Makosa ya kimatamshi yasahihishwe na mwalimu.*

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aunde makundi ya wanafunzi watatu watatu. Wanafunzi wafanye zoezi hili la kulinganisha kifungu cha habari "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu" wakizingatia mambo yafuatayo:*

**Tofauti au uhusiano baina ya vifungu vya habari hivi viwili:**

- Urefu wa kifungu cha habari.
- Mtiririko wa visa.
- Yaliyomo.
- Matumizi ya lugha.

*Wanafunzi wawasilishe kazi yao kundi moja baada ya jingine. Mwalimu asahihishe makosa yatakayojitokeza.*

**Majibu pendekezo**

- **Tofauti au uhusiano baina ya vifungu hivi viwili:**
- Vifungu vyote viwili vina ujumbe mmoja.
- Wahusika waliotumiwa katika vifungu vyote ni wale wale.
- Vinatofautiana sana kwa urefu. Kimoja kinaundwa na sentensi nyingi kingine ni chache.
- **Urefu wa vifungu vya habari :** Vifungu hivi viwili havina urefu mmoja. Cha kwanza ni kirefu sana kuliko cha pili. Kifungu cha kwanza kinaundwa na sentensi nyingi lakini kifungu cha habari cha pili kinaundwa na sentensi chache sana..
- **Mtiririko wa visa:** Katika kifungu cha kwanza visa vinafuatana kwa mantiki na mwandishi wake amevipanga visa kwa mfuatano mrefu. Katika kifungu cha habari cha pili visa vimepangwa kwa ufupi. Mwandishi wake amefanya muhtasari unaoegemea kwenye kifungu cha habari cha kwanza.
- **Yaliyomo:**Vifungu vya habari vyote vinabeba ujumbe mmoja. Yaliyomo ni sawa sawa lakini kifungu cha kwanza wameyaeleza kinaganaga, kifungu cha pili wamefanya muhtasari.
- **Matumizi ya lugha:** Lugha iliyotumiwa katika kifungu cha kwanza ni tofauti sana na kifungu cha pili. Katika kifungu cha kwanza kuna matumizi ya nahau, misemo, methali lakini katika kifungu cha pili wametumia lugha rahisi.

### 15.4.1 Zoezi la Ufahamu

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa ufasaha na kujibu maswali ya ufahamu. Mwalimu arekebishe makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.*

**Majibu pendekezo**

1. Katika kijiji cha Bananeza.
2. Gatete,Kamaliza, Mucyo, Muhoza, Gakire, babake na mama yake Gakire.
3. Mzozo na ugomvi katika familia ya Gakire.
4. Amani, usafi, adabu, uhifadhi wa mazingira, uzalendo, ushirikiano, utu, na kadhalika

5. Mucyo, Muhoza na Gakire walikuwa wanaenda na kutoka shuleni pamoja. Walikuwa wanazungumzia matatizo ya familia na kuyatafutia suluhisho.
6. Gatete na mkewe walikuwa wanapendana kati yao na majirani wote walikuwa wanaisifu familia yao.
7. Kauli hii ni kweli. Mucyo na Muhoza walitoa mchango wao katika kuuendeleza umoja wa familia ya rafiki yao Gakire. Walilizungumzia suala hili na wazazi wao na kuwaomba kurudisha amani katika familia ya jirani yao.
8. - Kuzungumza kwa kusema ukweli kati ya familia.
    - Kuomba msamaha kati yao
    - Kuwa na umoja na maridhiano kati yao.

### 15.4.2 Matumizi ya Msamiati wa Msingi

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kazi hii ifanywe kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Watumie kamusi kwa kueleza maana ya msamiati mpya, na kuutumia katika sentensi. Mwalimu achunguze kazi zinazofanywa na wanafunzi na kuwaomba wafanye mawasilisho.Mwalimu arekebishe makosa yanayoweza kujitokeza.*

**Majibu pendekezo:**

a. **Kusifu:** kueleza hali ya uzuri wa jambo, kitu au mtu.
b. **Utulivu:** hali ya kutoleta matatata; hali ya kutulia.
c. **Kupambana:** kushindana kwa maneno au vitendo.
d. **Dua :** maombi anayoombwa Mwenyezi Mungu tu.
e. **Jirani :** mtu aliye karibu na mahali unapoishi.
f. **Kurekebisha :** kutengeneza kilichokwenda kombo ili kiwe sawa.
g. **Chanzo:** kiini cha kitu au jambo asili, sababu.
h. **Ugomvi:** hali ya kugombana; mgogoro.
i. **Kudumu:** kuendelea kuishi au kuwapo kwa muda wote, kuishi milele.
j. **Kuwasili:** kufika mahali ulipoazimia kwenda baada ya mwenendo au safari.

**Zoezi la 5:**

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwanafunzi aelekezwe jinsi ya kufanya zoezi hili kwa kutumia mshale na kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B. Mwalimu asahihishe zoezi na kuwarekebisha wanafunzi.*

**Majibu pendekezo**

1. i
2. e
3. f
4. g
5. h

6. d
7. j
8. c
9. b
10. .a

### 15.4.3Sarufi: Nomino za Ngeli ya PA- M- KU  na Vivumishi vya Kumiliki

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili lifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili. Wanafunzi watazame sentensi katika vitabu vyao,kisha wajibu maswali. Wawasilishe kazi kundi moja baada ya jingine. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.*

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili lifanywe kibinafsi. Mwalimu asahihishe zoezi na kuwaelekeza wanafunzi kwenye majibu sahihi.*

1. Mimi ninaishi mahali pazuri. Mahali **kwangu** (changu, kwangu, pao) kunafurahisha.
2. Mukaneza anapenda kulala pahali safi. Pahali **pake** (kwangu, pake, kwao) ni safi.
3. Tunatembea mahali panapopendwa na watu kadhaa. Mahali **kwetu**(yetu, kwetu, yao) panajulikana.
4. Wanafunzi wangu husomea mahali papana. Mahali **mwao**(yangu, mwao, kwetu) ni pazuri pa kusomea.
5. Mtoto yule analala mahali panapopendwa na wazazi wake. Mahali **kwake** (yako, kwake, yetu) panapendwa na wazazi.

### 15.4.5 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 8:**

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya watatu watatu. Wanafunzi wasome kifungu cha habari katika vitabu vyao. Wafanye muhtasari kimaandishi pamoja na kuandika kwenye karatasi manila. Waonyeshe taratibu walizozitumia wakati wa kufanya muhtasari. Kila kundi liweke karatasi manila kwenye flipchati. Wawasilishe kazi yao. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi na kimatamshi.*

**Muhtasari pendekezo**

**Mchango wangu**

Umoja na ushirikiano vilikuwa sifa kubwa zilizokuwa zinaitawala familia ya Gatete na mkewe Kamaliza. Wazazi hawa waliwalea watoto wao vizuri na kuwapa maadili yaliyowasaidia kuishi kwa amani na marafiki zao. Watoto wao Mucyo na Muhoza walikuwa na rafiki yao Gakire.Familia ya kijana huyu ilikuwa ni tofauti na ile ya marafiki zake kwa sababu ilikuwa inaishi katika hali mbaya ya mizozo. Baada ya Mucyo na Muhoza kupata habari hiyo, walihuzunika sana na kuamua kutoa mchango wao wa kupata suluhisho la kudumu.

Vilevile waliwashirikisha wazazi wao katika suala hili na kuwaomba kuiokoa familia ya rafiki yao Gakire. Kwa njia ya mawasiliano ya uso kwa uso, familia zote mbili ziliutatua mzozo uliokuwepo.

**Zoezi la 9:**

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu amuombe mwanafunzi kuandika kifungu cha habari kwenye karatasi manila. Kila mwanafunzi awasilishe kimasimulizi kazi yake. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi na kimaandishi.*

### 15.4. 6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:**

*Mwalimu awaombe wanafunzi kuwasilisha vifungu vya habari walivyosoma. Kila mwanafunzi achague kifungu cha habari kimoja na kufanya muhtasari. Mwanafunzi awasilishe kazi yake. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi na kimatamshi.*

**Zoezi la11:**

*Zoezi hili lifanyike katika makundi ya wanafunzi watano watano. Wajadili masuala waliyoyapewa na kila kundi liwasilishe kazi. Mwalimu asahihishe makosa ya kimazungumzo yatakayojitokeza.*

### 15.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 12:**

*Zoezi lifanywe kibinafsi. Mwalimu awaombe wanafunzi watunge vifungu vya habari kwa kutumia vivumishi vya kumiliki vya majina ya ngeli ya PA- M-KU,  mwanafunzi aitolee muhtasari kimaandishi. Mwalimu asahihishe makosa.*

## SOMO LA 16: FANI KATIKA HADITHI SIMULIZI

### 16.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Dhana ya fani si neno jipya kwa wanafunzi wa kidato cha nne kwa sababu waliligusia katika mada ya pili "Lugha katika Sanaa".

### 16.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Vifaa vihitajiwavyo katika somo hili hutegemea aina ya kila zoezi. Kwa hiyo inambidi mwalimu atarajie zana husika kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mfano wa vifaa vinavyowezakupendekezwa ni kama vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu.
- Kitabu cha mwanafunzi.
- Flipchati na kalamu zake husika.
- Michoro mbalimbali yenye dhana ya umbo au funiko.
- Vitabu au majarida kuhusu hadithi simulizi.

## 16.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mwallimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

- Mbinu ya tafakari binafsi.
- Ushirikiano kwa jozi.
- Mbinu ya "waza – jozi – shiriki" kwenye kidokezo, majibu ya ufahamu, n.k.
- Kazi ya kimakundi kuhusu mazoezi ya matumizi ya msamiati wa msingi,
- Mijadala katika zoezi la kusikiliza na kuzungumza

**Tanbihi:**

Mwalimu awahudumie kipekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na tatizo walilo nalo.

Kwa mfano:

- Amuache akae mbele yule aliye na tatizo la kutona vizuri kwenye ubaoni;
- Atumia lugha ya mwili kwa kumsaidia mwanafunzi aliye na tatizo la kusikia au kusema.
- Utafiti kesi: Mbinu hii itumiwe hasa katika mazoezi ya kubuni hadithi simulizi.

## 16.4. MAJIBU

### 16.4.1. Swali Tangulizi

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu ayaunde makundi matatu ya wanafunzi na kugawa kwa kila kundi swali moja baadhi ya yale matatu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Baada ya mawasiliano katika makundi, wanafunzi watoe maoni hadharani.*

### 16.4.2. Majibu ya Ufahamu

Mwalimu amuombe mwanafunzi kufanya kazi hii kibinafsi na kushirikiana kwa jozi kwa ajili ya kukamilishana.

1. Wahusika wote wanaozungumziwa katika kifungu cha habari.
    - Mzee Furaha
    - Mkewe Shukuru
    - Watoto: Faida, Kagabo pamoja na Fikiri
    - Ndege mjumbe
    - Majirani au waalikwa
2. Ujumbe unaopatikana katika kifungu
    - Kuiheshimu kazi yoyote bila ubaguzi
    - Kutokata tamaa katika tatizo fulani
    - Kutenda mema kwa ajili ya wengine3

3. Kifungu hiki cha habari ni cha hadithi simulizi kwa sababu zifuatazo:
a. Kina funzo fulani ambalo aghalabu limetajwa mwishoni mwa hadithi.
b. Masimulizi yake yametumia wakati uliopita
c. Kimesimuliwa kwa lugha ya natharia
d. Wahusika wake ni mchanganyiko wa binadamu na wanyama (ndege)
e. Kimehusisha mbinu nyingine za fasihi simulizi kama vile wimbo, methali, nahau, misemo
f. Kina muundo rahisi wenye mwanzo, kati na mwisho.
g. Hadithi imetokea katika mandhari halisi (nyumbani).
4. Tatizo la uhaba wa chakula (njaa) pamoja na ufukara kwa jumla.
5. Sababu muhimu ya tatizo hilo ni ujinga ambao ulikuwa umeungwa mkono na kutoheshimu kazi pamoja na kubagua kazi fulani fulani.
6. Ukiviona vimeundwa. Husisha methali hii na kifungu cha habari.

Pasipo matendo matunda hayapatikani kamwe, yaani ukiyaona mafanikio usidhani kuwa yalitokea hewani, bali yalitokana na jasho la watendaji. Methali hii inahusiana na hadithi kwa sababu utajiri wa familia ya mzee Furaha haukubahatishwa bali ulipiganiwa na kufikiwa.

7. Mzee Furaha aliwapatia urithi wa aina tatu zifuaatazo: akili, utajiri pamoja na utu.
    - Urithi wa akili umeelezwa na jinsi mzee Furaha alivyowashughulikia watoto wake kusoma mpaka vyuo vikuu;
    - Urithi wa utajiri unajidhihirisha na tukio la watoto hao kuwa wataalamu baada ya kuhitimu masomo yao kutoka vyuoni na kutajirika kupitia kazi;
    - Urithi wa utu unaelezwa na moyo au tabia ya kuwatendea mema watu wote na wakati wowote.
8. Bila shaka ujumbe wa ndege mjumbe ulizingatiwa kama ifuatavyo:
    - Mzee Furaha hakuidharau kazi ya kilimo cha mahindi
    - Hakukata tamaa ya kupanda mahindi kwenye ardhi kubwa bila kuhangaikia soko la mavuno yake
    - Baada ya kushika mkia utajiri, familia ya mzee Furaha ilionyesha utu na huruma: Haikubagua majirani, mtu yeyote aliyekuwa katika mahitaji ya huduma alikuwa ameipata.

### 16.4.3. Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi fulani. Kila kundi lipewe msamiati wa kutolea maana na kutunga sentensi binafsi. Baadaye kila kundi liwasilishe kazi yake.*

***Maana pendekezo:***

a. **Urithi:** mtu, mali au vitu vinavyoachwa na marehemu na kupewa mtu fulani, agh. Wa ukoo; mirathi.

b. **Kitindamimba:** mtoto wa mwisho kuzaliwa; mziwanda.
c. **Kuonya:** kuhadharisha kwa kuonyesha hatari itakayotokea; kutoa mawaidha.
d. **Kuahidi:** kujipa sharti; kutoa ahadi.
e. **Kuhifadhi:** kuweka mahali pa salama; kuweka moyoni bila ya kusahau.
f. **Kutekeleza:** kufanya kama inavyotakiwa; kukamilisha.
g. **Kukuza:** kufanya kitu kionekane kikubwa; kuvuvumua.
h. **Kupata fur**sa: kupata nafasi ya kuweza kufanya jambo.
i. **Kuangamiza**: kuhiliki, kuharibu, kutesa, kusababisha matatizo au mikoshi.

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa jozi wanafunzi washirikiane kujaza sentensi husika. Baadaye mwalimu amchague mwanafunzi kwa kubahatisha akitumia mpira na kumuomba atoe jibu lililojadiliwa.*

a. **Walemavu** ni watu wa kuheshimiwa kama watu wengine. Wanapaswa kupewa haki zao na kuhudumiwa kisheria bila ubaguzi wowote.
b. Aliyefiwa na wazazi wake huitwa **mtoto yatima** lakini aliyepoteza mumewe huitwa **mjane.**
c. Urithi bora kwa mtoto leo ni akili. Kwa hiyo kila mzazi ana wajibu wa kuwalipia watoto wake**karo** za shule.
d. Mwanafunzi yeyote ambaye anafuata **maonyo** ya wazazi wake pamoja na walimu wake huwa na mwenendo mwema.
e. Amenunua vifaa vya nyumbani kwa **bei ghali.**

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Bainisha nahau au misemo pamoja na methali zilizotumiwa katika hadithi "Urithi wa wazazi"*

*Mwalimu ayaunde makundi matatu ya wanafunzi ; kundi la kwanza lipewe kubainisha nahau, la pili misemo na la mwisho methali. Kisha kila kundi liwasilishe kazi yake.*

**Nahau:** kukata tamaa, kupiga makofi, kuunga mkono, kutega sikio.

**Misemo:** siku nenda rudi, punde si punde, bega kwa bega,

**Methali:** Ukiviona vinaelea vimeundwa.

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Zoezi hili lifanywe kibinafsi, kisha kwa jozi.**

1. c
2. d
3. a
4. f
5. b
6. e

### 16.4.4. Sarufi: Usanifishaji wa Majina ya Ngeli ya PA-M-KU

**Zoezi la 6:**

*Mwalimu awachague/awavutie wanafunzi wawili kusoma sentensi husika, baadaye iwe fursa ya darasa lote.*

*Kazi hii ifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili wawili. Baada ya maoni kutoka kwa wanafunzi, mwalimu awaelekeze kwenye ukurasa wa maelezo ya ziada katika kitabu cha mwanafunzi.*

**Zoezi la 7:**

Chagua jibu sahihi kati ya haya yaliyowekwa katika mabano.

*Kazi hii iwe ya kibinafsi.*

a. Mahali **hapa**( humu, hapa, kule) panaitwa Umoja wetu.
b. Darasani **mle** (pale, mle, huku) mnaonekana uchafu.
c. Barabarani **kule** (kule, humu, pale) kumewekwa ndoo za taka.

### 16.4.5. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Soma tena kifungu cha habari "Urithi wa wazazi". Chunguza kwa makini mambo yafuatayo:

a. Maana ya fani katika hadithi
b. Aina ya wahusika wanaojitokeza hadithini pamoja na tabia zao
c. Mahali au mandhari hadithi ilipotokea
d. Muundo na mtindo wa hadithi
e. Lugha aliyoitumia msanii wa hadithi.

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi sita:

Kundi la kwanza lijishughulishe na maana ya fani, kundi la pili wahusika na tabia zao, la tatu mahali au mandhari ya hadithi pamoja na maelezo au vipengele vyake, la nne lizungumzie muundo, la tano mtindo, na la mwisho lugha aliyoitumia msanii.

Baada ya kuwasilisha maoni yao, wanafunzi waelekezwe kwenye maelezo ya ziada kwa ajili ya kuikosoa na kuikamilisha kazi yao.

**Mapendekezo ya majibu kwa zoezi hili**

**a. Maana ya fani**

Fani ni ufundi au mbinu anayoitumia msanii wa fasihi ili kutoa au kufikisha ujumbe kwa watu aliowakusudia.

**b. Wahusika:**

- Wazazi: Furaha na Shukuru
- Watoto: Faida, Kagabo, Fikiri.

- Ndege
- Majirani

**Tabia za wahusika:**

- Wazazi: utu, upendo, huruma, ushirikiano na umoja.
- Watoto: heshima, uadilifu, uerevu, uamuzi wa kufikia lengo fulani.
- Ndege: mhusika mtabiri, mshauri, mwenye lengo la kuiendeleza jamii kiuchumi.
- Majirani: watu wenye tabia ya ushirikiano, kuishi kwa amani na majirani zao bila wivu.

**c. Mandhari au mahali palipotokea kisa cha habari**

Kisa cha habari kimetokea katika familia ya Furaha na mkewe Shukuru. Tunampata Furaha chini ya mti pembeni mwa nyumba akimwangalia ndege mtini. Baadaye tunaiona familia ya Furaha na mkewe Shukuru, watoto pamoja na majirani zao wakisherehekea sikukuu nyumbani kwa familia hii.

**d. Muundo**

Katika hadithi hii msanii alitumia muundo wa msago, yaani muundo wa kusimulia matukio moja kwa moja; kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho kwa namna yalivyotukia.

**e. Mtindo**

- Wahusika ni wa aina ya mchanganyiko (binadamu na ndege)
- Msanii amechagua msamiati rahisi kuelewa.
- Msimulizi ametumia nafsi ya tatu wakati uliopita.
- Matumizi ya wimbo yamekuja kuleta burudani katika masimulizi.

**f. Lugha ya msanii**

Katika ufundi wake, msanii ameitumia lugha ya nathari. Tanzu za fasihi simulizi kama vile nahau, misemo pamoja na methali zimetumiwa ndani ya hadithi kuikuza na kuitukuza fasihi simulizi ya Kiswahili.

### 16.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Hadithi ya kutolewa na mwalimu inaweza kuwa imerekodiwa, imesimuliwa au imesomewa mwanafunzi. Hapa inategemea uchaguzi au mahitaji ya mwalimu. Kazi hii ifanyike katika makundi kulingana na vipengele vya swali.*

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili lifanyike katika makundi yaliyopangwa na mwalimu ambapo kila kundi litatoa kimasimulizi muhtasari na fani ya hadithi husika.*

**Zoezi la 11 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu atumie mbinu ya kazi zunguka (work gallery) ambapo maswali au maoni ya kujadiliwa huandikwa kwenye karatasi kubwa zaidi ya mbili na kuziweka kwenye ukuta.*

*Wanafunzi wajigawe katika makundi. Washiriki wa kundi la kwanza watoe upesi upesi maoni yao kwenye karatasi ya kwanza. Wanaposogelea karatasi ya pili, kundi la pili liifikie karatasi ya kwanza, na kadhalika. Kundi la tatu litapewa fursa kwenye karatasi ya kwanza wakati ambapo lile kundi lililotangulia litakuwa limefikia karatasi ya tatu, na kadhalika.*

### 16.4. 6. Utungaji

Hii ni kazi ya kibinafsi. Inaweza kufanyika darasani ama nyumbani.

# SOMO LA 17: MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI

## 17.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Panapozungumziwa fani maudhui huhusishwa pia. Vifungu vya habari vilivyoshughulikiwa katika mada ya kwanza na katika masomo matatu ya mada hii ya pili, zoezi la kutoa lengo kuu pamoja na mawaidha lilirudiwa mara nyingi.

## 17.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Sawa sawa na somo kuhusu fani, vifaa vihitajiwavyo katika somo hili hutegemea aina ya kila zoezi. Wajibu wa mwalimu ni kutarajia mwanzoni zana husika kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mfano wa vifaa vinavyoweza kupendekezwa ni kama vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Flipchati na kalamu zake husika
- Karatasi manila
- Michoro mbalimbali yenye dhana ya kuwekea kitu ndani.
- Vitabu au majalida kuhusu hadithi simulizi.

## 17.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mwalimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

- Mbinu ya “fikiri – shirikiana na mwenzako – changia maoni na wenzako” kwenye kidokezo, majibu ya ufahamu, n.k.
- Kazi ya kimakundi kuhusu mazoezi ya matumizi ya msamiati wa msingi,
- Mijadala katika zoezi la kusikiliza na kuzungumza

**Tanbihi:**

Mwalimu awahudumie kwa kipekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na tatizo walilo nalo.

- **Utafiti kesi:** Mbinu hii itumiwe hasa katika mazoezi ya ubunifu wa hadithi simulizi.

- **Utafiti wa kitekinolojia:** Utafiti juu ya kazi zilizofanywa na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili uendelezwe katika maktaba au chumba cha kompyuta shuleni au nyumbani.

## 17.4. Majibu

### 17.4.1. Swali Tangulizi

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amchague au amvutie mwanafunzi kufikiria hadithi anayoijua na kuisimulia mbele ya darasa. Baadaye wanafunzi washirikishwe katika kutoa ujumbe kutoka hadithi hiyo.*

### 17.4.2. Ufahamu

Kwanza kila mwanafunzi ajitahidi yeye mwenyewe kutoa jibu, kisha wawili wawili kwa ajili ya kukamilishana na kukubaliana kwa jibu moja. Wakati wa kuwasilisha kazi hii, majibu sahihi kuliko mengine yaandikwe ubaoni.

7. Wahusika wanaozungumziwa katika kifungu cha habari:
    - Kobe, mbayuwayu, Mfalme Simba, Fisi, Sungura, Kunguru, wazazi wake kobe na nyoka.
8. Ujumbe unaopatikana katika kifungu
    - Kuwa na matarajio ya kila kitu au jambo linalotakiwa kufanyika.
    - Kutoshawishwa wala kuongozwa na majivuno maishani na kuthubutu kuwa ushindi uko mikononi mwako milele na milele.
    - Kuwa na mashaka au tafakuri tunduizi juu ya jambo fulani.
9. Msanii ametumia wanyama kama wahusika na wanyama hawa wamepewa tabia za binadamu kwa kuwakilisha watu mbalimbali wenye tabia hizo katika jamii. Pembeni mwa dhamira kuu ambayo imeelezwa hapa juu, msanii ameziongeza dhamira ndogodogo kama vile ushirikiano wa kijamii, kukubali kushindwa, majivuno, hekima au busara, n.k.
10. Tabia za wahusika waliozungumziwa hadithini
    - Kobe: Mhusika mnyamavu, mtaratibu mwenye hekima, busara na matarajio katika mipango yake.
    - Mbayuwayu: mhusika mpinzani, mjuaji, mpuuzi na mwenye majivuno.
    - Fisi: Mhusika asiyejali kitujuu ya matumizi wa muda.
    - Nyoka: mhusika mshawishi, mjasiri.
11. Kwa nini kobe alijinyakulia ushindi dhidi ya mbayuwayu?
    - Alikuwa anajua wazi umuhimu wa tarajio kwa kila jambo.
12. "Wakati una mabawa"

- Kama umepewa fursa ya kutenda jambo litende wakati huo huo bila kuchelewa. Kobe alitarajia mashindano yake kabla ya siku yake kufika ndipo alipofanikiwa kuwa mshindi.
- Methali zingine zinazoeleza oni hili ni kama vile "Ngozi ivute ingali mbichi" au "Linalowezekana leo lisingoje kesho".

13. Somo linalopatanakatika hadithi:
    - Kazi yote inapaswa kuwa na mpango au matarajio
    - Majivuno maishani huleta hasara
    - Penye mshitaki na mshitakiwa pana mshindi na mshinde
    - Hakuna jambo lisilowezekana.

### 17.4.3. Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi fulani. Kila kundi lipewe msamiati wa kutolea maana na kutunga sentensi binafsi. Baadaye kila kundi liwasilishe kazi yake.*

***Maana pendekezo:***

a. **Mbayuwayu:** ndege mdogo mweusi mwenye mkia mrefu na manyoya meupe kwenye koo na mgongo na aghalabu huhamahama hasa wakati wa joto, hujenga kiota chake kwa matope.
b. **Tarajio:** kitu kinachotazamiwa kutokea; tegemeo.
c. **Mpuuzi:** mtu mwenye tabia ya kufanya mambo yasiyokuwa na maana; mtu asiyestahili kufuatwa mambo yake.
d. **Majivuno:** hali ya kujiona; malingo; kiburi; gogi, goto.
e. **Kuandaa:** kuweka tayari; kutayarisha.
f. **Kasi:** mbio sana, upesi sana, kwa haraka mno.
g. **Riadha:** michezo ya mazoezi ya viungo vya mwili kama vile kuvuta kamba, kwenda mbio, kuruka au kuogelea.
h. **Ghafla:** kwa kushtukia; bila ya kutarajia.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa jozi, wanafunzi washirikiane kujaza sentensi husika na kuwasilisha majibu yao. Jibu sahihi liandikwe ubaoni.*

**Majibu**

a. Wanafunzi hawana **budi** kukubali matokeo ya mtihani wowote.
b. Waalikwa wengi walikuja **kuhudhuria** sherehe za mwaka mpya.
c. Viongozi waliulizwa maswali **tele** kuhusu hatua za kupigana dhidi ya umaskini pamoja na rushwa.
d. **Kukiri** kosa ni sifa muhimu kwa kila binadamu.
e. Tunapaswa **kuharakisha** kazi yetu ili imalizike kwa wakati.

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi wapewe muda wa kupitia hadithi haraka. Mwanafunzi anayeipata hadithi kabla ya wengine aonyeshe mkono juu na kuitoa. Iandikwe ubaoni au mahali pengine.*

***Methali zilizotumiwa***

Asiyekubali kushindwa si mshindani

Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako

Bandubandu huisha gogo

Linalowezekana leo lisingoje kesho.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

***Mbinu ya "Fikiri – jozi – shiriki" itumiwe katika zoezi hili.***

| | |
|---|---|
| 1. Kuvulia kofia | a. Kufariki |
| 2. Kutia chumvi | b. Kufika kwenye kiwango cha juu zaidi |
| 3. Kuaga dunia | c. Kukasirika sana |
| 4. Kuvimba | d. Kuheshimu |
| 5. Kupamba moto | e. Kuongeza maneno zaidi ya yaliyokuwepo kwa kuchonganisha. |

**Zoezi la 6:**

*Mwalimu atumie mbinu ya"Fikiri – jozi – shiriki"*

a. Kamilisha methali zifuatazo

b. Zitolee maana yake

1. **Chelewa chelewa** utamkuta mtoto si wako.
    - Unapochelewa kutenda jambo au kazi utawakuta wengine wameishafanikiwa.
2. Bandu bandu **huisha gogo**
    - Si vizuri kutenda jambo haraka haraka au kwa ghafla; usitende jambo kwa pupa.
3. **Linalowezekana leo** lisingoje kesho
    - Andaa kazi yako kwa wakati bila kungoja wakati ujao.
4. Wakati **una mabawa.**
    - Usingoje kutenda jambo kesho au kesho kutwa.
5. Asiyekubali kushindwa **si mshindani.**

- Kushinda na kushindwa ni mambo mawili yanayokwenda pamoja. Katika mashindano inambidi mshiriki kukubali matokeo yake, mazuri au mabaya.

### 17.4.4. Sarufi: Usanifishaji wa Majina ya ngeli ya PA-M-KU

**Zoezi la 7:**

*Mbinu ya jozi itumiwe. Baada ya maoni kutoka jozi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwenye maelezo ya ziada katika kitabu cha mwanafunzi kwa ajili ya kukosoa au kukamilisha kazi iliyofanywa.*

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kazi hii iwe ya jozi

a. Mahali **papi pa**napatikana maisha bora?

b. Njiani **kupi ku**liandikwa maagizo kuhusu usafi na uhifadhi wa mazingira?

c. Chumbani **mpi m**nalala watoto?

### 17.4.5. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi sita:*

*Kundi la kwanza lijadiliane juu ya maudhui, kundi la pili dhamira, la tatu migogoro, la nne lizungumzie falsafa, la tano ujumbe, na la mwisho msimamo wa msanii katika kazi yake.*

*Baada ya kuwasilisha maoni yao, wanafunzi waelekezwe kwenye maelezo ya ziada kwa ajili ya kuikosoa na kuikamilisha kazi yao.*

*Mwishowe wanafunzi katika makundi yao washughulikie uchambuzi wa hadithi husika kwa kuonyesha vipengele vya maudhui.*

**Mapendekezo ya majibu kwa zoezi hili**

**a. Maana ya maudhui**

Katika kazi ya fasihi maudhui ni jumla ya mawazo yote yaliyozungumziwa pamoja na mtazamo wa mwandishi juu ya mawazo hayo. Maudhui hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusanii kazi yake ya kifasihi.

**b. Dhamira:**

- **Dhamira kuu:** Umuhimu wa kutarajia jambo/ Matunda ya kazi iliyotarajiwa
- **Dhamira ndogondogo:**
- Kukubali matokeo ya mashindano
- Kutoongozwa na majivuno katika maisha.
- Kuthamini ahadi
- Ushirikiano

**c. Migogoro**

- Mbio ya fisi kwenye arusi ya mtoto wa simba mfalme
- Mjadala kati ya mbayuwayu na kobe

- Mawasiliano kati ya kobe na nyoka
- Mashindano kati ya kobe na mbayuwayu.

**d. Falsafa**

Kutokana na maarifa yake katika ukweli wa jamii yake, busara na hekima, kobe alizithamini methali hizi: Asiyekubali kushindwa si mshindani; Linalowezekana leo lisingoje kesho. Kwa hiyo alijinyakulia ushindi dhidi ya mbayuwayu kwa kutarajia siku ya mashindano.

**e. Ujumbe**

Ujumbe kutoka hadithi hii umefikiwa kupitia dhamira kuu pamoja na dhamira ndogondogo kama ifuatavyo:

- Ushindi hutokana na kazi au jambo lililotarajiwa vizuri.
- Hakuna jambo lisilowezekana.
- Akili ni mali kila mtu ana zake.
- Mwisho wa majivuno ni majuto.

**f. Msimamo wa msanii**

Toka mwanzoni hadi mwishoni, msanii ameushikilia msimamo wake wa kwamba "Asiyekubali kushindwa si mshindani." Ametetea tena kuwa ushindi hutokana na matarajio.

### 17.4.6. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Hadithi ya kutolewa na mwalimu inaweza kuwa imerekodiwa, imesimuliwa au imesomewa mwanafunzi. Hapa inategemea uchaguzi au mahitaji ya mwalimu. Kazi hii ifanyike katika makundi kulingana na vipengele vya swali. Wakati wa kusikiliza wanafunzi wachukue kalamu na karatasi na kuandika dhamira kuu, ujumbe, migogoro, falsafa pamoja na msimamo wa msanii.*

**Zoezi la 11: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi sita (dhamira kuu, ujumbe, migogoro, falsafa, msimamo wa msanii) wanafunzi washirikiane kutayarisha maoni ya kuwasilisha mbele ya darasa.*

**Zoezi la 12: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu ayaunde makundi ya wanafunzi kulingana na idadi yao pamoja na mada za kujadiliwa. Wanafunzi washirikiane kubainisha mawazo makuu yanayopatikana katika mada husika na hatimaye kuutayarisha mhadhara wa kutolewa mbele ya darasa.*

*Mfano wa mwongozo wa maoni pendekezo :*

**Muda ni mali**

- Kazi ndiyo msingi wa utajiri
- Kila kazi hufanyika kwa kutegemea tarajio.

- Kutumia wakati wote kama ilivyo ni sawa na kuhifadhi pesa katika benki
- Dakika au saa inayopotea bure ni sawa na hasara ya kupoteza pesa.
- Kadiri muda unavyotumiwa vizuri ndipo mafanikio yanavyozidi kuongezeka.

Mwanafunzi aingiaye darasani bila ratiba ya masomo ni sawa na mkulima aendaye shambani bila jembe.

- Ratiba ya masomo ni mwongozo wa mwanafunzi katika ujifunzaji wake

Bila ratiba mwanafunzi :

- Hupotea katika kazi za shule
- Hujenga uhusiano mbaya kati yake na walimu
- Husababisha utovu wa nidhamu
- Hujenga mizozo baina ya wazazi na viongozi wa shule
- Hawezi kuendeleza akili yake.

Kwa mkulima, jembe ni kifaa cha kulimia. Bila jembe, mkulima :

- Hafanyi kitu chochote cha kilimo shambani
- Hupoteza muda wake kwa bure
- Husababisha ufukara katika familia hata nchini
- Huweza kusababisha vifo kutokana na njaa.

### 17.4. 6. Utungaji

**Zoezi la 13:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Hii ni kazi ya kibinafsi. Inaweza kufanyika darasani ama nyumbani. Katika zoezi hili inawabidi wanafunzi kutegemea utafiti katika maktaba, kwenye mtandao wa intaneti, n.k.*

# SOMO LA 18: UHAKIKI WA HADITHI SIMULIZI

## 18.1. Ujuzi wa Awali/ Utangulizi

Fani na maudhui ni mambo mawili yanayokamilishana katika kazi ya uhakiki. Katika masomo mawili yaliyotangulia, fani na maudhui vimeshughulikiwa kinaganaga. Kwa hiyo mwanafunzi amevielewa wazi vipengele vya fani na maudhui.

## 18.2. Zana na Vifaa vya Ufundishaji

Sawa sawa na somo kuhusu fani, vifaa vihitajiwavyo katika somo hili hutegemea aina ya kila zoezi. Wajibu wa mwalimu ni kutarajia mwanzoni zana husika kulingana na mahitaji ya wanafunzi. Mfano wa vifaa vinavyoweza kupendekezwa ni kama vifuatavyo:

- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi,

- Flipchati na kalamu zake husika
- Karatasi manila
- Michoro mbalimbali yenye dhana ya kuoana, kukamilishana.
- Vitabu au majarida kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi zimulizi.

## 18.3. Maelekezo kuhusu Kazi za Ujifunzaji

Mwalimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

- Mbinu ya "fikiri – jozi – shiriki"
- Kazi ya kimakundi na mhadhara
- Utafiti: Utafiti juu ya kazi zilizofanywa na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili uendelezwe darasani au maktabani kwa kutumia vitabu; au katika chumba cha kompyuta shuleni.
- Mhadhara.

**Tanbihi:**

Mwalimu awahudumie kwa Kipekee wanafunzi wenye mahitaji maalumu kulingana na tatizo walilo nalo.

## 18.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kila mwanafunzi ajitegemee kubainisha vipengele vya fani na maudhui kutokana na hadithi aliyofikiria*

### 18.4.1 Ufahamu

Zoezi hili liwe la kibinafsi. Wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa ufasaha na kujibu maswali ya ufahamu. Mwalimu asahihishe makosa yanayojitokeza katika majibu ya wanafunzi.

**Majibu pendekezo**

1. Sungura, swala, paa
2. Familia ya Mupenzi na Mariamu ilikuwa hodari sana.
3. Mupenzi alikuwa hodari katika utumiaji wa mishale na hakuweza kumkosa mnyama yeyote anayejitokeza machoni kwake.
4. Walikuwa wanampenda kwa kuwa kila wakati walikuwa wanamshauri na kumuonya aache tabia ya wizi na ukatili.
5. Alikutana na joka kubwa lenye vichwa saba.
6. Alijuta kwa sababu hakusikia maneno ya wazazi wake na akapata cha mtemakuni baadaye.
7. "Sikio la kufa halina dawa" ni methali inayohusiana sana na hadithi hii kwa sababu Fujofujo hakufuata mawaidha ya wazazi wake na alipata cha mtemakuni baadaye. Angesikia maonyo ya wazazi, asingekufa kifo kama kile.

### 18.4.2 Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi fulani. Kila kundi lipewe msamiati wa kutolea maana na kutunga sentensi binafsi. Baadaye kila kundi liwasilishe kazi yake.*

**Majibu pendekezo**

1. **Mwindaji :** mtu anayeshughulika na kuwatafuta wanyama porini na kuwaua kwa ajili ya chakula au kuzuia madhara.
2. **Kutabiri :** kueleza au kutoa habari ya mambo yatakayotokea kwa kutumia ujuzi au kwa kutafsiri ndoto.
3. **Kupe :** mtu anayepata mapato bila ya kutumia jasho lake ; mtu mwenye nguvu asiyefanya kazi bali hutegemea wengine wa kuishi.
4. **Mzoga:** mwili wa mnyama aliyekufa.
5. **Kujuta :** kuona huzuni au kusikitika kwa ajili ya jambo baya ulilolifanya.
6. **Mtukutu :** mtu au kiumbe asiyesikia la mtu ama aambiwalo.
7. **Kifo:** hali ya kukosa uhai.
8. **Joka:** nyoka mkubwa kuliko kawaidha
9. **Mawaidha:** maneno ya mafunzo ama maonyo hususan yenye mwongozo fulani.
10. **Upweke:** hali ya kukaa bila mwenzi kama vile rafiki, mke, mshirika, n.k.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwanafunzi ajaze nafasi kwa kutumia maneno aliyopewa. Mwalimu akosoe makosa yanayojitokeza.*

**Majibu**

1. Mtu yule huonekana kama **mwendawazimu** kutokana na maradhi yake ya akili.
2. **Mdadisi**wa masuala haya ametoweka.
3. **Swala**ni mnyama anayefanana na mbuzi.
4. Kula vyakula vya mafuta kila wakati **hudhuru** mwili hasa moyo
5. Mwindaji alimuua twiga kwa kutumia **mshale** wake.
6. Inaonekana kwamba mama yule ni **mjamzito.** Anakaribia kuzaa mtoto.
7. Kabla ya mvua kunyesha, mawingu hujitokeza kama **dalili**ya mvua hiyo.
8. Wanafunzi wale wana **matumaini,** ya kushinda mtihani wa Kiswahili mwaka huu.
9. **Uharibifuwa** mazingira ni mwiko kwa kila binadamu.
10. Usiwe na **hofu**ya kutoa wazo lako hadharani.

### 18.4. 3 Sarufi: Vivumishi vya Idadi vya Majina ya Ngeli ya PA-M-KU

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili lifanyike kwa ushirikiano wa wanafunzi wawili. Wanafunzi watazame sentensi katika vitabu vyao, wajibu maswali. Wawasilishe kazi kundi moja baada ya jingine. Mwalimu awaelekeze kwa majibu sahihi.*

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Zoezi hili liwe la kibinafsi*

**Majibu pendekezo**

a. Pahali **patatu** ( matatu, patatu,kutatu) patatembelewa wiki ijayo.
b. Pahali **sita** (pasita , msita, sita) panapatikana usafi.
c. Kalisa atamwonyesha mtoto wake pahali **patano** (tano, patano, mtano) pa kupanda miti.
d. Pahali **pawili** (mwili, pawili, kuwili) palifundishiwa masomo ya usawa wa jinsia.
e. Wageni wale waligundua pahali **pengi** (mwingi, pengi, nyingi) pa kutembelea sokwe mtu.
f. Usafi unatakiwa pahali **pengi** ( nyingi, pengi, wengi).

### 18.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mbinu ya “fikiri – jozi – shiriki” itumiwe.

**Maoni pendekezo:**

- Mwili unaonekana kama funiko la viungo vyake, na moyo ni mojawapo ya viungo hivyo vinavyofunikwa na mwili.
- Mwili na moyo havitenganiki. Vikitenganishwa kimoja dhidi ya kingine huwa ni mwisho wa mzunguko wa damu.

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu ayaunde makundi madogomadogo ya wanafunzi kulingana na vipengele vya fani na maudhui vitakavyoshughulikiwa. Kila kundi lipewe kipengele cha kuendeleza uhakiki. Wanafunzi waruhusiwe kufanya utafiti kupitia vitabu au mitandao ya intaneti.*

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Baada ya muda uliotolewa na mwalimu kumalizika, wanafunzi waandae kazi, na kutoa mbele ya darasa mhadhara wa kazi yao.*

**Maoni :**

- **Uhakiki wa fani**

a. **Wahusika na tabia zao**

Hadithi “Sikio la Kufa Halina Dawa” ni aina ya hekaya, yaani wahusika wake ni mchanganyiko wa binadamu pamoja na mizimu au miungu.

**Mupenzi na Mariamu:** wahusika wenye tabia ya uhodari katika kazi zao; wanaharakati wa umoja na amani, wenye maadili juu ya malezi bora, waaminifu.

**Fujofujo:** mhusika mdadisi, kupe pamoja na mpuuzi. Hakuwa na woga kugombana na mtu au mnyama yeyote hata mzimu.

Mzuka: mhusika mkali, mkatili, mwenye kuogofya; asiye na huruma.

b. **Mtindo:** Msaniialitumia mtindo wa masimulizi kwa kutumia nafsi ya tatu wakati uliopita.

c. **Muundo:** Msanii alitumia muundo wa moja kwa moja, yaanimsago. Matukio yamesimuliwa moja kwa moja, kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho.

d. **Lugha:** Msanii ametumia nahau, misemo pamoja na methali kuufikisha ujumbe wake.

*Nahau:* Kuwa mjamzito, kujifungua, kuishi kwa jasho la mwingine, kuamini macho yake, kuendelea na wembe ule ule, kifo kumkodolea macho, kukata tamaa, kuaga dunia.

*Misemo:* siku za usoni, miaka nenda rudi.

*Methali:* Sikio la kufa halina dawa, hauchi hauchi unakucha.

e. **Mandhari:** hadithi hii imetokea mahali pawili tofauti: nyumbani kwa Mzee Mupenzi na mkewe pamoja na porini.

- **Uhakiki wa maudhui**

a. **Dhamira:**

   - **Dhamira kuu:** Kuyafuata mawaidha ya wazazi.
   - Dhamira ndogondogo: dharau, uaminifu, upuuzi, hatima ya mtu.

b. **Migogoro:**

   - Tatizo la kupata mtoto wakati wa muda mrefu
   - Wasiwasi juu ya maisha ya Fujofujo
   - Huzuni kubwa kwa wazazi wa Fujofujo baada ya mtoto wao kupotea.

c. **Falsafa:** Msanii anakubali matokeo mazuri kwa mtu aliyeyaheshimu mawaidha ya wazazi au ya wakubwa wake. Anapoyapinga au kuyadharau vilevile balaa au matokeo mabaya ni lazima yamfikie.

d. **Ujumbe:** Msanii anataka kuhakikisha kuwa “Asiyesikia la mkuu huvunjika guu”, yaani inampasa kila mtoto kuyaheshimu mawaidha ya wazazi kwa ajili ya kuandaa maisha mema katika siku za usoni.

e. **Msimamo wa msanii:** “Sikio la kufa halina dawa” ni kichwa cha hadithi. Msanii ameushikilia msimamo wake kuwa mpango au dalili za kifo haziwezi kubadilishwa na mtu yeyote. Hapa anakubali kuwa kila mtu huwa na hatima yake.

### 18.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Hadithi ya kutolewa na mwalimu inaweza kuwa imerekodiwa, imesimuliwa au imesomewa mwanafunzi. Hapa inategemea uchaguzi au mahitaji ya mwalimu. Kazi hii ifanyike katika makundi kulingana na vipengele vya swali. Wakati wa kusikiliza wanafunzi wachukue kalamu na karatasi na kuandika wahusika, dhamira kuu na ujumbe. Baadaye kazi iwasilishwe mbele ya darasa.*

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kazi hii ifanyike katika makundi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kushirikiana na kutoa maoni tofauti yanayoyagusia masuala mtambuka husika. Baadaye wawasilishe kazi yao mbele ya darasa.*

### 18.4.6. Utungaji

*Hii ni kazi ya kibinafsi. Inaweza kufanyika darasani ama nyumbani. Katika zoezi hili inawabidi wanafunzi kutegemea utafiti katika maktaba, kwenye mtandao wa intaneti, n.k.*

## 18.5. Muhtasari wa Mada

**MUHTASARI, FANI NA MAUDHUI KATIKA HADITHI SIMULIZI** ni mada ya tatu katika kitabu cha Kiswahili, Kidato cha nne. Mada hii imeundwa na masomo matano kama ifuatavyo:

**Somo la kwanza: Maana ya muhtasari na sifa zake**

Somo hili linagusia maana ya muhtasari wa habari pamoja na sifa zihitajiwazo ili muhtasari uwe unapendeza.

**Somo la pili: Taratibu za kutoa muhtasari mzuri**

Kama mojawapo ya kazi za kifasihi, muhtasari huwa na taratibu za kufuata wakati wa kutoa muhtasari wa kazi ya fasihi fulani. Kwa hiyo, somo hili limezizingatia taratibu muhimu za kuiongoza kazi ya kutoa muhtasari mzuri.

**Somo la tatu: Fani katika hadithi simulizi**

Kila kazi ya sanaa huwa na umbo lake linaloitofautisha na kazi zingine. Umbo au funiko hilo ndilo liitwalo fani. Somo hili limeyataja mambo muhimu yanayoiunda fani ya hadithi simulizi.

**Somo la nne: Maudhui katika hadithi simulizi**

Fani yenyewe haitoshi kuifanya kamilifu kazi ya sanaa. Ni lazima maudhui yashirikishwe kuunga mkono na kuambatanishwa na fani. Katika somo hili la nne, vipengele vya maudhui ndani ya hadithi simulizi vilitiliwa mkazo ili mwanafunzi aweze kueleza kimsingi tofauti iliyopo kati ya fani na maudhui.

**Somo la tano: Uhakiki wa hadithi simulizi**

Msanii wa kazi za fasihi simulizi huongozwa na fani na maudhui katika ufundi wake. Ndipo anapohitilafiana na wasanii wengine kulingana na ubingwa wake wa kuoanisha fani na maudhui katika kazi yake. Katika somo la tano, mwanafunzi amefahamu maana ya uhakiki, mhakiki ni mtu gani pamoja na kuhakiki kazi ya sanaa. Ameshirikishwa pia kimatendo kuihakiki hadithi simulizi kwa kuzingatia pamoja vipengele vya fani na maudhui.

## 18.6. Maelezo ya Ziada

Sehemu hii inahusu maelezo ya ziada kwa mwalimu. Sehemu hii inamsaidia mwalimu kuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu mada.

## 18.7. Tathmini ya Mada

*Mwalimu ayaunde makundi ya wanafunzi kulingana na idadi yao pamoja na idadi ya kazi husika. Wanafunzi wasome hadithi " Jongoo na chura". Wafanye muhtasari wa hadithi pamoja na kuonyesha fani na maudhui vya hadithi hii. Wabainishe majina ya ngeli ya PA-M-KU- yaliyotumiwa hadithini na kueleza kanuni za matumizi yake.Kila kundi liwasilishe kazi yao mbele ya darasa. Mwalimu asahihishe makosa ya kimaandishi na kimatamshi.*

**Mwongozo wa majibu pendekezo**

**UHAKIKI WA"JONGOO NA CHURA"**

**Mfano wa muhtasari pendekezo**

Jogoo na Chura walikuwa marafiki sana. Chura alikuwa na tamaa ya kuwa na ngozi nyororo na laini kama ile ya jongoo. Jongoo alimueleza mbinu anazotumia kutengeneza ngozi yake. Chura alimzuia na kumhakikishia kuwa ameelewa. Kutokana na kusikia vibaya kwa chura, alifika nyumbani na kumuamrisha mkewe kumueka katika mafuta yaliyochemka. Chura alijiweka katika mafuta. Kwa bahati nzuri akanusuliwa na mkewe. Ujinga wa chura ndio uliosababisha kubabuka ngozi na kupelekwa hospitalini.

A. **Uhakiki wa fani**

1. **Wahusika na tabia zao**

Hadithi "Jongoo na chura" ni aina ya hurafa, yaani wahusika wake ni wanyama tu kama ifuatavyo:

- **Chura**

Ni mhusika mkuu mwenye tabia ya tamaa, majivuno, mjuaji, mjinga.

- **Tamaa:** Chura alionyesha tabia ya tamaa mwanzoni mwa hadithi. Alikuwa anatamani ngozi nyororo kama ile ya jongoo.
- **Majivuno:** Chura alidhihirisha tabia hii wakati jongoo alipoanza kumwelezea jinsi ngozi yake ilivyokuwa nyororo na laini. Alimkata kauli kwa majivuno kumuonyesha kwamba ameshaelewa.

- **Mjuaji:** Tabia hii huonekana wakati chura alivyoonyesha kwamba ameelewa maelezo ya jongoo na wakati alipofika nyumbani alijifanya mjuaji kwa mkewe kumbe ni mjinga mtupu.

- **Ujinga**: Ujinga wa chura hudhihirishwa wakati aliposisitiza kutumbukizwa katika mafutayaliyochemshwa bila kufikiri kuhusu kitakachofuata.

- **Jongoo**

Alikuwa mshauri mzuri, mwenye ukweli na anayependa kusifiwa.

- **Mshauri mzuri:** Jongoo alimshauri chura ingawa hakufuata ushauri wake.
- **Mwenye ukweli:** Ukweli wa jongoo huonekana mwishoni mwa hadithi wakati alipowaambia ukweli wazee na majirani wa chura.
- Jongoo alikuwa anapenda kusifiwa kwa kuwa katika hadithi alifurahi kuambiwa kwamba alikuwa na ngozi nyororo.
- **Mkewechura** alikuwa **na busara au hekima:** Yeye aliyahisi/ aliyachungulia mambo makali ambayo yangalimsibu mumewe kama angalijitumbukiza katika mafuta ya moto katika kikaango
- Majirani wa chura walikuwa na **moyo wa kusaidiana.** Wakati mke wake chura alipowaita, walikuja na kutoa mchango wa kumpeleka mgonjwa hospitalini bila kusitasita.
- Wazee waliohudhuria msiba walikuwa wasikivu kwa kuwa walimtega masikio jongoo na hawakumshtaki makosa.

**2. Muundo**

Msanii wa hadithi ya jongoo na chura alitumia muundo msago. Alisimulia matukio kuanzia tukio la kwanza hadi la mwisho kwa namna yalivyotukia. Alitumia muundowa moja kwa moja.

**3. Mandhari**

Katika hadithi ya Jongoo na Chura kuna mandhari ya kubuni. Mahali ambapo Jongoo na Chura walikuwa hapajulikani waziwazi kutokana na kuwa hadithi hii ni ya kubuni.

**4. Mtindo**

Hadithi ya Jongoo na Chura ni hadithi ya kimasimulizi iliyowekwa katika maandishi kwa mtindo wa kinathari. Katika hadithi hii msimulizi hutumia lugha ya kisanaa ambayo ni rahisi kueleweka kwa kila mzungumzaji wa Kiswahili.

**5. Lugha**

Msanii wa hadithi jongoo na chura alitumia nahau kama :

- Kukata kauli
- Kupigwa na bumbuazi .

B. Uhakiki wa maudhui

1. **Dhamira**

**Dhamira kuu**:Hasara ya majivuno. Chura alijivuna na mwishowe akapata hasara.

Kuna watu wasioweza kusikiliza vizuri maonyo waliyoyapewa na wengine, wakajivuna na wakawakata kauli wenzao kabla ya kuelezwa vizuri baadaye wakajiweka balaani kama mzee Chura.

**Dhamira ndogondogo**

Urafiki kati ya chura na jongoo

**Tamaa :** Chura alikuwa na tamaa ya kuwa na ngozi nyororo na laini

**Haki ya kijamii :** Majirani wa chura hawakumhukumu jongoo baada ya balaa uliotokea. Walimtega masikio na kuamua kuwa Chura alisababisha balaayake mwenyewe kwa ujinga wake.

**Maridhiano :** Mke wake chura hakumkasirikia jongoo baada ya balaa iliyomfika mume wake. Majirani zake chura nao walihudhuria wakati wa balaa ya jirani yao.

**Umuhimu wa wazee katika jamii:** Chura alipofikwa na janga, wazee waliitwa ili wakate shauri kama Jongoo amekosea au la.

2. **Migogoro**

Msanii aliiunda migogoro kama ifuatavyo:

- Tamaa ya chura kubadili mwili wake wa kawaida na kupata ngozi nyororo
- Madai ya kuyasikiliza vyema mashauri ya jongoo
- Sharti za chura kutumbukizwa kwenye kikaango
- Mahakama ya jadi au haki ya kijamii

3. **Falsafa**

Msanii ameelewa sana tabia tofauti za watu wa jamii anayoitolea ujumbe: urafiki, tamaa, majivuno, pamoja na mahakama ya kijadi.

4. **Ujumbe**

- Kusikiliza kwa makini au kufikiri sana kabla ya kutenda jambo. Ni lazima kuwa na tafakuri tunduizi kabla ya kutenda jambo.
- Kutoongozwa na shauku: Wahenga walisema kuwa tamaa mbele mauti nyuma. Haya ni kusema kwamba ni lazima mtu aridhike na jinsi alivyo bila tamaa ya kuharakisha mchakato wa kufikia lengo.

5. **Msimamo wa msanii :** Urafiki baina ya mtu na mwingine huendelea hata baada ya shida au janga fulani.

- Hii ni sehemu ya majibu kwa kila swali la tathmini kutoka kitabu cha mwanafunzi .

- Kitabu cha mwalimu kinapendekeza maswali ya ziada na majibu yatumiwayo kutathmini uwezo upatikanao katika mada.
- Maswali yote ya tathmini yanapangwa kwa lengo la kutathmini uwezo upatikanao katika mada..

## 18.8. Mazoezi ya Ziada

### 18.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji

Mapendekezo ya maswali na majibu ya kuwasaidia wanafunzi wenye uwezo chini.

***Chagua jibu sahihi kati ya yale ambayo yamewekwa katika mabano***

1. Mimi ninaishi mahali pazuri. Mahali (kwao, kwangu, pao) panafurahisha.
2. Mukaneza anapenda kulala pahali safi. Pahali (kwangu, pake, kwao) ni safi.
3. Tunatembea mahali panapopendwa na watu kadhaa. Mahali (yetu, kwetu, yao) panajulikana.
4. Wanafunzi wangu husomea mahali papana. Mahali (yangu, mwao, kwetu) ni pazuri pa kusomea.
5. Mtoto yule analala mahali panapopendwa na wazazi wake. Mahali (yako, kwake, yetu) panapendwa na wazazi.

**Majibu:**

1. Mimi ninaishi mahali pazuri. Mahali kwangu kunafurahisha.
2. Mukaneza anapenda kulala pahali safi. Pahali pake ni safi.
3. Tunatembea mahali panapopendwa na watu kadhaa. Mahali kwetu panajulikana.
4. Wanafunzi wangu husomea mahali papana. Mahali mwao ni pazuri pa kusomea.
5. Mtoto yule analala mahali panapopendwa na wazazi wake. Mahali kwake panapendwa na wazazi.

### 18.8.2. Mazoezi Jumuishi

1. ***Sahihisha sentensi zifuatazo kwa kuzingatia matumizi bora ya vivumishi vya kuuliza pamoja na viambishi nafsi vya vitenzi ambatana.***

a. Mahali wapi kunapatikana maisha bora?
b. Njiani ipi paliandikwa maagizo kuhusu usafi na uhifadhi wa mazingira?
c. Chumbani papi kunalala watoto?
d. Dirishani mpi mmewekwa orodha ya vitambulisho vya shule?
e. Mguuni wapi pamezungumziwa kuwa na kidonda?

2. ***Tega sikio hadithi fulani uliyopewa. Zungumzia wahusika wake, dhamira pamoja na ujumbe, baadaye wasilisha kazi yako mbele ya darasa.***

**Majibu ya swali la 1**

a. Mahali **papi pa**napatikana maisha bora?

b. Njiani **kupi ku**liandikwa maagizo kuhusu usafi na uhifadhi wa mazingira?

c. Chumbani **mpi m**nalala watoto?

d. Dirishani **kupi ku**mewekwa orodha ya vitambulisho vya shule?

e. Mguuni **kupi ku**mezungumziwa kuwa na kidonda?

**Majibu ya swali la 2**

*Hadithi ya kutolewa na mwalimu inaweza kuwa imerekodiwa, imesimuliwa au imesomewa mwanafunzi. Hapa inategemea uchaguzi au mahitaji ya mwalimu. Kazi hii ifanyike katika makundi kulingana na vipengele vya swali. Wakati wa kusikiliza wanafunzi wachukue kalamu na karatasi na kuandika wahusika, dhamira kuu na ujumbe. Baadaye kazi iwasilishwe mbele ya darasa.*

### 18.8.3. Mazoezi ya Nyongeza

Mapendekezo ya maswali na majibu kwa wanafunzi werevu wenye kipaji cha hali ya juu.

*Kwa mwongozo wa maelezo hapo juu fanya muhtasari wa kifungu hiki cha habari cha hapo chini kwa njia ya maandishi na masimulizi.*

**Sungura na Mamba**

Hapo zamani Mamba alikuwa na meno mazuri sana. Wanyama wengi waliyapenda meno yake. Baadhi yao walisikia wakitia chumvi kuwa meno ya mamba yalikuwa na thamani sawa na dhahabu.

Mamba huyo alipotangaza nia yake ya kujipatia jiko karibu kila mnyama aliyekuwa na binti mzuri alitaka binti yake aolewe naye. Hivyo mabinti wengi walionekana wakijipitisha mbele ya Mamba huku mmoja akiwa amekuwa vizuri ili kuweza kuliteka penzi lake.

Hali hiyo haikumpendeza kabisa Sungura kwani miongoni mwa wasichana waliotia fora kwa uzuri, alikuwa mmoja ambaye alimpenda sana, Sungura alikuwa akiwaza la kufanya ili kumwangusha mamba.

Siku moja Sungura alipita nyumbani kwa mamba, na kumkuta amelala fofofo chini ya kivuli cha mti huku meno yake mazuri yakionekana waziwazi. Hapo Sungura aliweza kuyaona maganda mengi ya njugu nyasa na akagundua kuwa mamba alikuwa akitafuna karanga.

Siku nyingine Sungura alikuja tena nyumbani kwa mamba na kumwambia”Rafiki yangu nimekuchukulia zawadi nzuri uipendayo.”Zawadi gani?” “Njugu nyasa”, alijibu Sungura huku akimwonyesha mamba mfuko uliojaa karanga.

Mamba alipouona mfuko huo, aliurukia mfuko akaliingiza domo lake refu ndani na kuanza kutafuna kwa pupa. “Mama wee !” Mamba alisikika akilia huku mikono yake akishikilia mdomo wake ambao sasa umejaa damu. Meno yake mengi yaling’oka pia. Kumbe ndani ya mfuko ule Sungura aliweka mawe mengi na njugu nyasa chache tu.

Mamba alipojaribu kutafuna alichofikiria kuwa ni karanga, meno yake mengi yaling'oka.

Sungura alipoona mbinu yake imefaulu, aliondoka na kuelekea kwake kwa furaha. Siku moja jioni, wanyama wengi walishangaa kumuona Sungura alikuwa amevaa miwani na kupepesuka ovyo. Kumbe alikuwa akisherehekea ushindi wake dhidi ya mamba.

Habari za mamba kuing'olewa meno yake zilienea kwa haraka sana. Wasichana wote walipopata habari hizo, walibadilisha mawazo yao ya kutaka kuolewa na mamba ambaye sasa alikuwa kibogoyo na kuchukiza sana.

*Zoezi hili liwe la kibinafsi. Mwalimu amuombe mwanafunzi kusoma kifungu cha habari. Mwanafunzi afanye muhtasari wa kifungu cha habari kimaandishi na baadaye asimulie hadithi mbele ya darasa. Mwalimu arekebishe makosa ya kimaandishi na kimasimulizi yaliyojitokeza.*

# MADA KUU YA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

4

## MADA NDOGO YA 4: MIDAHALO NA MIJADALA

### Uwezo Upatikanao katika Mada

Kuweza kuelewa mwongozo wa midahalo na mjadalo na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujiandaa na mdahalo kwa kutafiti na kuandika hoja atakazotumia, kujua jinsi ya kutoa amri kwa vitenzi.

### Ujuzi wa Awali

Kwenye mada ya tatu katika kidato cha nne, mwanafunzi alisoma masomo yenye uhusiano na mada hii. Masomo hayo ni: ufahamu, muhtasari, fani na maudhui katika hadithi simulizi. Masomo haya yalipanua ujuzi wa mwanafunzi na kumwezesha kufahamu na kuongea Kiswahili kwa ufasaha. Pia katika kidato cha tatu wanafunzi walijifunza somo la mdahalo na mjadala.

Masomo hayo ya awali yatamsaidia mwanafunzi kufahamu mada kuu ya nne ambayo ni UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO pia yatamsaidia kusoma kwa urahisi mada ndogo ambayo ni, « MIDAHALO NA MIJADALA » . Mwalimu hatapoteza muda wake kwa kuwafundisha wanafunzi maneno mwafaka ya kutumia katika maongezi ya lugha ya Kiswahili. Kwa ufupi, ujuzi uliotokana na mada za awali utamsaidia mwalimu kupata muda wa kutosha wa kuendelea na mada hii.

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro, majadiliano, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, kuandika, kuzungumza, na katika mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

- **Mafunzo kuhusu amani na mwenendo mwema**

Midahalo na mijadala ni aina za majadiliano zinazotumiwa ili kudumisha amani na maendeleo katika jamii. Mwalimu anapofundisha :

- Katika mdahalo au mjadala wanafunzi wanakuwa na mitazamo tofauti kuhusu mada fulani. Ingawawanatofautiana kimawazo si sababu ya kugombana au kuleta chuki kati yao. Lakini mijadala na midahalo ni njia bora mojawapo ya kujielimisha na kuongeza ujuzi kutoka mada husika. Mambo haya yote hufanyika kwa amani na heshima.

- Wanafunzi watunge vifungu kuhusu mada ambazo huzungumzia namna ya kudumisha amani na maendeleo katika jamii.
- Mifano ya sentensi itakayotolewa na wanafunzi iwe inasisitizia umuhimu wa amani katika maendeleo ya jamii.

- **Mila na desturi na uchunguzi wa viwango**

Kwa kufanya kazi kuhusu mada za midahalo na mijadala, wanafunzi wawe na desturi ya kuheshimu muda na kutimiza malengo yao katika kazi. Mwalimu awasaidie kufahamu kwamba ni lazima kuheshimu kazi na kutimiza malengo ya kazi kwa muda.

- **Elimu kwa wote au Elimu isiyo na ubaguzi**

Baadhi ya mada zitakazungumziwa katika mada hii zitawaelezea wanafunzi umuhimu wa elimu kwa wote. Wewe mwalimu, unalazimika kuwaonyesha wanafunzi kwamba elimu haina mpaka na kwamba kila yeyote ana uhuru wa kupata elimu bila ubaguzi wa aina yoyote. Kwa mfano, katika uundaji wa makundi mwalimu ahakikishe kwamba kila mwanafunzi na hata wale wenye mahitaji maalum wanashirikishwa katika midahalo na mijadala.

- **Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia**

Katika vifungu, mijadala na midahalo au katika mifano ya sentensi, mwalimu kwa kutumia majadiliano awasaidie wanafunzi kufahamu mbinu za kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa na namna inayotumiwa ili wazazi wazae watoto ambao wana uwezo wa kuwalea kama ipasavyo na kukidhi mahitaji yao.

- **Mazingira na maendeleo endelevu**

Mwalimu kupitia mazoezi ya midahalo na mijadala au ya msamiati na sarufi, anaweza kuwasaidia wanafunzi kufahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira katika maisha ya watu.

- **Usawa wa jinsia**

d. Mwalimu katika mifano yote, ni lazima kutoa mifano inayoonyesha usawa wa jinsia.
e. Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia.
f. Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili wanafunzi waelewe kuwa wavulana na wasichana wanaposhirikiana wanatimiza malengo kwa urahisi.
g. Mada zinazojadiliwa, zilete dhana ya usawa wa jinsia.

## Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada

Kwa kutangulia mada, mwalimu awaulize maswali yafuatayo ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua mada hii na kuzusha shaukuya kutafuta ujuzi utakaopatikana katika ujifunzaji wa mada hii.

Mwalimu auulize maswali yafuatayo:

1. Majadiliano ni nini?
2. Kuna aina zipi za majadiliano?
3. Mdahalo ni nini?
4. Mjadala ni nini?
5. Jadili umuhimu wa mdahalo na mjadala

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Somo la | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza: maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | **Maanaya mdahalo na mjadala** | **Maarifa na ufahamu:**<br>• Kuonyesha uwezo wa kufanya mdahalo na mjadala kutokana na maandalizi ya awali yaliyoegemea katika utafiti.<br>• Kueleza jinsi ya kutoa amri kwa kutumia hali ya kushurutisha kwa vitenzi<br>**Stadi:**<br>Kujiandaa awali kabla ya mdahalo au mjadala kwa utafiti na kupangilia hoja za mdahalo na mjadala<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>Kuonyesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano | 10 |
| 2 | **Tofauti na uhusiano kati ya Mdahalo na mjadala** | **Maarifa na ufahamu :**<br>Kukumbuka tofauti na uhusiano uliopo kati ya mdahalo na mjadala<br>**Stadi:**<br>Kutofautisha na kuhusisha mdahalo na mjadala<br>**Maadili na mwenendo:**<br>Ushirikiano, urafiki na kujiamini | 10 |

<table>
<tr><td>3</td><td>Utekelezaji wa mdahalo</td><td>Maarifa na ufahamu:<br>Kukumbuka taratibu za kufuata wakati wa kutoa hoja katika makundi<br>Stadi:<br>• Kutumia ishara za mwili kulingana na hoja inayotolewa<br>• Kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia na kuridhisha<br>• Kuonyesha upande wake katika kutoa hoja zake (mtetezi au mpinzani)<br>Maadili na mwenendo mwema:<br>• Kushindana kwa hoja bila kupigana wala kugombana<br>• Kukubali na kutokubaliana na kuheshimu mawazo ya watu wengine</td><td>14</td></tr>
<tr><td>4</td><td>Utekelezaji wa mjadala</td><td>Maarifa na ufahamu:<br>• Kutafsiri mazingira ya mada na kuijadili bila upotovu wowote<br>• Kutambua lugha inayofaa katika majadiliano<br>Stadi:<br>• Kutoa suluhisho katika majadiliano kwa kutetea hoja zinazomkera<br>Maadili na mwenendo mwema:<br>• Kusikiliza mawazo ya watu wengine hata kama hakubaliani nayo</td><td>13</td></tr>
<tr><td colspan="3">Tathmini ya mada</td><td>2</td></tr>
<tr><td colspan="3">Vipindi vya mada</td><td>49</td></tr>
</table>

# SOMO LA 19: MAANA YA MDAHALO NA MJADA

## 19.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Somo hili linahusu maana ya mdahalo na mjadala. Mwalimu aanze somo kwa kuwasisimua wanafunzi.

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kukumbuka na kufahamu zaidi somo lililotangulia. Atakapomaliza kuwauliza maswali ya kuwakumbusha somo la awali, mwalimu awasaidie wanafunzi kuingia katika somo linalohusika ambalo ni "Maana ya mdahalo na mjadala". Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yawezekanayo ili kuwafanya wanafunzi wagundue somo lenyewe.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro ulioko katika kitabu cha mwanafunzi kuhusu maana ya mdahalo na mjadala. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Tazameni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- Watu unaowatazama kwenye mchoro huo wanafanya nini?
- Eleza shughuli za watu hao kwenye mchoro hapo juu.
- Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na mtu wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine. Mwisho wake mwalimu atoe maoni yake kuhusu yaliyofanywa na wanafunzi kwa kurekebisha yaliyofanywa kwa namna isiyo bora.

Kutokana na majibu tofauti yaliyotolewa, mwalimu asisitizie yale ambayo yanawaingiza wanafunzi katika somo jipya.

## 19.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute na atumie ipasavyo vifaa ambavyo vitamsaidia kutimiza malengo ya somo. Baadhi ya vifaa vinavyohitajika ni pamoja na:

- Kitabu cha mwanafunzi.
- Meza duara.
- Redio.
- Runinga.
- Taarifa zilizorikodiwa.
- Vifaa vya kunasia sauti.
- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati na vinginevyo

Mwalimu anaweza kutafuta zana zingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo. Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake. Mwalimu kwa ubunifu wake aandae vifaa vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo.

## 19.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika kipindi hiki, mwalimu atafute mbinu mwafaka zinazomuezesha kufanikisha malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atayazingatia yafuatayo:

- Njia shirikishi: Wanafunzi wagawanyike katika makundi na mchango wa kila mwanafunzi katika kundi udhihirike. Mbinu hii itumiwe kwa maswali ya ufahamu, misamiati, sarufi na utungaji.
- Njia isiyoshirikishi: Mwanafunzi apewe kazi yake binafsi kwa kutunga sentensi, kujibu maswali kuhusu sarufi na kuongea mbele ya wenzake bila woga
- Maswali na majibu: wanafunzi waulizane maswali kati yao na kuyatolea majibu wao wenyewe kwa kusaidiwa na mwalimu au mwalimu awaulize wanafunzi maswali kwa kutumia namna kadhaa. Mwalimu atumie mbinu hii katika sarufi na matumizi ya lugha.
- Utafiti: wanafunzi wapewe kazi ya nyumbani ya kufanya utafiti kuhusu maana ya mdahalo na mjadala kwa kutumia vitabu na tovuti.

## 19.4 Majibu

**Zoezi la 1a:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchoro huo.*

### 19.4.1 Majibu ya Ufahamu

1. Kila mwaka wanafunzi hukutana katika shughuli za mazungumzo na majadiliano kwa madhumuni ya kukuza uwezo wao wa kuzungumza kwa ufasaha lugha ya Kiswahili.
2. Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya jambo moja maalumu. Katika mdahalo wazungumzaji hupata fursa ya kuonyesha fikra zao na mawazo yao kuhusu mada iliyotolewa. Kwa kuwa majadiliano haya huzihusisha pande mbili zenye misimamo tofauti. Katika mdahalo ni lazima tuwe na mwenyekiti na katibu. Mwishoni mwa mdahalo ni lazima kuwe na upande mmoja ulioshinda.
3. Mjadala ni mazungumzo juu ya jambo maalumu yanayofanywa kwa kutolea hoja jambo hilo. Katika mjadala hakuna pande zenye misimamo tofauti. Na mwishoni mwa mjadala hakuna mshindi. Kiongozi anatoa suluhisho.
4. Mdahalo unaongozwa na mwenyekiti.
5. Kazi ya katibu katika mdahalo ni kuandika maoni yaliyotolewa na wasemaji wa kila upande, kuyasomea hadhira maoni hayo, kuhesabu kura na kuzitangaza.
6. Katika mdahalo kuna pande mbili: upande wa utetezi na wa upinzani.
7. Katika mjadala hakuna upande wowote.

8. Mjadala una lengo la kukuza uwezo wa kufikiri na kutafuta masuluhisho kwa masuala yanayoikumba jamii.
9. Stadi zinazopatikana katika mdahalo na mjadala ni kumpa mwanafunzi uwezo wa kushawishi watu katika hadhira na kutambua binafsi kipawa chake cha kuzungumza na haiba yake mbele ya wenzake, kuzoea kuheshimu muda aliopewa na kuweza kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri, kukuza stadi ya utumiaji wa lugha, kusikiliza na kupima maoni na hoja za wenzao, kuelewana na wengine kutoka sehemu mbalimbali za nchi, kuheshimiana kulingana na mawazo tofauti yanayotolewa na kila mzungumzaji, kudumisha udugu, umoja, amani na maridhiano kati yao. Kukuza uwezo wa mawasiliano, majadiliano, mahojiano, ujuzi wa kutoa maoni yake na kujitambua katika jamii yake.
10. Kutokana na kifungu hiki nilijifunza mengi. Miongoni mwa hayo ni pamoja na maana ya mdahalo na mjadala, namna mdahalo na mjadala unavofanywa, wahusika wa mdahalo na wa mjadala, lengo na umuhimu wa mdahalo na mjadala .

### 19.4.2 Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo na Mjadala

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Sentensi pendekezo**

1 Wanafunzi wengi wanapenda kushiriki katika mdahalo.
2 Mwenyekiti hutoa suluhisho mwishoni mwa mjadala.
3. Katibu anaandika hoja zinazotolewa na wasemaji.
4 Washiriki wa mjadala wanatoa maoni ya kuinua uchumi.
5. Msemaji mkuu anatetea mada iliyochaguliwa.
6. Upande wa upinzani unapinga maoni ya upande wa utetezi.
7. Mwenyekiti anahakikisha kuwa wasemaji wanaheshimiana.
8. Wanafunzi wawe na nidhamu katika mazungumzo ya kila mwaka.
9. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na mwenendo mwema.
10. Mdahalo unamsaidia mwanafunzi kujua haiba yake.

**Zoezi la 3:**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.*

| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| B | F | G | i | m | j | k | a | n | b | l | d | c | h | c |

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuzingatia maana ya kila neno. Mwalimu awaelekeze wanafunzi na ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anashiriki.*

Majibu

1. Katika mdahalo mwenyekiti ndiye ambaye anachagua atakayesema.
2. Anayeshiriki katika mazungumzo anakuza utumiaji wa lugha.
3. Washiriki wa mjadala ni lazima watoe maoni yao bila kuegemea kwa upande wowote.
4. Mjadala ni mazungumzo yanayohusisha watu wengi.
5. Midahalo na mijadala humsaidia mwanafunzi kutambua kipawa chake.
6. Mdahalo humsaidia mshiriki kuwa na moyo wa kuheshimu mawazo ya wengine.
7. Kuelewa mada ni chanzo cha kutoa maoni mazuri.
8. Katibu wa mdahalo anaandika hoja zilizotolewa na wasemaji.
9. Kila mtu aliyealikwa anaombwa kushiriki katika majadiliano.
10. Mwanafunzi wa lugha anajizoeza kutumia matamshi mazuri wakati wa mdahalo.

### 19.4.3 Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha katika Vitenzi vyenye Kiambishi Tamati -a hali yakinishi.

**Zoezi la 5 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wajadili kuhusu maana ya sentensi zenye dhana ya kushurutisha.*

1. **Simama** utoe maoni yako.
2. **Wapigieni** makofi washindi.

Baadaye mwalimu aombe wanafunzi watoe sentensi tano zenye dhana ya kushurutisha

Hii ni mifano pendekezo ya sentensi hizo:

1. Jiungeni katika makundi ya watu wanne wanne.
2. Soma kifungu cha habari.
3. Andikeni maoni mnayoyatoa.
4. Toa maoni yako kuhusu maana ya mjadala.
5. Kabla ya kuzungumza, omba ruhusa mwenyekiti.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi kwa kuiga mfano uliotolewa, waelekezwe katika kujibu maswali ya zoezi hili.*

*Majibu*

1. “Timiza kazi yako ya shule kuhusu mjadala”. Mama alimuamrisha mtoto wake.
2. Mwalimu alimuomba mwanafunzi akisema, “Futa ubao tuandike mada ya mdahalo”.
3. Baada ya kuamkia wanafunzi, mwalimu aliwaambia, “ Jiungeni kwa makundi ya utetezi na upinzani”.
4. Kama uko kwenye upande wa utetezi, tetea mada iliyotolewa.
5. Kama uko kwenye upande wa upinzani, unga mkono wapinzani.
6. Mwenyekiti alimuambia msemaji mkuu: “Toa mawazo yako”.
7. Pigieni makofi washindi.
8. Kiongozi wa mjadala aliiambia hadhira: “Nyamazeni tuanze mjadala”.
9. Katibu aliombwa na mwenyekiti: “Andika mawazo yote yatakayotolewa”.
10. Ikiwa unataka kukuza maongezi yako ya lugha, hudhuria midahalo na mijadala.

**Zoezi la 7:**

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, watunge sentensi kumi kwa kutumia hali ya kushurutisha kisha kila kundi limchague mwasilishaji awasilishe sentensi walizotunga. Kutokana na sentensi zitakazotolewa na wanafunzi mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuhakiki na kurekebisha sentensi zilizotungwa na wanafunzi.*

### 19.4.4 Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo na Mjadala

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, wapange maneno kwa utaratibu unaofaa ili yaweze kuleta maana katika sentensi kamili. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.*

**Majibu:**

1. Mjadala humsaidia mwanafunzi kukuza hali ya udadisi na kukuza uwezo wa kitaaluma.
2. Mdahalo huwafanya wanafunzi kuepukana na uoga wa kuzungumza hadharani.
3. Katika mjadala kila yeyote ambaye ana la kusema huonyesha ishara.

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kisha wajibu maswali kuhusu maelezo waliyoyasoma. Mwalimu awaelekeze katika kusoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi.*

**Majibu**

1. Mdahaloni, majadiliano baina ya watu wengi juu ya mada fulani. Unahusisha pande mbili yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani.
2. Mjadala ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Unaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.
3. Wajibu wa kiongozi wa mjadala ni kuendesha mjadala, kumpa fursa anayetaka kusema, kuhakikisha kuwa kila msemaji anaheshimu muda, kutoa suluhisho mwishoni mwa mjadala.
4. Washiriki wa mdahalo ni mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetezi na upinzani, na wasikilizaji washiriki.
5. Watu wanaoshiriki katika mjadala ni kiongozi wa mjadala na hadhira.

### 19.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano katika Jamii

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu aombe wanafunzi kufanya makundi ya wanafunzi wawili wawili, kishawajadili kuhusu "**Nafasi ya midahalo na mijadala katika jamii**" akisisitizia umuhimu wa majadiliano kama vile midahalo na mijadala katika kudumisha amani katika jamii.

- Mawazo yanayoweza kutolewa na wanafunzi:
- Midahalo na mijadala huleta uelewano kati ya watu.
- Midahalo na mijadala hudumisha amani katika jamii.
- Midahalo na mijadala ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.
- Midahalo na mijadala hutumiwa kama wenzo bora ya kutatua migogoro kati ya watu.
- Midahalo na mijadala huwasaidia watu kuwaheshimu watu wengine na kusikiliza na kuheshimu maoni ya wengine ingawa wana maoni tofauti na yako.

### 19.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watunge kifungu cha habari kuhusu mada walizopewa kwa kuzingatia matumizi ya hali ya kushurutisha kwa vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja na ambavyo vina kiambishi tamati-a*

Hapa, mwalimu awaombe wanafunzi kuelekeza fikra zao kwenye nafasi ya majadiliano katika kudumisha amani na maendeleo katika jamii.

Mawazo yanayoweza kutolewa na wanafunzi

i. "Majadiliano huimarisha ushirikiano"

- Majadiliano huwawezesha watu kuelewana
- Mawasiliano huwajulisha watu tatizo lililopo na kuwawezesha kuweka mikakati ya kutatua tatizo hilo.

- Majadiliano ni namna bora ya kutatua migogoro kwa njia ya amani
- Majadiliano huimarisha amani na maendeleo

ii. "Nafasi ya mijadala katika maendeleo ya jamii"

- Mijadala huleta uelewano kati ya watu.
- Mijadala hudumisha amani katika jamii.
- Mijadala ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.
- Mijadala hutumiwa kama wenzo bora wa kutatua mogogoro kati ya watu.
- Mijadala huwasaidia watu kuwaheshimu watu wengine na kusikiliza na kuheshimu maoni ya wengine ingawaje wana maoni tofauti na yako.

## SOMO LA 20: MDAHALO NA MJADALA

### 20.1 Ujuzi wa Awali/Utangulizi

Mwalimu amuulize mwanafunzi mmoja mmoja maswali ambayo yataowasaidia wanafunzi wote kukumbuka na kufahamu zaidi somo la awali, mwalimu ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anakumbuka maana ya mdahalo na mjadala. Watakapomaliza kujibu maswali ya kujikumbusha maana ya mdahalo na mjadala mwalimu awaombe wanafunzi kuchukua vitabu vya Kiswahili watazame mchoro unaohusu uhusiano na tofauti kati ya mdahalo na mjadala.

*"Eleza yale unayoyaona kwenye mchoro hapo juu".*

Kila kundi limchague mwanafunzi mmoja wa kuwasilisha kazi walioifanya. Kutokana na majibu mengi yatakayotolewa, mwalimu awaelekeze wanafunzi kugundua somo lenyewe linahusu nini.

### 20.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

- Mchoro wa watu wanaozungumza katika mdahalo na mjadala
- Kitabu cha mwanafunzi.
- Kamusi ya Kiswahili Kanifu.
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu,
- Kitabu cha mwanafunzi.
- Meza duara.
- Redio.
- Runinga.
- Taarifa zilizorikodiwa.
- Vifaa vya kunasia sauti.
- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati na vinginevyo

Mwalimu atumie kifaa kimoja kati vifaa hivyo vilivyotolewa, anaweza pia kuchanganya na kubadili vifaa kutokana na malengo pamoja na mazingira ya shule.

## 20.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu achague mbinu mbalimbali zitakazomuezesha kufika kwenye malengo ya somo husika. Katika somo hili mwalimu asisitizie:

- Utumiaji wa makundi ya wanafunzi: Kwa sababu mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji ni lazima mbinu hii itumiwe ili kumushirikisha mwanafunzi katika mambo yote yanayofanyiwa darasani. Wanafunzi watumie makundi yao kwa kufanya kazi zote watakazoopewa na mwalimu na zile zipatikanazo katika kitabu cha mwanafunzi.
- Kazi binafsi kwa mwanafunzi: Kila mwanafunzi apewe kazi au mazoezi yake binafsi kama vile kusoma kifungu cha habari, kufanya majaribio, mitihani mbalimbali na hata kazi za nyumbani.
- Maswali na majibu: Mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali nao watoe majibu kwa maswali hayo. Wanafunzi nao waulizane maswali na wamuulize mwalimu maswali tofauti; mwalimu aelekeze kazi zote zifanyikazo darasani.
- Maelezo ya mwalimu: Mwanzoni na mwishoni mwakila kazi au zoezi, mwalimu atoe maelezo yatakayosaidia katika kutimiza malengo ya somo. Ingawa mwanafunzi ndiye kiini cha ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu analazimika kumpa mwanafunzi maelezo muhimu yatakayomsaidia kutimiza kazi na kufahamu somo pamoja na kutimiza malengo ya somo.

## 20.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchoro.*

### 20.4.1 Majibu ya Ufahamu:

1. Watu wanaohusika na lugha ya Kiswahili hujiuliza maswali kuhusu mdahalo na mjadala.
2. Mada ya mdahalo huchaguliwa kwa kupiga kura.
3. Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala na mdahalo

   Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani. Kumuezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakati anapoandika insha au habari. Kumuezesha mtu kutambua kipaji alicho na cho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira. Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
4. Mjadala na mdahalo huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.

Katika mjadala na mdahalo kuna mada ambayo hutolewa mawazo

Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa

Katika mdahalo na mjadala hakuna anayeruhusiwa kotoa hoja bila kumuomba ruhusa kiongozi.

5. Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetezi, upinzani na hadhira lakini kwenye mdahalo kuna kiongozi na hadhira tu.

   Katika mdahalo kuna wasemaji wakuu wanaotetea na wale wasiokubaliana na mada lakini

   kwenye mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi.

   Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani.

   Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.

6. Wahusika wa mdahalo ni mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetezi, wasemaji wakuu wa upande wa upinzani na hadhira lakini wahusika wa mjadala ni kiongozi (viongozi) wa mjadala na hadhira.

7. Watetezi hutoa hoja zao kwa kukubaliana na mada ya mdahalo.

8. Katika mjadala wasemaji hutoa maoni yao kwa kukubaliana au kwa kutokubaliana na mada na wasemaji wengine.

9. Mwishoni mwa mdahalo hadhira hupiga kura ili kujua washindi na washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; mwishoni kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kwa ujumla kutokana na mawazo yaliyotolewa. Katika mjadala hakuna washindi wala washinde.

10. Ninawashauri kutochagua mada ambazo hazitawawezesha kutimiza malengo yao kwani zinazozungumziwa katika midahalo hutofautiana na zile zinazojadiliwa katika mijadala.

### 20.4.2 Msamiati kuhusu Tofauti na Uhusiano kati ya Mdahalo na Mjadala

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuchunguza matumizi yake katika kifungu kuhusu mdahalo na mjadala.*

1. Watetezi wa mada kuhusu uimarishaji wa malezi kwa wote ndio waliopata ushindi.
2. Mwishoni mwa mdahalo, hadhira inalazimika kupiga kura ili kujua washindi.
3. Kila mtu analazimika kuunga mkono wale wanaotetea kwamba wazazi ni muhimu katika malezi ya watoto wao.

4. Kila mpenzi wa lugha ya Kiswahili analazimika kufahamu kuhitilafiana kwa mjadala na mdahalo .
5. Anayeshiriki mara nyingi katika mijadala na midahalo hukuza uwezo wake wa kuongea hadharani bila uoga.
6. Msemaji alichukua fursa ili aeleze kwamba malezi kwa wote hudumisha amani na maendeleo ya nchi.
7. Msemaji anaweza kutetea au kutokubaliana na mada.
8. Msemaji mkuu wa upande wa utetezi anatoa maoni yake kwa kutokubaliana na mada pamoja na maoni ya watetezi.
9. Mdahalo na mjadala hufanyika kwa madhumuni ya kudumisha amani, urafiki na uelewano katika jamii.
10. Majadiliano hutumiwa kama wenzo bora wa kutatua migogogro kati ya watu ili kujenga umoja.

**Zoezi la 3 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.*

| A | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | d | m | i | e | l | c | g | h | n | o | k | b | f | j | a |

**Zoezi la 4:**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watafute maneno yanayoweza kutumiwa katika majadiliano. Mwalimu awaelekeze wanafunzi.*

Baadhi ya maneno yaliyo kwenye mraba :

1. MADHUMUNI
2. MADA
3. ROHO
4. UROHO
5. HOJA
6. KWA NIABA
7. INAMAANISHA
8. MAANA
9. MRABA
10. RIDHAA
11. HADHIRA
12. EBU
13. ILE

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuzingatia maana ya kila neno. Mwalimu awaelekeze wanafunzi na ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anashiriki.*

**Majibu:**

1) Madhumuni ya mjadala si kushindana bali ni kutoa hoja kuhusu jambo fulani.
2) Wasemaji wakuu kwa upande wa utetezi katika mdahalo wanaitetea mada.
3) Mwenyekiti ndiye anayempangia msemaji mkuu muda wa kutoa hoja.
4) Katika mjadala hakuna kuwania ushindi.
5) Uhusiano unaohusisha mdahalo na mjadala ni lengo la kukuza uwezo wa maongezi miongoni mwa wanafunzi kwa kukuza kiwango chao cha msamiati.
6) Katika mdahalo msemaji mkuu anaweza kukiuka ukweli kwa lengo la kupata ushindi.
7) Katika mdahalo na mjadala hakuna anayeruhusiwa kutoa hoja bila kuomba fursa kwa mwenyekiti.
8) Mdahalo na mjadala ni wenzo bora wa kutatua migogoro inayoweza kuzuka kati ya watu au kati ya makundi.
9) Watu wanapaswa kufahamu kwamba kuna tofauti na uhusiano kati ya mdahalo na mjadala
10) Katika mdahalo, kila mtu ambaye ana la kusema
11) Katika mdahalo, kila mtu ambaye ana la kusema hutoa ishara ya kumjulisha kiongozi kwamba anahitaji fursa ya kusema.

### 20.4.3 Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha kwa Vitenzi vyenye Kiambishi Tamati -a katika Hali Kanushi.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

1.Wanafunzi wawili wawili watafute katika kifungu cha habari kuhusu “Uhusiano wa mdahalo na mjadala” huku wakitafuta sentensi zenye vitenzi ambavyo viko katika hali ya kushurutisha; kisha waeleze ikiwa vitenzi hivyo viko kwenye hali yakinishi au kanushi. Mwalimu achunguze ikiwa kila mwanafunzi anashiriki katika zoezi na arahisishe utimizaji wa malengo ya zoezi.

**Sentensi zenye dhana ya kushurutisha ni:**

- Usiongozehoovyo hovyo. (hali kanushi)
- Usishindwe kuongoza mdahalo ipasavyo. (hali kanushi)
- Msisahau kwamba mdahalo na mjadala ni nyenzo timamu za kuimarisha stadi ya maongezi ya Kiswahili. (hali kanushi)
- Msichague mada ambazo hazitawasaidia kutimiza malengo. (hali kanushi)

2. Kwa kuiga mifano waliyoipata kwenye kifungu cha habari walichokisoma, kwa makundi ya wawili wawili, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi kumi ambazo zina vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja na vyenye kiambishi tamati "-a" kwa umoja na wingi katika hali kanushi.

**Mifano ya sentensi:**

Hali ya kushurutisha, hali kanushi

Umoja Wingi

1. Usiseme uongo wakati wa majadiliano. Msiseme uongo wakati wa majadiliano.
2. Usiige tabia mbaya ya watu. Msiige tabia mbaya ya watu.
3. Usishindanie bure, shindania amani. Msishindanie bure, shindanieni amani.
4. Usishindwe kuzuia ubaguzi wa kijinsia. Msishindwe kuzuia ubaguzi wa kijinsia.
5. Usiharibu mazingira. Msiharibu mazingira.
6. Usizuie maendeleo endevu ya nchi. Msizuie maendeleo endevu ya nchi.
7. Usitupe tatataka njiani. Msitupe tatataka njiani.
8. Usivute sigara. Msivute sigara.
9. Usitumie dawa ya kurevya. Msitumie madawa ya kurevya.
10. Usikawie kumpeleka shuleni mtoto wako. Msikawie kuwapeleka shuleni watoto wenu.

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi waunde makundi ya wanafunzi wanne wanne, wasome maelezo muhimu na waweke sentensi za hapo chini kwenye wingi.*

1. Msiseme hadharani bira ruhusa.
2. Msipige kelele kwenye midahalo au mijadala.
3. Msiwaangalie watu kwa shingo upande wakati wa midahalo na mijadala.
4. Msiwazomee watu wakati wa maongezi
5. Msitoe mawazo hadharani kwa mambo ambayo humuyajui.
6. Msionyeshe kuwa mna uoga wa kuongea hadharani.
7. Msiwanyime fursa wale ambao wana hoja.
8. Msilete fujo kwenye midahalo au mijadala.
9. Msijidanganye kuwa midahalo ni maana ya pili ya mijadala.
10. Msiwazuie wanafunzi kufanya majadiliano.

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi kuiga mifano iliyopo kwenye kitabu cha mwanafunzi kisha waweke sentensi walizopewa katika hali ya kushurutisha. Hali yakinishi au kanushi. Mwalimu ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anashiriki.*

**majibu:**

1. Wewe, chagua mada ya mjadala.

2. Walimu, msiandae midahalo ambayo si lazima.
3. Ninyi msipende fujo katika mjadala.
4. Wewe, andaa mdahalo kuhusu usawa wa kijinsia.
5. Walimu, msikataze wanafunzi kutoa hoja kuhusu mada fulani
6. Ninyi msikubaliane na upande mwingine.
7. Wapinzani, msiunge mkono watetezi.
8. Watetezi, teteeni mada.
9. . Mwenyekiti, ongoza majadiliano.
10. Washiriki, toeni mchango wenu.

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aombe kila mwanafunzi kufanya zoezi hili kwa kuweka sentensi alizopewa katika hali kanushi. Mwalimu asahihishe majibu ya kila mwanafunzi na aelekeze wanafunzi kuandika majibu ubaoni.*

Majibu

1. Usipige kelele katika mdahalo.
2. Kiongozi, usimpangie kila msemaji muda mrefu sana.
3. Walimu, msisaidie wanafunzi kufanya mdahalo kila mara.
4. Wapinzani, msitetee mada.
5. Wanafunzi, msizungumze hadharani kila wakati.

### 20.4.4 Matumizi ya Lugha: Maana ya Mdahalo na Mjadala

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, wapange maneno kwa utaratibu unaofaa ili yaweze kuleta maana katika sentensi kamili. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.*

**Majibu pendekezo**

1. Kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kuhusu mada iliyojadiliwa.
2. Katika mjadala hakuna pande mbili yaani upinzani na utetezi.
3. Mdahalo na mjadala huwawezesha wanafunzi kuongea hadharani.

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kisha wajibu maswali kuhusu maelezo waliyoyasoma. Mwalimu awaelekeze katika kusoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi.*

**Majibu**

1. Uhusiano kati ya mdahalo na mjadala
    - Mdahalo na mjadala huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.
    - Katika mdahalo na mjadala kuna mada ambayo hutolewa mawazo
    - Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa.

- Katika mdahalo na mjadala hakuna anayeruhusiwa kutoa hoja bila kumuomba ruhusa kiongozi.

2. Tofauti iliyopo kati ya mdahalo na mjadala

   - Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetetezi na upinzani na hadhira lakini kwenye mjadala kuna kiongozi na hadhira tu.
   - Katika mdahalo kuna wasemaji  wakuu wanaotetea au wasiokubaliana na mada lakini kwenye mjadala kila yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi.
   - Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani.
   - Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.

### 20.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza: Majadiliano

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aombe wanafunzi kufanya makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadili kuhusu nafasi na umuhimu wa midahalo na mijadala katika kudumisha amani na mshikamano katika  jamii. Wanafunzi wakimaliza kujadili katika makundi, mwalimu awaombe wanafunzi wachangie na wengine mawazo waliyayatoa. Yale yaliyotolewa yasirudiwe.*

**Mawazo yanayoweza kutolewa na wanafunzi:**

- Midahalo na mijadala huleta uelewano kati ya watu.
- Midahalo na mijadala hudumisha amani katika jamii.
- Midahalo na mijadala ina mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi.
- Midahalo na mijadala hutumiwa kama nyenzo bora za kutatua migogoro kati ya watu.
- Midahalo na mijadala huwasaidia watu kuwaheshimu watu wengine na kusikiliza na kuheshimu maoni ya wengine ingawa wana maoni tofauti na yako.

### 20.4.6 Kuandika: Utungaji

**Zoezi la 13:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watunge  kifungu cha habari kuhusu mada waliyopewa "Mijadala Ndiyo Njia ya Kuinua Jchumi katika Jamii Nyingi za Kiafrika." Kazi hii ifanyike kwa makundi ya wanafunzi wanne wanne. Hapa mwalimu awaruhusu wanafunzi kuchangia kazi walizozifanya.*

**Mawazo pendekezo**

- Mijadala huwawezesha watu kugundua matatizo yanayukumba uchumi wa jamii fulani.

- Mijadala inawawezesha watu kutoa mbinu bora za kuinua uchumi kwa kuondoa umasikini.
- Mijadala huleta ushirikiano, upendo na amani; mambo haya ni muhimu katika maendeleo endelevu ya uchumi wa kila jamii.
- Mijadala huwaelezea wanajamii malengo ya jamii na mbinu za kutimiza malengo hayo ili kuinua uchumi.

## SOMO LA 21: UTEKELEZAJI WA MDAHALO

### 21.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada ndogo ya nne inahusu mdahalo na mjadala. Wanafunzi wana ujuzi kuhusu mada hii. Ujuzi wa awali walio nao wanafunzi ni :

- Maana ya mdahalo
- Maana ya mjadala
- Mambo yafanyikayo katika mjadala namdahalo
- Uhusiano kati ya mdahalo na mjadala
- Tofauti iliyopo kati ya mdahalo na mjadala

Katika somo hili, mwalimu aanze kwa kuwauliza wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kukumbuka pamoja na kuzingatia masomo waliyayasoma wakati uliopita. Kisha mwalimu awachangamshe wanafunzi, awapatie kazi ambazo zitawaingiza katika somo jipya. Awaulize maswali kwenye makundi ili wanafunzi wenyewe wagundue somo ambalo linatarajiwa kusomwa.

Kazi ya kuwaingiza wanafunzi katika somo husika ifanywe kwa kuwaomba wanafunzi kutazama michoro inayohusiana na mdahalo na mjadala inayopatikana kwenye kitabu cha mwanafunzi, kisha wajibu maswali yanayoambatana na michoro, kutokana na mitazamo pamoja na majibu tofauti kutoka kwa wanafunzi, mwalimu ajiegemeze kwenye maoni na mitazamo tofauti ya wanafunzi, kisha aanzishe somo jipya.

### 21.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute na atumie ipasavyo vifaa ambavyo vitamsaidia kutimiza malengo ya somo. Baadhi ya vifaa hivyo ni pamoja na:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Meza duara,
- Redio,
- Runinga,

- Taarifa zilizorekodiwa,
- Vifaa vya kunasia sauti,
- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati na vinginevyo

Mwalimu anaweza kutafuta zana zingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa zana hizo.

## 21.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika kipindi hiki, mwalimu atafute mbinu mwafaka zinazomuwezesha kufanikisha malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atayazingatia yafuatayo:

- **Njia shirikishi:** wanafunzi wagawike katika makundi na mchango wa kila mwanafunzi katika kundi udhihirike. Mbinu hii itumiwe wakati wa utekelezaji wa mdahalo ambapo wanafunzi wanalazimika kushirikiana katika makundi ya watetezi na wapinzani, mbinu hii pia itumiwe kwa masuali ya ufahamu, masamiati, sarufi na utungaji.
- **Njia isiyoshirikishi:** Kila mwanafunzi apewe kazi yake binafsi kwa kufanya kazi ya nyumbani, kutunga sentensi, kujibu maswali kuhusu sarufi na kutoa maoni yake kwa kutetea au kutotetea mada na kuongea hadharani bila uoga.
- Maswali na majibu: Wanafunzi waulizane maswali kati yao na kuyatolea majibu wao wenyewe kwa kusaidiwa na mwalimu. Mwalimu naye awaulize wanafunzi maswali na wayatolee majibu hasahasa kwenye sehemu ya ufahamu, sarufi na matumizi ya lugha.
- Majadiliano: Katika somo hili wanafunzi wapewe mada tofauti, wajigawe katika makundi madogo ili watafute mawazo kuhusu mada fulani; halafu watoe maoni yao kwa njia ya maongezi na majadiliano katika mdahalo.
- Utafiti: Kakati wa kujiandaa na mdahalo, wanafunzi wafanye utafiti ili wapate ujuzi wa kutosha kuhusu mada itakayojadiliwa. Kabla ya mdahalo, wanafunzi wasaidiwe kupata taarifa kwenye vitabu, magazeti, redio, au kwenye tovuti.

## 21.4. Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha wajibu maswali haya:

xi. Eleza wanachofanya watu unaowaona kwenye mchoro.

xii. Eleza wajibu wa mzazi katika malezi ya mtoto.

xiii. Fafanua majukumu ya walimu katika elimu ya watoto.

Makundi manne yaruhusiwe kuwasilisha namna walivyojibu maswali haya, na mwalimu asisitizie yale majibu ambayo yatawasaidia wanafunzi kugundua somo husika.

### 21.4.1 Maswali ya ufahamu

1. Mada ya mdahalo huu ni « Wazazi ndio wenye jukumu ya kwanza katika malezi ya watoto wao ».
2. Katibu wa mdahalo ni Muhire
3. Aliyetoa hoja ya kwanza kwenye upande wa utetezi ni Mutabazi. Yeye alieleza kwamba wazazi ndio wanaowapatia watoto wao malezi ya msingi ambayo yanawasaidia kufanikiwa maishani.
4. Kayitesi yuko katika upande wa upinzani.
5. Uwamahoro hakubaliani na mawazo ya Kayitesi. Kwa sababu ya maoni yake. Yeye ameeleza kwamba malezi ya mtoto si jukumu la wazazi tu bali ni jukumu la kila mtu.
6. Majina ya watu wote ambao walitoa mawazo wakiitetea mada ya mdahalo ni:
   - Mutabazi
   - Uwamahoro
   - Furaha
7. Mawazo matatu ambayo yalitolewa na upande wa utetezi:
   - Wazazi ndio wanaotoa malezi ya msingi kwa watoto wao.
   - Wazazi wana jukumu la kuwatunza watoto.
   - Wazazi huwanunulia watoto vifaa vya shule.
   - Wazazi hulipa karo kwa elimu ya watoto wao.
   - Wazazi hufuatilia karibu jinsi watoto wao wanavyoelimishwa na kuwashauri
   - Watoto huiga tabia za wazazi wao.

8. Maoni ya wapinzani:
   - Malezi ya mtoto ni jukumu la kwanza la kila mtu.
   - Watu mbalimbali wanaomzunguka mtoto ndio wanaochangia sana katika malezi yake
   - Serikali ina wajibu mkubwa katika malezi ya watoto
   - Serikali hujenga shule kwa ajili ya elimu ya watoto
   - Serikali ndiyo ambayo huwahimiza wazazi kupeleka watoto shuleni
   - Walimu na viongozi wa shule nao wana mchango mkubwa katika malezi ya watoto.
   - Walimu na viongozi wa shule hulea watoto kwa kuwasaidia kurekebisha tabia zao mbaya na kuwa na mienendo mizuri
   - Walimu na viongozi wa shule huelimisha watoto
9. Walioshinda ni watetezi.
10. Maoni tofauti hapa yatolewe na wanafunzi wakielekezwa na mwalimu.

**Baadhi ya maoni anayoweza kutoa:**

- Kwa maoni yangu ni kwamba wazazi sio peke yao wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto.
- Kuna watu wengi sana wanaohusika katika malezi ya watoto.
- Walimu, viongozi wa shule,  wanafamilia, taifa na wengine.
- Wananchi wote wanatakiwa kushirikiana ili watoto wote wapate malezi bora.

### 21.4.2 Msamiati kuhusu Utekelezaji wa Mdahalo

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuchunguza matumizi yake katika kifungu kuhusu utekelezaji wa mdahalo.*

**Sentenzi pendekezo:**

1. Kupewa malezi ni haki ya kila mtoto.
2. Ninataka kumkaribisha Bwana Mugisha ili atoe mchango wake kuhusu maendeleo ya yamii.
3. Elimu kwa wote ni nyenzo bora ya kupambana na umaskini.
4. Tunahitaji kuhifadhi mazingira ili tuwe na maisha mazuri.
5. Watu ambao hawana amani hawawezi kupata maendeleo.
6. Watu wengi hupenda kuunga mkono mawazo ya kishujaa.
7. Mimi sikubaliani na wale wanaoamini kwamba malezi ya watoto ni jukumu la wazazi tu.
8. Kuna shule nyingi zilizojengwa na serikali ili kutekeleza mradi wa elimu kwa wote.
9. Wapinzani, bakini pale mnapoketi.
10. Wazazi waungane mkono na serikali kwa kulipa karo kwa wanafunzi.

**Zoezi la 3:**

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kutumia mshale na kuhusisha maneno katika sehemu A  na maana zake katika sehemu B.

| A | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | d | f | h | j | n | c | l | g | m | a | b | o | k | i | e |

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aombe kila mwanafunzi kupanga herufi zilizotolewa ili kufanya maneno ya Kiswahili sanifu, kisha mwalimu awaombe wanafunzi kuandika majibu ubaoni (mwanafunzi mmoja baada ya mwingine).*

**Majibu:**

WASHIRIKI
JUKUMU
MDAHALO
MWENYEKITI
MHESHIMIWA
MAJADILIANO
MADA
MABWANA
WATETEZI
KATIBU

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kila mwanafunzi ajaze sentensi kwa kutumia maneno aliyopewa kwa kuzingatia maana ya kila neno. Mwalimu awaelekeze wanafunzi na ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anashiriki.*

**Majibu**

1. Mwenyekiti anawaomba **wasikilizaji washiriki** kuwapigia makofi washindi wa mdahalo.
2. Walimu nao wana umuhimu mkubwa katika **malezi** ya watoto.
3. Tabia za watu wanaoishi karibu na mtoto **zinaathiri** malezi yake.
4. Mimi **sikubaliani** na msemaji aliyesema kwamba wazazi ndio wenye jukumu la kwanza katika malezi ya watoto.
5. Waheshimiwa mliokusanyika hapa leo, **mada** ya majadiliano yetu ni ‘‘Wake na waume wana uwezo sawa’’.
6. Malezi ya watoto ni **jukumu** la kila mwananchi.
7. Ahsante sana Kayitesi kwa kutoa **maoni** yako.
8. **Wazazi** wana mchango mkubwa katika mwenendo mwema wa watoto wao.
9. Nami **ninaunga mkono** mtazamo wa wapinzani wa mada.
9. Baada ya kusomewa mawazo yaliyotolewa, hadhira **hupiga kura.**

### 21.4.3 Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha katika Vitenzi Mkopo, Hali Yakinishi na Hali Kanushi.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wajadili kuhusu maana ya sentensi zenye vitenzi vya mkopo ambavyo vina dhana ya kushurutisha.

1. Wapinzani, bakini pale mnapoketi.
2. Msifikiri kwamba mawazo yaliyotolewa na watetezi ni kweli.
3. Jaribu kupaza sauti.
   - Sentensi ya kwanza inazingatia kitenzi kubaki, kiko kwenye hali ya kushurutisha, hali yakinishi inawaamuru wapinzani kubaki mahali wanapokaa.
   - Sentensi ya pili ina kitenzi kufikiri ambacho kiko kwenye hali ya kushurutisha, hali kanushi, inawaamuru na kuwahimiza watu kutowaza kwamba mawazo yote yatolewayo na watetezi ni kweli.
   - Sentensi ya tatu inazingatia kitenzi kujaribu ambacho kiko kwenye hali ya kushurutisha, hali yakinishi na inamuomba mtu kupaza sauti.

Baadaye mwalimu aombe wanafunzi watoe sentensi tano zenye dhana ya kushurutisha katika hali yakinishi na hali kanushi.

Hii ni mifano pendekezo ya sentensi hizo:

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| Baki pale unapokaa. | Usibaki pale unapokaa. |
| Jaribu kupiga makofi. | Usijaribu kupiga makofi. |
| Rithi mali ya wazazi wako. | Usirithi mali ya wazazi wako. |
| Sahau mambo hayo. | Usisahau mambo hayo. |
| Fuzu mwaka kesho. | Usifuzu mwaka kesho. |

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kuhusu hali kanushi ya vitenzi vyenye viambishi tamati ambavyo ni -e, -i na -u kisha wajibu maswali kuhusu maelezo waliyoyasoma. Mwalimu awaelekeze katika kusoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi linalohusu umoja au wingi wa sentensi.*

**Majibu:**

1. **Wasilini** haraka kwenye majadiliano.
2. **Jaribuni** kueleza mawazo yenu waziwazi.
3. **Jibuni** maswali yote mnayoulizwa kwenye midahalo.
4. **Karirini** mawazo yote yaliyotolewa kama ninyi ni makatibu.

5. **Fikirin**i takribani mara mbili kabla ya kudokeza maoni yenu.
6. **Sihi** mwenzako akuunge mkono.
7. **Samehe** anayekusababisha kutopata ushindi katika mdahalo.
8. **Kubali** matokeo ya kura mwishoni mwa mdahalo.
9. **Kidhi** mahitaji ya mtoto wako ili awe na malezi bora.
10. **Salimuni** wenzenu ambao mmekutania kwenye midahalo.

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

**Katika makundi ya wawili wawili, mwalimu awaongoze wanafunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia hali ya kushurutisha ya vitenzi ambavyo vimo katika mabano.**

1. Ninyi mshiriki katika maongezi.
2. Usiwakejeli wenzako wanaotoa mawazo kinyume na yako.
3. Wewe usimruhusu mtu kuwatukana wengine ambao hawaungi mkono mawazo yake.
4. Usiathiri vibaya malezi ya mtoto wako.
5. Wewe amini kwamba majadiliano ni wenzo bora wa kudumisha amani na upendo.

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu ahimize wanafunzi kusoma maelezo muhimu kuhusu hali kanushi ya vitenzi vyenye viambishi tamati ambavyo ni -e, -i na -u kisha katika makundi ya watatu watatu waweke sentensi kwenye wingi au umoja*

1. Msidharau mawazo ya wengine mdahaloni.
2. Usisahau kutumia matamshi bora katika majadiliano.
3. Msiwadhuru wenzenu.
4. Msikubali kushindwa kwa sababu ya kutopaza sauti.
5. Usidhani kwamba midahalo ni kama mijadala.
6. Msiwasamehe watu wanaonyanyasa wanawake.
7. Msisalimu hadhira kwa uoga.
8. Mkipewa jaribio kuhusu mfano wa mdahalo, msinakili.
9. Msiwasihi watu kukubaliana na mawazo ambayo hayalengi kudumisha amani.
10. Msijaribu kusema uongo wakati wa majadiliano.

### 21.4.4. Matumizi ya Lughakuhusu Utelekezaji wa Mdahalo

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kisha wajibu maswali kuhusu utekelezaji wa mdahalo. Mwalimu awaelekeze katika kuyasoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi.*

**Majibu pendekezo**:

1. Wadau wote wanaohusika katika malezi ya watoto ni:
   - Wazazi
   - Walimu
   - Wasamaria
   - Viongozi wa shule
   - Wanafamilia
   - Serikali
2. Wajibu wa kila mhusika anayehusika na malezi ya watoto:

   **a. Wazazi :**
   - Hutoa malezi ya msingi
   - Hukidhi mahitaji ya watoto
   - Huwasaidia watoto wao kupata elimu
   - Huwafundisha wanafunzi mwenendo mwema na maadili na kadhalika

   **b. Walimu**
   - Hufundisha watoto.
   - Huwashauri watoto.
   - Ni mfano wa kuigwa na wanafunzi

   **c. Wasamaria**

Hutoa misaada kwa watoto na kwa familia zao

**d. Viongozi wa shule**
- Huwasaidia watoto kupata elimu.
- Huwashauri wanafunzi.
- Ni mfano wa kuigwa na wanafunzi

**e. Wanafamilia**
- Hutoa malezi ya msingi
- Hukidhi mahitaji ya watoto
- Huwasaidia watoto kupata elimu
- Huwafundisha wanafunzi mwenendo mwema na maadili
- Huathiri vizuri tabia za watoto

**f. Serikali**
- Hujenga shule ili watoto wote wapate malezi.
- Hulipia wanafunzi karo.
- Huwalipa walimu mshahara ili wafundishe watoto.
- Hutoa mwelekeo wa elimu

**Majukumu ya wahusika wa mdahalo:**

- Mwenyekiti: Huwa na majukumu ya kuongoza mdahalo kama ipasavyo, kumpangia kila msemaji muda wa kutoa maoni yake, kuongoza upigaji kura ili kujua washindi na kutoa suluhisho la mdahalo.
- Katibu:Ana jukumu la kuandika mawazo yote yaliyotolewa na kila msemaji na kuyasomea hadhira mwishoni mwa mdahalo. Katibu tena huandika , huhesabu na hutangaza matokeo ya kura.
- Wasemaji wakuu: Kwa kila upande unalazimika kutoa maoni yao kwa kutetea au kutokubaliana na mada kutokana na pande zao. Wanatoa mawazo yao ili pande zao ziweze kushinda. Kila anayepewa fursa analazimika kutumia muda aliopangiwa.
- Washiriki:Nao wanafuata mdahalo na wanaweza kushiriki kwa kuunga mkono upande mmoja kati ya utetezi na upinzani; pia wanashiriki kwa kupiga kura ili washindi wa mdahalo wapatikane.

**Mambo ya kuepuka katika mdahalo ni haya yafuatayo:**

- Kupiga kelele
- Kusababisha fujo
- Kupoteza muda kwa bure
- Kutumia lugha yenye matusi
- Kutoheshimu wenzako
- Kukejeli amri kutoka kwa mwenyekiti

Na kadhalika

### 21.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuchagua mada moja kati ya mada tatu walizopewa. Awasaidie kuchagua mwenyekiti na katibu, kisha awaombe kujipanga katika makundi ya watetezi na wapinzani. Mwalimu awasaidie wanafunzi kupata muda na namna ya kuandaa maoni watakayodokeza kwa kufanya utafiti kwa kutumia vitabu, magazeti, tovuti na kadhalika. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutekeleza mdahalo darasani.*

**Baadhi ya maoni pendekezo**

- Mada ya kwanza “Wavulana wana uwezo sawa na wasichana”.
- Mvulana na msichana wana uwezo sawa wa kushinda masomo shuleni.
- Hakuna tofauti iliyopo kati ya nguvu za mvulana na za msichana.
- Mvulana na msichana wana haki sawa.
- Wavulana na wasichana wana mchango sawa katika maendeleo endelevu ya nchi.

**14. Ukimwi ndio ugonjwa wa kwanza unaoathiri zaidi maendeleo ya jamii.**

| **Mawazo ya watetezi** | Mawazo ya wapinzani |
|---|---|
| **a. Ukimwi ndio ugonjwa ambao hauna dawa wala kinga.**<br>**b. Ukimwi ndio unaoua watu sana.**<br>**c. Ukumwi unasababisha umaskini.**<br>**d. Ukimwi unapunguza idadi ya wananchi wenye nguvu za kujenga nchi.**<br>**e. Ukimwi huwasababisha watu kukata tamaa ya kujiendeleza na kuendeleza nchi yao.** | a. Magonjwa yote kwa ujumla ndiyo yanayokumba maendeleo ya kijamii.<br>b. Ujinga ndio unaokumba maendeleo ya jamii.<br>c. Migogoro na kutoelewana kati ya wananchi, hukumba maendeleo ya jamii.<br>d. Utumiaji wa madawa ya kulevya ndio unaokumba maendeleo ya jamii.<br>e. Uvivu ndio unaokumba maendeleo ya jamii |

**3. Malezi kwa wote ni jukumu la kila mwanchi.**

| **Baadhi ya mawazo ya watetezi** | **Baadhi ya mawazo ya wapinzani** |
|---|---|
| a. Kila mtu analazimika kushiriki katika malezi ya watoto.<br>b. Kila mwananchi anaathiri malezi ya wototo.<br>Kila mwananchi anafahamu c. umuhimu wa malezi kwa wote.<br>d. Kila mwananchi anaathiriwa na ukosefu wa malezi ya watoto. | a. Malezi kwa watoto ni jukumu la wazazi.<br>b. Malezi kwa wote ni jukumu la serikali.<br>c. Malezi kwa wote ni jukumu la anayetaka malezi.<br>d. Malezi kwa wote ni jukumu la walimu. |

### 21.4.6 Utungaji

**Zoezi la 12: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi watunge kifungu cha habari kuhusu moja wapo ya mada walizopewa. Hapa, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashiriki.

1. Serikali ndiyo ambayo ina jukumu kubwa la elimu ya watoto.

**Baadhi ya mawazo yatakayotolewa na wanafunzi:**

- Serikali hujenga shule tofauti.
- Serikali hupanga miradi tofauti ili kila mtoto apate elimu.
- Serikali huwahudumia wanafunzi mbalimbali wanaostahili misaada.
- Serikali hulipa mishahara kwa walimu wanaowawezesha wananchi kupata elimu.

- Serikali huadhibu yeyote anayekuwa kipingamizi kwa malezi ya watoto.

2. Bila elimu hakuna maendeleo.
1. Elimu hukuza uchumi wa nchi.
2. Elimu huwatoa wananchi katika umaskini.
3. Elimu huwasaidia wananchi kufahamu haki na majukumu yao katika kuendeleza nchi.
4. Elimu ni nyenzo bora ya kupata maendeleo ya nchi.
5. Elimu hukuza uwezo wawananchi wa kufikiri.

## SOMO LA 22: UTEKELEZAJI WA MJADALA

### 22.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Somo hili linahusu utekelezaji wa mjadala. Mwalimu aanze somo kwa kuwasisimua wanafunzi.

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kukumbuka na kufahamu zaidi somo lililotangulia. Atakapomaliza kuwauliza maswali ya kuwakumbusha somo la awali, mwalimu awasaidie wanafunzi kuingia katika somo linalohusika ambalo ni "Utekelezaji wa mjadala". Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yawezekanayo ili kuwafanya wanafunzi wagundue somo lenyewe.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro ulioko katika kitabu cha mwanafunzi kuhusu utekelezaji wa mjadala. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: Tazameni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo :

- Watu unaowatazama kwenye mchoro huo wanafanya nini?
- Eleza shughuli za watu hao kwenye mchoro.
- Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na mtu wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine. Mwisho wake mwalimu atoe maoni yake kuhusu yaliyofanywa na wanafunzi kwa kurekebisha yaliyofanywa kwa namna isiyo bora.

Kutokana na majibu tofauti yaliyotolewa, mwalimu asisitizie yale ambayo yanawaingiza wanafunzi katika somo jipya.

### 22.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute na atumie ipasavyo vifaa ambavyo vitamsaidia kutimiza malengo ya somo. Baadhi ya vifaa vinavyohitajika ni pamoja na:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Meza duara,

- Redio,
- Runinga,
- Taarifa zilizorekodiwa,
- Vifaa vya kunasia sauti,
- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati na vinginevyo

Mwalimu atafute zana zingine ambazo hazikuorodheshwa hapo juu kulingana na upatikanaji wa wazo. Vifaa hivi viandaliwe kulingana na mazingira ya shule na uwezo wake. Mwalimu kwa ubunifu wake aandae vifaa vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo.

## 22.3 Mbinu za kufundishia na Kujifunza

Katika kipindi hiki, mwalimu atafute mbinu mwafaka zinazomwezesha kufanikisha malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atayazingatia yafuatayo:

- **Njia shirikishi:** Wanafunzi wagawike katika makundi na mchango wa kila mwanafunzi katika kundi udhihirike. Mbinu hii itumiwe kwa mwaswali ya ufahamu, msamiati, sarufi na utungaji.
- **Njia isiyoshirikishi:** Mwanafunzi apewe kazi yake binafsi kwa kutunga sentesi, kujibu maswali kuhusu sarufi na kuongea mbele ya wenzake bila uoga
- **Maswali na majibu:** Wanafunzi waulizane maswali kati yao na kuyatolea majibu wao wenyewe kwa kusaidiwa na mwalimu au mwalimu awaulize wanafunzi maswali kwa kutumia namna kadhaa. Mwalimu atumie mbinu hii katika sarufi na matumizi ya lugha.
- Majadiliano: Mada nyingi na tofauti zitolewe na wanafunzi wafanye majadiliano huhusu mada hizo kwa kutoa maoni yao kwa njia ya mjadala na mwalimu awe mwelekezaji.
- **Utafiti**: Wakati wa kujiandaa na mjadala, wanafunzi wafanye utafiti ili wapate ujuzi wa kutosha kuhusu mada itakayojadiliwa. Kabla ya mjadala, wanafunzi wasaidiwe kupata taarifa kwenye vitabu, magazeti au kwenye tovuti.

## 22.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wahusika wanaowaona kwenye mchoro huo, matatizo yanayosababishwa na madawa ya kulevya, na funzo walilopata kutokana na wanayoyaona kwenye mchoro.*

### 22.4.1 Majibu ya Ufahamu

1. Tatizo la kwanza linalokwamisha maendeleo ni matumizi ya madawa ya kulevya. Wanaotumia madawa hayo hawawezi kujiendeleza na kuendeleza jamii yao kwa sababu ubongo wao umeisha haribika na fikra zao si kamili.

2. Ninakubaliana na maoni ya msemaji wa kwanza kwa sababu matumizi ya madawa ya kulevya ni hatari kwa maisha ya binadamu. Yule anayetumia madawa hayo hawezi kujiendeleza.
3. Madawa ya kulevya ni kama kokeni, heroini, miraa na bangi.
4. Madhara yanayotokana na matumizi ya madawa ya kulevya ni kuharibika kiakili, kuwa na magonjwa ya saratani, kuwa na ufukara, ….
5. Tatizo lililotajwa kwa mara ya pili ni la magonjwa mbalimbali kama malaria, ukimwi, kisukari,…. Watu wenye maradhi hayo wanatumia mali nyingi kutibiwa, wakapoteza muda mrefu wakiwa hospitalini. Kwa hiyo, wao hukosa muda wa kujiendeleza na kuendeleza nchi yao. Magonjwa haya yanapojitokeza yanaiangamiza sana jamii na husababisha vifo vya watu wengi ambao wangetoa mchango wao wa kuendeleza nchi.
6. Utumiaji wa pombe unaweza kukwamisha maendeleo ya jamii. Wanaokunywa pombe sana, wanageuka walevi. Na walevi hawawezi kujiendeleza na kuendeleza jamii yao, kwa sababu badala ya kufanya kazi, wanazururazururavilabuni. Hawawezi kupanga miradi ya kujiendeleza.
7. Wanaoruhusiwa kunywa pombe ni watu walio na umri wa miaka juu ya kumi na minane, wasio na ugonjwa au sababu zingine zinazowakataza kunywa pombe. Lakini hakuna anayeruhusiwa kunywa pombe sana na kuwa mlevi.
8. Umaskini unaweza kukwamisha maendeleo ya jamii wakati jamii hiyo inapokosa rasilimali ya kuanzisha na kutekeleza miradi yake ya kujiendeleza.
9. Ni kweli kwamba ujinga unaweza kukwamisha maendeleo katika jamii. Aliye na ujinga, hawezi kutofautisha mambo mazuri na mabaya na hawajui jambo muhimu la kufanya ili waendelee na waendeleze jamii yao.
10. Mjadala huu unanifundisha kutotumia madawa ya kulevya, kutokunywa pombe sana, kujilinda maradhi tofauti, kupata elimu ya kunisaidia kuendelea, kuwa namwenendo mzuri,…..

### 22.4.2 Msamiati kuhusu Maana ya Mdahalo na Mjadala

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno yanayofuata, wachunguze matumizi yake katika kifungu cha habari walichosoma hapo kuhusu utekelezaji wa mjadala. Mwalimu awaongoze.*

**Sentensi pendekezo**

1. Matumizi ya madawa ya kulevya yanakwamisha maendeleo.
2. Ugonjwa wa malaria unaathiri maendeleo ya jamii nyingi barani Afrika.
3. Mwenyekiti wa mjadala aliwakaribisha washiriki.
4. Madawa ya kulevya yanaleta madhara mbalimbali katika jamii.
5. Matumizi mabaya ya pombe huharibu maisha ya binadamu.

6. Ufukara ni kipingamizi cha maendeleo.
7. Serikali ya Rwanda ilijitahidi kupambana dhidi ya maradhi yanayoambukiza na yasiyoambukiza.
8. Mambo yanayoangamiza vijana ni matumizi ya madawa ya kulevya na ukosefu wa kazi.
9. ya ukimwi haijapatikana.
10. Miradi mingi imeanzishwa kupambana na umaskini nchini Rwanda.

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waelekezwe jinsi ya kufanya kazi hii kwa kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B.

| A | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | o | i | h | b | k | a | n | m | f | l | j | g | c | d | e |

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, wakamilishe maneno yafuatayo kwa kutumia herufi zinazokosekana ili yaweze kuleta maana. Mwalimu aongoze kazi ya wanafunzi na kuhakikisha kwamba wote wanashiriki kwenye kazi hiyo.*

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | U | L | E | V | Y | A | |
| M | A | R | A | D | H | I | |
| W | A | E | P | U | K | E | |
| K | I | N | G | A | | | |
| J | I | T | I | H | A | D | A |
| F | U | K | A | R | A | | |
| M | j | I | N | G | A | | |
| S | E | R | I | K | A | L | I |
| E | L | I | M | U | | | |
| M | I | R | A | D | I | | |

## 22.4.3 Sarufi: Matumizi ya Hali ya Kushurutisha katika Vitenzi vyenye Silabi Moja Hali Yakinishi na Kanushi

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wawali wawili, wanafunzi wajadili kuhusu maana ya sentensi zenye dhana ya kushurutisha ya vitenzi vyenye silabi moja, kisha watunge sentensi tano kama hizi :

1. **Njooni** tupange miradi ya kujiendeleza.
2. Mwingine **atupe** maoni yake.
3. **Msinywe** pombe kwa sababu pombe ni hatari kwa maisha.

**Hii ni mifano pendekezo ya sentensi:**

1. **Kula** chakula hiki upate nguvu za kuzungumza..
2. **Kunywa** uji uliomo jagini kabla ya kuenda majadilioni
3. **Njoo** hapa utoe mchango wako katika mjadala wa leo.
4. **Usinywe** pombe nyingi.
5. **Usimpe** mtoto wako madawa ya kulevya.

Zoezi la 6: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu awaambie wanafunzi wakamilishe sentensi kwa kutumia hali ya kushurutisha ya vitenzi ambavyo vimo katika mabano.

Majibu

Mama alimkataza mtoto wake, "Usinywe pombe".

Kula chakula hiki ukimalize upate afya nzuri.

Mkurugenzi alimshauri mzazi, "Mpe mtoto malezi bora"

Njooni tuhudhurie mjadala wa leo.

Ukitaka kuwa na maisha mazuri, usile chakula chenye mafuta mengi.

Zoezi la 7: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili, watunge sentensi kumi kwa kutumia hali ya kuomba kisha kila kundi limchague mwasilishaji awasilishe sentensi walizotunga. Kutokana na sentensi zitakazotolewa na wanafunzi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kwa kuhakiki na kurekebisha sentensi zilizotungwa.

**Mifano:**

Msikilizaji aheshimu maoni ya msemaji.

Sisi sote tujenge nchi yetu.

Tusiharibu maisha yetu kwa kutumia madawa ya kulevya.

Watoto wasinywe pombe kwa hali yoyote.

Usile chakula kichafu.

Ili ufike kwa maendeleo, jipange sawa sawa.

Msijaribu mambo yanayoweza kuhatarisha maisha yenu.

Katika mjadala, msipoteze muda.

Aliye tayari asimame atoe mchango wake.

Wajawazito wasinywe pombe.

### 22.4.4 Matumizi ya Lugha: Utekelezaji wa Mjadala

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajaze sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa kwa kuzingatia maana ya kila neno. Mwalimu awaelekeze wanafunzi na ahakikishe ikiwa kila mwanafunzi anashiriki.*

**Majibu**

1. Mshiriki aliye tayari aje atoe mchango wake.
2. Matumizi ya madawa ya kulevya ni hatari kwa maisha ya watu.
3. Tumtege sikio msemaji mwingine atoe maoni yake.
4. Ukimwi hauna dawa wa chanjo.
5. Watu wanaolewa wanaitwa walevi.
6. Watu wanaokumbwa na ufukara nao wanaweza kujiendeleza.
7. Miradi mbalimbali imeanzishwa kwa ajili ya kupambana na umaskini.
8. Elimu huondoa ujinga katika jamii.
9. Mjadala unaanzishwa na kufungwa na kiongozi.
10. Mwishoni mwa mjadala kiongozi wake anatoa suluhisho.

**Zoezi la 9** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi katika makundi ya wawili wawili wasome maelezo muhimu kisha wajibu maswali kuhusu maelezo waliyoyasoma. Mwalimu awaelekeze katika kusoma, kujibu maswali na kutoa suluhisho kuhusu matokeo ya zoezi.

**Majibu:**

1. Matatizo mengine yanayoweza kukwamisha maendeleo ya jamii ya Rwanda ni ukosefu wa kazi, uzazi usio wa mpango, ardhi ndogo, na matumizi mabaya ya ardhi hiyo
2. Kwa maoni yangu matatizo haya yanaweza kuepukwa kwa kujitafutia ajira, mtu kuzaa watoto anaoweza kuwatunza au kufuata uzazi wa mpango, kutumia vizuri ardhi na kuiboresha kwa kutumia mbolea.
3. Mambo ya kuzingatia katika utekelezaji wa mjadala: Kupewa fursa ya kuzungumza, kuheshimu muda uliopewa, kutokiuka mada inayojadiliwa, kutopiga kelele wakati wa mjadala, … .

### 22.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 10:*****(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Mwalimu aombe wanafunzi kufanya makundi ya wanafunzi wawili wawili, wajadili kuhusu mojawapo ya mada zilizotolewa.

**Mawazo yanayoweza kutolewa na wanafunzi:**

1. Namna bora ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ukimwi:
    - Kutofanya ngono
    - Kutumia kondomu
    - Kutochangia vifaa vyenye ncha kali
    - Kutotumia madawa ya kulevya

2. Mikakati ya kuepuka maambukizi ya malaria:
    - Kukata vichaka karibu na nyumba
    - Kutengeneza visiwa na vitu vingine ambavyo vinaweza kuwa na maji pale ambapo mbu wanaweza kuzaliwa.
    - Kufunga milango na madirisha jioni.
    - Kulala kwenye chandarua

### 22.4.6 Utungaji

Zoezi la 11: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watunge kifungu cha habari kuhusu mojawapo ya mada walizopewa. Hapa, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashiriki.*

Mawazo yanayoweza kutolewa na wanafunzi

**i. Juhudi zinazoweza kufanyika ili kuzuia vijana kutumia madawa ya kulevya:**

i) Kuwapangia kazi vijana

ii) Kuwazoeza kufanya michezo mbalimbali

iii) Kupeleka vijana katika shule za ufundi ambazo zinawasaidia kujitafutia ajira

iv) Kupa vijana uwezo wa kuanzisha shughuli mbalimbali

v) Kusaidia vijana kujiundia katika vyama vya ushirika

vi) Kuhamasisha vijana kujitafutia ajira

**ii. Juhudi zinazoweza kufanyika ili kutoa malezi kwa wote:**

- Kuhamasisha watu wote kujua jukumu zao.
- Kujenga shule zinazotosha na kuzipatia uwezo na vifaa vinavyohitajika.
- Kupeleka watoto wote shuleni wakati wanapokamilisha miaka ya kuenda shule, kuanzia chekechea hadi shule za upili.
- Kujenga shule za kusaidia wale wasiokuwa na bahati ya kupata elimu awali.
- Kujitahidi kuwasaidia wenye ulemavu kuenda shuleni na kuwatafutia vifaa vya kuwasaidia kujifunza kwa urahisi

### 22.5.. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya nne" Midahalo na Mijadala" ina vipengele vinne yaani masomo makuu manne yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika, sarufi, na maelezo muhimu. Somo la kwanza linaeleza maana ya mdahalo na mjadala. Somo la pili ni uhusiano na tofauti kati ya mdahalo na mjadala. Somo la tatu linafafanua utekelezaji wa mdahalo na Somo la nne linaloeleza utekelezaji wa mjadala. Katika kila somo kuna kipengele cha sarufi ambacho kinagusia hali ya kushurutisha ya vitenzi vya Kiswahili sanifu.

## 22.6. Maelezo ya Ziada

**a) Maelezo muhimu kuhusu "Maana ya mdahalo na mjadala"**

- Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya mada fulani. Unahusisha pande mbili yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani.
- Mdahalo unawasaidia wanafunzi kushiriki katika utetezi au upinzaniwa jambo fulani.
- Mdahalo unaongozwa na mwenyekiti akisaidiwa na katibu.
- Mjadala ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Unaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.
- Mjadala unaongozwa na mtu mmoja ambaye anazusha mawazo na kuhakikisha ikiwa kuna mwenendo mwema kati ya washiriki wa mjadala huo.
- Mwenyekiti wa mjadala ndiye anayetoa muhtasari wa mawazo yaliyotolewa. Mada zinazojadiliwa katika mjadala ni zile ambazo zinahitaji ufafanuzi kutokana na mchango wa mawazo ya wengi.
- Anayetoa hoja yake, anaweza kuunga mkono maoni ya mwenzake au kuyapinga kwa minajili ya kutoa mchango wake wa kutatua tatizo linalojadiliwa.

**b) Uhusiano kati ya mjadala na mdahalo**

- Mjadala na mdahalo huhusisha watu wengi wanaojadiliana kuhusu jambo fulani.
- Katika mjadala na mdahalo kuna mada ambayo hutolewa mawazo, na mada hiyo ndiyo ambayo inamulikia mjadala na mdahalo. Kiongozi wa mdahalo au mjadala hulazimika kuwaongoza wasemaji kutokiuka mada.
- Mdahalo na mjadala huwa na malengo sawa ya:

    - Kukuza uwezo wa kitaaluma na hali ya udadisi kwa washiriki wa mjadala na mdahalo
    - Kukuza uwezo wa kushawishi watu hadharani ili wakubaliane na mawazo ya msemaji kuhusu jambo fulani.
    - Kumuwezesha mtu kupanga mawazo yake kwa mfuatano mzuri wakatianapoandika insha au habari.

- Kumuwezesha mtu kutambua kipaji alichonacho cha kuzungumza bila aibu mbele ya hadhira.
- Kukuza stadi ya utumiaji wa lugha kwa kutumia msamiati na matamshi bora ya lugha.
- Kumuzoeza mtu kusikiliza na kupinga au kutetea maoni na hoja za wengine.
- Kuwapa watu wasaa wa kuelewana na wengine kutoka maeneo mbalimbali.

**c) Tofauti kati ya mdahalo na mjadala**

- Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetetezi na upinzani na hadhira lakini kwenye mdahalo kuna kiongozi na handhira tu.
- Katika mdahalo kuna wasemaji wakuu wanaotetea au wasiokubaliana na mada lakini kwenye mjadala yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi.
- Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani.
- Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.

## 22.7. Tathmini ya Mada

**Majibu ya tathmini ya mada kuu ya nne**

***i. Mwalimu awahimize wanafunzi wafanye kazi kuhusu mdahalo:***

a) Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuchagua mada moja ya mdahalo. Awasaidie kuchagua mwenyekiti na katibu. Kisha awaombe wajipange katika makundi ya watetezi na wapinzani. Mwalimu awape muda wa kuandaa hoja watakazozitoa kwa kufanya utafiti katika vitabu, magazeti, tovuti na kadhalika. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anafanya utafiti huo.

b) Mwalimu awaombe wanafunzi watekeleze mdahalo walioandaa.

**Baadhi ya hoja pendekezo**

1. Walimu ni bora kuliko wazazi katika malezi ya watoto.

| Utetezi | Upinzani |
|---|---|
| Walimu wanafundisha watoto | Wazazi wanawatunza watoto |
| Wanawashauri watoto | Wanawalipia karo |
| Wanawahimiza kuwa na tabia na nidhamunzuri | Wanawapa mwelekeo wa maisha |

| | |
|---|---|
| Walimu ni kielelezo kwa wanafunzi | Wanawapeleka shuleni |
| | |

2. Madawa ya kulevya hukwamisha maendeleo zaidi kuliko magonjwa.

| Utetezi | Upinzani |
|---|---|
| Madawa ya kulevya yanaharibu maisha | Kuna magonjwa ambayo hayatibiwi |
| Yanayeyusha ubongo | Mtu mgonjwa hukaa muda mrefu hospitalini |
| Wanaoyatumia wanabadilika kitabia wakawa na tabia mbaya | Familia hutumia mali nyingi kwa mgonjwa |
| Magonjwa yanaweza kutibiwa kwa urahisi | Magonjwa yanasababisha vifo vya watu wengi kuliko matumizi ya madawa ya kulevya. |

**i Mwalimu awaambie wanafunzi wafaanye kazi kuhusu mjadala.**

a) Mwalimu awaongoze wanafunzi kuchagua mada moja kati ya mada zilizotolewa. Wamchague pia mwenyekiti wa mjadala. Kisha mwalimu awahimize wanafunzi kuandaa mjadala kwa kufanya utafiti katika vitabu, magazeti, tovuti na kadhalika.

b) Mwalimu awaombe watekeleze mjadala walioandaa.

**Baadhi ya maoni pendekezo**

1. Usawa wa jinsia katika kuimarisha maendeleo ya nchi
    - Usawa wa jinsia unaimarisha maendeleo ya nchi
    - Waume na wake wanafanya kazi bega kwa bega
    - Ushirikiano wa waume na wake unainua uchumi wa nchi
    - Utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakuwa rahisi

2. Malezi kwa wote ni jukumu la kila mwananchi
    - Kila mwananchi ana mchango wake katika malezi ya watoto
    - Kila mwananchi atoe mchango wake kujenga shule za kufundishia
    - Kila mwananchi apeleke watoto shuleni
    - Kila mwananchi ahakikishe kuwa kila mtoto anapewa haki zake
    - Kila mwananchi amlee mtoto yeyote kama wake.

3. Madhara yanayosababishwa na magonjwa yasiyoambukizwa
    - Vifo vya watu
    - Kupoteza nguvu za kufanya kazi
    - Kulazwa hospitali muda murefu

- Kupoteza mali ya familia katika matibabu

iii. Mwalimu aangalie kuwa kila mwanafunzi alitunga kifungu cha habari. Ahakiki kuwa mwanafunzi alitumia vitenzi tofauti katika hali ya kushurutisha.

## 22.8. Mazoezi ya Ziada

### 22.8.1. Mazoezi ya urekebishaji

a) Sarufi: Tumia vitenzi vifuatavyo katika hali ya kushurutisha katika umoja na wingi.

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kulima | *lima* | *limeni* |
| Kucheza | *cheza* | *chezeni* |
| Kuimba | *imba* | *imbeni* |
| Kukimbia | *kimbia* | *kimbieni* |
| Kujadili | *jadili* | *jadilieni* |
| Kusoma | *soma* | *someni* |
| Kuleta | *lete* | *leteni* |
| Kusafisha | *safisha* | *safisheni* |
| Kusifu | *sifu* | *sifuni* |
| Kuandika | *andika* | *andikeni* |

b)Nini maana ya mdahalo?

c) Nini maana ya mjadala?

**Majibu**

a) **Sarufi**

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **wingi** |
| Kulima | *Lima* | *Limeni* |
| Kucheza | *Cheza* | *Chezeni* |
| Kuimba | *Imba* | *Imbeni* |
| Kukimbia | *Kimbia* | *Kimbieni* |
| Kujadili | *Jadili* | *Jadilieni* |
| Kusoma | *Soma* | *Someni* |

| | | |
|---|---|---|
| Kuleta | *Leta* | *Leteni* |
| Kusafisha | *Safisha* | *Safisheni* |
| Kusifu | *Sifu* | *Sifuni* |
| Kuandika | *Andika* | *Andikeni* |

b) Mdahalo ni majadiliano baina ya watu wengi juu ya mada fulani. Unahusisha pande mbili yaani upande wa utetezi na upande wa upinzani.

c) Mjadala ni mazugumzo juu ya jambo fulani. Unaweza kufanyika katika makundi madogo madogo au makubwa.

### 22.8.2 Mazoezi Jumuishi

**a) Sarufi:** Tumia vitenzi vifuatavyo katika hali ya kushurutisha hali kanushi.

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kulima | *usilime* | *msilime* |
| Kucheza | *usicheze* | *msicheze* |
| Kuimba | *usiimbe* | *msiimbe* |
| Kukimbia | *usikimbie* | *msikimbie* |
| Kujadili | *usijadili* | *msijadili* |
| Kusoma | *usisome* | *msisome* |
| Kuleta | *usilete* | *msilete* |
| Kusafisha | *usisafishe* | *msisafishe* |
| Kusifu | *usisifu* | *msisifu* |
| Kuandika | *usiandike* | *msiandike* |

**b)** Kwa mapana na marefu tofautisha mdahalo na mjadala.

**c)** Fanyeni mdahalo kuhusu mada ifuatayo “Bila elimu ya shule hakuna maendeleo ya kudumu.”

**Majibu:**

**a) Sarufi:**Tumia vitenzi vifuatavyo katika hali ya kushurutisha hali kanushi.

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kulima | *Usilime* | *Msilime* |
| Kucheza | *Usicheze* | *Msicheze* |
| Kuimba | *Usiime* | *Msiimbe* |
| Kukimbia | *Usikimbie* | *Msikimbie* |
| Kujadili | *Usijadili* | *Msijadili* |

| | | |
|---|---|---|
| Kusoma | *Usisome* | *Msisome* |
| Kuleta | *Usilete* | *Msilete* |
| Kusafisha | *Usisafishe* | *Msisafishe* |
| Kusifu | *Usisifu* | *Msisifu* |
| Kuandika | *Usiandike* | *Msiandike* |

**b) Tofauti kati ya mdahalo na mjadala**

- Tofauti ya kwanza kati ya mdahalo na mjadala ni wahusika. Katika mdahalo kuna mwenyekiti, katibu, wasemaji wakuu wa upande wa utetetezi na upinzani na hadhira lakini kwenye mdahalo kuna kiongozi na hadhira tu.
- Katika mdahalo kuna wasemaji wakuu wanaotetea au wasiokubaliana na mada lakini kwenye mjadala yeyote anayetaka kutoa hoja anaruhusiwa na kiongozi.
- Kwenye mdahalo kuna pande mbili yaani upande wa utetezi na wa upinzani lakini kwenye mjadala hakuna makundi ya utetezi na upinzani.
- Mdahalo ni mashindano na mwishoni mwake washindi hupigiwa makofi lakini kwenye mjadala hakuna washindi; kiongozi wa mjadala anatoa suluhisho kutokana na mawazo yaliyotolewa. Mjadala si mashindano.

**c) Mambo ya kuzingatiwa:**

- Kupanga makundi
- Kueleza mada
- Kupanga viongozi wa mdahalo (mwenyekiti, katibu, ...)
- Watetezi na wapinzani kujadiliana
- Maamuzi ya mdahalo

### 22.8.3 Mazoezi ya Nyongeza:

**a) Sarufi:**Weka vitenzi vifuatavyo katika hali ya kushurutisha, umoja na wingi, katika hali kanushi

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kuja | *njoo/kuja* | *njooni/kujeni* |
| Kunywa | *kunywa* | *kuyweni* |
| kudharau | *dharau* | *dharauni* |

**b) Kuandika: Fanyeni mjadala kuhusu mada ifuatayo:** “Kupewa nafasi katika ngazi za uongozi kwa wanawake kulichangia kikubwa katika maendeleo ya nchi ya Rwanda.”

**Majibu:**

*a) Sarufi*

| Kitenzi | **Hali ya kushurutisha** | |
|---|---|---|
| | **Umoja** | **Wingi** |
| Kuja | *Usije* | *Msije* |
| Kunywa | *Usinywe* | *Msinywe* |
| Kula | *Usile* | *Msile* |
| Kupa | *Usipe* | *Msipe* |
| kudharau | *usidharau* | *Msidharau* |

***b) Mambo ya kuzingatiwa:***

- Kusoma na kuelewa vizuri mada
- Kutafuta viongozi wa mjadala
- Kukumbushana taratibu za mjadala
- Kutumia vizuri muda uliopangwa
- Kuepukana na fujo na kelele
- Kupaza sauti unapotoa maoni kuhusu mada
- Kutoa maoni kwa madhumuni ya kutimiza lengo la mjadala
- Kutumia lugha kwa ufasaha
- Kuwaheshimu wengine
- Kupanga mawazo yako kabla ya kupata fursa

# MADA KUU YA 5: UTUNGAJI

5

## MADA NDOGO: INSHA ZA MASIMULIZI AU KUBUNI NA UANDISHI WA RIPOTI

### Uwezo Upatikanao katika Mada

Kumuwezesha mwanafunzi kuzingatia mwongozo wa kutunga insha za masimulizi kulingana na mada iliyotolewa na kuzitolea muhtasari darasani kwa njia ya mazungumzo; kuandika ripoti rahisi; kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine.

### Ujuzi wa Awali

Kwenye mada ya nne katika kidato cha nne, mwanafunzi alisoma masomo yenye uhusiano na mada hii. Masomo hayo ni: maana ya mdahalo na mjadala, uhusiano na tofauti kati ya mdahalo na mjadala, mfano wa mdahalo na mjadala. Masomo haya yalipanua ujuzi wa mwanafunzi na kumuwezesha kuwasiliana na wengine, kutoa hoja zake mbele ya hadhira nakuheshimu maoni ya wengine. Yalimpa tena uwezo wa kutumia na kuongea Kiswahili kwa ufasaha. Pia katika mada ya tatu ya kidato cha nne wanafunzi walijifunza masomo ya ufahamu, fani na maudhui. Masomo hayo ya awali yatamsaidia mwanafunzi kufahamu mada kuu ya tano ambayo ni UTUNGAJI,pia yatamsidia kusoma kwa urahisi mada ndogo ambayo ni, « INSHA ZA MASIMULIZI AU KUBUNI NA UANDISHI WA RIPOTI.» Mwalimu hatapoteza muda wake kwa kuwafundisha wanafunzi maneno mwafaka ya kutumia katika maongezi ya lugha ya Kiswahili. Kwa ufupi, ujuzi uliotokana na mada za awali utamsaidia mwalimu kupata muda wa kutosha wa kuendelea na mada hii.

### Kuingizwa kwa Masuala Mtambuka katika Mada

Katika masomo ya mada hii kwenye vifungu, michoro, majadiliano, utumiaji wa msamiati katika sentensi, matumizi ya lugha, utungaji, kuzungumza, na mazoezi au kazi na sarufi; mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia masuala mtambuka yafuatayo:

#### Mafunzo kuhusu amani na maadili

Katika vifungu vya insha za masimulizi, za kubuni na ripoti, ni aina za utungaji zinazotumiwa kwa kusisitiza mafanikio ya kuishi kwa amani na maadili katika jamii. Hayo huonekana hasa katika vifungu vya "Mafanikio ya kudumu"na "Kioja katika Mbuga ya Mwanga".

**Mwalimu anapofundisha:**

- Wanafunzi watunge vifungu kuhusu mada ambazo huzungumzia namna ya kudumisha amani na maadili katika jamii.
- Mifano ya sentensi itakayotolewa na wanafunzi iwe inasisitizia umuhimu wa amani na maadili katika jamii.

**Mila na desturi na kuzalisha kuzalisha bidhaa kwa kuzingatia viwango vya ubora**

Katika vifungu vya insha kama « Usafi wa Mavazi Yetu », mwandishi anaonyesha umuhimu wa usafi wa mavazi na usafi wa mwili kama njia ya kujiheshimu na kuhimiza watu wengine kuwa na usafi kila mahali.

**Mwalimu anapofundisha :**

- Wanafunzi watunge vifungu kuhusu mada ambazo huzungumzia namna ya kuzingatia usafi na kujua kuchagua vitu safi kama mila na desturi na kuzalisha kwa viwango.
- Mifano ya sentensi itakayotolewa na wanafunzi iwe inasisitizia umuhimu wa usafi.

**Elimu Jumuishi**

Baadhi ya mifano ya sentensi huonyesha namna wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu na wenye matatizo ya kimwili (wasioona au wasiosikia vizuri, wasiotembea vizuri, n.k.) hushirikishwa katika nyanja zote za ufundishaji na ujifunzaji. Isitoshe, katika uundaji wa makundi jambo hili linapaswa kutiliwa mkazo.

Mwalimu analazimika kuwaonyesha wanafunzi kwamba elimu haina mpaka na kwamba yeyote ana uhuru wa kupata elimu bila ubaguzi wa aina yoyote.

**Mazingira na Maendeleo Endelevu**

Katika vifungu vya "Kioja katika Mbuga ya Mwanga" na "Ripoti kuhusu kazi za umuganda" kuna uhimizaji wa kuhifadhi mazingira kwa ujumla.

Mwalimu kupitia mazoezi ya insha na ripoti au ya msamiati na sarufi, anaweza kuwasaidia wanafunzi kufahamu umuhimu wa kuhifadhi mazingira katika maisha ya watu.

**Usawa wa jinsia**

- Mwalimu katika mifano yote, ni lazima atoe mifano inayoonyesha usawa wa jinsia.
- Katika mazoezi ya kutunga sentensi, ni vizuri kutunga sentensi ambazo zinaeleza na zinatoa maelezo kuhusu usawa wa jinsia.
- Kazi katika makundi, ni vizuri kupanga wasichana na wavulana katika kundi moja ili wanafunzi waelewe kuwa wavulana na wasichana wanaposhirikiana wanatimiza malengo kwa urahisi.
- Mada zinazojadiliwa, zilete dhana ya usawa wa jinsia.

**Mafunzo kuhusu uzalishajimali**

Katika kifungu « Mafanikio yangu », mwandishi anaonyesha wazi njia ya kujitafutia ajira kwa kuandaa mradi na kuwapa watu wengi kazi.

Katika mazoezi tofauti, mwalimu awahimize wanafunzi kuwa na ufahamu kuhusu sera ya uzalishajimali na kuandaa miradi tofauti.

## Mwongozo kuhusu Zoezi la Utangulizi wa Mada

Kwa kutangulia mada, mwalimu awaulize maswali yafuatayo ambayo yatawasaidia wanafunzi kufunua kuhusu mada hii.

1. Utungaji ni nini?
2. Insha ni nini?
3. Kuna aina gani za insha?
4. Ripoti ni nini?
5. Jadili umuhimu wa utungaji wa insha.
6. Jadili umuhimu wa utungaji wa ripoti.

Wanafunzi katika makundi ya wanne wanne watumie dakika kumi wakijibu maswali ya hapo juu. Mwalimu ajiegemeze kwenye majibu yatakayotolewa ili afahamu ujuzi wanafunzi walio nao kuhusu mada.

## Orodha ya Masomo na Tathmini

| Somo la | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza: maarifa na ufahamu,stadi na maadili na mwenendo mwema | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| 1 | Maana ya insha | **Maarifa na ufahamu:**<br>- Kuonyesha uwezo wa kutunga insha kutokana na maandalizi ya awali yaliyoegemea katika utafiti.<br>- Kueleza jinsi ya kutumia usemi wa asili na wa taarifa<br>Stadi:<br>Kujiandaa awali kabla ya utungaji wa insha kwa utafiti na kupangilia hoja za insha.<br>Maadili na mwenendo mwema:<br>Kuonyesha moyo wa kufanya kwa bidii. | 7 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | Aina za insha | **Maarifa na ufahamu :**<br>Kukumbuka na kutoa aina za insha<br>**Stadi:**<br>Kuorodhesha aina za insha, kuonyesha tofauti na uhusiano wa insha hizo.<br>**Maadili na mwenendo:**<br>Ushirikiano, urafiki, kujiamini na kufanya kwa bidii. | 7 |
| 3 | Insha za masimulizi | **Maarifa na ufahamu:**<br>Kukumbuka taratibu zakupanga mawazo na kuandika insha za masimulizi<br>**Stadi:**<br>- Kutumia msamiati unaofaa na unaoeleweka<br>- Kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia na kuridhisha<br>- Kufanya mtiririko mzuri wa mawazo<br>Maadili na mwenendo mwema:<br>- Kutotumia lugha ya matusi<br>- Kutumia mawazo mema ya kusaidia msomaji na jamii kwa ujumla | 9 |
| 4 | Insha za kubuni | **Maarifa na ufahamu:**<br>-Kutafsiri mazingira ya mada na kuijadilia bila upotovu wowote<br>-Kutambua lugha inayofaa katika insha za kubuni<br>**Stadi:**<br>Kuandika insha ya kubuni kwa kufuata utaratibu wa uandishi wa insha za kubuni.<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>-Kufuata shauri na mifano inayopatikana katika insha za masimulizi. | 9 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Maana ya ripoti | **Maarifa na ufahamu:**<br>- Kuonyesha uwezo wa kutunga ripoti kutokana na maandalizi ya awali yaliyoegemea katika mambo yaliyotokea.<br>- Kueleza jinsi ya kutumia usemi wa asili na wa taarifa<br>**Stadi:**<br>Kuandika ripoti kwa kufuata utaratibu wa uandishi wa ripoti<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>-Kuandika mambo yaliyotokea bila kuongeza au kupunguza yaliyotokea. | 10 |
| 6 | Utunzi wa ripoti | **Maarifa na ufahamu:**<br>-Kufanya ripoti kuhusu jambo fulani lililotokea.<br>-Kutambua lugha inayofaa katika ripoti<br>**Stadi:**<br>Kuandika ripoti kuhusu tukio au jambo fulani kwa kufuata utaratibu wa uandishi wa ripoti.<br>**Maadili na mwenendo mwema:**<br>-Kutoenda mbali na ukweli uliotokea. Kutoongeza au kupunguza yaliyotokea. | 7 |
| Tathmini ya mada | | | 2 |
| Vipindi vya mada | | | 51 |

## SOMO LA 23: MAANA YA INSHA

### 23.1: Ujuzi wa Awali / Utangulizi

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali ambayo yatawasaidia kukumbuka na kufahamu zaidi somo lililotangulia. Atakapomaliza kuwauliza maswali ya kuwakumbusha somo la awali, mwalimu awasaidie wanafunzi kuingia katika somo linalohusika ambalo ni "Maana ya Insha." Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yawezekanayo ili kuwafanya wanafunzi wagundue somo lenyewe.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awaambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro uliopo kwenye kitabu cha mwanafunzi kuhusu maana ya insha. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. « Anaweza kuwaambia: Tazameni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo »:

- Watu unaowatazama kwa mchoro huo wanafanya nini?
- Eleza shughuli za watu hao kwenye mchoro hapo juu
- Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro huo na kichwa cha habari hapo chini?

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na mtu wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine. Mwisho wake mwalimu atoe maoni yake kuhusu yaliyofanywa na wanafunzi kwa kurekebisha yaliyofanywa kwa namna isiyo bora.

### 23.2: Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atumie vifaa ambavyo vitamsaidia kutimiza malengo ya somo.

Baadhi ya vitabu vinavyomsaidia ni pamoja na:

- Mtaala wa somo la Kiswahili
- Kitabu cha Kiswahili cha mwanafunzi
- Kitabu cha Kiswahili cha mwalimu
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu

Mwalimu kwa uwezo wake aandae vingine mwenyewe vya kumsaidia kufanikisha somo.

### 23.3: Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Mwalimu achague mbinu inayofaa kulingana na aina ya zoezi husika. Kwa mfano:

- Mbinu ya tafakari binafsi
- Ushirikiano kwa jozi na makundi
- Mbinu ya "Waza -jozi -shiriki" kwenye kidokezo, majibu ya ufahamu, n.k.
- Kazi ya kimakundi kuhusu mazoezi ya matumizi ya msamiati wa msingi,
- Majadiliano katika zoezi la kusikiliza na kuzungumza

### 23.4 Majibu

**Zoezi la 1 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watazame mchoro kisha wajibu maswali. Mwalimu achunguze maswali yanayotolewa na wanafunzi.*

### 23.4. 1Maswali ya Ufahamu

Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu: Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu. Majibu ni haya yafuatayo:

1. Insha ni utungaji ambao hulenga kumpa mwanafunzi uwezo wa kutunga habari yeye mwenyewe na kuiwasilisha kwa watu wengine kwa kutumia njia ya mazungumzo au maandishi.

2. Kwa kuwasilisha habari kunatumiwa njia ya mazungumzo na maandishi

3. Hii ni insha ya maelezo kwa sababu inatoa maelezo kuhusu insha. Inaeleza maana ya insha.

4. Somo la insha linamsaidia mwanafunzi kutunga habari yeye mwenyewe na kuiwasilisha kwa watu wengine kwa kutumia njia ya mazungumzo au maandishi

5. Insha yoyote ina  sehemu kuu tatu muhimu: utangulizi; kiini na hitimisho.

Utangulizi:Sehemu hii huzingatia fasili ya jambo linalozungumziwa

Kiini: Hii ndiyo sehemu kuu ya insha na huzingatia mawazo makuu ambayo hupangwa katika aya zenye mtiririko wa mawazo.

Hitimisho : Sehemu hii ya insha inaelezea muhtasari wa maudhui yote yaliyoelezwa katika Insha nzima. Hutoa msisitizo kwa yaliyojadiliwa na huwa na maoni na mapendekezo ya mwandishi kuhusu jambo lililotungiwa insha

6. Utangulizi unafaa uwe wa kuvutia ili msomaji awe na hamu ya kuendelea kuisoma insha hiyo. Kwa hiyo, mwandishi hueleza maana ya mada ambayo huchukuliwa kama anwani au kichwa cha insha alichopewa

7. Kwa sababu kiini huzingatia mawazo makuu makuu ambayo hupangwa katika aya zenye mtiririko wa mawazo huonyesha kwa undani maana ya jambo linalotungwa, kwa hoja na uthibitisho

8. Tofauti ni kuwa utangulizi ni sehemu ya mwanzowa insha. Hitimisho: ni sehemu au kipande cha mwisho wa insha.

9. Ndiyo mwanafunzi anahitaji ujuzi kuhusu insha katika maisha yake ya kila siku kwa sababu katika masomo mengi anaombwa kutunga insha. Tena ukiwa na ujuzi wa kutunga insha vinakusaidia sana kutoa hoja au kujieleza. n.k.

10. Wanafunzi wengi wanaogopa swali la kutunga insha kwa kuwa hawana ujuzi na uwezo wa kutosha kuhusu utungaji wa insha.

### 23.4.2  Msamiati kuhusu Maana ya Insha.

**Zoezi la 2: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe wanafunzi kutazama katika kamusi kisha watungesentensi kwa kutumia maneno.

1. **Dhahiri :** Kila mwanafunzi anaelewa somo la insha kwa sababu mwalimu alieleza somo hilo dhahiri
2. **Nathari:** Kwa kutunga insha, hadithi au tamthilia tunatumia maandishi ya kinathari.
3. **Mtungo:** Adili na ndugu ze ni mtungo wa Shaabani Robert
4. **Mantiki:** Kalisa anapata alama chache kwa sababu alitunga insha yake bila mantiki.
5. **Kubuni:** Baada ya kumaliza shule ya sekondali, nitabuni hadithi nyingi kuhusu haki za watoto.
6. **Kutafiti:** Watafiti kabla ya kutangaza ripoti, wanatafiti mada husika.
7. **Kipawa / kipaji:** Mwanafunzi mwenye kipawa katika muziki hupendwa na wenzake.
8. **Kuvutia:** Mtaala unaoegemea uwezo ni mtaala wa kuvutia
9. **Uamuzi:** Nchi yetu ilichukuwa uamuzi wa kujiunga na nchi zingine kimaendeleo.
10. **Aya:** katika uandishi wa insha, mwandishi hutumia aya tofauti sana sana kwenye kiini cha insha.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu aombe kila mwanafunzi kuhusisha maneno katika sehemu A na maana zake katika sehemu B. wanafunzi watumie Kamusi ya Kiswahilin Kanifu.*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mtaalamu | f. Mtu mwenye ujuzi au elimu ya jambo fulani. |
| 2. Uthibitisho | j. Tendo la kuthibitisha; ushahidi, ushuhuda. |
| 3. Makala | c.Maandiko kuhusu mada au jambo fulani yanaoandikwa katika jarida au gazeti. |
| 4. Maoni | d. Maneno yaoneshayo fikira za mtu juu ya jambo fulani |
| 5. Nyenzo | h. Vitu vya kutengenezea vitu vingine |
| 6. Hoja | b. Pendekezo |
| 7. Fursa | a. Nafasi ya kuweza kufanya jambo |
| 8. Kufaa | g. Kuwa katika hali ya kutumika. |
| 9. Kuzingatia | i.Kutia moyoni na kufikiria |
| 10. Mtiririko | e. Hali ya kitu au jambo kuendelea au kufanyika moja kwa moja bila kukatika. |

Zoezi la 4: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika jozi la wanafunzi, mwalimu awaambie wanafunzi wakamilishe sentensi kwa kutumia maneno yanayofaa kati ya haya yafuatayo: mtungo, utangulizi, kiini, hitimisho, aya,tatu,utungaji, insha, nyenzo,sehemu

1. Kwenye utangulizi mwandishi hueleza maanaya mada/anwani/kichwa alichopewa.
2. Insha ni aina ya utungajiambao humpa mwanafunzi uwezo wa kubuni.
3. Insha ina sehemu kuu tatu :utangulizi, kiini na hitimisho.
4. Sehemu kuu ya insha ni kiini.

5. Kila aya hujitosheleza kwa kila kitu katika kulielezea jambo moja tu au hoja moja tu.
6. Hitimisho linaelezea muhtasari wa maudhui yote yaliyoelezwa katika insha nzima.
7. Insha ni mtungo wa maneno kwa mtindo wa kinathari juu ya jambo fulani.
8. Insha ina sehemu kuu tatu.
9. Mtungo huu ni nyenzo muhimu sana kwa mtu kwa kumuwezesha kubuni.
10. Sehemu kuu ya insha ni kiini.

### 23.4.3: Sarufi: Usemi wa Asili na Usemi wa Taarifa ( katika wakati uliopo)

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wachunguze sentensi katika sehemu A na sentensi zilizotolewa katika sehemu B ili waweze kujibu maswali yanayofuata hapo chini*

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| «Ninapenda somo la Kiswahili.» Mwanafunzi anasema. | Mwanafunzi anasema kuwa anapenda somo la Kiswahili |
| «Tunalima shamba».wanasema walimaji. | Walimaji wanasema wanalim shamba. |

**Majibu**

1. Sentensi kutoka sehemu A ni maneno yaliyosemwa na mtu,ambayo yamerudiliwa na mwingine bila kuongeza wala kutoa kitu ( usemi halisi)

Sentensi kutoka sehemu B maneno aliyoandikwa na mtu mwingine kwa namna nyingine. Hapa kuna mabadiliko ya alama za vituo na sarufi lakini ujumbe unabakia ule ule (usemi wa taarifa)2. Sentensi za sehemu A na sentensi za sehemu B zote zina maana isipokuwa mabadiliko ya muundo.

3. -Watalaamu wengi wanasema kwamba insha ni aina ya utungaji

-« Aya ni mfululizo wa sentensi zinazoendeleza wazo moja. Au fungo la maneno lenye maana kamili; paragrafu».Kamusi ya karne 21 inaeleza.

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Katika makundi ya wanafunzi watano: Mwalimu awaombe wanafunzi wajadili tofauti ya usemi wa asili na usemi wa taarifa

**Majibu kuhusu usemi halisi na usemi wa taarifa**

1. «Mama yangu analima shamba.» Kabanyana anatangaza.
2. Wazazi wanasema kwamba mtoto mzuri anamsaidia mlemavu.
3. Rurangwa anasema kwamba mama yake anapanda miti ili wawe na hewa nzuri.
4. « Ninaunda kundi moja na huyu kijana mwenye matatizo ya kuona.» Anasema Muhorakeye.
5. Kankindi anasema kuwa mama yake anafanya biashara.

### 23.4.4 Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya watu wawili wawili kuchunguza maneno na kuyapanga maneno kwa utaratibu unaofaa.*

1. Utungaji wa insha humpa pia fursa nzuri ya kuendeleza na kukuza kipawa
2. Urefu wa aya hutegemea uwezo wa mwandishi wa kufafanua wazo
3. Aya ni mkusanyiko wa sentensi zinazoendeleza wazo moja
4. Kwa kawaida utangulizi hauzidi aya moja.
5. Insha yoyote ina sehemu muhimu kuu tatu

**Zoezi la 8 *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)*:**

Mwalimu anachunguza majibu ya wanafunzi na kuyalinganisha na majibu hapa chini

1. Kwa maoni yangu insha ni utungaji au mtungo uliondikwa kwa lugha ya mjazo au nathari kuhusu kitu, mtu au tukio fulani .
2. Kwa kutunga insha ni lazima kueshimu sehemu za insha kwa kuwa bila kuheshimu sehemu hizo utungaji unakosa mantiki na itakuwa vigumu kuelewa ujumbe wa insha.
3. Sifa kuu tano za insha ni :
    - Insha ina sehemu kuu tatu : utanguluzi, kiini, hitimisho.
    - Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki
    - Tumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada
    - Maelezo yote yatolewe kwa undani
    - Maelezo yatolewe kwa njia ya kuvutia.

### 23.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 9: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaongoze kujadiliana kuhusu nafasi ya insha katika masomo tofauti.*

**Mambo ya kuzingatia:**

- Maana ya insha na matumizi yake (maelezo muhimu)
- vipengele muhimu vya insha: utangulizi, kiini, na hitimisho.
- Sifa za insha ( kutazama maelezo katka maelezo muhimu ya insha)
- Masomo ambayo mara nyingi walimu wanaomba wanafunzi kutunga insha. Sana sana masomo ya lugha kama vile Kiingereza, Kinyarwanda na Kifaransa.

### 23.4.6 Utungaji

Zoezi 10: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anawaongoza kwa kutunga insha katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kwenye ukurasa moja ya mada unayotaka.*

**Mambo ya kuzingatia katika utungaji huu**

- Vipengele muhimu vya insha: utangulizi, kiini, na hitimisho.
- Ifikirie mada/kichwa/anwani kwa muda.
- Yaandike mambo muhimu yatakayokuongoza katika kuiandika insha
- Maelezo yote yatolewe kwa undani na kwa njia ya kuvutia.
- Kutumia vizuri alama za uakifishaji
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki
- Tumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada.
- Lugha iwe ya adabu na isiyo ya matusi

## SOMO LA 24: AINA ZA INSHA

### 24.1 Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu aina za insha. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu aina za insha, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama michoro iliyoko kwenye Kitabu cha Mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu michoro. Anaweza kuwaambia: « Angalieni kwa makini michoro hii na kujibu maswali yafuatayo »:

- Eleza wahusika vitu unavyoviona kwenye michoro.
- Matukio haya yanafanyikia wapi?
- Ni shughuli zipi unazoziona kwenye michoro?
- Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha somo na michoro?

### 24.2 Zana za Kujifunzia

iii. somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika zomo hili, zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,

- Michoro ya mavazi,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 24.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili mwalimu atatilia mkazo kwenye:

- Utumiaji wa makundi ya wanafunzi: kwa sababu mbinu zote za ujifunzaji zinapaswa kumweka mwanafunzi juu ya mambo yote darasani, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya matendo yote watakayoombwa na mwalimu, kwa kufanya kazi na mazoezi yaliyo ndani ya kitabu cha mwanafunzi.
- Kazi binafsi kwa mwanafunzi: itakapokuwa lazima kila mwanafunzi atapewa kazi/zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya utungaji binafsi au kwa kufanya tathmini).
- Maswali na majibu: mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali na wao watamjibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi wanaweza kumwuliza mwalimu naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.
- Maelezo ya mwalimu: mbali na kuwa mwanafunzi amepewa kipaumbele katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu angali msuruhifu katika somo. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 24.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha wajibu maswali haya:*

1. Eleza wahusika unaowaona kwenye mchoro.
2. Wahusika hao wako wapi na wanafanya nini?
3. Kuna uhusiano wowote kati ya mchoro na kichwa cha habari hapo chini?

Makundi manne yaruhusiwe kuwasilisha namna walivyojibu maswali haya, na mwalimu asisitizie yale majibu ambayo yatawasaidia wanafunzi kugundua somo husika.

### 24.4.1 Majibu ya Ufahamu

Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu.

1. Vazi ni nguo ya aina yoyote inayovaliwa mwilini
2. Kwa sababu vazi husaidia binadamu kujikinga na hali ya hewa.
3. Mavazi ya kike, mavazi ya kiume na mavazi mahususi.
4. Mtu akivaa nguo ya mtindo fulani mara nyingi utamaduni wake au uraia wake hutambulika waziwazi.Mifano : kuna mavazi na mitindo ya kinyarwanda, mavazi ya kimasai, ya kichina. Vitenge huonyesha utamaduni wa kiafrika. Kanga huenyesha utamaduni wa kitanzania.
5. Nguo za kijeshi, sare za manafunzi, sare za wachezaji, surupwenye
6. Ni vazi la mahususi kwa sababu huvaliwa kwa wakati maalun tu.
7. Nguo hutegemeana sana na utamaduni wa jamii husika kwa sababu mtu anaweza kuvaa vazi fulani likiwa zuri kulingana na utamaduni wake lakini likaonekana kuwa baya kwa watu wenye utamaduni tofauti na wake. Mifano : kuvaa bikini, chupi, nguo fupi na kutembea barabarani, kwa Wazungu ni jambo la kawaida lakini kwa Wanyarwanda ni jambo la aibu.
8. Chawa, tekenya, viroboto.
9. Ni lazima kwa sababu jambo hili hufanyika kwa kuaangamiza bakteria walioepukana na mionzi ya jua.
10. Ni vizuri kuwa na usafi wa nguo zetu pamoja na wa miili yetu.

### 24.4.2. Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wafanye utafiti na kueleza msamiati.*

1. **Pamba**: sufu ya mmeailiyo nyeupe na laini inayotumiwa kutengenezea nguo.
2. **Staha:** heshima inayoambatana na haya au aibu ya kutenda jambo lisilo zuri mbele ya wengine; hadhi, adabu.
3. **Pambo**: kitu kinachoongeza uzuri ; urembo.
4. **Maridadi** : safi, enye kupendeza macho.
5. **Mahususi:** enye kuhusika na kitu au mtu mmoja.
6. **Akiiga**: akitenda jambo kama afanyavyo mwingine.
7. **Chawa:** mdudu mdogo akaaye mwilini mwa binadamu hasa katika nywele na nguo chafu na hunyonya damu.
8. **Tekenya**:funza, mdudu mdogo kama kiroboto ambaye huingia katika miguu ya watu na wanyama.
9. **Kiroboto**: mdudu mdogo sana anayeuma na kufyonza damu na hupenda kukaa kwenye vumbi, manyoa ya paka au ya mbwa.
10. **Laika (ma):** unywele laini unaomea kwenye sehemu za mwili za mwili kama vile miguuni, kwapani, kifuani, n.k.

**Zoezi la 3: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajaribu kutunga sentensi.*

*Mifano ya sentensi*

1. **Pamba**: Wakati wa badiri kali watu huvaa nguo zenye pamba ndani.
2. **Staha:** Siku hizi watu wengi huvaa nguo sisizoonyesha staha ya kibinadamu.
3. **Pambo**: Herini ni pambo la mwilini.
4. **Maridadi** :Kwa sababu ya rangi zake tofautitofauti kipepeo huonekana maridadi sana.
5. **Mahususi:** Mzee Yakobo ana koti la mahususi kwa sababu analivaa kwenye Sikukuu ya Krisimasi tu.
6. **Akiiga**: Katika maisha kila siku mtoto hua akiiga matendo ya watu wazima.
7. **Chawa:** ni lazima tufue nguo zetu ili tuepukane ka chawa.
8. **Tekenya:** kila siku kabla ya kulala vizuri unawe miguu yako ili usiingiliwe na tekenya.
9. **Kiroboto**: Ni lazima tufue nguo zetu, tupige deki au tufagilie nguo zetu kwa kunyunyizia maji ili tusishambuliwe wa viroboto.
10. **Laika (ma):** Malaika ya kwapani yasiponyolewa hutoa harufu mbaya.

**Zoezi la 4: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watafute majina ya mavazi kwenye mraba.*

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | C | V | K | I | T | E | N | G | E |
| S | H | I | I | A | Z | A | P | A | L |
| K | U | R | K | F | N | M | I | U | U |
| T | P | A | O | F | U | I | E | N | B |
| S | I | D | I | R | I | A | K | I | E |
| O | S | H | A | T | I | K | A | I | G |
| K | A | B | U | T | I | U | S | N | A |
| S | U | R | U | A | L | I | I | U | N |
| I | S | U | K | I | L | O | K | B | N |
| V | E | L | I | S | U | T | I | Y | P |

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waunge fungu la A na fungu la B ili kujenga sentensi zenye maana.*

1f, 2h, 3g, 4i, 5a, 6b, 7j, 8e, 9c, 10d.

### 24.4.3. Sarufi

**Zoezi la 6: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wachunguze sentensi kisha wazigeuze katika usemi wa taarifa.*

*Majibu pendekezi*

1. Kagabo anasema kuwa mwanafunzi alifua sare zake.
2. Kagabo amesema kwamba mwanafunzi alifua sare zake.
3. Kagabo amesema kwamba mwanafunzi amefua sare zake.
4. Kagabo alisema kuwa mwanafunzi alifua sare zake.
5. Kagabo alisema kuwa mwanafunzi alifua nguo zake.

**Zoezi la 7: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wageuze sentensi katika usemi wa taarifa.*

1. Mkurugenzi alimwambia mkuu wa wilaya kwamba wanafunzi walipanda miti shuleni.
2. Mama amemueleza mkurugenzi. Mama amemueleza mkueugenzi kwamba Kalisa hakihudhulia shule vizuri kwa sababu ya ugonjwa.
3. Mwalimu alimwambia mwenzake kuwa wanafunzi walisafisha darasa.
4. Mwalimu mkuu aliwambia mwanafunzi kuwa nguo za shule zilichanika na alipaswa kutafuta nyingine mpya.
5. Kamasa aliapa mbele ya wazazi wake kwamba hakuiba vitabu maktabani.
6. Mwalimu alitaka kujua sababu iliyomfanya mwanafunzi kuchelewa.
7. Mkuu wa tarafa amemuuliza raia mahali alipozaliwa./ Mkuu wa tarafa ametaka kujua alipozaliwa raia.
8. Mwanahistoria anaelezakwamba Rwanda ilitawaliwa na Wajerumani.
9. Muuguzi alitaka kujua mara alizotapika mtoto usiku wa siku iliyotangulia.
10. Mshukiwa amedai mahakamani kwamba yeye hajafanya kitendo chochote cha uharifu.

**Zoezi la 8: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wageuze sentensi katika usemi wa asili.*

1. "Niling'olewa jino bovu hapo kabla." Daktari wa meno aliaambiwa na mgonjwa.
2. "Wanafunzi walipanda miti kwenye mlima wa Nyamagumba mwaka uliopita."Mkurugenzi alimueleza Waziri wa Elimu.
3. "Mwanangu amepewa maziwa?" Mama ameuliza.
4. "Tumewakamata wezi watatu."Walindausalama walieleza.
5. "Wanyarwanda walikuwa wakiishi kwa amani na upendo katika enzi za jadi."Waziri wa Utamaduni aliwaambia wananchi.

6. “Uungwana ulikuwa nguzo ya maisha ya Wanyarwanda.”Mzee aliwaambia wajukuu wake.
7. “Kwa nini hujafunga mkanda wa gari?” Polisi wa doria alimuuliza dereva.
8. Mwalimu ametaka kujua tarehe ya kuzaliwa kwa mwanafunzi.
9. “Mauwaji ya kimbari dhidi ya Watutsi yalirudisha nyuma nchi yetu katika nyanja zote.”Mwalimu wa Historia aliwaambia wanafunzi.
10. “Serikali imetayarisha chanjo dhidi ya polio”.Waziri wa Afya aliliambia Baraza la Mawaziri.

### 24.4.4. Matumizi ya Lugha:

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waandike majina ya makundi.*

1. Sanaa
2. Sayari
3. Wanyamapori
4. Wadudu
5. Samani

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Majibu kuhusu insha*

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu mawsali kukusu insha***.**

Kuna insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za masimulizi, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

1. Ni aina ya insha ya maelezo kwa sababu inaeleza vazi na usafi wake.
2. Ni nini tofauti iliyoko baina ya insha ya wasifu na insha ya masimulizi. Insha ya wasifu hutoa sifa za kitu, mtu, hali au jambo fulani ilhali insha ya masimulizi husimulia au hueleza tukio fulani maalum la kweli au la kubuni kwa njia ya kisanaa.
3. Kwa sababu gani mara zote mwandishi wa insha ya methali hulazimishwa kutetea methali aliyopewa? Mara zote mwandishi wa insha ya methali hulazimika kutetea methali iliyotolewa kwa sababu methali hujaa mambo ya hekima na huchaguliwa kwa kutaka kutoa fundisho kwa ja mii.

### 24.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaambie wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kujadili kuhusu mada zifuatazo, kisha wawaelezee wenzio.*

1. “Umuhimu wa mavazi”.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kujikinga na hali ya hewa
- Kuficha utupu wa mtu
- Kupamba mwili wa mtu
- Kuonyesha utamaduni

2. "Umuhimu wa kuvaa sare za shule kwa wanafunzi."

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kutambulisha mwanafunzi
- Kutambulisha shule
- Kutofautisha wanafunzi na raia wengine
- Usafi wa wanafunzi
- Usalama wa mwanafunzi
- Kuweka wanafunzi kwenye kiwango kimoja (kimawazo)
- "Umuhimu wa kuvaa viatu."
- Mambo ya kuzingatiwa

3. Umuhimu wa kuvaa viatu."

**Mambo ya kuzingatiwa**

4. "Umuhimu wa kusafisha nguo zetu"

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kuonekana maridadi
- kujiheshimu
- Kujikinga na magonjwa yatokanayo na uchafu
- Kutokuwa tatizo kwa wengine

### 24.4.6. Kuandika

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amwambie mwanafunzi kutunga kifungucha habari kwa kutoa hoja na maelezo kamili kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo.*

1. "Mabadiliko ya mavazi nchini Rwanda".

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Mitindo ya mavazi ya zamani
- Mitindo ya mipya leo

2. "Umuhimu wa kutotumia nguo za mitumba nchini Rwanda." **Mambo ya kuzingatiwa**

- Kuimarisha sera ya kutumia vitu vinavyotengenezewa nchini Rwanda
- Kujikinga na magonjwa yatokanayo na nguo za mitumba

- Kujiheshimu (kutotumia mavulio)

3. “Wadudu wanaotokana na uchafu na madhara yao.”

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kutaja mifano ya wadudu watokanao na uchafu na kueleza madhara ya kila mmoja.
- Kutaja njia zinazoweza kutumiwa kwa kuwaangamiza.

## SOMO LA 25: Insha ya Masimulizi

### 25.1 Ujuzi wa Awali

Mwalimu aulize wanafunzi maswali kuhusu somo lililotangulia na kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa kuyajibu maswali haya. Mwalimu ahakikishe kuwa wanakumbuka vizuri somo la 23 “ maana ya insha” na somo la 24 “aina ya insha”. Baada ya kujibu maswali hayo, mwalimu awaambie wanafunzi kuchukua vitabu vya Kiswahili na kutazama mchoro kwenye ukurasa husika, kisha awaulize wanafunzi maswali kuhusu mchoro walioutazama. Mwalimu anaweza kuwauliza maswali yafuatayo:

1. Elezea wahusika unaowaona kwenye mchoro.
2. Unadhani watu hawa wanafanya nini?
3. Tukio hili linatukia wapi?
4. Kuna uhusiano wowote kati ya kichwa cha habari na mchoro?

Kutokana na maswali yaliyouliza na majibu yaliyotolewa, mwalimu aombe wanafunzi wajaribu kufumbuwa somo linahusu nini.

### 25.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

- Mtaala  wa Kiswhili
- Kitabu cha mwanafunzi,
- Kamusi  ya Kiswahili sanifu,
- Kitabu cha mwongozo wa mwalimu
- Kalamu , chaki na ubao.

### 25.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

- **Utumiaji wa makundi ya wanafunzi**: Mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne kulingana na jumla ya idadi ya wanafunzi darasani. Wanafunzi wafanye kazi wanayopewa na mwalimu kila mwanafunzi akishiriki kwa kutowa mchango wake kujibu maswali waliopewa. Mwalimu achunguze kwa makini namna kazi inavyofanyika katika makundi kwa kutumia muda vizuri na kutoa msaada ikiwa unahitajika. Makundi haya yahusishe wasichana na wavulana.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**: Kwa kusaidia kila mwanafunzi na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa, mwalimu awape wanafunzi kazi ya binafsi. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake bila msaada wa mwalimu au mwanafunzi mwenzake.

- **Mihadhara**: Mwalimu atumie njia hii kwa kuwapa wanafunzi fursa ya kutumia lugha. Wanafunzi wajitokeze mbele ya wenzao watoe maelezo yao kuhusu mada husika. Maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzao iwezekanavyo. Mwalimu aongoze mihadhara hii na kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa kwa kutega sikio na kuuliza maswali. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wote wanashindwa kujibu vilivyo.

- **Maelezo ya mwalimu**: Mwalimu kwa ujuzi wake ahakikishe kwamba maelezo anayotoa yanawawezesha wanafunzi kuelewa somo wanalojifunza. Ikiwa mwalimu anatambua kasoro fulani, ni lazima awaelezee wanafunzi vya kutosha akisisitizia kasoro aliyoitambua.

## 25.4Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoonekana kwenye michoro hiyo. (Wanafunzi wataangalia mchoro na kuzungumzia vile wanavyoona)*

### 25.4.1 Maswali ya Ufahamu

**Mwalimu anawaomba wanafunzi katika makundi kujibu maswali ya ufahamu**

1. Kabatesi alipokuwa mtoto mdogo hakubahatika kulelewa na wazazi wake kwani walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake.
2. Kabatesi alipewa zawadi nyingi baada ya kumaliza masomo yake ya shule za Sekondari Kabatesi kwa kuwa alipata cheti kilichokuwa na alama nzuri. Jambo hili liliwafurahisha watu wengi: walimu na majirani zake. Wengi waliompongeza siku hiyo walimletea zawadi nyingi.
3. Masomo ya muda mfupi aliyoyafuata yalihusukuandaa miradi midogo midogo ya kujendieleza na jinsi ya kuifanikisha.Aliomba mkopo ili aweze kutekeleza mengi aliyokuwa amejifunza katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo
4. Kabatesi aliweza kufaidika kutokana na masomo ya muda mfupi akapewa cheti katika maandalizi na utekelezaji wa miradi ya kimaendeleo.
5. Alipomaliza masomo yake katika shule za sekondari, Kabatesi alipata stashahada iliyokuwa na alama nzuri. Alipewa kazi ya ukalimani. Kazi hiyo ilikuwa furasa nzuri ya kuonyesha uwezo wake na kutekeleza mengi aliyokuwa amejifunza katika shule za sekondari.

6. Alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia jambo alilifuatalia mpaka lilipokamilika. Mfano : Kabatesi alikuwa na fikira nyingi kuhusu jinsi ya kutumia shamba lake kubwa ambalo alilokuwa ameachiwa na wazazi wake. Kwa kutimiza mpango wake baada ya kumaliza shule zake za sekondari alisoma masomo ya muda mfupi kuhusu kuwawezesha kuandaa miradi midogo midogo ya kujendieleza na jinsi ya kuifanikisha. Alipata kazi ya ukalimani, kufungua akaunti, kuomba mkopo kutoka benki na kutumia fedha hizo kwa kuandaa mradi wa kilimo na ufugaji. n.k.
7. Kabatesi aliweza kuboresha maisha ya watu wengine kwa kuajiri baadhi ya vijana waliokuwa pamoja katika mafunzo ya muda ule mfupi, kila mmoja akapewa jukumu lake.
8. Kabatesi alipewa tuzo kwa kubadilisha maisha ya watu wengi. Alitengeneza ajira kwa watu wengi.
9. Alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Alikuwa msichana aliye na mawazo na mtazamo imara wa maisha kiasi kwamba watu walishangaa kutokana na tabia na mienendo yake. Alifanya kazi yake kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake.Alifanya kazi yake kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake. Na utulivu na upendo ni baadhi ya sifa zinazomtambulisha kijana huyu ambaye amewashangaza wengi wanaofahamu.
10. Kabatesi anachukuliwa kuwa mfano kwa vijana wenginekwa kuwa alijulikana kote nchini kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu. Alipewatuzo la mtu aliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine.
11. Ndiyo ninapata funzo kwa kifungu hiki kama vile:
    - Kuwa mwanafunzi au mfanyakazi mwenye bidii.
    - Kutokata tamaa
    - Kuwa na malengo au mipango maishani mwa mutu.
    - Kuwa mtu mwenye mawazo na mitazamo imara wa maisha.
    - Somo la kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu
    - N .k.

    a. Mvumilivu hula mbivu : Kabatesi wazazi wake walifariki angali mdogo akachukuliwa na kulelewa na shangazi yake. Kayitesi baada ya kifo cha mama yake alivumilia maisha ya kuwa yatima kwa wazazi wote baadaye akawa tajiri maarufu aliechangia kuyaboresha maisha ya majirani zao kwa kuwapatia kazi.

b. Mchumia juani hulia kuvulini: Kabatesi alikuwa mwanafunzi mwenye bidii tangu shule za chekechea hadi kiwango alichofikia. Kabatesi alikuwa anatumia nguvu zake zote. Alifanya kazi kazi ya ukalimani kwa bidii kiasi kwamba watalii wengi walifurahia huduma yake. Alikuwa msichana asiyekata tamaa na kila aliposhikilia jambo alilifuatalia mpaka lilipokamilika. . Aliandaa vizuri mradi wa kilimo na ufugaji, akajenga vibanda vya mifugo yake. Baadaye alikuwa alipata mali nyingi na kuanza kujulikana kote nchini kwa uwezo wake wa kufanya mambo mengi kwa muda mfupi na kwa ukamilifu. serikali ilimpatia tuzo kwa watu waliochangia kubadilisha maisha ya watu wengine. Kabatesi alikuwa miongoni mwa matajiri maarufu. Kwa machache, kabatesi alikula matunda kutoka kazi aliyoifanya kwa muda mrefu.

## 25.2 Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anawaomba katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kutumia kamusi ya Kiswahili sanifu kwa Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno yafuatayo. Chunguza matumizi yake katika kifungu cha habari hapo juu.*

1. Kuandaa: Mwanafunzi mzuri anaanda masomo yake kabla ya kuanza wiki.
2. Karo: Mwanzoni mwa mwaka wa masomo , wazazi wanalipia watoto wao karo.
3. Tafrija: Watu walikuwa wengi katika tafrija ya ndoa ya kaka yangu.
4. Kusherehekea: Wanyarwanda wengi walisheherekea ushindi wa timu ya taifa "Amavubi" katika mchezo wa mpira wa miguu.
5. Ajira: Waziri Mkuu anahamasisha watu kujitafutia ajira kutokana na uhaba wa kutoa kazi kwa serikali.
6. Zawadi: Kaka yangu aliwapatia wazazi wetu zawadi nzuri kwa malezi bora waliotupatia.
7. Hodari : Katika mbio za baiskeli, mnyarwanda hadari alishika ushindi dhidi ya wananchi wageni.
8. Kukera: Utumiaji mbaya wa mali ya serikali ni swali linalokera viongozi wakuu wa nchi.
9. Kukata tamaa : yule kijana alifaidika katika maisha yake kwa kuwa wazazi wake walimuunga mkono badala ya kumkata tamaa.
10. Akaunti: Jirani yangu alifungua akaunti katika benki" songa mbele" ili apate mkopo wa kumsaidia kufanya biashara.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anaomba kila mwanafunzi kuhusisha maneno kutoka sehemu A na maana yake kwenye sehemu B.*

**Masahihisho**

| Sehemu A | Sehemu B |
|---|---|
| 1. Mkalimani | f. Mtu afasiriye papo kwa papo mazungumzo kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. |
| 2. Utalii | j.Hali ya kusafiri mbali au kuvinjari huku na huko ili kuyafurahia mandhari. |
| 3. Shahada | h. Cheti au karatasi maalumu anayopewa mtu baada ya kupata mafunzo fulani katika chuo. |
| 4. Mshahara | a.Malipo ya mwezi anayopewa mwajiriwa kwa kazi aliyofanya; janguo. |
| 5. Yatima | i.Mtoto ambaye mzazi wake au wazazi wote wamekufa. |
| 6. Stashahada | b.Cheti maalumu chenye hadhi ya chini kuliko shahada |
| 7. Mtaji | c. Mali inayotumika kuanzishia au kupanulia biashara au shughuli yoyote ya kuzalisha mali |
| 8. Mwaliko | e. Mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria mahali |
| 9. Tabia | d.Matendo ambayo mtu amezoea kuyafanya mara kwa mara;mwenendo;mazoea; desturi. |
| 10. Kudumu | g. Kuendelea kuishi au kuwepo kwa muda wote. |

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anaomba wanafunzi katika makundi yawatatu watatu kupanga vizuri herufi za hapa chini ili ziunde maneno ya Kiswahili*

Hodari

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| a | d | H | o | i | r |

Jukumu

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| m | u | K | u | j | u |

Mkalimani

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| n | i | m | K | I | m | l | a | wa |

Mkopo

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| o | O | k | p | m |

Benki

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| k | i | b | n | e |

**Zoezi la 5: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anaomba kila mwanfunzi kukamilisha sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo yanayofaa:*

1. Hapa nchuni Rwanda watoto wengi wanaanzia msomoyao **shule za chekechea**
2. Ili wanafunzi wafaulu katika mtihani wa taifa ni lazima wasome kwa **bidii.**
3. Wanakijiji wengi wanaomba mkopo kutoka benki kama **suluhisho** la ukosefu wa mitaji ya kifedha.
4. Kuna uhusiano wa karibu wa kazi ya **ukalimani** na utafsiri.
5. Wanafunzi wenye tabia ya **utulivu** wanapata alama nzuri katika masomo yao
6. Serikali ya Rwanda **inawapongeza** wasichana wanaosoma sayansi.
7. Wanafunzi waliofanya kazi katika makundi kwa **ukamilifu** wamepata alama nyingi.
8. Kalisa a**nahifadhi** pesa zake kwenye benki ili aruhusiwe kupata mkopo.
9. Wazazi wana majukumu ya kawalisha na kulipa karo za watoto wao.
10. Mjomba wangu alijenga **vibanda** vitatu vya kuku wake

### 25.4.3: Sarufi : Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa.

**Zoezi la 6 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anaomba wanafunzi katika makundi ya wawili wawili kusoma maelezo muhimu kuhusu usemi halisi (wakati ujao) na usemi wa taarifa na kujibu maswali. Haya ni majibu ya maswali:*

1. Kalisa alituambia kwamba angemsaidia mama yake kuosha vyombo nyumbani.
2. Mwalimu alisema darasani kuwa wanafunzi wangecheza pamoja na wale wenye matatizo ya kutembea.
3. Waziri wa elimu alisema kuwa tungeshinda mtihani wa taifa mwaka huo.
4. Kalisa alitukumbusha kwamba tungesoma kuhusu mauaji ya kimbari dhidi ya watutsi mwaka 1994.

5. Mkuu wa kata alisema katika mkutano kuwa wangewasaidia watoto wenye matatizo ya kutembea vizuri katika maisha yao ya kusoma.
5. Baba alimwambia mtoto kuwa yeye angelima mahindi na yule dada yake.
6. Mwanafunzi alimwambia mzazi wake kuwa wangecheza mpira wa miguu na timu jirani.
7. Mfanyakazi alisema katika mkutano kwamba wangelipwa mishahara yao kabla ya kuondoka.
8. Gasore alimshauri mkulima kuwa shamba lake lingeitaji kupaliliwa.
9. Mama yangu aliniambia kuwa angetoa mchango wake kuhusu mazingira na maendeleo ya kudumu.

### 25.4.4 : Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu anauliza katika kundi la wanafunzi wanne wanne kwa kujibu maswali hapa chini.*

**Mwalimu anachunguza kama wanafunzi wamesoma vizuri maelezo muhimu na kuyaelewa.**

1. Insha ya masumulizi ni mtungo unaosimulia tukio fulani, kisa au tukio la kweli au la kubuni.
2. Ili kazi ya  uandishi wa insha ya masimulizi ifauluni lazima mazungumzo haya agawanyike katika sehemu kuu tatu: mwanzo, kati, na mwisho na izungumzie ukweli wa jambo linalozungumziwa.

### 25.4.5: Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Serikali ya Rwanda inawahimiza wananchi kujitafutia ajira kutokana na uhaba wa kazi. Jadilieni kuhusu namna ya kujitafutia kazi.*

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Maana ya kazi
- Njia za kujitafutia ajira
- Uwezo wa binafsi kwa mtu
- Mwenendo wa kufanya kazi vizuri
- N.k

### 25.4.6: Utungaji

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Baada  ya kusoma kifungo kuhusu insha za masimulizi "mafanikio ya kudumu."Wewe mwanafunzi,tunga  insha ya masimulizi kuhusu tukio fulani, kisa au tukio la kweli au la kubuni .*

**Mambo ya kuzingatia kwa kutunga insha ya masimulizi:**

- Insha yenye sehemu tatu : utangulizi, kiini na hitimisho.
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki
- Kutumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada
- Maelezo yote yatolewe kwa undani
- Maelezo yatolewe kwa njia ya kuvutia.
- Kutumia vizuri sarufi na alama za uakifishaji n.k

## SOMO LA 26: INSHA YA KUBUNI

### 26.1. Ujuzi wa Awali/Marudio/Utangulizi

Mada hii inajishughulisha na msamiati na majadiliano kuhusu utungaji wa insha. Mwalimu aanze somo kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi watajibu maamkizi ya mwalimu kisha mwalimu atangulize somo kwa kuwauliza maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali haya yanapaswa kuwa na uhusiano na somo jipya.

Mwalimu atakachofanya ni kuwashirikisha wanafunzi wake ili waweze kuwasiliana kuhusu aina za insha, kisha atafanya chochote ili awawezeshe wanafunzi kufika kwenye kile anachotaka kufundisha.

Baada ya kufanya kazi hii, mwalimu awambie wanafunzi kufanya makundi na kutazama mchoro ulioko kwenye Kitabu cha Mwanafunzi. Kisha awaulize maswali kuhusu mchoro. Anaweza kuwaambia: **« Angalieni kwa makini mchoro huu na kujibu maswali yafuatayo »:**

- Eleza wahusika unaowaona kwenye michoro.
- Matukio haya yanafanyikia wapi?
- Ni shughuli ipi inayofanyika hapo?
- Unafikiria nini kuhusu mitazamo ya wahusika?
- Kuna uhusiano gani kati ya kichwa cha habari na picha?

### 26.2. Zana za Kujifunzia

Ili somo liweze kufika kwenye malengo yake, ni lazima mwalimu ajaribu kutafuta zana za ufundishaji zitakazomsaidia kufanikisha somo lake ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi na malengo ya somo husika. Katika zomo hili, zana muhimu ni:

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti,
- Michoro ya wanyama,
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kuelewa somo akitilia mkazo kuhusu hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

Vifaa hivi vitaandaliwa kulingana na mazingira ya shule. Kwa hiyo, mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyo kumsaidia kufanikisha somo lake. Mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ndiyo sababu yeye mwenyewe ajibunie vifaa visaidizi mbalimbali.

## 26.3 Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Katika hatua hii, mwalimu atatafuta mbinu mbalimbali zitakazomwezesha kufika kwenye malengo ya somo lake. Katika somo hili, mwalimu atatilia mkazo kwenye:

**Utumiaji wa makundi ya wanafunzi:** kwa sababu mbinu zote za ujifunzaji zinapaswa kumweka mwanafunzi juu ya mambo yote darasani, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya matendo yote watakayoombwa na mwalimu, kwa kufanya kazi na mazoezi yaliyo ndani ya kitabu cha mwanafunzi.

**Kazi binafsi kwa mwanafunzi:** itakapokuwa lazima kila mwanafunzi atapewa kazi/zoezi lake binafsi (kwa mfano: kusoma kifungu cha habari, kufanya utungaji binafsi au kwa kufanya jaribio).

**Maswali na majibu:** mara nyingi somo huwa na majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali na wao watamjibu maswali hayo. Vilevile wanafunzi wanaweza kumwuliza mwalimu naye akawajibu. Tena maswali na majibu haya yanaweza kuwa kati ya wanafunzi wenyewe.

**Maelezo ya mwalimu:** mbali na kuwa mwanafunzi amepewa kipaumbele katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu angali msuruhifu katika somo. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## 26.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, tazameni michoro hapo juu kisha mtoe maoni yenu kuhusu kile kinachoonekana kwenye michoro hiyo. (Wanafunzi wataangalia mchoro na kuzungumzia vile wanavyoona).*

### 26.4.1. Maswali ya Ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu.*

1. Alikuwa mpatanishi na mganga
2. Waombolezaji wa kijadi walijipanga kwa msitari mrefu na kumuaga mpatanishi na tabibu wao kitamaduni kwa kuimba nyimbo za kijadi na kubeba mikoba yake ya utabibu pamoja na mgwisho wake wa uungwana
3. Wafalme na wanyama kutoka mbuga jirani, na wanyama wa mbuga ya Mwanga.
4. Kifo cha Mzee Ngedere ni hasara kubwa kwa kijiji kile.

5. Kuilaza roho ya Mzee Ngedere mahali pema.
6. Alikwa akivaa joho na miwani
7. Ni Kunguru
8. Alikuwa akitaka kuchukua madaraka yake.
9. Gunia lilikuwa likitikisika kwa sababu ya Mzee Fuko na wake zake waliokuwa wakitaka kutoka katika shimo lao lililokuwa chini ya gunia.
10. Mwili wa Kasisi Nyati ulilowa maji kwa sababu ya hofu.

### 26.4.2. Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watatumie kamusi na kueleza maneno ya msamiati.*

1. **Kioja:** kiroja, jambo la ajabu
2. **Mazishi:** shughuli na taratibu zinazohusu maziko.
3. **Waliamua:** walikata shauri
4. **Walimiminika:** walikuja kwa wingi, walijaa.
5. **Nyoyo:** mioyo
6. **Majonzi:** hali ya kutokuwa na furaha kutokana na tukio la kusikitisha, simanzi, huzuni, sikitiko, jitimai, ghamu.
7. **Kasri:** jumba la kifalme
8. **Joho:** vazi pana linalofanana na koti refu ambalo mbele liko wazi.
9. **Walijizatiti:**walikuwa tayari kwa jambo fulani.
10. **Uchochezi:** tabia ya kuwatia watu maneno ili wapate kupigana au kutukanana, uchonganishi

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watoe neno jingine lililotumiwa katika kifungu lenye maana sawa na ya lile lililopigiwa mstari chini.*

1. Njema au ya kupendeza
2. Mgangabingwa
3. Majonzi
4. Mgwisho
5. Anawajali
6. Yanayojili
7. Shetani
8. Kuhimili
9. Zikalowa
10. Mungu

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunziwatunge sentensi mbili kwa kwa kuonyesha maana mbili tofauti za maneno.*

**Sentensi pendekezi**

1. Fuko:
    - Katika shamba la viazi vitamu mna **fuko** wengi sana.
    - Katika **fuko** la kuku wetu kuna mayai matano.

2. **Paa:**

**Paa** la darasa letu linapaswa kukarabatiwa.

Nilipoenda kwenye Mbuga ya Akagera niliwaona **paa**.

3. **Chungu**
    - Mama alitumia **chungu** kwa kupika nyama.
    - **Chungu** walishambulia mzinga wa nyuki na kuwafurusha nyuki wote.

4. **Kanga**
    - **Kanga** wale huishi vichakani.
    - Alimnunulia **kanga** mamake.

5. **Wimbi**
    - Walipotumbukuza jiwe mtoni **mawimbi** yalionekana.

6. **Hivi sasa kuna wimbi kubwa la vijana kujiajiri**

7. **Kiboko**
    - **Kiboko** ni mnyama mwenye nguvu nyingi sana.
    - Elimu ya leo haitolewi kwa **kiboko**.

8. **Kifaru**
    - Jangili aliwekwa jela kwa sababu ya kumuua **kifaru.**
    - **Kifaru** kilitumiwa kwa kuwafukuza waasi.

9. **Duma**
    - **Duma** aliyetorokea kijijini alirudishwa mbugani jana.
    - Jeshi letu **liliduma** waasi wengi.

10. **Swala**
    - Serikali yetu ilileta simba ili kupunguza idadi kubwa ya **swala** katika Mbuga ya Akagera.
    - Waisilamu waliswali **swala** ya Ijumaa katika uwanja wa wazi.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wakamilishe methali.*

1. Halimuumizi mwanawe.
2. Haliwiki mjini.
3. Hukimbiza ubawa wake.
4. Ndiye mla nyama.
5. Huruka kwa ubawa wake.
6. Hazimzuii ng'ombe kunywa maji.
7. Hakosi kamba mguuni.
8. Kabla hawajanguliwa/hawajatotolewa
9. Tembo hulitia maji.
10. Hafikii mbinguni.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wafanye utafiti na wataje majina vikembe (watoto) wa wanyama.*

1. Shibli
2. Neili/mwanakondoo
3. Papi
4. Kitungule
5. Kinda

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajaze mapengo kwa kuiga mfano waliopewa*

Mfarika...............mtamba....................beberu

**Tembe/koo..........jimbi............shangazi**

**Mfalme............dada**

**Babu ............. boi**

**Kiota.................mfalme**

### 26.4.3. Sarufi

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunziwachunguze sentensi kisha waziweke katika usemi wa taarifa.*

1. Chui alimwamrisha Kasisi Nyati kumaliza mambo yake haraka ili wamzike Mzee Ngedere.

2. Mfalme Simba alimkatiza Kunguru kwa kumwambia aache kuwatisha./ Simbwa alimshurutisha Kunguru kuacha kuwatisha.
3. Mzee Kobe alimwomba Mungu kuilaza roho yake mahali pema.
4. Binti Sungura alimwambia kuenda na kuanza mambo yake.
5. Bwana Chui alisikia akiwasihi wenzake wasikimbie./ Bwana chui alisikika akiwaomba wenzake kutokimbia.

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunziwageuze sentensi katika usemi wa taarifa.*

1. Mama alimwamrisha mtoto kuenda nje.
2. Mwalimu aliwashauri/ aliwaomba wanafunzi kusafisha darasa.
3. Mama alimtaka  Kalisa aende amtume. Mama alimwamrisha Kalisa kuenda akamtume.
4. Maria alimwonya/ alimsihi Rubyogo kutogombana na wenzake tena.
5. Baba alimshauri mtoto wake kuvuta ngozi ikingali mbichi.

**Zoezi la 10:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunziwageuza sentensi katika usemi wa asili.*

1. “Tafadhali tunzeni vitabu vizuri.” Mwalimu aliwaonya wanafunzi
2. “Karibisheni wageni!” Shangazi alitwambia.
3. “Msisogee karibu na moto!” Mama aliwakanya watoto.
4. “Onana nami baada ya wiki mbili!” Daktari alikiambia.
1. “Tafadhali, vizuri upige mswaki mara mbili kwa siku.” Dakatari wa meno alimwambia mgonjwa

### 26.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 11:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunziwajaze jedwali kwa kuchagua majina katika orodha ya maneno waliyopewa.*

| Ndege | Mnyamapori |
|---|---|
| Hua<br>Bundi<br>Njiwa<br>Kikwara<br>Tai<br>Flamingo<br>Gogota<br>Kware<br>Kware<br>Kanga<br>Koho | Chui<br>Duma<br>Pakashume<br>Mbweha<br>Fisi<br>Funo<br>Ngiri<br>Ngedere<br>Swala<br>Choroa<br>Kulungu<br>Nungu |

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali kuhusu aina za insha mwa kufuta maagizo.*

1. Kifungu cha habari ni insha ya kubuni.

**Kwa sababu:**

a. Wahusika: ni wa kujiundia na wanafanya matendo yasiyowezekana kutendwa nao.

b. Mandhari: mahali panaposimuliwa ni pa kubuni.

c. Yanayosimuliwa hayakutokea. Yalitoka katika ubunifu wa mwaandishi.

2. Ndiyo!Ninakubaliana na hoja hii kwa sababu kazi ya utungaji yoyote inatokana na ubunifu wa mwaandishi. Mwaandishi anakaa na kufikiri namna ya kutunga kazi hiyo.

### 26.4.5. Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 13:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu awaagize wanafunzi, katika makundi yao ya watatu watatu, kujadili kuhusu mada zifuatazo:*

1. Umuhimu wa Wanyamapori kwa Nchi ya Rwanda".

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kuvutia watalii
- Kuingizia fedha nchi kutoka kwa watalii

2 "Umuhimu wa Wanyama wa wafugwao nchini Rwanda."

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kuliwa kama nyama
- Kutoa mambo mengine yanayosaidia maishani (mayayi, ngozi, maziwa, mafuta,...)
- Kutoa mbolea
- Kuleta fedha

### 26.4.6 Kuandika

**Zoezi la 14: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu amwaagize wanafunzi, kutunga kifungu cha habari kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo:*

4. “Mikakati ya kulinda wanyamapori nchini Rwanda.”

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kupiga marufuku uwindaji haramu
- Kuwatengea mbuga
- Kukataza wananchi kufanyia shughuli zao katika mbuga za wanyama

5. “Umoja wa Wananchi ni Uti wa Mgongo wa Maendeleo ya jamii.”

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Ushirikiano katika mambo ya kijamii
- Ushirikiano katika mambo ya kiuchumi
- Ushirikiano katika mambo ya kisiasa

# SOMO LA 27: RIPOTI

## 27.1. Ujuzi wa Awali /Utangulizi

Mada hii inahusika na uandishi wa ripoti juu ya mada iliyotolewa na kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine. Mwalimu aanze somo kwa kuwauliza wanafunzi somo walilojifunza wakati uliopita. Wanafunzi wajibu maswali husika. Kisha mwalimu awachangamshe kwa kuwasimulia habari aliyoifuata kwenye redio au aliyoisoma katika gazeti. Mwalimu aombe wanafunzi kuwapasha wenzao habari nyingine waliyosikiliza kwenye redio au runinga au tukio lolote waliloshuhudia. Baadaye, mwalimu awaweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwapa kazi kutoka kwenye vitabu vya Kiswahili. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yafuatayo :

1. Eleza wahusika unaowaona kwenye picha hii.
2. Wahusika hawa wako wapi?
3. Eleza shughuli inayofanyika kwenye mchoro

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na msimamizi wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine.

## 27.2. Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufikia malengo ya somo lake. Mwalimu anaweza kutumia vifaa vifuatavyo :

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti au rekodi
- Magazeti
- Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasadia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kwenye hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

## 27.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Mwalimu atafute mbinu za kumfikisha kwenye malengo ya somo.Hapa chini kuna mbinu tofauti za kurahisisha maendeleo ya somo darasani.

- **Njia shirikishi**

Njia shirikishi hutumia **makundi ya wanafunzi.** Mwalimu awape wanafunzi kazi ya kufanyiwa katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne, n.k kulingana na idadi ya wanafunzi darasani. Mwalimu achunguze mara kwa mara jinsi kazi inafavyonyika. Wakati wowote, mwalimu atumie muda vizuri na atoe msaada ambapo unahijika. Makundi yaundwe na mchanganyiko wa wasichana na wavulana, na wanafunzi wenye shida za kibinafsi kama walemavu na wengineo. Baada ya kazi katika makundi wanafunzi wamulike matokea ya kazi yao kwa darasa ili wanafunzi wote wapate kujua mafanikio ya wanafunzi wenzao.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**

Katika somo hili, kuna mazoezi ya kutosha ambayo ni ya kufanywa kibinafsi kwa kusaidia kila mwanafunzi kuelewa kiundani na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. Aidha, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi mazoezi hayo wakiwa katika makundi.

- **Maswali na majibu**

Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na na kuyajibu wenyewe, wanafunzi kwa wanafunzi. Hivi ni kusema kwamba maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kupitisha maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi peke yao. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa na wanafunzi, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu ajibu ikiwa inatakiwa.

- **Maelezo ya mwalimu:**

Mwalimu atambuwe ujuzi unaohitaji mwelekeo na maelezo ya ziada. Mwalimu ahakikishe kwamba vikwazo vyote vinatoweka iwezekanavyo. Katika hatuua hii wanafunzi wapewe pia fursa ya kutoa maoni yao kuhusu maelezo ya mwalimu.

## 27.4 Majibu

**Zoezi la 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchoro.*

### 27.4.1Maswali ya Ufahamu

**Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu.**

1. Ripoti ni maelezo yanayotolewa kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea.
2. Ripoti huandikwa kwa madhumuni ya kutoa taarifa ili iweze kufanyiwa kazi au kuhifadhiwa kama kumbukumbu.
3. Kuna ripoti ya polisi, ripoti ya daktari, ripoti ya tume , ripoti ya utafiti na ripoti ya kazi.
4. Matumizi ya nambari husaidia kuipa ripoti mpangilio mzuri na wenye nidhamu.
5. Ripoti hutumia sentensi fupi fupi zinazowakilisha mambo muhimu kwa uwazi.
6. Ni vyema lugha inayotumiwa katika ripoti iteuliwe kwa uangalifu na isiwe na hisia au sifa ya kuathiri vibaya wanaosoma ripoti.
7. Ripoti huandikwa kwa madhumuni ya kutoa taarifa ili iweze kufanyiwa kazi au kuhifadhiwa kama kumbukumbu. Ripoti huandikwa pia kwa madhumuni ya kuarifu watu kuhusu mabadiliko muhimu au maendeleo ya shughuli fulani.

Ripoti inaweza tena kuagiza utekelezaji fulani, kupendekeza kufanyika kwa jambo fulani na kupima au kutathmini utendakazi fulani au maendeleo yaliyofikiwa.

8. Mwandishi wa ripoti hutakiwa kuwa muangalifu ili aweze kutoa ufafanuzi mzuri wa jambo analolifanyia ripoti kwani mapendekezo yake huathiri kwa kiwango kikubwa uamuzi unaochukuliwa kuhusu jambo hilo.
9. Ripoti ina sehemu kuu nne ambazo ni kichwa, utangulizi, kiini na mwisho wa ripoti.
10. Ripoti nzuri ni ile ambayo hutumia lugha nyepesi, kufafanua jambo kwa kina na kufuata mfumo wa ripoti kama inavyopendekezwa.

### 27.4.2 Msamiati

**Zoezi 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watunge sentensi sahihi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

**Zifuatazo ni sentensi pendekezo**

1. Anajadili kuhusu **matokeo** ya utafiti alioufanya.
2. Ninasoma ripoti kuhusu machafuko ya hewa.
3. Umewahi kusikia **taarifa** ya habari kwenye redio leo hii ?
4. Watu hufanya **shughuli** mbali mbali kwa kujiendeleza kiuchumi.
5. Ripoti huandikwa kwa **madhumuni** ya kuarifu watu kuhusu mabadiliko muhimu.
6. Ripoti huandikwa kwa madhumuni ya **kuarifu** watu kuhusu mabadiliko muhimu.
7. **Walipendekeza** mkutano ahairishwe.
8. Kitendo hiki kinaomba **utendakazi** mkubwa.
9. Walimu hutumia **mbinu** mbali mbali za kufundishia.
10. **Kiini** cha maradhi yake ni uvutaji sigara.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waoanishe maneno kutoka fungu la A na maana zake katika fungu la B*

**Majibu**

1. d
2. e
3. b
4. i
5. j
6. h

7. a
8. g
9. c
10. f

### 27.4.3 Sarufi

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wachunguze sentensi kisha watunge sentesi kama hizo.Hizi ni sentensi pendekezi*

1. "Unafanya nini?" Kalisa aliuliza.
2. "Utarudi lini?" Mama yake alitaka kujua.
3. "Ninyi ni wanafunzi?" Karake aliuliza
4. Baba yake alitaka kujua wakati mtoto angerudi.
5. Mwalimu aliuliza wanafunzi kama walifanya mazoezi waliyoachiwa.

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wachunguze sentensi kisha wazigeuze katika usemi wa taarifa.*

1. "Wewe ni mwalimu?" Mtoto aliuliza.

**Mtoto alitaka kujua ikiwa yeye alikua mwalimu.**

2. "Utafanya ripoti ya mkutano lini?" Mwenyekiti alitaka kujua.

**Mwenyekiti alitaka kujua wakati angefanya mkutano.**

4. "Utaenda shuleni lini?" Mama aliuliza

**Mama alitaka kujua wakati angeenda shuleni.**

4. "Kwa nini ripoti ya kifedha haijaonekana?" Katibu mtendaji aliuliza.

Katibu mtendaji alitaka kujua sababu ya ripoti ya kifedha kutoonekana.

Katibu mtendaji aliuliza/ alitaka kujua sababu ripoti ya kifedha ilikua haijaonekana.

5. "Mlichagua mada gani?" Mwalimu alitaka kujua.

Mwalimu alitaka kujua mada waliyochagua.

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wachunguze sentensi kisha wazigeuze katika usemi halisi.*

**Majibu**

1. Karisa alitaka kujua ikiwa mgeni wake angerudi siku ambayo ingefuatia.
   **"Utarudi kesho ?" Karisa aliuliza mgeni.**
3. Kariza aliuliza sababu ya kukosa kazi.

**“Kwa nini nilikosa kazi ?” Kariza aliuliza.**

5. Mwalimu aliuliza wanafunzi jinsi wangeshinda mtihani wakati hawakutaka kujifunza.

   **“Mtashindaje mtihani wakati hamtaki kujifunza ?” Mwalimu aliuliza wanafunzi.**

7. Mama aliwauliza watoto wake ikiwa walifanya kazi aliyowapatia.

   **“Je, mlifanya kazi niliyowapatia?” Mama aliwauliza watoto wake.**

9. Manzi alitaka kujua ikiwa angeshiriki katika mkutano.

**“Je, nitashiriki katika mkutano?” Manzi aliuliza.**

### 27.4.4. Matumizi ya Lugha

**Zoezi la 7: (*Angalia katika kitabu cha mwanafunzi*)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wakamilishe maneno kwa kutumia herufi zinazokosekana ili yaweze kuleta maana.. :*

**Majibu**

| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | k | a | w | a | i | d | a | | | | |
| 2. | m | a | p | a | t | o | | | | | |
| 3. | l | e | n | g | o | | | | | | |
| 4. | p | e | n | d | e | k | e | z | o | | |
| 5. | k | i | i | n | i | | | | | | |
| 6. | u | t | a | n | g | u | l | i | z | i | |
| 7. | u | t | e | k | e | l | e | z | a | j | i |
| 8. | p | o | l | i | s | i | | | | | |
| 9. | m | a | e | n | d | e | l | e | o | | |
| 10. | u | t | a | r | a | t | i | b | u | | |

**Zoezi la 8: (*Angalia katika kitabu cha mwanafunzi*)**

*katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi wajadili mada walizopewa kuhusu ripoti. Mwalimu ahakikishe kwambawanafunzi wote wanashiriki katika mjadala huo.*

1. Ripoti kuhusu ziara wanafunzi wa shule yako waliyofanya katika jumba la makumbusho.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Lengo la ziara
- Mahali na tarehe walifanya ziara hiyo
- Mambo waliyoyaona

- Watu walioulizwa maswali katika ripoti
- Funzo  kutokana na ziara hiyo
- Mapendekezo kuhusu waliyoyaona

2. Ripoti kuhusu kongamano la lugha ya Kiswahili uliloshiriki

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Lengo la ziara
- Mahali na tarehe kongamano lilifanyika
- Watu waliohudhuria kongamano
- Mambo yaliyozungumziwa
- Watu walioshirikishwa katika ripoti
- Funzo kutokana na kongamano hilo.
- Mapendekezo.

### 27.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza.

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Mwalimu agawe makundi ya wanafunzi wanne wanne. Kisha makundi mawili mawili yajadili kuhusu mojawapo wa mada walizopewa.*

1. Ripoti kuhusu mchango wa mwanafunzi katika maisha yake ya shule mahali anaposoma.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kushiriki katika masomo yote
- Kuheshimu kanuni za shule
- Kuboresha usafi shuleni
- Mapendekezo (Uelimishwaji wa wazazi, uwajibikaji wa viongozi katika kutatua

shida za wanafunzi, n.k.)

2. Ripoti kuhusu klabu za wanafunzi katika shule zinazopatikana katika tarafa yako.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Umuhimu wa klabu za wanafunzi
- Aina za klabu
- Wanamemba wa klabu
- Vitendo vinavyofanywa na klabu
- Mapendekezo (kupewa muda, vifaa vya kutumia,kuheshimu kanuni za shule, n.k.)

### 27.4.6 Kuandika

**Zoezi la 10: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa kuzingatia maana ya ripoti, wanafunzi watunge kifungu cha habari kuhusu moja ya mada zifuatazo:*

**Mambo ya kuzingatiwa**

3. Shida za wanafunzi shuleni.
    - Ukosefu wa karo za shule
    - Uwajibikaji duni wa wazazi
    - Ukosefu wa vifaa vya kujifunzia
    - Safari ndefu, n.k.

4. Kuboresha elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Sababu ya kuandika ripoti hii
- Matatizo yanayowakumba wanafunzi wenye ulemavu
- Aina ya ulemavu
- Vifaa maalum vya kutumia
- Uelimishwaji wa walimu

## SOMO LA 28: UTUNZI WA RIPOTI

### 28.1. Ujuzi wa Awali/Utangulizi

Mada hii inahusika na uandishi wa ripoti juu ya mada iliyotolewa na kuelewa jinsi ya kumnukuu mtu mwingine. Kwa kuanza somo hili, mwalimu awaulize wanafunzi somo walilojifunza wakati uliopita. Wanafunzi wajibu maswali husika. Kisha mwalimu awachangamshe kwa kuwasimulia habari aliyoifuata kwenye redio au aliyoisoma katika gazeti. Mwalimu aombe wanafunzi kuwapasha wenzao habari nyingine waliyosikiliza kwenye redio au runinga au tukio lolote waliloshuhudia. Baadaye, mwalimu aweke wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwapa kazi kutoka kwenye vitabu vya Kiswahili. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yafuatayo.

1. Eleza wahusika unaowaona kwenye picha hii.
2. Wahusika hawa wako wapi?
3. Eleza shughuli inayoendelea kwenye mchoro huu.
4. Watu wambao hawakushiriki katika kitendo hicho watajuaje yaliyotokea hapo?

Wanafunzi wapewe dakika tatu na kila kundi liwe na msimamizi wa kuwasilisha matokeo yake bila kurudia yaliyosemwa na makundi mengine. Mwisho wake mwalimu asahihishe wanafunzi ikiwa inatakiwa kufanya hivyo.

## 28.2 Zana au Vifaa vya Kujifunzia

Mwalimu atafute zana za ufundishaji ambazo zitamsaidia kufikia malengo ya somo lake. Mwalimu anaweza kutumia vifaa vifuatavyo :

- Kitabu cha mwanafunzi,
- Mwongozo wa mwalimu,
- Vinasa sauti au rekodi
- Magazeti

5. Ubao, chaki na vifaa vinavyoweza kuwasadia wanafunzi kuelewa somo kwa kutilia mkazo kwenye hali za wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalum.

## 28.3. Mbinu za Kufundishia na Kujifunza

Mwalimu atafute mbinu za kumfikisha kwenye malengo ya somo.Hapa chini kuna mbinu tofauti za kurahisisha maendeleo ya somo darasani.

- **Njia shirikishi**

Njia shirikishi hutumia **makundi ya wanafunzi**. Mwalimu awape wanafunzi kazi ya kufanyiwa katika makundi ya watu wawili, watatu, wanne, n.k kulingana na idadi ya wanafunzi darasani. Mwalimu achunguze mara kwa mara jinsi kazi inafavyonyika. Wakati wowote, mwalimu atumie muda vizuri na atoe msaada ambapo unahijika.

Makundi yaundwe na mchanganyiko wa wasichana na wavulana, na wanafunzi wenye shida za kibinafsi kama walemavu na wengineo. Baada ya kazi katika makundi wanafunzi wamulike matokea ya kazi yao kwa darasa ili wanafunzi wote wapate kujua mafanikio ya wanafunzi wenzao.

- **Kazi binafsi kwa mwanafunzi**

Katika somo hili, kuna mazoezi ya kutosha ambayo ni ya kufanywa kibinafsi kwa kusaidia kila mwanafunzi kuelewa kiundani na kuhakikisha kwamba lengo la somo limetimizwa. Kila mwanafunzi ajibu maswali peke yake. Aidha, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi mazoezi hayo wakiwa katika makundi.

- **Maswali na majibu**

Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuuliza maswali na na kuyajibu wenyewe, wanafunzi kwa wanafunzi. Hivi ni kusema kwamba maswali ya wanafunzi yajibiwe na wanafunzi wenzake iwezekanavyo. Mwalimu ajaribu kupitisha maswali na majibu katika hali ya majadiliano kati yake na wanafunzi ama wanafunzi peke yao. Mwalimu ajibu maswali ambayo wanafunzi wanashindwa kujibu vilivyo. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kujibiwa na wanafunzi, na vile vile wanafunzi wamwulize mwalimu na wanafunzi wengine wajibu, mwisho wake mwalimu ajibu ikiwa inatakiwa.

**Maelezo ya mwalimu:**

Mwalimu atambuwe ujuzi unaohitaji mwelekeo na maelezo ya ziada. Mwalimu ahakikishe kwamba vikwazo vyote vinatoweka iwezekanavyo. Katika hatuua hii wanafunzi wapewe pia fursa ya kutoa maoni yao kuhusu maelezo ya mwalimu.

## 28.4. Majibu

**Zoezi ya 1:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Kwa makundi ya wanafunzi wawili wawili, mwalimu awaombe watazame mchoro kwa makini kisha waeleze wanayoyaona kwenye mchoro.*

### 28.4.1 Maswali ya Ufahamu

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wasome kifungu cha ripoti, kisha wajibu maswali ya ufahamu.*

**Majibu :**

1. Ripoti kuhusu kazi za umuganda zilizofanyika katika Tarafa za Kabaya na Hindiro Wilayani Ngororero tarehe 27 Aprili hadi tarehe ya 10 Mei 2018.
2. Tukio hili liliyukia katika Tarafa za Kabaya na Hindiro Wilayani Ngororero tarehe 27 Aprili hadi tarehe ya 10 Mei 2018.
3. Kamati iliundwa na watu watano ambapo watu wawili walitoka Wizara ya Serikali za Mitaa na watu watatu kutoka Wizara ya Maafa.
4. Lengo lake lilikuwa kuchunguza athari za umuganda katika kutafuta suluhu kwa maafa yaliyosababishwa na mmomonyoko wa ardhi.
5. Maafa hayo yalisababishwa na mvua kubwa zilizobabisha mmomonyoko wa udongo.
6. Serikali ya Rwanda imeipa kipaumbele sera ya kazi za umuganda kama njia kujitegemea nakuboresha uchumi,maisha na maendeleo ya wanajamii wote.
7. Shughuli zilizofanywa kwa kupunguza maafa hayo ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa miundombinu, uboreshaji usafi na uhifadhi wa mazingira.
8. Kuna umuhimu wa kupanda miti kwenye milimakwa kukabiliana na mmomonyoko wa ardhi.
9. Vifaa hivyo vinatia ndani rato, toroli, fyekeo, ngazi za kisasa, sululu na nyundo.
10. Alipendekeza hayo kwa sababuilibainika kuwa kuna wale ambao bado hawajauona umuhimu wa kazi za umuganda.

### 28.4.2 Msamiati

**Zoezi la 2:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watunge sentensi wakitumia maneno waliyopewa.*

**Mwanafunzi anaweza kutunga sentesi kama hizi::**

1. Aliadhibiwa kwa kutumia maneno ya **kuchochea** uhasama.
2. Raia waliokumbwa na mafuriko wamepewa msaada wa **a.**
3. Wazazi wana **wajibu** wa kulisha na kusomesha watoto wao.
4. Raia wamefukia **madimbwi** barabarani kwa kuyawezesha magari kupita.
5. Tunalazimishwa kukata **vichaka** vinavyozunguka makao yetu kwa kufukuza mbu asababishaye malaria.
6. Mwalimu **alitushurutisha** kusoma magazeti ya Kiswahili.
7. Watu hupenda kujenga nyumba katika **msimu** wa kiangazi.
8. **Mradi** wa ufugaji wa kuku umempatia faida kubwa.
9. Usawa wa jinsia ni mojawapo wa **maswala mtambuka.**
10. Usipoepukana na uvutaji wa sigara **utaathirika**kwa madhara yake.
11. **Wannachiwamechangia** pesa za kukamilisha ujenzi wa shule yetu.
12. Barabara, umeme, shule, hospitali n.k hiyo ni **miundombinu** inayowezesha shughuli mbalimbali kufanyika kwa ufanisi.
13. Tusisubiri watu wengine kutoka **ng'ambo** kutufanyia yale ambayo tanaweza kuyafanya wenyewe.
14. Alikuwa anatumia **fyekeo** kwa kukata nyasi kando na nyumba yake.

**Zoezi la 3:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi waoanishe maneno kutoka fungu la A na maana zake katika fungu la B*

**Majibu**

1. e
2. f
3. j
4. c
5. a
6. b
7. d
8. i
9. h
10. g

**Zoezi la 4:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wakamilishe sentensi kwa kutumia maneno waliyopewa.*

**Majibu**

1. Alikuwa anatumia **fyekeo** kwa kukata nyasi zilizoota kando ya barabara.

2. Usawa jinsia ni mojawapo wa **masuala mtambuka** katika nchi ya Rwanda.
3. Chapakazi alifanya kazi aliyopewa kwa muda mfupi kwa **kudhihirisha** ubingwa wake.
4. Maendeleo ya nchi yoyote hutegemea ujenzi wa miundombinu.
5. Tulianzisha **mradi** wa ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha sementi.

## 28.3 SARUFI : Usemi Halisi/Usemi wa Asili

**Zoezi la 5:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame sentensi walizopewa kisha watoe maoni yao kuhusu muundo wa sentensi hizo.*

Maelezo ambayo wanafunzi wanaweza kuyatoa ni haya yafuatayo:

- Kumetumiwa alama za mtajo mwanzo na mwisho wa maneno yaliyosemwa. {“ ”}
- Sentensi katika alama za mtajo huanza kwa herufi kubwa.
- Kumetumiwa alama ya kuuliza, na alama zingine kabla ya alama za kufungia.

Kutokana na maelezo ya wanafunzi, mwalimu awaombe kutoa maana ya usemi wa asili (usemi halisi).

**Zoezi la 6:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

Wanafunzi katika makundi yao wafanye zoezi hili kwa kuweka alama sahihi kwenye sentensi walizopewa.

**Majibu:**

1. “Ninampenda mke wangu.” Karangwa alisema.
2. “Umewezaje kuubeba mzigo huu peke yako?” Mama aliniuliza.
3. “Utarudi kesho?” Mama yake alitaka kujua.
4. “Malizeni kazi mliyopewa.” mwalimu alituamrisha.
5. “Mtahitaji vikombe vingapi vya chai?”Mwenye hoteli alituuliza.

**Usemi wa taarifa**

**Zoezi la 7:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi watazame sentensi walizopewa kisha watoe maoni yao Kuhusu muundo wa sentensi hizo.*

**Maelezo pendekezi ya wanafunzi kuhusu muundo wa sentensi:**

- Alama za kufungulia au kufungia maneno yaliyotamkwa haziwekwi.
- Alama ya kuuliza na ya mshangao hazitumiwi.
- Maneno **‘kuwa’** na **‘kwamba’** au **‘ya kwamba**’hutumiwa.

Baada ya maelezo ya wanafunzi, mwalimu awaombe kutoa maana ya usemi wa taarifa.

**Zoezi la 8:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wanafunzi wachunguze sentensi kisha wazigeuze katika usemi halisi.*

**Majibu**

1. Baba alituahidi kwamba angetupeleka mjini kutembea tungeshinda mtihani mwaka ambao ungefuata.

**"Nitawapeleka mjini kutembea mkishinda mtihani mwaka ujao." Baba alituahidi.**

2. Katibu alitangaza kuwa kungekuwa na mkutano wa wanachama wote ambao walikuwa wamesajiliwa mwezi huo Jumanne iliyopita.

**"Kutakuwa na mkutano wa wanachama wote ambao wamesajiliwa mwezi huu Jumanne iliyotangulia." Katibu alitangaza**

3. Mshauri aliwasisitizia watoto kuwa kuna umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hilo lingeongeza siku zao duniani.

**"Kuna umuhimu kuwatii wazazi wenu; Hili litaongeza siku zenu duniani." Mshauri aliwasisitizia watoto.**

4 Kiranja alitaka kujua sababu ya Afida kuchelewa darasani siku hiyo.

**"Afida, kwa nini leo umechelewa darasani?" Kiranja aliuliza.**

5. Mwenye hoteli alitaka kujua jumla ya vikombe vya chai tungehitaji.

**"Mtahitaji vikombe vingapi vya chai?" Mwenye hoteli alitaka kujua.**

6. Mwanafunzi alimwambia kwamba angefaulu katika somo la Kiswahili.

**"Nitafaulu katika somo la Kiswahili." Mwanafunzi alimuambia.**

7. Mkuu wa shule alitahadharisha wanafunzi kutoharibu miti.

**"Msiharibu miti" Mkuu wa shule alitahadharisha.**

8. Mwalimu alitaka sote kuenda uwanjani tukashangilie timu yetu.

**"Nendeni nyote uwanjani mkashangilie timu yenu." Mwalimu alituamrisha.**

9. Kasisi alimshauri Kazimoto kuacha tabia zake ya ulevi.

**"Kazimoto, acha tabia zako ya ulevi." Kasisi alimshauri.**

**"Acha tabia zako ya ulevi." Kasisi alimshauri Kazimoto.**

10. Chapakazi alisema kuwa aliyekuwa akimtesa hakuwa adui yake bali alikuwa rafiki yake wa karibu.

**"Anayenitesa si adui yangu bali ni rafiki yangu wa karibu." Chapakazi alisema.**

**Zoezi la 9:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi yao, wanafunzi wafanye zoezi kwa kuandika sentensi walizopewa katika usemiwa taarifa.*

**Majibu:**

1. " Sitathubutu kumpa  pesa zangu"  Zawadi alisema

**Zawadi alisema kwamba hangethubutu kumpa pesa zake**.

2. "Ninampenda mke wangu sana" Yohana anatuarifu

Yohana anatuarifu kuwa anampenda mke wake sana.

3. "Mimi nitawakaribisha wageni leo jioni kisha nitaondoka kwenda kwangu kesho"    Fatuma alimuambia Juma.

**Fatuma  alimuambia Juma kwamba yeye angewakaribisha wagenisiku hiyojioni kisha angeondoka kwenda kwake siku ambayo ingefuata.**

4. "Rudieni darasani." Mwalimu aliamuru wanafunzi.

**Mwalimu aliamuru wanafunzi kurudi darasani.**

5. "Mkiendelea na tabia hiyo yenu, huenda msifanye vizuri katika mtihani"

Mwalimu aliwaonya wanafunzi.

**Mwalimu aliwaonya wanafunzi kuwa wangeendelea na tabia hiyo yao, huenda hawangefanya  vizuri katika mtihani.**

6. "Mabasi hayapiti hapa siku hizi, kwa nini ?" Maria aliulizaMaria alitaka kujua sababu  gani mabasi yalikua hayapiti hapo siku hizo.

**Maria aliuliza/alitaka kujua sababa ya mabasi kutopita hapo siku hizo.**

7. Mama alinionya "Unamochezea mna hatari."

   **Mama alinionya kwamba nilimokua nikichezea mlikua na hatari.**

8. Mwalimu mkuu alisema "Nyote mliorudi shuleni mkichelewa mtafanya mtihani mwingine maana wenzenu walimaliza kufanya mtihani tangu juzi."

**Mwalimu mkuu alisema kwamba wote waliorudi shuleni wakichelewa wangefanya mtihani mwingine kwa kuwa wenzao walikuwa wamemaliza kufanya mtihanisiku mbili zilizotangulia.**

9. "Ulienda shule jana?  Bakari aliniuliza.

**Bakari aliniuliza ikiwa nilienda shule siku iliyotangulia.**

10. "Toka nje" Mama  alimuamuru mwanawe.

**Mama alimuamuru mwanawe kutoka nje.**

**Zoezi la 10 : *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili , wanafunzi wageuze sentensi na kuziandika katika usemi halisi au usemi wa taarifa kulingana na jinsi wanavyoichunguza kila sentensi.*

**Majibu:**

1. "Utaondoka lini?" Mama alimuuliza mgeni.

**Mama alimuuliza mgeni wakati angeondotoka.**

2. "Njoo hapa." Baba aliniamuru.

**Baba aliniamuru kwenda hapo.**

3. Mwalimu aliniuliza jinsi nilivyofanya kazi ya nyumbani.

**"Ulifanyaje kazi ya nyumbani?" Mwalimu aliniuliza.**

4. Mama alituagiza kusafisha sebule kabla ya kwenda shuleni.

**"Safisheni sebule kabla ya kwenda shuleni" Mama alituagiza.**

5. "Hatutakua na mvua ya kutosha mwaka huu." Wakulima walisema.

**Wakulima walisema kwamba hawangekua na mvua ya kutosha mwaka huo.**

6. "Jua ni gimba kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto." Mwalimu alituarifu.

**Mwalimu alituarifu kuwa jua ni gimbi kubwa lenye nuru kali lililoko angani ambalo hutoa mwanga na joto.**

7. "Tafadhali, msivute bangi kamwe kwani ni hatari kwa afya yenu" Mwalimu mkuu aliwasihi wanafunzi.

**Mwalimu mkuu aliwasihi wanafunzi kutovuta bangi kamwe kwani ilikua hatari kwa afia yao.**

8. Baba alituahidi ya kuwa angetununulia zawadi za kupendeza tungefanya vizuri katika mtihani.

**"Nitawanunulia zawadi za kupendeza mkifanya vizuri katika mtihani." Baba alituahidi**

### 28.4.4 Matumizi la Lugha

**Zoezi la 11: *(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi wanafunzi watoe mambo muhimu ambayo yanaweza kuzingatiwa katika maandalizi ya ripoti inayohusu kujitoa shuleni kwa wanafunzikufuatia maelezo waliyopewa.*

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Sababu za kujitoa shuleni

- Upande wa wanafunzi
- Upande wa wazazi
- Upande wa shule (walimu na viongozi wa shule)
- Mapendekezo (uwajibikaji wa Serikali za mitaa,wazazi na viongozi wa shule )

### 28.4.5 Kusikiliza na Kuzungumza

**Zoezi la 12:** ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, wanafunzi wafanye mazungumzo kuhusu sherehe ya ndoa wakilenga mambo wanayotaka kuripotia. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashiriki katika mazungumzo hayo.*

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Mahali na wakati sherehe zilifanyika
- Mavazi
- Magari
- Walioshiriki katika sherehe hizo (upande wa bibi arusi na bwana arusi)
- Mahari iliyotolewa
- Vinywaji
- Chakula
- Uungaji mkono n.k.

### 28.4.6 Kuandika

Zoezi la 13: ***(Angalia katika kitabu cha mwanafunzi)***

*Wanafunzi watunge ripoti kuhusu mada walizopewa wakizingatia mfumo wa kuandika ripoti. Wanafunzi watachaguwa wenyewe mada ambayo wataandika ripoti kuhusu.*

**Ziara uliyoifanya.**

- Mambo ya kuzingatiwa
- Mahali na wakati ziara ilifanyika
- Lengo la ziara
- Watu uliokutana nao
- Mambo uliyoyaona
- Mambo uliyojifunza

2. Kongamano la lugha ya Kiswahili ulililoshiriki.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Lengo la ziara
- Mahali na tarehe kongamano lilifanyika

- Watu waliohudhuria kongamano
- Mambo yaliyozungumziwa
- Watu walioshirikishwa katika ripoti
- Funzo kutokana na kongamano hilo.
- Mapendekezo.

3. Taarifa ya habari uliyoisikiliza au uliyoisoma.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Mada ya taarifa
- Mambo yanayozungumziwa
- Mapendekezo
- Chombo cha habari: redio, gazeti,televisheni.

4. Mchezo wa mpira baina ya timu ya shule yenu na shule jirani.

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Timu zilizoshiriki mchezo.
- Siku na wakati mchezo ulichezwa.
- Mashabiki
- Mabao yaliyoingizwa

## 28.5. Muhtasari wa Mada

Mada hii ya tano" **Utungaji: insha za masimulizi au kubuni na uandishi wa ripot**i" ina vipengele sita yaani masomo makuu sita yanayohusiana na mada husika. Kila somo lina vipengele vidogo kama vile: mchoro, kifungu cha habari, maswali ya ufahamu, matumizi ya msamiati, sarufi, matumizi ya lugha, kusikiliza na kuzungumza, kuandika, na maelezo muhimu. **Somo la kwanza** linaeleza maana ya insha. **Somo la pili** niaina za insha.**Somo la tatu** ni insha ya masimulizi. **Somo la nne** ni insha ya kubuni. S**omo la tano** linaeleza dhana ya ripoti na aina zake. **Somo la sita** ambalo ni la mwisho linahusu utunzi wa ripoti. Katika kila somo kuna kipengele cha sarufi ambacho kinagusia usemi wa asili na usemi wa taarifa.

## 28.6. Maelezo ya ziada

### i. Maelezo muhimu kuhusu Insha

**Fasili ya Insha**

insha ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo. Kwa hiyo tunaweza kusema kuwa, utungaji ni utoaji wa mawazo binafsi kutoka akilini mwa mtu kuhusiana na mambo mbalimbali katika jamii, kisha kuyaweka wazi kwa njia ya mdomo au maandishi.

- **Sehemu Kuu za Insha:**

Insha hugawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

**·Utangulizi(Mwanzo)**

Katikasehemuhiiinampasamwandishiatoemaelezomafupinamaanayahabarialiyopewa.

**·Kiini cha insha(Kati)**

Inamlazimu mwandishi afafanue kwa mapana mada anayoishughulikia huku akitoa mifano hai inayoendana na hali halisi. Kwa kawaida sehemu hii hueleza kwa ukamilifu kila hoja iliyodokezwa katika utangulizi.

**· Hitimisho (Mwisho)**

Inampasa mwandishi kutoa mapendekezo (maoni) ya msingi au kusisitiza kwa ufupi yale aliyoyaelezea katika habari yenyewe. Mwisho wa insha huonyesha uhusiano uliopo kati ya utangulizi na maelezo yaliyomo ktika mwili.

- **Taratibu za Kutunga Insha:**
- Soma kwa makini mada/kichwa/anwani uliyopewa zaidi ya mara moja, ili uielewe vizuri.
- Ifikirie mada/kichwa/anwani kwa muda.
- Yaandike mambo muhimu yatakayokuongoza katika kuiandika insha
- Maelezo yote yatolewe kwa undani na kwa njia ya kuvutia.
- Kutumia vizuri alama za uakifishaji
- Kupanga mawazo katika mtiririko wenye mantiki
- Tumia msamiati mwafaka kwa kutegemea mada.
- Lugha iwe ya adabu na isiyo ya matusi
- Andika methali, misemo na nahau ambazo unadhania zinaweza kukufaa katika
- utungaji.
- **Aina za insha**

Insha ni za aina nyingi kulingana na namna zilivyoandikwa au kulingana na kusudi lake. Katika utungaji wa insha kuna insha za wasifu, insha za picha, insha za mdokezo, insha za masimulizi, insha za methali, insha za hoja na insha za kubuni.

1. **Insha za wasifu**

Insha za wasifu ni aina za insha ambazo hueleza sifa za mtu, kitu au jambo fulani. Insha za aina hii husimulia sifa, maisha au maelezo mengine muhimu kuhusu mtu fulani, kitu fulani au jambo fulani. Ni kusema kuwa katika aina hizi za insha mwandishi anaandika kuhusu uzuri au ubaya wa mtu, kitu au jambo fulani.

**2. Insha za picha**

Insha za picha ni aina za insha ambazo hueleza picha iliyotolewa. Kusema kwamba mwandishi hueleza mambo anayoyaona kwenye picha/mchoro ni kusema kwamba mwandindi huyu analazimika kufanya andiko lenye mfuatano wa mawazo kulingana na mfuatano wa picha au michoro aliyopewa.

**3. Insha ya mdokezo**

Insha za mdokezo ni aina za insha ambazo mwandishi hupewa mwongozo wa kufuatilia katika utunzi wake. Kwa mfano, mwandishi anaweza kupewa orodha ya hoja kadha kutokana na kichwa kilichotolewa akajenga insha. Vilevile anaweza kupewa utangulizi au kimalizio cha insha na kuagizwa aendelee na insha au aanze insha aliyopewa.

**4. Insha za methali**

Insha ya methali ni aina ya insha ambayo mada yake huwa ni methali ambayo mwandishi anaomba kujadilia. Katika uandishi wa insha ya aina hii, mwandishi ni lazima atoe hoja kwa kukubaliana na methali iliyotolewa. Hili ni kwa sababu methali hujaa mambo ya hekima.

**5. Insha za hoja**

Insha za hoja ni aina ya insha ambazo mwandishi analazimishwa kutoa hoja zinazotetea mada na nyingine zinazopinga mada. Mwishoni mwa insha hii, mwandishi anaonyesha msimamo wake kulingana na mada iliyotolewa.

**6. Insha za masimulizi**

Insha za masimulizi ni aina ya insha ambazo ndani yake mwandishi anasimulia au anaeleza tukio fulani maalum la kweli au la kubuni kwa njia ya kisanaa.

**7. Insha za kubuni**

Insha za kubuni ni aina ya insha ambazo hutungwa kuhusu mawazo yanayozuliwa na ambayo si matukio ya kawaida. Ni kusema kwamba mwandishi hubuni mandhari, wahusika, matukio, nk.

**ii.Maelezo muhimu kuhusu uandishi wa ripoti**

Unapoandika ripoti inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo:

Hakikisha kuwa umeelewa shughuli inayohusika

- Hakikisha unajua urefu unaohitajika na masuala unayopaswa kuyagusia
- Kusanya maelezo yote unayohitaji kuhusiana na ripoti hiyo.
- Yapange maelezo yako vizuri. Zipitie hoja zako ili uondoe mawazo ambayo yanaweza kuwa yamerudifishwa au yamerudiwa.
- Yaangalie mawazo yako ili kubainisha ni yapi ambayo yanapaswa kutangulia na yanafuatwa na yapi.
- Unapoandika ripoti yako hakikisha kuwa unaitumia lugha yako. Usiridhike

tu na maneno unayoyapatawakati wa uchunguzi wako. Kuandika ripoti kwa lugha na maneno yako huonyesha kuwa umeielewa.

- Unaweza kuuboresha uwezo wako wa kuandika ripoti kwa kujitahidi kuyaelewa maelezo yanayohusika na kujitahidi kuyaeleza kivyake.
- Baada ya kuandika nakala ya kwanza ya ripoti unaweza kuiboresha kwa kupnguza mambo ambayo sio muhimukatika ripoti hiyo.
- Lugha inayotumiwa katika uandishi wa ripoti lazima izingatie wasomaji wa ripoti inayohusika. Kwa mfano, ikiwa wasomaji ni wanafunzi wa shule lugha yake haipaswi kuwa na ugumu au utata wa kisayansi.

## 28.7 Tathmini ya Mada ya Tano (majibu)

1. Katika makundi yao, wanafunzi watunge insha kulingana na chaguo lao badhi ya mada walizopewa.

i. Siku ya kuadhimisha mwaka mpya.

Mambo ya kuzingatiwa :

- Umuhimu wa siku hiyo
- Mahali na tarehe tukio lilitukia
- Walioalikwa
- Burudani
- Chakula, n.k.

ii. Safari yangu mjini Kigali.

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Umuhimu wa kusafiri
- Lengo la safari yangu
- Muda wa safari
- Mambo niliyoyaona
- Funzo kutokana na safari, n.k.

ii. Utoto wangu.

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Umuhimu wa kusimulia jambo hili
- Tabia za utotoni
- Malezi ya wazazi wangu,
- Funzo au maadili, n.k.

Likizo iliyopita.

**Mambo ya kuzingatiwa :**

- Kazi nilizozifanya

- Mahali nilipotembelea,
- Funzo au maadili, n.k

2. Kazi hii ifanyike kibinafsi ; kila mwanafunzi aandike ripoti kuhusu mada inayohusika akizingatia mtindo wa kuandika ripoti.

**Mambo ya kuzingatiwa :**

**i. Kichwa cha ripoti** (Tarehe ya kuwasilishwa)

**ii.Utangulizi** (lengo la ripoti)

**iii. Mwili** (Matokeo)

. Usafirishaji wa madawa ya kulevya

. Watumiaji wa madawa hayo

. Athari (kiafya, kiuchumi, kiusalama)

**iv. Mapendekezo**

. Sheria

. Uwajibikaji wa serikali za mitaa

. Uelimishaji wa wanajamii

**v. hitimisho**

3. Kazi hii ifanyike kibinafsi ; kila mwanafunzi ageuze sentensi alizotolewa ziwe katika usemi wa taarifa au usemi halisi.

i. "Nyote mwende uwanjani kushangilia timu yenu."Mwalimu alitushurutisha

ii. Katibu mtendaji wa tarafa alisema kuwa mtoto ni mtoto akiwa wa kiume au wa kike.

iii. Mwalimu aliuliza Faida sababu ya kuchelewa darasani siku hiyo.

iv. "Msiharibu mazingira."Mkuu wa shule alitahadharisha wanafunzi.

iv. Mama alisema kwamba jinsi unavyomlea mtoto ndivyo anavyokua.

v. Mwanafunzi alimwambia,"Nitafaulu katika somo la Kiswahili."

vi. Au "Utafaulu katika somo la Kiswahili." Mwanafunzi alimwambia.

vii. Mwalimu alituarifu kuwamwezi ni gimba linalozunguka dunia na linang'ara usiku.

viii. Katibu alitangaza,"Kutakuwa na mkutano wa wanachama wote mwezi huu Jumanne ijayo."

## 28.8. Mazoezi ya Ziada

### 28.8.1. Mazoezi ya Urekebishaji

**a) Sarufi: Geuza sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa**

1. "Ninaenda kulima shamba langu." Mwanangu anasema.

2. “Tunasoma vizuri somo la Kiswahili.” Wanafunzi wanasema.

3. “Tunawasaidia wenzetu wenye matatizo ya kutembea.” Mkuu wa wilaya alitangaza.

4. “Mji mkuu wa Rwanda ni Kigali.” Richard Kant alitangaza.

5. “Jina langu ni Chapakazi.” Jirani yangu alijibu.

**1Jibu maswali yafuatayo kuhusu utungaji.**

1. Nini maana ya insha?
2. Taja aina tatu za insha?
3. Eleza maana ya ripoti.

**Majibu**

**a. Sarufi**

1. Mwanangu anasema kwamba anaenda kulima shamba lake.
2. wanafunzi wanasema kuwa wanasoma vizuri somo la Kiswahili.
3. Mkuu wa wilaya alitangaza kwamba waliwasaidia wenzao wenye matatizo ya kutembea. Au
3. Mkuu wa wilaya alitangaza kwamba tuliwasaidia wenzetu wenye matatizo ya kutembea.
4. Richard Kant alitangaza kuwa mji mkuu wa Rwanda ni kigali.
5. Jirani yangu alijibu kwamba jina lake ni Chapakazi.

**b)**

1. Insha ni mtungo wa kinathari unaozungumzia suala au kusimulia kisa fulani. Kisa hicho au suala hilo ndilo mada ya utungo huo.
2. Aina za insha ni insha za wasifu, insha za kubuni, insha za maelezo, insha za methali, insha na picha, n.k.
3. Ripoti ni maelezo yanayotolewa kuhusu mtu, kitu au jambo fulani lililotokea. Aidha, ripoti ni taarifa inayohusiana na shughuli au jambo fulani lililofanywa au kufanyika.

### 28.8.2. Mazoezi Jumuishi

**a) Sarufi: andika sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa**

1. “Kesho tutaenda kupanda miti.” Mwalimu mkuu aliwaarifu wanafunzi.
2. “Jana tulijipimisha ugonjwa wa UKIMWI.” Bi harusi alimwambia mkuu wa tarafa.
3. “Wazazi walikopesha fedha kutoka benki kwa kuandaa mradi wa ufugaji.” Rafiki yangu aliniandikia.
4. “Kalisa alipatanisha mume na mke walipopambana.” Mwanamke aliwajulisha wenzake.
5. “Kesho tutamkumbuka Kalisa aliyeuawa katika mauaji ya kimbari ya 1994.”

Mjane mmoja aliwatangazia majirani.

b) Tunga insha ya masimulizi nyenye mada ifuatayo: “safari yangu ya kwanza mjini Kigali”.

**Majibu**

**a)Sarufi**

1. Mwalimu mkuu aliwaarifu wanafunzi kuwa siku iliyofuata/siku moja baadaye wangeenda kupanda miti.
2. Bi harusi alimwambia mkuu wa tarafa kwamba walijipimisha ugonjwa wa UKIMWI siku moja kabla.
3. Rafiki yangu aliniandikia kwamba wazazi wake walikopesha fedha kutoka beki kwa kuandaa mradi wa ufugaji.
4. Mwanamke aliwajulisha wenzake kuwa Kalisa alipatanisha mume na mke walipopambana.
5. Mjane mmoja aliwatangazia majiraki kwamba siku iliyofuata/ siku moja baadaye wangemkumbuka Kalisa aliyeuawa katika mauaji ya kimbari ya 1994.

**Mambo ya kuzingatiwa:**

- Kufuata taratibu zote za kutunga insha.
- Kufuata taratibu zote za kutunga insha za masimulizi.
- msamiati kuhusu mambo ya kusafili (basi, tiketi, nauli, kituo cha mabasi, ....)
- Sehemu za mji wa Kigali (madhari)
- Shughuli mbalimbali zinazofanyika mjini Kigali
- Na kadhalika

### 28.8.3. Mazoezi ya Nyongeza

**Fanya mazoezi yafuatayo**

**1. Geuza sentensi zifuatazo katika usemi wa taarifa.**

1. “Fanya haraka mazoezi haya!” Mwalimu alimwamrishamwanafunzi.
2. “Njoo hapa tuzungumze kuhusu mradi huu!” Baba aliniambia.
3. “Fungeni madaftali yenu tupige deki!” Kiranja wa darasa alituonya.
4. “Mwezi wa Machi una siku ngapi?” Mzazi wangu aliniuliza.
5. “Umechunguza muda kabla ya kununua bidhaa?” Daktari alimuuliza mgonjwa.

**2. Geuza sentensi zifuatazo katika usemi halisi.**

1. Mnunuzi alimuuliza muuzaji bei ya kikapu kimoja.
2. Daktari aliniambia nikaonane naye baada ya wiki mbili.
3. Mshukiwa aliapa mbele ya hakimu kuwa hakuiba mali ya tajiri.

4. Mshitakiwa alikili mbele ya majaji kuwa alikuwa na hatia.
5. Baba alimshuri mtoto wake kuwa na maadili.

Tunga ripoti ya mechi ya soka iliyokutanisha timu ya shule yako na shule jirani Jumamosi iliyopita.

**Majibu**

**a)Usemi wa taarifa**

1. Mwalimu alimwamrisha mwanafunzi kufanya haraka mazoezi hayo.
2. Baba alinishurutisha kuenda pale ili wazungumze kuhusu mradi ule.
3. Kiranja wa darasa alituonya kufunga madaftali yetu ili tupige deki.
4. Mzazi wangu alitaka/aliniuliza idadi ya siku za mwezi wa Machi.
5. Daktari alimuuliza mgonjwa ikiwa alichunguza muda kabla ya kununua budhaa.

**b) Usemi halisi**

1. “Kikapu kimoja ni bei gani?” Mnunuzi alimuuliza muuzaji.
2. “Onana nami baada ya wiki mbili!” Daktari aliniambia.
3. “Sijaiba/ sikuiba mali ya tajiri.” Mshukiwa aliapa mbele ya hakimu.
4. “Nini hatia!” Mstakiwa alikili mbele ya majaji.
5. “Mtoto wangu, vizuri uwe na maadili.” Baba alimshauri mtoto wake.

**c)Ripoti**

**Mambo ya kuzingatiwa**

- Kichwa cha ripoti
- Tarehe ya mechi
- Utangulizi
- Matokeo
- Mapendekezo
- Hitimisho
- Msamiati kuhusu mchezo wa mpira wa miguu( goli, bao, wachezaji, refa, golikipa, mabeki, washambuliaji......)

# MAREJEO


Kitula G.K., (2014), Taaluma ya Uandishi, JKF, Nairobi

Kitula G.K., (2010), Mazoezi na Marudio ya Kiswahili, Kenya Literature Bureau, Nairobi

Mdee J.S, K. Njogu, Shafi (2012), Kamusi ya Karne ya 21, Longhorn Publishers, Nairobi

Method S. A. et al., (2013), Johari ya Kiswahili. International print -o- Pac Limited Dar es salaam.

Mlaga. W. K. (2017). Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21. Heko Publishers Ltd. Dar es salaam.

Mlaga. W. K. (2017). Historia ya Kiswahili Nchini Rwanda: Kielelezo cha Nafasi ya Utashi wa Kisiasa katika Ustawi wa Lugha, Katika Jarida la Kioo cha Lugha., Juz. 15, kur. 1 – 17

Mohamed, Mohamed A. (1996), Sarufi Mpya, Press And Publicity Centre, Dar es salaam

Ndalu A. (1997), Mwangaza wa Kiswahili, Printpack, Nairobi.

Niyirora E. & Ndayambaje L. (2012). Kiswahili Sanifu kwa Shule za sekondari, Tan Prints Publisher, New Delhi

Niyomugabo C. (2013). Mafunzo ya Kiswahili, Fountain Publisher, Kampala

Nkwera V. M.F. (1978) Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo. Dar-es-salaam: Tanzania Publishing House:

Ntawiyanga S., na Jacqueline M. Kinya (2016), Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2. Longhorn Publishers, Nairobi.

Ntawiyanga S., Muhamud A, Kinya J.M. na Sanja L (2017). Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 3. Longhorn Publishers, Dar es salaam.

Nyangwine, J.A. Masebo Nyambari (2010), Kiswahili kidato cha 3&4, Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

REB (2015), Muhtasari wa Somo la Kiswahili, kidato cha 4-6, Mchepuo wa Lugha, Bodi ya Elimu Rwanda.

REB (2016), Masomo ya Kiswahili Sanifu, Morani, Nairobi.

REB (2016), Masomo ya Kiswahili Sanifu, Maorani, Nairobi.

Salim K.Bakhressa, Islam K. Islam, Fuad A ali (2008), Kiswahili Sanifu, Oxford University Press, East Africa Ltd, Kigali.

TUKI (1996), English-Kiswahili Dictionary, Mkuki na Nyota Publishers, Dar es salaam.

TUKI (1996), Kamusi ya Kiswahili Toleo la pili, English Press Ltd, Nairobi.

TUKI (2004), Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili, Oxford University Press, Nairobi.

TUKI (2013), Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo laa 3, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Wamasati W.A, (-), Quick Fire Revision Kiswahili, Bookmania Stationers, Nairobi.

Wamitila, K.W., (2011), Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi, Focus Books, Nairobi.

Wamitila, K.W., (2009), Mwenge wa Uandishi Mbinu za Insha na Utunzi, Printwell Industries

LTtd, Nairobi

Wizara ya mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987), Kitabu cha Kiswahili IV B, Taasisi ya Elimu ya Rwanda, Kigali.

Wizara ya mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987), Kitabu cha Kiswahili IV – VA, Taasisi ya Elimu ya Rwanda , Kigali.

Wizara ya mafunzo ya Msingi na Sekondari (1987) Kitabu cha Kiswahili IV- VC,Taasisi ya Elimu ya Rwanda, Kigali.